

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Tano – Tarehe 5 Februari, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mhe. Dkt. Adelardus Lubango Kilangi

**NAIBU SPIKA:** Katibul

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA - K.n.y MWENYEKITI  
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu shughuli za kamati kwa mwaka 2017.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 55

**Changamoto Zinazowakabili Wale mavu**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** alluliza:-

Watanzania wenyе ulemavu wanakabiliwa na kero mbalimbali za kimaisha ikiwemo ukosefu wa ajira kama ilivyo kwa Watanzania wengine, aidha, zipo changamoto za jumla kama vile kijana mwenye ulemavu wa ngozi asiye na ajira ana changamoto ya mahitaji ya kujikimu na pia ana changamoto za kipekee za mahitaji ya kiafya na kiusalama.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu umuhimu wa kuwatazama vijana wenyе ulemavu mbalimbali kwa namna ya pekee na kama zipo sera na mikakati ya kiujumla kwa vijana wote nchini?

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Waziri Mkuu sijui nani anayejibu maswali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE  
ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa lkupa Alex, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wale mavu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE  
ULEMAVU alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua vijana wenyе ulemavu kuwa ni kundi mojawapo mionganі mwa Watanzania wenyе ulemavu nchini ambalo linakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazorudisha nyuma maendeleo yao. Mojawapo ya changamoto hizo ni ukosefu wa ajira, huduma za afya, uwezo mdogo wa kuyamudu mahitaji ya kujikimu, umaskini na changamoto ya kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kundi hilli la watu wenyе ulemavu wakiwemo vijana wenyе ulemavu, Serikali iliunda Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu ambalo kazi yake kubwa ni kutoa ushauri kwa Serikali na wadau mbalimbali wanaohusika na masuala ya watu wenyе ulemavu juu ya namna bora ya kushughulikia changamoto zao, kuzijumuisha zile za kundi la vijana wenyе ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kuunda Kamati za Wenye Ulemavu kuanzia ngazi ya Mkoa, Halmashauri ya Wilaya, Kata na Mtaa/Kijiji. Kazi kubwa ya Kamati hizi ni kuhakikisha kuwa masuala ya watu wenyе ulemavu yanazingatiwa katika mipango yote ili kuondoa kero mbalimbali wanazokumbana nazo ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu elimu, ajira, afya na mikopo ya uvezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nichukue pia fursa hii kuwakumbusha na kuwahimiza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kusimamia ipasavyo utekelezaji wa suala hili ambalo liko kisheria na pia ikizingatiwa kuwa maagizo kadhaa yamekwishatolewa kwa maneno na kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha vyuo vya mafunzo ya ufundu vya watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kuajiriwa na kijajiri na kupata ujuzi mbadala wa kumudu maisha yao.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naishukuru Serikali kwa majibu yake, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja natambua jitihada za Serikali za kuweka mfumo kwa ajili ya kuwafikia walemavu, lakini suala la mfumo ni moja na suala la kufikisha huduma wanazohitaji kwa maana ya kuwfanyia upendeleo chanya (*positive discrimination*) ni lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa namna gani Serikali sasa imeweza kuwafikishla rasillimali fedha na rasillimali mafunzo watu wenye ulemavu kwenye vikundi vyao, tofauti na kuwajumuisha kwenye vikundi vingine ambapo mahitaji yao mahususi hayawesi kutimizwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa namna gani na kwa kiwango gani Serikali inadhani inaweza kuwapatia nafuu kwenye yale mambo ya msingi kwa mfano Bima ya Afya. Tuchukulie mfano mlemavu wa ngozi akipata ruzuku kwenye bima ya afya una uhakika wa kuhakikisha anakingwa kwa bima, kitu ambacho anakihitaji kama Watanzania wengine lakini yeche anakihitaji zaidi? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ulemavu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu nimpongeze sana kwa jinsi ambavyo anafuatilia na kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza linauliza ni jinsi gani Serikali imeweza kuwapatia vikundi vya watu wenye ulemavu fedha. Niki-refer kwamba swali lake

lilikuwa linauliza kwa habari ya vijana; kuna mfuko wa maendeleo ya vijana ambao mfuko huu unawawezesha vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielezee kidogo kwamba kinachotakiwa kufanyika ni kwamba vijana wanatakiwa wajunge kwenye vikundi, wakishajunga kwenye vikundi mbalimbali, kwenye maeneo yalipo wanatakiwa pia kuwe na *SACCOS*. Kwa hiyo, kama Serikali tunapeleka hela kwenye zile *SACCOS* halafu baada ya kupeleka hela kwenye zile *SACCOS* vile vikundi vinapewa kuititia zile *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo kikubwa ambacho kinapatikana kwenye hivi vikundi ni kwamba wakati ule wa kurejesha wanatakiwa warejeshe riba ya asilimia 10. Katika hilo riba ya asilimia 10, asilimia tano inabaki kwenye kikundi husika, asilimia mbili inabaki kwenye Halmashauri na asilimia tatu inaenda Serikalini. Kwa hiyo, hiyo ni njia mojawapo ambayo kama Serikali tunavipatia hivi vikundi fedha lakini pia kuna hii mifuko ya uwezeshaji kiuchumi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kikubwa ambacho ninapenda niongelee hapa, nitoe wito kwa Halmashauri mbalimbali wawahamasishe watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi, kwa sababu hizi hazitolewi kwa matu mmoja mmoja. Wawahamasishe watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi, yakiwepo makundi ya vijana lakini pia na makundi mengine ambayo sio ya vijana ili waweze kunufaika na hizi fedha ambazo zinatolewa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ameongelea kwa upande wa afya, kwa upande wa afya ametolea mfano wa watu wenye ualbino. Kwa upande wa watu wenye ualbino tayari Serikali imekwisha kuziagiza Halmashauri kwamba zinapoagiza dawa kutoka *MSD* zihakikishe zinajumuisha mafuta ya watu wenye ualbino katika madawa ambayo wanaagiza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine la pili ameongelea kwamba kwanini Serikali haitoi bima ya afya kwa watu wenye ulemavu. Niseme wazi kwamba Serikali, hicho ni kitu ambacho kama Serikali tunakichukua, hatuna *specific* kwamba hii ni bima ya afya kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Lakini watu wenye ulemavu wasiokuwa na uwezo wanatibiwa baada ya kutambulika kwamba hawa watu hawana uwezo wa kugharamia mahitaji yao. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Ally Saleh ya kuuliza swali la nyongeza, naomba maswali ya nyongeza yawe mafupi ili wengi tupate fursa ya kuuliza maswali. Ukipishauliza swali refu leo hii nitakuwa natakata hapa kwa sababu Waheshimiwa Wabunge mnaotaka kuuliza mpo wengi, sasa mkitumia muda mrefu kujieleza muda wote unaisha kwenye maelezo, wengine kwenye swali la nyongeza unataka utoe na mfano. Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jana tu nilimpongeza Waziri Mkuu kwenye *twitter* kwa tamko lake ambalo limesema kila Wizara na Idara itoe taarifa kila mwaka imetenga kiasi gani kwenye kuimarishe huduma kwa watu wanaoishi na ulemavu. Nafikiri hili ni tamko zuri sana na linafaa kupongezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imejipangaje, utaratibu huu tutaanza kuuona katika mwaka huu wa fedha? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu kama Serikali tumeu-*plan* kwamba uanze kuonekana katika bajeti ya mwaka huu wa fedha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Sasa mmeshaona mifano hapa, ninyi ambao bado mmesimama. Mheshimiwa Badwel swali la nyongeza.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa hawa wale mavu ili waweze kupata hizi ajira na huduma zingine mbalimbali ni lazima wapiti shule, vyuo na taasisi zingine ili waweze kukubalika katika hili eneo la ajira. Sasa kwa kuwa wanapitia katika shule mbalimbali ambazo zina matatizo mengi na inawafanya wasiweze kupata elimu vizuri kwa mfano Shule ya Viziwi Kigwe ambayo hakuna maji kwa muda mrefu na shule ile ni ya kitaifa na inachukua wanafunzi wengi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea maji wanafunzi wa shule ya wasiosikia Kigwe? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali niseme kwamba hilo tumelichukua na kwa sababu ni suala mtambuka, tutafanya mawasiliano ndani ya Serikali kwa maana Wizara ya Maji ili tuweze kuona jinsi gani tunaweza tukapeleka maji katika Shule ya Kigwe, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelee na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 56

### **Kituo cha Afya Mtina**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna vituo vitatu vya afya ambapo Kituo cha Afya Mtina kina zaidi ya miaka 30 hakijafanyiwa ukarabati na pia hakuna wodi ya wazazi.

Je, ni lini Serikali itajenga wodi ya wazazi katika kituo hicho na kufanya ukarabati ili kiweze kutoa huduma bora kwa wakazi wa Kata za Nasya, Semeni, Nyerere, Angalia na

wakazi wa Kata ya Mchesi, Vijiji vya Likumbula, Tuwemacho na Namasakata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina vituo vitano ambapo vituo vya afya viwili viro katika Jimbo la Tunduru Kusini na vitatu katika Jimbo la Tunduru Kaskazini. Kituo cha Afya Mtina kilianzishwa mnemo mwaka 1970 na kimekuwa kikiendelea kutoa huduma za kujifungua na huduma za matibabu ya kawaida kwa kipindi chote. Kwa sasa chumba cha kupumzikia akina mama baada ya kujifungua kimetengwa ndani ya wodi ya kawaida ya wanawake. Serikali kuititia wadau wa maendeleo (*Walter Reed Program*) waliweza kufanya ukarabati wa jengo la tiba na matunzo (*CTC*) kwa wagonjwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa msingi wa wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya Mtina unaendelea kuititia fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo la Tunduru Kusini ambapo kiasi cha shilingi milioni nne zilitolewa. Aidha, Halmashauri katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 imetenga kiasi cha shilingi milioni 10 kwa ajili ya ukarabati na kuboresha Kituo cha Afya Mtina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Tunduru, Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Mkasale kilichopo katika Jimbo la Tunduru Kusini. Aidha, Halmashauri inajenga wodi mbili za upasuaji katika Hospitali ya Wilaya, nyumba ya mganga katika zahanati ya Naikula, ukarabati wa nyumba

mbili za watumishi katika Kituo cha Afya Mchoteka na kuendeleza ujenzi wa zahanati ya Legezamwendo kuitia mapato yake ya ndani. Serikali itaendelea kuboresha vituo vya kutolea huduma za afya kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swal la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante na Mheshimiwa Naibu Waziri asante kwa majibu mazuri. Kwa kuwa kituo hiki kinahudumia zaidi ya Kata Tano, Kata ya Mtina, Lukumbulem Mchesi, Masakata na Tuwemacho.

Je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kuboresha kituo hiki ili kiweze kutoa huduma za upasauji kwa wakina mama na wajawazito?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kampeni ya mwaka 2010 Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga kituo cha afya katika Kata mbili za Nalase ambazo zipo katika Mji mmoja na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imekuwa inatenga kila mwaka na mpaka sasa imeishia kujenga msingi tu. Je, ni lini Serikali itaona haja ya kutimiza ahadi ile ya Rais wa Awamu ya Nne ili wapate kituo cha afya pale Nalasi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati jinsi ambavyo Mheshimiwa Mpakate anapigania kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma ya afya iliyo bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swal la kwanza ameuliza lini, na unaweza ukaona nia njema ya Serikali jinsi ambavyo inahakikisha huduma ya afya inapatikana na hasa katika ujenzi wa vituo vya afya katika kata husika. Hii ndio maana katika Halmashauri yake tumeanza na hiyo Kata ya

kwanza na hiyo kata nyingine kwa kadri pesa itakavyopatikana. Nia njema ya Serikali ni kuhakikisha vituo vya afya vinajengwa katika kata zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, ni kweli kwamba kuna ahadi iliyotolewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne kwamba vingejengwa vituo vya afya katika kata mbili alizozitaja na yeye mwenyewe amekiri kwamba katika hizo kata mbili kazi ambayo imefanyika mpaka sasa hivi ni ujenzi wa msingi. Naomba nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na wananchi aendelee kuwashimiza ujenzi sio msingi tu, hebu waendelee kujenga mpaka kufikia usawa wa lenta na Serikali itaenda kumalizia ujenzi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Qulwi Qambalo swali la nyongeza.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Wilaya ya Karatu ina zaidi ya umri wa miaka 20 na haina hospitali ya wilaya. Hivi sasa uongozi wa wilaya unakamilisha taratibu za kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Je, Serikali iko tayari sasa kuanza kutenga fedha katika bajeti inayokuja ili kuanza ujenzi wa hospitali hiyo? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Serikali iko tayari kuanza kutenga, nia na azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba ujenzi wa Hospitali za Wilaya unafanyika katika Wilaya 64 zote ambazo hatuna hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ambavyo yeye mwenyewe amesema katika swali lake, ndiyo wameanza kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Naomba tuongeze kasi ya kutenga hilo eneo, lakini pia

kutokana na Halmashauri yenyewe kwa sababu ni hitaji letu, tuanze kutenga pesa na Serikali ije kumalizia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi hii, kwa kuwa Kituo cha Afya cha Mwese ni cha muda mrefu sana, kina zaidi ya miaka 40 hakijafanyiwa ukarabati wa aina yoyote na Serikali iliahidi kukikarabati kituo hicho. Je, Serikali ni lini itapeleka fedha kwa ajili ya kituo hicho ili kiweze kuwasaidia wananchi wa Kata hiyo ya Mwese?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya Mwese ambacho ni cha muda mrefu, je, ni lini Serikali itakuwa tayari kutenga pesa ili kufanya ukarabati?

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana kwamba ni kiu ya Waheshimiwa Wabunge wengi wangependa vituo vya afya viweze kukarabatiwa, na ndiyo maana Serikali kwa kujua umuhimu huo tumeanza na vituo vya afya 205, si haba. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira awamu kwa awamu na kwa kasi tunayoenda nayo naamini muda si mrefu na kituo cha afya cha kwake kitapata fedha.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Serikali imesema kwamba itakarabati vituo 205 kikiwemo pia na Kituo cha Afya cha Malya, ninapenda kujua Mheshimiwa Waziri, ni *formula* gani mnayotumia kupelekwa kwa baadhi ya vituo vya afya shilingi milioni 500 na vingine milioni 400 wakati mlichagua kwamba vituo vyote 205 vikarabatiwe kwa pamoja. Ni *formula* gani mnayotumia? Lakini ni lini pesa zingine ambazo mliahidi kwamba mtapeleka shilingi milioni 500 kwa kila kituo, kwa nini 400 na kwa nini 500? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni *formula* gani ambayo inatumika katika kupeleka kupeleka fedha katika vituo vyatya afya sehemu nyingine milioni 500 sehemu nyingine milioni 400?

Mheshimiwa Naibu Spika, *formula* zipo nyingi, kwanza ya kwanza inategemea na *source of funding*, ni nani ambaye ameleta fedha ili ziweze kwenda kwenye kituo cha afya. Lakini pia *formula* nyingine ni namna ambavyo ukarabati unaohitajika, kuna baadhi ya maeneo ni majengo machache tu ndiyo ambayo yanaongezwa kiasi kwamba ikipelekwa shilingi milioni 400 inatosha kabisa kuweza kufanya ujenzi ule ukakamilika. Kwa hiyo, inategemea *source* lakini pia na ukarabati ni kwa kiasi gani unakwenda kufanyika katika eneo husika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 57

#### **Matibabu Bure kwa Mama Wajawazito**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, Serikali ilimaanisha nini kusema kuwa matibabu ni bure kwa kinamama wajawazito?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba

kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mama wajawazito ni moja ya makundi maalum wanaostahili kupata huduma za matibabu bure kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Uchangiaji wa Huduma za Afya wa mwaka 1997. Aidha, mwongozo umeweuka bayana kuwa akina mama wajawazito ni haki yao kupewa huduma zote bila malipo na sio zile tu zinazohusu huduma za ujauzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwongozo uliopitiwa mwaka 2009/2010, imetamkwa bayana kuwa huduma ya afya kwa mama wajawazito ni bure ikiwa na maana kwamba mara tu mwanamke anapokuwa na ujauzito, huduma zote kuanzia kliniki ya ujauzito, pale atakapouguu maradhi yoyote pamoja na huduma ya kujifungua, sanjrari na kumuona daktari, kupatiwa vipimo, kupewa dawa na kufanyiwa upasuaji pale utakapohitajika kufanyiwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuondoa adha kwa wananchi, Wizara imeanzisha utaratibu wa kutenga bajeti itakayotumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vinavyohitajika wakati wa kujifungua (*delivery parks*), *delivery parks* hizo watapewa akina mama wajawazito wanapokaribia kujifungua ili wawe wanatembea na vifaa hivyo. Hii itapunguza kero kwa akina mama kujinunulia vifaa vyao wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali inazikumbusha halmshauri kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sera hii ili akina mama wajawazito wapate huduma za matibabu bure kama Mwongozo wa Uchangiaji wa Mwaka 1997 na Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wananchi wanaombwa kutoa taarifa kuhusu hospitali zinazotoza fedha kwa ajili ya matibabu kwa akina mama wajawazito ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi ni kwa muda mrefu sasa Sera ya Matibabu Bure kwa mama wajawazito ya mwaka 2007 imeendelea kuwabagua akina mama wanaopata *miscarriage* kwa kuwatoza garama za kusafishwa.

Je, Serikali haioni kwamba hii ni ajali kama ajali nyingine, hivyo basi akinamama hawa ambao walikuwa wana kiu ya kupata watoto wanastahili kufarijiwa kwa kusafishwa bila malipo? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, ni ipi sasa kauli ya Serikali juu ya mabadiliko ya kisera ili ianze kuwa-include akina mama wanaopata *miscarriage* na wale ambao mimba inatunga nje ya kizazi kuanza kupata matibabu bure na sio kuwaweka kwenye *group* (orodha) ya magonjwa ya akina mama ambayo kimsingi yanalipiwa kwa asilimia 100? Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza lilikuwa limejielekeza kwa nini akina mama ambao mimba zao zinaharibika ama kwa lugha ya kitaalam *miscarriage*, kwa nini nao wasipate matibabu bure?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba huduma za akinamama wajawazito kuanzia mwanzo wa mimba mpaka mwisho ni bure, hii inakwenda sambamba na tiba ambayo inaambatana na

mimba kuharibika. Ninaomba tu niseme kwamba huduma hii ni bure kwa mujibu wa sera yetu lakini kama suala hili halitekelezeki kama inavyotakiwa katika sera niseme tu kwamba totalichukua na kutoa maelekezo katika mamlaka husika ili sasa hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini sambamba na hilo, sasa hivi Serikali tunafanya mapitio ya Sera ya Afya, tutaweka utaratibu mzuri wa kuweza kulisimamia jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Selasini, swalii la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, akina mama wengi wajawazito wanapata madhara na kufariki hasa wanapokuwa na *referral* kutoka zahanati kwenda vituo vya afya na hospitali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma ya *ambulance* ili hawa akina mama wanapopata matatizo vijijini waweza kufikishwa haraka kwenye vituo vya afya na zahanati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunatambua kwamba kumekuwa na changamoto ya kuwasafirisha akina mama wajawazito kwenda katika sehemu za kupata huduma, na kwa kiasi kikubwa kwa kweli kumekuwa na mutikio mkubwa sana wa akinamama kujifungulia katika vituo vya afya, hivi tunavyoongea sasa hivi ni zaidi ya asilimia 60 ya akina mama wajawazito wanajifungulia katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini sambamba na hilo, Serikali imeendelea kuboresha vituo vya afya na fedha kama alivyosema Naibu Waziri TAMISEMI, zaidi ya vituo 205 vimefanyiwa maboresho kwa kujenga *theater*, wodi ya akina

mama kujifungulia ili hizi huduma za kujifungulia ziweze kuwa karibu zaidi. Lakini sambamba na hilo, Serikali imeendelea kutoa magari (*ambulance*) katika vituo vyta afya na hospitali za wilaya, na kadri muda unavyokwenda tutakuwa tunaziongeza ili tuweze kufikia vituo vyote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, akinamama mmesimama, nadhani swali hili tuwasikie akina baba watutetee akina mama, si ndiyo jamani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, tatizo la akina mama kujifungua mara nyingi wakati mwingine linaletwa pia na matatizo ya baadhi ya ma-nurse ambao huwa wanawanyanyaapaa akina mama wenzao wanapotaka kujifungua.

Sasa sijui Serikali ina mpango gani au huwa inachukua hatua gani kuwadhibiti hawa akinamama ambao wana tabia za kuwanyanyasa akina mama wenzao wanapotaka kujifungua? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na tatizo la baadhi ya watoa huduma kutoa lugha zisizokuwa sahihi kwa wagonjwa ambao wanafika katika hospitali, na hili ni jambo ambalo ni kinyume kabisa na maadili na taaluma za afya ikiwa ni pamoja na ma-nurse.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuimarisha mabaraza yetu na hivi karibuni, wiki iliyopita tu, Mheshimiwa Waziri alitoa kauli ya kuhakikisha kwamba watoa huduma wote, ikiwa ni pamoja na madaktari na ma-nurse, wanakuwa wanatoa huduma nzuri ambayo inazingatia maadili na miiko ya kazi ambayo wanayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naendelea kulisisitiza hilo, na tumeendelea kuimarisha mabaraza yetu na tumeanza kuchukua hatua kwa wale ambao wanakiuka taratibu hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali fupi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mkanganyiko katika utaratibu wa upatikanaji wa vitambulisho kwa wazee ili waweze kupata huduma za afya ambapo baadhi ya maeneo wazee hawa wamekuwa wanatakiwa kuchangia baadhi ya gharama.

Sasa Serikali inaweza kutoa kauli ni upi wajibu wa halmashauri na upi wajibu wa wazee hawa ili waweze kupata vitambulisho ili wapate huduma za afya bure? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, swali hili tulikuwa tunatetewa akina mama, au unamaanisha akina mama wazee? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni agizo la Serikali kwamba Halmashauri zitoe vitambulisho vya wazee ili waweze kutambulika kirahisi wanapokwenda kutafuta matibabu ya afya. Na hii inaendana na Sera ya Afya ya mwaka 2007 ambayo inasema kwamba wazee watapata matibabu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho hivi vinapaswa vitolewe bure kwa sababu halmshauri zinagharamia. Inawezekana kwamba zile gharama ndogondogo kama upigaji wa picha ambazo wanatakiwa wazee nao wazigharamie ambayo sio gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapenda kusema tu kwamba gharama ya kitambulisho ni bure na Halmashauri zinatakiwa zigharamie hilo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini sasa aulize swali lake.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa swali la kwangu ndio linafuata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa manyoni Magharibu.

Na. 58

**Watumishi na Viongozi wa Halmashauri Waliostaafu  
Zamani Kupatiwa Kadi za Bima ya Afya**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Sasa hivi baadhi ya watumishi wa Halmashauri kama vile Wakurugenzi na wengine wanapostaa fu hupatiwa kadi ya bima ya afya pamoja na familia zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia kadi kama hizo watumishi na viongozi wa Serikali waliostaafu kabla ya utaratibu huo kuanzishwa ikizingatiwa kuwa wengi wao walilitumikia Taifa hili kwa uadilifu na uaminifu mkubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango wa wastaafu waliowahi kuwa watumishi na viongozi wa Umma katika maendeleo ya Taifa hili. Kwa

sababu utaratibu wa kuwapatia bima ya afya wastaafu waliowahi kuwa viongozi na watumishi wa Umma ni kupitia Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura Namba 395, Toleo la Mwaka 2015 kwa kuzingatia vigezo na masharti yafuatayo:-

(i) Mstaafu husika lazima awe alikuwa mwanachama mchangaji wa mfuko kabla ya kustaafu.

(ii) Mstaafu awe amefikisha umri wa kustaafu kwa hiari miaka 55 au kwa lazima au miaka 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia utaratibu huu, wanachama wastaafu wanaokidhi masharti na vigezo vilivyoainishwa, hupatiwa bima ya afya inayomuwezesha kupata huduma za matibabu yeye mwenyewe pamoja na mwenza wake hadi mwisho wa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uhitaji wa huduma za afya na changamoto za upatikanaji wa huduma hizi kwa wastaafu na wananchi wengine walio nje ya utaratibu huu, mfuko umeweka utaratibu wa kujeungu kwa hiari kupitia utaratibu wa mwanachama binafsi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare swalii la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulize swalii la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu haya mfuko huu unatambua tu viongozi na watumishi wa umma, lakini watumishi wa sekta za kisiasa kama Wabunge na viongozi wengine hawapo katika mfumo huu. Je, Serikali sasa iko tayari kuwaingiza watumishi wa kisiasa wakiwemo Wabunge katika utaratibu huu ambaa unaifikia miaka 55 au 60 waweze kupatiwa kadi za afya na wawe ni wanachama?

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama Serikali inakubali, je, ni lini utaratibu huu utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge ndio wanatunga sheria na nataka nimuombe sana Mheshimiwa Massare, kama jambo hili kwa umuhimu wake alipitishe katika Tume ya Utumishi wa Bunge lijadiliwe halafu sasa lifikishwe Serikalini kwa taratibu nyingine kufuatwa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maida Abdallah.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, Serikali inaweza kutuambia ni kwa nini wazee kama baba na mama wa Mbunge hawakuwekwa mionganii mwa wategemezi katika bima ya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taratibu wa Sheria ya Bima ya Afya, inatambua yule mwenye kadi, mwenza wake na watoto wake, wategemezi wengine; baba, mama, walezi, wale wako nje ya utaratibu huo. Kwa hiyo, niendelee kuwasisitiza Waheshimiwa Wabunge kwamba changamoto hii na sisi tumeiona, tunaendelea kuitafakari kuangalia jinsi bora zaidi ya kuweza kulifanyia kazi ili hawa nao waweze kunufaika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba swali la nyongeza.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, tunafahamu kwamba sekta zisizo rasmi zinachangia sana Pato la Taifa na wengi wao wako kwenye hatari ya kupata ajali na magonjwa kama watu wa bodaboda. Serikali ina mpango gani wa kurasimisha na kuwaweka katika mpango wa bima ya afya sekta isiyo rasmi, hasa vijana wetu wa bodaboda? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunatambua kwamba sekta isiyo rasmi nayo ina mchango mkubwa sana katika ukuaji na kuchangia katika uchumi wa nchi yetu, lakini sisi kupitia bima ya *NHIF* na *CHF* tunatambua makundi haya na kwa kupitia vikundi vyao kuna mfumo wa bima ambao wanao ambao wanaweza kukata kwa kupitia vikundi vyao. Lakini hata hivyo, kwa mtu mmoja mmoja sasa hivi tunakuja na utaratibu wa *CHF* iliyoboreshwa ambayo nayo itakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kutoa huduma kwa mtu mmojammoja ambaye atakuwa anahitaji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu Mbunge wa Geita Mjini sasa aulize swalii lake.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba swalii langukwa niaba ya wananchi wa Geita Mjini ijibewe.

Na. 59

**Uhaba wa Dawa na Madaktari - Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Liko tatizo la uhaba wa dawa na madaktari katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa dawa na Madaktari wa kutosha wanakuwepo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kanyasu Constantine John, Mbunge wa Geita Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu zilizopo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto zinaonyesha kuwa Hospitali ya Mkoa wa Geita ilipandishwa hadhi kutoka iliyokuwa Hospitali ya Wilaya ya Geita na kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018. Hata hivyo, kutokana na idadi kubwa ya walengwa wa huduma kwenye hospitali hiyo, hospitali ya Wilaya ya Geita imekuwa ikipata mgao mkubwa wa fedha za kununulia dawa, vifaa tiba na vitendanishi kuliko hospitali za Mkoa isipokuwa Hospitali ya Mkoa wa Tanga na ile ya Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hali hiyo, Hospitali ya Geita katika mwaka wa fedha 2015/2016 ilitengewa fedha za Kitanzania shilingi 141,939,184 na katika mwaka wa fedha 2016/2017 ilipokea kiasi cha shilingi 278,666,525 kiasi ambacho ni takribani mara mbili ya mgao wa mwaka wa fedha 2015/2016. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Hospitali hii baada ya kupandshwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, mgao wake umeongezeka na kufikia fedha za Kitanzania shilingi 368,287,841; hadi kufikia mwezi Desemba 2017, Hospitali hii ilikuwa imepokea kiasi cha milioni 168,609,586.94 kwa ajili ya kununua dawa kuititia bohari ya dawa. Hali ya upatikanaji wa dawa kwa sasa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita ni asilimia 90 kwa zile dawa muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna jumla ya Madaktari Bingwa 451 nchi nzima. Wizara imeweka utaratibu wa kutoa ufadhilli wa masomo ya Uzamili kwa Madaktari Bingwa kila mwaka wa fedha kwa uwiano wa wanafunzi 100 ndani ya nchi na 10 nje ya nchi. Jumla ya madaktari 236 wanaendelea na masomo na tunataraji ndani ya miaka mitatu watakuwa wamehitimu na kurudi vituoni. Wizara imeanzisha utaratibu wa kuwatawanya Madaktali Bingwa ili kuweka uwiano katika Mikoa yote nchini na sasa jumla ya Madaktari Bingwa 74 ambaao walikuwa wakifadhiliwa na Wizara walihitimu masomo ya udaktali bingwa kwenye fani mbalimbali, taratibu za kuwapandisha vyeo na kuwatawanya kulingana na uhitaji katika Mikoa zinaendelea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu swalii la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ingawa hakuwa na takwimu kabisa kwenye eneo la madaktari maana yake amekili upungufu uliopo nilioutaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Geita inahudumia takribani wagonjwa 400 kila siku. Na mwaka jana wakati Waziri wa Afya amefanya ziara kwenye Hospitali hiyo aligundua kwamba mpaka wakati tunatoka kwenye bajeti tulikuawa bado tunaichukulia Hospitali ya Geita kama Hospitali ya Wilaya, haikuwa kwenye Hospitali za Mkoa na ndiyo sababu mpaka leo pale tuna *specialist* mmoja ambaye ni *surgeon* hatuna kabisa *Physiotherapy Doctor*, hatuna mtu wa mionzi, hatuna *gynaecologist*, hatuna mtu wa usingizi kwa sababu ilikuwa inachukuliwa kama Hospitali ya Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swalii langu kwa kuwa tumeongeza vituo vingine vya Nyamkumbu na Kasamba tumejenga *theater* kwa ajili ya upasauji na kuna wataalam wengi wamezagaa ambaao wanaomba ajira. Ni lini Wizara

italeta wataalamu wanaoweza kukudhi kiwango cha Hospitali ya Mkoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Geita ambapo nimesema hatuna wataalam tuna ujenzi wa Hospitali ya Mkoa baada ya kuchukua Hospitali ya Wilaya ambayo tulifanya kuwa Hospitali ya Mkoa, tunajenga Hospitali y Mkoa, lakini *speed* ni ndogo. Nini kauli ya Serikali ili kuifanya ile Hospitali ya Halmashauri irudi kwa wananchi na huduma ziweze kupungua gharama yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ilikuwa ni kuhusiana na idadi ya wataalam. Ni kweli lazima nikiri katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita kuna changamoto kubwa sana ya Madaktari Bingwa na hilo sisi tumeliona kama nilivyojibu katika swali langu la msingi. Ni kwamba tunaendelea kuhakikisha kwamba tunafanya *training* ya kutosha Madaktari Bingwa na pale watakopatikana basi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita tutaipa kipaumbele kuongeza idadi ya Madaktari Bingwa ili waweze kutoa huduma pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lake lingine la pili lilikuwa lina husiana na kwa nini sasa Serikali isiongeze mkono wake katika ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na ile iliyokuwepo pale iweze kurudi kuwa Hospitali ya Wilaya.

Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mwishoni mwa mwaka jana Serikali ilifanya maamuzi ya kuziondoa Hospitali za Rufaa za Mkoa kutoka ngazi za Serikali za Mitaa na kuzipeleka Serikali Kuu. Jukumu hilo sasa na sisi tumelipokea, tumekabidhiwa rasi na mimi nimuhaidi tu Mheshimiwa Mbunge sasa na sisi tutajielekeza nguvu zetu kuhakikisha kwamba tunazijenga na kuziboresha Hospitali za Rufaa za Mkoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftah swalii la nyongeza.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana nilikuwa naomba kuuliza swalii la nyongeza kwamba sasa hivi Tanzania kuna dawa hizi ambazo zinaitwa *tressa medicines* ambazo zinatolewa kwenye Hospitali za Rufaa ama Hospitali za Mikoa tu na kwamba kule vijijiini kwenye Zahanati na Vituo vya Afya hizi dawa hazitolewi za magonjwa kama *BP*, magonjwa *HIV*, Kifua Kikuu sasa swalii langu; nilikuwa naomba kujua kwa sababu wananchi wanapata tabu sana kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta dawa hizi kwenye Hospitali za Mikoa na Hospitali za Rufaa.

Je, Serikali ipo tayari hivi sasa kufundisha wale *Medical Assistant's* kule vijijiini ili dawa hizi ziweze kutolewa kule vijijiini? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa ufanuzi, tumapoongelea suala la *tressa medicines* tuna maanisha kwamba ni dawa zile muhimu na ambazo sisi zina tusaidia katika sekta ya afya kubaini na kuangalia kwamba zile dawa muhimu zipo. *Tressa medicines* sio dawa ambazo unasemasajui kwa lugha ya kitaalam mnasemaje kwamba ni dawa ambazo ni muhimu ambazo ziliikuwa zinatakiwa kutolewa katika sehemu fulani *tressa medicine* ni *general term* ambayo sisi tunaitumia kuhakikisha kwamba tunazibaini na kuzipatia zile dawa muhimu kule ambapo tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda niendelee kwa kusema kwamba sasa hivi ndani ya Serikali na mwanzoni mwa mwezi huu tumetoa mwongozo wa utoaji wa dawa katika ngazi mbalimbali. Mwongozo huu kwa jina la kitaalam tunaitwa *standard treatment guideline* hapo siku za nyuma kila ngazi ilikuwa inajitolea dawa holela na kadri walivyokuwa wanaiona. Na hii changamoto tulikuwa

tunaipata sana katika Hospitali kubwa makampuni ya dawa yana kuja yanamwambia mto huduma andika dawa hii wakiwa wanampa na ye ye motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati sisi Serikali tunaagiza dawa nyingi kwa pamoja unakuta sasa mgonjwa anaandikiwa dawa anaambiwa dawa hazipo. Serikali imeongeza sana bajeti ya dawa kutoka bilioni 30 mwaka 2015/2016 kufikia bilioni takribani 270 katika mwaka wa 2017/2018 ni zaidi ya mara tisa ndani ya miaka miwili. Kwa hiyo, hali ya upatikanaji wadawa sasa hivi nchini ni nzuri sana pamoja na hizi *tressa medicines*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lako lingine la nyongeza ilikuwa sasa kutokana na mwongozo huu, umeweka utaratibu dawa gani kwa ugonjwa gani zitakuwa zinapatikana na kwamba hivyo vituo vya afya vitatakiwa kuzingitia dawa gani na kutoa matibabu kwa kulingana na ule mwongozo wa utoaji dawa ambao kama na sisi Serikali tumetoa. Tunatambua kwamba baadhi ya maeneo ambayo tunachangamoto ya watumishi tunaendelea kutoa mafunzo ili na wale watumishi waweze kutoa tiba kwa wale wagonjwa wanaofika pale ambapo hamna madaktari kwa kuzingatia milongozo ambayo na sisi tutakuwa tumewapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo ya Mkao wa Geita yanafanana na matizo ya Mkao wa Katavi. Mkao wetu wa Katavi hauna Hospitali ya Mkao na hauna pia Hospitali ya Rufaa.

Je, ni lini sasa Serikali itamaliza ujenzi wa Hospitali ya Mkao wa Katavi na kuleta Madaktari Bingwa wa magonjwa mbalimbali kama upasuaji wa macho, meno kwa sababu siku nyingine watu wanavimba ufizi wanashindwa kupasua? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Mkoa wa Katavi nimeutembelea ikiwa ni sehemu ya Mikoa 12 ambayo nimetembelea ndani ya miezi minne tangu nimeteuliwa kuwa Naibu Waziri. Nimeiona changamoto hiyo katika Mkoa wa Katavi, lakini kama nilivyojibu katika swala langu la msingi ni kwamba sasa hivi Serikali imechukua majukumu ya kuendesha Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachokuomba Mheshimiwa Taska Mbogo na Wabunge wengine wa Mkao wa Katavi ni kuendelea kuihimiza Serikali yetu ya Mkao kuhakikisha kwamba wanatenga eneo na kuanza maandalizi ya awali na sisii kama Serikali tutaendelea kujipanga kuhakikisha kwamba tunajenga Hospitali ya Rufaa ya Katavi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 60

### **Kituo cha Afya cha Kambi ya Migombani Unguja**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Majengo ya Kituo Afya cha Kambi ya Jeshi Migombani Unguja ni chakavu na pia ni siku nydingi sana.

Je, ni lini Serikali itajenga kituo hicho ili kiwe cha kisasa na kiendane na wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANO YA NCHI (K.n.y.  
WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Jeshi cha Migombani Zanzibar ni moja ya vituo vya tiba ambavyo huanzishwa katika kila Kikosi cha JWTZ ili kutoa huduma ya mwanzo ya tiba kwa Wanajeshi na familia zao, watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na wananchi wanaishi jirani kabla ya kupelekwa katika hospitali za rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni, kweli majengo ya kituo hicho na vituo vingine vya JWTZ yamechakaa na kwa sababu ni ya muda mrefu. Kutokana na uchakavu huo wa Kituo cha Kambi ya Migombani na sehemu nyingine, ni matazamio ya Wizara kuvi karabati upya vituo vyote katika mwaka wa fedha 2018/2019 kadri hali ya upatikanaji wa fedha itakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha swalii la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kuwa haya maswali tumekuwa mara kwa mara tunauliza na hakuna utekelezaji. Je, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri nusu mwaka wa fedha unakwishwa. Ni majengo mangapi yamekarabatiwa kwa upande wa Zanzibar na ni vituo vingapi vya kambi vya Kambi za Jeshi kwa upande wa Zanzibar vimekarabatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili kwa kuwa hivi vituo vya afya tunavyoviulizia ambavyo viro kwenye makambi ya Jeshi havihudumii tu majeshi na familia zao, zinahudumia pia na jamii zilizowazunguka na hasa hichi kituo nilichokiulizia kiko sehemu ambapo ajali zinatokea mara kwa mara.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha vituo vyote vya majeshi vinapata dawa kwa wakati muafaka na sitahiki zinazofaa kwa wakati muafaka? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANO YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilivyojibu katika majibu ya msingi kwamba kwa bajeti ya mwaka 2018/2019 Serikali imeazimia kuvifanyia ukarabati vituo vyote ikiwemo vya Zanzibar na kikiwemo hiki cha kwenye Brigedi ya Nyuki, Migombani. Kwa hiyo, mwaka wa fedha 2018/2019 bado haujaisha kadri ambavyo fedha kama ambavyo nimesema zitapatikana basi vituo hivi pamoja na hiki cha Migombani vitafanyiwa ukarabati. Sambamba na kuvipatia huduma nyingine muhimu kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa kwa hatua za awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ikumbukwe kwamba vituo hivi kwa kawaida vinatumika kwa ajili ya kutoa huduma za awali kabla ya kuweza kuwapeleka wagonjwa wenye matibabu makubwa katika Hospitali za Kikanda kwa upande wa Zanzibar ikiwemo Hospitali ya Jeshi ya Bububu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano. Mhehimiwa Joel Mwaka Makanyaga Mbunge wa Chilonwa sasa aulize swali lake.

Na. 61

#### **Kurejesha Utaratubu wa Kuweka Matuta Barabara Kuu**

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA** aliuliza:-

Serikali imefanya kazi kubwa kujenga mtandao wa barabara za kiwango cha lami nchini, kipindi cha nyuma

barabara kuu zilikuwa zinawekwa matuta ili kudhibiti ajali, lakini hivi karibuni Serikali imefuta utaratibu wa kuweka matuta kwenye barabara hizo na hivyo kuwa chanzo kikubwa cha ajali zinazosababisha majeruhi, ulemavu na vifo. Kwa mfano, eneo la Buigiri, Wilaya Chamwino lina ajali nyingi kutokana na barabara kukosa matuta.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kurejesha utaratibu wa kuweka matuta kwenye barabara?

(b) Kama utaratibu wa matuta hauwezekani, je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuyaondoa matuta yote kwenye barabara kuu ili kuondoa malalamiko ya wananchi kwa viongozi wao kwenye maeneo ambayo hayana matuta?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Mwakanyaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa majibu ya swali namba 61 la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga Mbunge wa Chilonwa, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuboresha usalama barabara na kurekebisha sehemu hatarishi kwenye barabara kuu na barabara za mikoa nchi nzima ikiwemo barabara ya Morogoro - Dodoma eneo la Buigiri ili kupunguza ajali za barabarani. Hatua zilizochukuliwa na Serikali kupunguza ajali za barabarani ni pamoja na kuweka au kurudisha alama zote muhimu za barabarani ikiwemo za kudhibiti mwendo, kuweka michoro ya barabarani na kurekebisha kingo za madaraja zilizoharibika, uwekaji wa matuta na kadhalika kama ilivyokuwa ikifanya kipindi kilichopita.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 *TANROADS* itaendelea kuweka vivuko vya watembea kwa miguu (*zebra crossing*) na alama zote muhimu nchini pale tutakapohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali napenda sasa kujibu swal la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga Mbunge wa Chilonwa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ajali za barabaran zina sababisha majeruhi, ulemavu na vifo kwa watu wetu ikiwa ni pamoja na kusababisha hasara kubwa kiuchumi kwa Taifa letu. Moja ya njia ambayo Serikali imekuwa ikitumia kupunguza ajali kwenye baadhi ya sehemu ni kuweka matuta ya barabaran. Hata hivyo, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, kiutaalam hairuhusiwi kuweka matuta kwenye barabara kuu. Aidha, matuta yaliyowekwa katika barabara kuu yaliwekwa kwa lengo la kupunguza ajali za barabaran kama njia ya mpito. Wizara inafanya utafiti kupata njia mbadala ya kupunguza ajali kabla ya uondoshaji wa matuta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mpito, Serikali inaendelea kurekebisha matuta ambayo yalijengwa bila kuzingatia viwango vilivyomo kwenye Mwongozo wa Wizara wa Usanifu wa Barabara (*Road Geometric Manual* ya 2011) kulingana na upatikanaji wa fedha.

Aidha, inapobainika kuwa kuna haja ya kuweka matuta kwenye barabara, matuta hayo yatawekwa kulingana na viwango vilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joel Makanyaga swal la nyongeza.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba niulize swal moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Buigiri ni eneo linalojulikana kwamba kuna Shule ya Watoto Wasiona kabisa na wengine wana uono haffiu. Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya kulishughulikia suala hili la usalama barabarani katika eneo la Buigiri kwa umuhimu na haraka ili kuondokana na tatizo la ajali pale Buigiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna kituo kwa ajili ya wasioona sehemu za Buigiri kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge. Kiutaratibu tunategemea sehemu zenyе mahitaji maalum kama hayo kuwe na watu ambaо wanawaongoza wanaovuka barabara ili wasiweze kupata ajali. Lakini hata hivyo, nimshauri na kumueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tutaendelea kutafuta utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba watu wenye mahitaji maalum kama hao wanapokuwa wanavuka na kutumia barabara zetu wanasaidiwa ili wasiweze kupata madhara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsantekwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Naomba nimuulize Waziri, kwa vile imethibitika kwamba baadhi ya ajali zinazotokea barabarani au zinasababishwa na ubovu wa barabara, au zinasababishwa na ukosefu wa alama mahususi za barabarani jukumu ambalo amekebidhiwa wakala wa barabara yaani *TANROADS*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwajibisha *TANROADS* pale ambapo sababu ya ajali inaonekana ni kutotekeleza wajibu wa wakala huyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna ubovu wa barabara na Serikali imekuwa ikiendelea kufanya jitihada za kurekebisha ubovu huo kuhakikisha kwamba barabara zetu kuu na barabara za mikoa zimapitika kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito tu kwa Watanzania wenzetu, kumetokea tabia ya hivi karibuni wananchi kuchukua hatua wenyewe ya kuweka matuta barabarani na hicho kimekuwa ni chanzo kimojawapo cha ajali mbalimbali kwa sababu wanapoweka matuta bila kuwashauri au bila kuwaambia *TANROADS* ina maana yale matuta yanakuwa hayana alama na magari yanapokuja yanafika, yanavamia yale matuta na kusababisha ajali. Niwashauri Watanzania, tunawaomba wasiweke matuta barabarani bila kuviambia vyombo husika vinyavyohusika na barabara ili kuweka alama kuwaonyesha madereva kwamba kuna tuta mbele wanakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge Ndugu yangu Joseph Mhagama kwamba *TANROADS* wanajitahidi sana kufanya kazi zao kwa uadilifu na kwa umakini wa hali ya juu kuzingatia usalama wa Watanzania. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq swalii la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii kuweza kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la uwekaji kiholela wa matuta kwenye baadhi ya barabara za mitaani na hivyo kusababisha usumbufo mkubwa kwa watumiaji wa vyombo vyaa moto na ikizingatiwa kwamba wananchi hawa hawana utalaam wowote. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na kadhia hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa namueleza Mheshimiwa Joseph Mhagama, ninatoa wito kwa Watanzania, barabara hizi zinajengwa kwa gharama kubwa sana ya pesa za Watanzania. Tunapoweka matuta bila vyombo vinavyohusika hasa *TANROADS* kufahamu tunaharibu barabara zetu ambazo tumezijenga kwa gharama kubwa sana. Kitu ambacho Serikali tunakifanya, tunapanga mkakati wa kuwasiliana na Wizara ya mambo ya ndani kitengo cha usalama barabarani kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi namna ya matumizi bora ya barabara bila kuleta ajali kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sana Watanzania wasijichukulie maamuzi ya kuweka matuta barabarani hata kwa kugongwa kwa mbuzi tu isipokuwa wawasiliane na taasisi zinazohusika tusaidie kama kuna umuhimu wa kuweka matuta tutaweka, lakini kwa utaratibu ambaao unaeleweka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela swali la nyongeza.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, changamoto zilizopo katika Jimbo la Chilonwa linafanana kabisa na changamoto zilizopo katika Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna ujenzi ambaao unaendelea kutoka katika Mkoa wa Tabora barabara ya Inyonga - Ipole kuelekea Mpanda. Barabara hii inajengwa lakini wakandarasi hawaweki alama za ujenzi kwamba kuna madaraja yanajengwa, kuna mashimo yamechimbwa na jambo hili limekuwa linasababisha ajali nyingi kwa wakazi wa Mpanda, kwa wakazi wa Mkoa wa Katavi.

Nini tamko la Serikali kuhakikisha inatoa maekelezo kwa hawa wakandarasi ili kupunguza ajali za barabarani katika Mkoa wa Katavi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swalii lake la ujenzi wa barabara ya kutoka Katavi mpaka Tabora. Ni kweli Serikali tumeanza ujenzi wa barabara hiyo na hatua tunayokwenda nayo sasa ni hatua ya *mobilization* yaani makandarasi kwa sasa wanakusanya vifaa vya ujenzi katika maeneo hayo, bado kabisa kazi ya ujenzi haijaanza. Mara itakapoanza kazi ya ujenzi tutaweka alama kuhakikisha kwamba watumiaji wote wanaotumia barabara hiyo wako salama.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini sasa aulize swalii lake.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya watu wangu wa Tanga ambao nawapenda sana na wao wanapenda sana, naomba swalii lao namba 62 lijibiwe.

Na. 62

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kisasa-Tanga**

**MHE. MUSSA B. MBAROUK** aliuliza:-

Tanga kuna uwekezaji wa bomba la mafuta toka Hoima - Chongoleani, viwanda mbalimbali vya saruji, vivutio vya utalii vya *Amboni Caves*, Magofu ya Tongoni na *Saadani National Park*:

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanja cha ndege kikubwa na cha kisasa katika Jiji la Tanga?

**NAIBU SPIKA:** Unawanunulia soda kila siku nini hao? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

## NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini ambaye anapendwa sana na wapiga kura wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwaja cha ndege cha Tanga ni mionganoni mwa viwanja 11 nchini vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kugharamiwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Transport Sector Support Project*. Viwanja vingine vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ni *Lake Manyara*, Musoma, Iringa, Songea, Kilwa Masoko, Lindi, Moshi, Njombe, Simiyu na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu huu ulikamilika mwezi Juni, 2017 na ulihusisha usanifu wa miundombinu ya viwanja hivi kwa ajili ya upanuzi na ukarabati ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza majadiliano na Benki ya Dunia ili kupata mkopo wa kugharamia ukarabati na upanuzi wa baadhi ya viwanja hivi kwa kuzingatia mapendekezo ya *report* ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao ulizingaia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukuaji wa shughuli za uchumi, utalii na mahitaji ya usafiri wa anga. Katika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina huo, kiwanja cha ndege cha Tanga ni mionganoni mwa viwanja vilivyopewa kipaumbele kwa mahitaji ya ukarabati hivyo katika majadiliano ya awali, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kugharamia ukaratabi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unaopendekezwa utahusisha mradi wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na barabara ya kiungio kwa kiwango cha lami. Ukarabati wa maeneo ya maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo kubwa la kisasa la abiria pamoja na miundombinu yake, usimikaji wa taa pamoja na mitambo ya kuongozea

ndege. Baada ya ukarabati unaopendekezwa kiwanja kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege aina ya ATR 72 yenye uwezo wa kubeba abiria 70 au ndege za kufanana na hiyo na kitawezza kutumika kwa saa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa majadiliano kati ya Serikali na Benki ya Dunia yanaendelea yakiwemo mapitio ya awali ya *report* za miradi inayopendekezwa pamoja na maandalizi ya taarifa mbalimbali zinazohitajika kabla ya mkataba wa mkopo kusainiwa na baadae kutangazwa zabuni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk swalii la nyongeza.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kabla sijauliza swalii langu la nyongeza kwanza niipongeze timu yangu ya *Coastal Union* ya Tanga ambayo imepanda daraja mwaka huu, lakini pia niwapongeze timu ya *African Sports* kwa kubakia katika ligi daraja la kwanza. Maswali yangu ya nyongeza ni kama ifuatavyo:- (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ukarabati unaofanywa na ambaao ulishawahi kufanywa uwanja wa ndege wa Tanga, katika eneo la Magomeni kuna nyumba zaidi ya 228 ambazo zilifanyiwa *evaluation* mwaka 2008 lakini mpaka leo hawajalipwa. Lakini pia kuna nyumba nyingine 802 ambazo nazo zinahitajiwa kuvunjwa ili kupanua uwanja ule wa ndege.

Sasa je, nataka kujua, Serikali ni lini itawalipa Wananchi wale fidia ili kuweza kufanya ukarabati huu mkubwa unaotakiwa kufanywa kufuatia ufadhili wa Benki ya Dunia?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, kwa kuwa Jiji la Tanga sasa hivi *route* za ndege zimeongezeka na kuna shughuli nyingi za mipango ya kiuchumi amabzo zinafanyika. Je, ni lini *Bombardier* itaanza kwenda Tanga? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk hivi juzi ulikuwepo Morogoro? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba zote ambazo zilifanyiwa *evaluation* kwa ajili ya malipo ya fidia, shughuli za fidia zinafanyika na *evaluation* imekwishafanyika na tunafahamu idadi ya pesa zinazodaiwa lakini tuko kwemnye uhakiki kupertia Wizara ya Fedha ya kulipa fidia hiyo, kwa hiyo, wakati Wizara ya Fedha itakapomaliza kupertia fidia hiyo, malipo yatafanyika kwa watu ambao wataathirika na upanuzi wa uwanja wa ndege huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, *Bombadier* itaanza lini safari za kwenda Tanga, kiutaratibu *Bombadier* wanafanya biashara pamoja na kutoa huduma kama mashirika mengine ya ndege kwa hiyo, hilo tutalichukua, tutawapelekeea *ATCL* basi waje wafanye tathmini ya masuala ya soko, usalama na mambo mengine ambayo yanahuksika kabla ya kupeleka ndege kufanya shughuli za safari za uwanja huo wa Tanga, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnanipa wakati mgumu sana, Mheshimiwa Gekul naomba ukae una maswali mengi tayari kwenye hii karatasi tafadhalii. Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Kata ya Makole, Manispaa ya Dodoma walisitishiwa uendelezaji wa nyumba zao kwa ajili ya upanuzi wa uwanja wa ndege ulioko hapa wakati huo kuna wananchi wa Kata ya Msalato 89 wanaidai Serikali tangu mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua wananchi wa Msalato watalipwa lini lakini pili wananchi wa Makole waliositishiwa uendelezaji wa nyumba zao...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti wewe ni swali la nyongeza linaulizwa moja na umeshauliza. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na upanuzi wa uwanja wa ndege au tutautumia sasa hivi hapa Dodoma na wananchi wa Makole madai yao ya fidia yanashughulikiwa kupitia Wizara ya Fedha na sasa hivi Wizara ya Fedha wako kwenye uhakiki wa kuhakikisha kwamba wanalipa hayo madai yao wakati watakapomaliza uhakiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Segerea swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri kutokana na tamko lake la juzi, Jimbo la Segerea katika Kata ya Kipawa kuna wananchi 1,800 wanabubiri malipo tangu mwaka 1992 na juzi alisema kwamba waondoke. Sasa nilitaka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini sasa atawafanya malipo yao watu wa Kata ya Kipawa, Mtaa wa Kipunguni na wanahusika viyi kuondoka kabla hawajalipwa malipo yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna wananchi wanatakiwa wapishe eneo la uwanja wa ndege wa *Julius Kambarage Nyerere International Airport* ambao walivamia miaka ya nyuma, lakini Serikali ya Awamu ya Tano iliamua kwamba walipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya hao kuna wananchi 59 ambao tayari wamekwishapokea malipo yao kwa ajili ya kupisha upanuzi wa uwanja huo. Tunaowazungumza na ambao nilitoa agizo waondoke ni hao wananchi 59 na bado

naendelea kusitiza kwamba hao wananchi 59 ambao tayari wamekwishakupokea malipo yao ya fidia, wanatakiwa waondoke wapishe upanuzi wa uwanja wetu wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikiri kwamba kuna baadhi ya wananchi ambao hawajalipwa kwa sababu mbalimbali, kuna baadhi walifungua kesi na kuna wengine ambao hawajafungua kesi lakini hawakuridhika na fidia, hao bado tunaendelea kutafuta utaratibu mwingine wa kuwashawishi kwa njia moja au nyingine ili waweze kupisha upanuzi wa uwanja huo wa ndege.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mkao wa Mara una shughuli nyingi sana ambazo zingeweza kuliongezea Taifa letu uchumi kwa maana ya utalii, tuna Ziwa Victoria lakini pia makumbusho ya Baba wa Taifa. Katika majibu yake Naibu Waziri ametueleza kwamba wamefanya usanifu pia kwenye uwanja wa ndege wa Musoma, ningependa kujua uwanja wa ndege wa Musoma na wenyewe upo kati ya viwanja vilivyopewa *priority* maana yake umetaja Tanga tu kama ndiyo umepewaa kipaumbele na unaanza kukarabatiwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Kwenye jibu langu la msingi wakati najibu kuhusu uwanja wa ndege wa Tanga nilieleza viwanja 11 ambavyo vimeshafanyiwa Upembizi yakinifu na usanifu wa kina na uwanja wa Musoma ukiwemo. Ni kweli kwamba viwanja vyote vimepewaa kipaumbele kinacholingana na pesa itakapopatikana kama nilivyoeleza tutafuta mkopo kutoka Benki ya Dunia, pesa itakapopatikana basi viwanja vyote vitapewaa kipaumbele kujengwa kwa sababu tunahitaji viwanka vyote vya Mikao

viwe na kiwango kizuri ambacho ndege yoyote inaweza ikashuka, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Wizara ya Maliasili ya Utalii, Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega sasa aulize swali lake.

Na. 63

### **Migogoro ya Ardhi na Mipaka**

**MHE.DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Migogoro ya ardhi na mipaka ya vijiji na hifadhi bado imeendelea kuwa tatizo sugu licha ya kuwepo kwa ahadi na kauli mbalimbali na Serikali.

Je, mgogoro wa Pori la Akiba Kijereshi na Sayanka katika Wilaya ya Busega utatatuliwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Akiba la Kijereshi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 65.7 ilitangazwa rasmi na tangazo la Serikali Na. 215 la mwaka 1994. Pori hilo lilitabidhiwa rasmi kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori mwaka 2005 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu. Pori la Akiba la Kijereshi limepakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa upande wa Kaskazini na Kijiji cha Lukungu upande wa Mashariki, Mwamalole, Mwakiroba, Kijilishi, Igwata na Muungano upande wa Kusini Mashariki mwa pori hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvamizi wa mapori haya ya akiba kwa kilimo, makazi na ufugaji umesababisha

ongezeko la matukio ya wanyamaporii kuharibu mazao na kudhuru wananchi. Aidha, hali hii imesababisha migogoro baina ya wananchi na mamlaka ya usimamizi wa wanyamaporii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua migogoro kati ya wakulima, wafugaji na maeneo ya hifadhi nchini Serikali imechukua hatua mbalimbali. Wizara kwa kushirikiana na wananchi imetambua na kuweka mipaka kwenye maeneo ya hifadhi ikiwemo Pori la Akiba la Kijereshi na Hifadhi ya Misitu wa Sayanka. Hadi mwisho wa Januari, 2018 jumla ya vizingi 74 vimesimikwa katika pori la Akiba Kijereshi, Aidha, katika Hifadhi ya Misitu wa Sayanka jumla ya vizingi 67 vimesimikwa, hatua hii imesaidia kupunguza migogoro ya mipaka kati ya wananchi na hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, taitizo lilllobaki kwa sasa ni baadhi ya wananchi kutaka kulima na kuanzisha makazi ndani ya Hifadhi ya Misitu ya Sayanka na wengine kutaka kulima ndani ya mita 500 kutoka mpaka wa Pori la Akiba la Kijereshi kinyume cha Sheria ya Misitu na Wanyamaporii.

Wizara kwa kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega na Halmashauri ya Wilaya ya Busega inaendelea kutoa elimu na kufanya vikao na mikutano na wananchi wanaozunguka Pori la Akiba Kijereshi. Mikutano hiyo inalenga kuwakumbusha wananchi umuhimu wa uhifadhi na kuepusha kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 500 kutoka mpaka wa pori la Akiba. Katazo hilo ni kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamaporii Namba 5 ya mwaka 2009. Aidha, Serikali inatoa wito kwa wananchi kuacha kuvamia maeneo ya hifadhi ili kudumisha uwepo wa bioanuai kwa faida yetu ya sasa na vizazi vijavyo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na napenda nipongeze majibu ya

Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu haya yamejikita kuelezea taarifa ambayo siyo sahihi, kwa sababu migogoro mingi imekuwa ikichochewa na uhamishaji wa mipaka na ndio malalamiko ya wananchi katika maeneo husika, kwa vile Serikali imekuwa ikihaidi muda mrefu kwamba kuwe na mpango shirikishi kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi ili kuainisha mipaka vizuri zaidi, kitu ambacho kitaondoa migogoro na migongano iliyopo.

Je, ni lini sasa Serikali kupitia majibu haya, kwa sababu suala hili siyo mara ya kwanza au ya pili kuuliza hapa Bungeni, ni lini Serikali itakaa na wananchi wa maeneo husika ili kutatua mgogoro wa namna hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili Mheshimiwa Naibu Waziri aliyeuwepo wakati ule *Engineer Ramo Makani* alitembelea maeneo husika yaliyotajwa kwa maana kwamba pori la Akiba la Kijereshi kwa wananchi wa kijiji cha Kijereshi, Mwakiloba, Lukungu na Mwamalole na akajione mwenyewe kwamba wananchi wana haki kwa kile wanachokizungumza, vilevile alikwenda Pori la Akiba la Sayanka akajiona mipaka imehamishwa wananchi wamekuwa miaka yote wanalima kabla ya mipaka kuwekwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari sasa kuja ujionee uhalisia huu na uondokane na taarifa potofu ambazo zinazotolewa na wataalam wako? Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu naomba niitumie nafasi hii kumpongeza sana kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya kwa kweli akina Masunga na Hasunga nadhani ni machachari sana, hongera sana Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijibu maswali yake. Kuhusu matatizo na migogoro mbalimbali ambayo ipo katika maeneo mengi, ni kweli kabisa tumebaini kwamba kuna migogoro mingi ambayo aidha, imesababishwa na kutokushirikisha vizuri wananchi ama kutokana na sababu mbalimbali ama kuongezeka kwa idadi ya watu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika maeneo mengi, kwanza tuliunda Kamati ya Kitaifa shirikishi ambayo ilishirikisha Wizara mbalimbali ambayo sasa imebainisha maeneo mbalimbali yenye migogoro na hivi sasa ipo katika hatua ya mwisho ya kubainisha na kutoa ushauri ili tuweze kufanya uamuzi ni maeneo yapi Serikali iweze kuyaachia kwa wananchi na maeneo yapi yabaki chini ya hifadhi. Baada ya taarifa hiyo kukamilika hivi karibuni nadhani kwamba taarifa hili itatolewa Bungeni na Wabunge wote watapata nafasi ya kuweza kujua.

Kuhusu kukaa na wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Chegeni mimi naomba nimuambie tu kwamba Serikali tuko tayari kukaa na wananchi ili kuweza kupitia mipaka hatua hadi hatua, mimi nimuahidi baada ya Bunge hili tutakaa naye tutapanga kwamba ni lini twende tukawatembelee ili na nijiridhishe kabisa kwamba madai anayoyasema na wananchi wanayoyasema kweli yanahuusu hiyo mipaka na kama mipaka imesogezwa basi tuweze kuchukua hatua stahiki katika maeneo haya aliyyotaja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Kiwelu swali la nyongeza.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu ya Naibu Waziri amesema Kamati ya Kitaifa iliyoundwa, ninapenda kujua ni lini Kamati hiyo itakamilisha taarifa hiyo na kuileta ndani ya Bunge ili matatizo hayo yaweze kukoma? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba Kamati ya Kitaifa ambayo ilikuwa inashirikisha zaidi ya Wizara tano iliundwa kupitia maeneo mbalimbali na kupitia nchi nzima kuona migogoro ambayo iko katika maeneo mbalimbali. Kamati hiyo imeshatoa tayari matokeo ya awali ambayo yamebainisha kila kitu ni maeneo gani ambayo yapo kwenye matatizo, baadhi ya maeneo ambayo yamebainishwa ni pamoja na vijiji 366 viko ndani ya hifadhi.

Kwa hiyo, basi juzi tumekaa na hiyo Kamati imetoa tena *draft* nyingine tumetoa maelekezo ni imani yangu ndani ya kipindi cha miezi miwili, Kamati hiyo itakamilisha kabisa hiyo taarifa na itawasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge na kutoa taarifa kamili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere swalii la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Bunda na Vijiji vya Honyari, Kihumbu, Maliwanda, Sarakwa, Kyandege mpaka wao kati ya pori la Akiba la Gruneti na Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hapa kutoka mpaka wa Mto Lubana kwenda kwa wananchi ni mita 500 ningependa kujuua kutoka mpaka mto Lubana kwenda porini ni mita ngapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika hili eneo la Gruneti kuna mipaka ambayo ipo lakini itakuwa ni vigumu sana kumpa taarifa kamili umbali uliopo kati ya huo mto na hilo eneo

analolisema. Kwa hiyo naomba nitumie nafasi hii kuwambia kuwa nitakaa nae, tutaenda kutembelea hilo eneo ili tuone kwamba kuna umbali wa mita ngapi ambazo zinahusisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa swalil la nyongeza.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kuna mgogoro katika Pori la Akiba la Kimisi na maeneo ya Rweizinga – Mguruka katika Kata ya Bwelanyange, mwaka jana Bunge liliilekeza Serikali iende katika hayo maeneo na kutatua migogoro hii, lakini mpaka hivi sasa Serikali haijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujuu ni lini Mheshimiwa Waziri utaambatana na mimi ili tuende kwenye Kata ya Bwelanyange maeneo ya Rweizinga na Mguruka ili kushirikisha wananchi katika kuweka mipaka mipya katika pori la Akiba la Kimisi na Kata ya Bwelanyange? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika maeneo aliyoitaja kulikuwa kuna matatizo na wananchi walikuwa na malalamiko kuhusu mipaka na naomba nimhakikishie kwamba niko tayari wakati wowote mwezi wa Machi, mwaka huu nitatembelea katika Mkoa wa Kagera na tutakapokuwa huko basi tutapata nafasi ya kwenda kuititia na kuongea na wananchi juu ya mipaka hiyo yote aliyoitaja katika maeneo ya Bwelanyange na maeneo mengine yote aliyoitaja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swalil lake.

Na. 64

## **Hitaji la Eneo la Kilimo kwa Wananchi wa Jimbo la Ulanga**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Sehemu kubwa ya Jimbo la Ulanga imezungukwa na Hifadhi ya *Selous Game Reserve* hivyo kufanya wananchi wa Kata za Mbuga, Ilonga, Kataketa na Lukunde kukosa maeneo ya kilimo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa maeneo hayo maeneo ya kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Akiba Selous lilianzishwa kati ya mwaka 1896 na 1912 na Serikali ya Kikoloni ya Wajerumani. Wajerumani waliligawa pori hilo katika maeneo manne ambayo ni Ulanga, Kusini, Muhoro na Matandu. Mnamo mwaka 1951 pori hili lilitasajiliwa rasmi kwa GN/Na. 17 chini ya *Fauna Conservation Ordinance CAP. 302*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Akiba la Selous ni muhimu sana kiuchumi, kiikolojia na kiutamaduni siyo tu kwa Taifa letu bali pia Kimataifa. Pori linalingizia Taifa fedha za Kitanzania na za kigeni kupitia utalii, lina misitu ya lindima inayosaidia upatikanaji wa maji, linachangia kudhibiti mabadiliko ya tabia ya nchi na makazi na mazalia ya viumbe hai wakiwemo wanyamapori, samaki na viumbe wengine. Kutokana na umuhimu huo Umoja wa Mataifa umelitambua eneo hili kuwa urithi wa dunia. Sambamba na hilo Serikali ya Kikoloni ilianzisha pori tengefu la Kilombero mwaka 1952 ili kuunganisha mfumo wa kiikolojia katika maeneo hayo awili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua changamoto za matumizi ya ardhi katika maeneo yaliyotajwa, Serikali inatekeleza mpango wa Kilombero na *Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project*, mradi huu unahusisha kutatua matatizo ya mipaka ya vijiji na mapori ya hifadhi yaliyo katika Wilaya ya Ulanga, Malinyi na Kilombero pamoja na kuwawezesha wananchi kumiliki ardhi kupitia hati miliki za kimila.

Aidha, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia mradi wake wa *Land Tenure Support Programme (LTSP)* inaendelea kuhakiki mpaka wa pori tengefu la Kilombero ambalo nisehemu ya Wilaya ya Ulanga na kupima ardhi ya vijiji kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi kwa wananchi na hatimaye kupata hati za kumiliki. Serikali inaamini kuwa kupitia miradi hii miwili changamoto ya matumizi ya ardhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makazi zitatatuliwa kikamilifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, swalii la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa nafasi ya pekee napenda nkipongeze Chama changu cha Mapinduzi kwa kutimiza miaka 41 ya utawala bila kung'oka, na kwa utendaji huu tuna miaka 41 mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri atakuwa shahidi tangu hili pori lianzishwe ni miaka mingi sasa na watu wameongezeka kwa kiasi kikubwa, sheria hizi zilizoanzisha mapori ndiyo sheria hizi hizi zilizoanzisha vijiji, inapotokea maeneo wanayoishi wananchi yakagundulika madini wananchi wanatolewa, lakini wananchi wanapohitaji kulima maeneo ya mapori wanaambiwa sheria zizingatiwe. Kwa nini sheria ziko *bias* upande mmoja kwa kuwaonea wananchi ambaao ni wanyonge?

(b) Mheshimiwa Waziri tulikuwepo nae Ulanga wiki mbili zilizopita ameona jiografia ya Ulanga ilivyo ngumu maeno yote ya matambalale ambayo wananchi wanaweza wakalima ni Mapori Tengefu, ni Hifadhi na Bonde la mto Kilombero, naomba busara zitumike ili wananchi wapate maeneo ya kilimo kwa sababu wameongezeka kwa kiasi kikubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wakati tunapata Uhuru idadi ya wananchi wa Tanzania ilikuwa haizidi milioni tisa na ardhi ilikuwa hivi, lakini miaka karibu 56 ya Uhuru wananchi wa Tanzania wameongezeka kwa kiwango kikubwa sana, sasa tuko karibu millioni 52 lakini ardhi haljaongezeka. Kwa hiyo naomba nimuambie Mheshimiwa Mbunge kwamba kutokana na ongezeko la watu ndiyo maana kumekuwa na presha kubwa sana katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo naomba nimhakikishie kwamba sheria zilizotungwa sio kwamba ziko *bias*, sheria ziko vizuri kabisa, sheria zinaainisha maeneo yaliyohifadhiwa, maeneo ambayo yanafaa kwa makazi, maeneo yanayofaa kwa ufugaji, maeneo yanayofaa kwa kilimo kwa hiyo hili lazima tulismamie ipasavyo. Siyo kwamba sheria zinapendelea labda kitu fulani na Serikali yetu itaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa maeneo ya kulima yale yanayostahili na yale yaliyohifadhiwa yaendelee kuhifadhiwa kwa mijibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swalı lake la pili ni kweli kwamba tutatumia busara kubwa sana katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo hili la Ulanga wanapata eneo la kulima, kufuatia hatua hiyo na ziara ambayo tumeifanya hivi karibuni kama alivyosema yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ameunda Kamati ya Wajumbe 22 kwa sababu ya ukubwa wa Bonde lenyewe la Kilombero lilivyo ili kuweza kubainisha, kuweza

kupitia maeneo yote na waone ni maeneo gani yahifadhiwe, maeneo gani yatafaa kwa kilimo ili kusudi wananchi wapate kuelekezwa ipasavyo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBER M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Mpigamiti pamoja na Kikulyungu ni vijiji ambavyo vimepakana na hifadhi ya Selous katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, lakini kuna mgogoro mkubwa sana wa ardhi kati ya Kikulyungu pamoja na Selous.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri utaweza kutatua mgogoro huu ambaao umedumu zaidi ya miaka 10 na watu tayari washapoteza maisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika eneo hili kuna migogoro mingi na kuna eneo kubwa ambalo kwa kweli kuna matatizo. Naomba nikuhakikishie hata jana nilikuwa karibu na pori la Selous katika maeneo ya Mbwande nikishughulikia matatizo ambayo yanafanana na namna hii. Kwa hiyo, katika eneo lako hili la Mpigamiti pamoja na Kikulyungu ambako kuna matatizo naomba niseme kwamba ninalichukua tutaendelea kulifanyia kazi na tutashirikiana na wewe ili kuweza kutafuta ufumbuzi wa hili tatizo ambalo limedumu kwa muda mrefu kusudi wananchi wa eneo lako wapate kufaidika na wapate kufurahi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani zaidi ya vijiji 12 vinavyozunguka Pori la Akiba la Mkungunero hawafanyi kazi ya kilimo kwa sababu ya mgogoro mkubwa ambao umedumu zaidi ya miaka 10, kati ya wafanyakazi wa pori la Akiba la Mkungunero na wakulima wanaozunguka pori lile. Suala hili limeshafika Serikalini, lakini hakuna hatua zinazochuliwa. Wabunge wa Majimbo Mheshimiwa Juma Nkamia na Mheshimiwa Dkt. Ashatu wanapata shida sana wakati wa kampeni na hata wakati wa kuwatemebelea wananchi wao.

Je, ni lini sasa matatizo haya yatakwisha mpaka halisi wa pori la Mkungunero litabainishwa ili wakulima wale wafanye kazi yao kwa uhuru na kwa amani? (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na tatizo la muda mrefu la vijiji hivi 12 katika pori la Akiba la Mkungunero ambapo wananchi walikuwa wanagombania mipaka, hili ni mojawapo ya eneo ambalo Kamati ya Kitaifa imeyapitia na wenyewe tumeipitia tumeona kweli kuna mgogoro ambao unatakiwa kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumuomba Mheshimiwa Felister Bura kwamba katika hili eneo Serikali iliagiza kwamba maeneo yote yenye migogoro yawekewe mipaka na muda wa mwisho ulikuwa ni tarehe 31 Desemba, 2017. Hivi sasa tunafanya tathmini kupitia maeneo yote sio tu katika eneo hili la Mkungunero, katika mapori yote ya akiba na mengine yote kuangalia baada ya kuweka mipaka na vagingi katika haya maeneo ni maeneo yapi ambayo yana migogoro, ni maeneo kiasi gani tunatakiwa tuyaacie ama tuendelee kuyahifadhi na wananchi watafutiwe maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya yote kukamilika basi Waheshimiwa Wabunge watajulishwa na hatimae tutajua kabisa kwamba wananchi sasa watatatuliwa haya matatizo na hili tatizo la Mkungunero na vijiji hivi 12 vyote vitakuwa vimepata ufumbuzi wa kudumu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na. 65

**Bei ya Kahawa Ikilinganishwa na Gharama za Uzalishaji**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y MHE. PETER J. SERUKAMBA)** aliuliza:-

Bei ya kahawa ni ndogo ikilinganishwa na gharama za uzalishaji.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha bei ya zao la kahawa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima kwa kuwapatia ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, lene sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya kahawa duniani ikiwa ni pamoja na kahawa ya Tanzania hutegemea bei katika masoko mawili ya rejea duniani ambayo ni Soko la Bidhaa la New York (*New York Commodities Market*) kwa kahawa ya *Arabica* na Soko la *London International Financial Futures and Options Exchange* kwa kahawa ya *Robusta*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa bei katika masoko hayo huathiri moja kwa moja bei kwa nchi zote wazalishaji wa kahawa ambapo mwenendo huo pia huathiri bei katika soko la mnada wa kahawa na bei ya wakulima Tanzania. Bei ya kahawa katika masoko ya rejea pia hutokana na kiasi kilichopo na mahitaji (*demand and supply*) ya kahawa duniani kwa wakati husika. Aidha, kwa kuwa wanunuzi hununua kahawa kwa bei ya mwali pwani (*FOB*) ambayo hujumuisha bei ya mkulima na gharama, zao za ununuzi kwa hivyo bei ya kahawa haizingatii kabisa gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la kahawa pia hukabiliwa na ada na tozo mbalimbali ambazo huongeza gharama za kufanya biashara na hivyo kusababisha wanunuzi wengi kwenda kununua kahawa katika nchi jirani ambako hakuna ada na tozo nydingi na hivyo kutoa bei nzuri ukilinganisha na bei za ndani. Hali hiyo husababisha wakulima kutorosha kahawa nje ya nchi ili waweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haiwezi kupandisha bei ya kahawa kwa kuwa bei hiyo hutokana na masoko rejea ya dunia. Hata hivyo, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuwaongeza kipato wakulima. Mikakati hiyo ni pamoja na kufuta ada na tozo zipatazo 17 katika sekta ya kahawa ili kumpunguzia mkulima mzigo wa malipo ambayo wanunuzi huweka kwenye gharama zao za ununuzi; kuongeza ushindani katika mnada kwa kuwaondoa wanunuzi wa kahawa vijijini ili wakanunue kahawa mnadani kwa ushindani, kuimarisha, kufufua na kuanzisha Vyama Vikuu vya Ushirika katika kila Mkoa unaolima kahawa na Vyama vya Msingi kwa maana ya *AMCOS* katika kila kijiji ili kukusanya kahawa ya wakulima, wanachama na kuipeleka mnadani. Aidha, *AMCOS* zimehamasishwa kuanzishwa viwanda vya kuchakata kahawa ili kupata kahawa bora na yenye bei nzuri na kuimarisha usimamizi kwa zao la kahawa katika ngazi na hatua zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali huwapatia wa kahawa ruzuku kwa kupunguza bei ya miche bora ya

kahawa inayozalishwa na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania, vilevile Mamlala za Serikali za Mitaa zinazolima kahawa nchini zimeagizwa zote kuanzisha bustani za kuzalisha miche bora kulingana na mahitaji ya wakulima wao na kuigawa bure na pia kuhakikisha inapandwa na kutunzwa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa tunafahamu kwamba soko la kahawa bei yake imekuwa ikipanda na kushuka, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuanzisha ruzuku maalum kwa ajili ya wakulima wa kahawa ili hata soko linapoporomka mkulima asipate maumivu sana kwenye upande wa mauzo? (*Makofi*)

Pili, tunaamini kwamba Vyama vyetu vya Ushirika vinayo nafasi kubwa sana ya kuhakikisha wakulima wan chi hii wananaufaika. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinaimarika na kuwa msaada kwa wakulima? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu ruzuku katika bei ya mazao. Naomba niseme kwamba bei ya ruzuku kwa upande wa Serikali, sisi tunatoa mazao yote katika *standardization* na vilevile tutaangalia siku zijazo kuhusu Vyama vya Ushirika kama vinafanya vizuri basi tutaoa hiyo *standardization* na ruzuku katika vyama na mazao yote yanayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake (b) ni kuhusu Vyama vya Ushirika. Serikali tumejipanga kuhakikisha

kwamba tunafanya *total transformation*, vilevile *operations* katika Vyama vya Ushirika. Ni kweli vingi havifanyi vizuri na tumeangalia kabisa vingine hata havifanyiwi mahesabu lakini kama Serikali, kama nilivyosema tumefanya *total transformation* kuhakikisha kwamba Vyama vya Ushirika vitakuwa vinafanyiwa mahesabu, vitakuwa vinafanyiwa ukaguzi ili tuweze kupata bei nzuri na mazao bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote naomba niwataarifu kwamba hivi majuzi mwezi uliopita Tume ya Vyama vya Ushirika imeundwa na tayari imeshaanza kazi. Nashukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda, swalii la nyongeza.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swalii dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya matatizo yaliyosababisha wakulima wapate shida sana na zao la kahawa kuporomoka ni utendaji mbovu wa hivyo Vyama vya Msingi na Vyama vya Ushirika. Mwaka huu tunakwenda kwa mara ya kwanza kwa kuwa na Chama Kikuu cha Ushirika na Mkoa ambacho kitanunua kahawa kwa niaba ya wakulima.

Je, Serikali imejiandaa vipi kuwaandaa Watendaji Wakuu wa Vyama vya Msingi kwa sababu tumbakiwa na muda mchache na uwezo wao unaweza ukawa ni mdogo huko nyuma walishatuletea hasara, kwa mfano, Mbinga, hoteli ya Mbiki, ma-*godown*, viwanja na majengo yote yako kwa Msajili wa Hazina....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus, umeshauliza swalii moja. Mheshimiwa Naibu Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika,

kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia sana katika suala zima la Vyama vya Ushirika hususan katika Jimbo lake la huko Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Jimbo la Mbinga na lenyewe limekuwa likilima sana zao hili la biashara la kimkakati la kahawa na ni kweli naomba nikiri kwamba vyama vingine vya ushirika vimekuwa havifanyi vizuri. Lakini kama nilivyomjibu Mheshimiwa Mbunge Stanslaus Mabula, katika maswali yake mawili ya nyongeza ni kwamba Serikali imejipanga sawasawa kufanya *total transformation* katika suala zima la Vyama vya Ushirika na tumejipanga kuingia kwa miguu miwili. Tutakuwa tunafanya mafunzo ya mahesabu na vilevile kuhakikisha kwamba ukaguzi utakuwa unafanyika kwa kina ili tuweze kupata mazao bora ambayo pia yatakuwa yanatupatia bei nzuri. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Masaba swali la nyongeza.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nami nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Kigoma Kaskazini linafanana kabisa na tatizo la wananchi wa Mkoa wa Simiyu kwa wakulima wa pamba. Katika Mkoa wa Simiyu kumezuka wadudu waharibifu wanaoharibu zao la pamba na mahindi na hitaji la dawa za wakulima hawa ni sawa na chupa milioni moja na laki nne, lakini mpaka sasa wakulima hawa wamepatiwa chupa 350 tu ni sawa na asilimia 25. (*Makof!*)

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuwasaidia wakulima hawa ili kuhakikisha kwamba mazao hayo hayaharibiki? Ahsante. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Gimbi Masaba kwa swali lake la kuhusu pamba pamoja na wakulima wa zao la pamba na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanatoka katika Mikoa inayolima pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa habari njema naomba niseme tu kwamba Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba zao la pamba ambalo mdudu wa kweleakwelea pamba mbegu zake zinaharibika. Serikali imeshatoa shilingi bilioni tatu tayari kuhakikisha kwamba mpango huu wa dharura na tatizo hili la dharura linafanyiwa kazi na vilevile shirika la FAO limeshatupatia *US dollar* milioni 250 kwa ajili ya kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba niwahakikishie kabisa wakulima wa pamba kwamba tatizo hili litatatuliwa hivi karibuni. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na Mheshimiwa Pauline Phillip Gekul sasa aulize swali lake.

Na. 66

### **Ushuru wa Mazao**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Halmashauri ya Mji wa Babati inaidai *NFRA* ushuru wa zaidi ya shilingi milioni 90 katika kipindi cha mwaka 2014/2015.

Je, ni lini fedha hizo zitalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa ununuzi wa nafaka mwaka 2014/2015 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) ulinunua tani 1,127.826 za mahindi zenye thamani ya shilingi 6,063,913,000 kutoka kwa wakulima na vikundi vya wakulima katika Mji wa Babati. *NFRA* ilipaswa kulipa kwa Halmashauri ya Mji wa Babati ushuru wa shilingi 181,917,390 ambazo ni asilimia tatu ya thamani ya mahindi yaliyonunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wakala ulilipa ushuru wa mazao kwa tani 4,400,000 zenye thamani ya shilingi 66,000,000 na kubaki na deni na deni la ushuru wa mazao kwa tani 7,727.686 zenye thamani ya shilingi 115,917,390.00. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti wakala ulishindwa kulipa kiasi chote cha ushuru kwa wakati kutokana na kuongezeka kwa ununuzi wa mahindi zaidi ya melengo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wakala ulilipa deni lote la ushuru wa mazao kwa Halmashauri ya Babati kwa awamu mbili ambapo tarehe 10 Agosti, 2015 ullilipa shilingi 23,000,000 na kumalizia deni la shilingi 92,917,390 tarehe 27 Januari, 2016. Aidha, kwa sasa Wakala umelipa ushuru wa mazao kwa Halmashauri zote ilikonunua mahindi na hakuna deni lolote kuhusu ushuru wa mazao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kulitendea haki swali langu maana yake ni swali la muda mrefu miaka mitatu, lakini hizo fedha tumeshazipokea na tumezisahau.

Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa *NFRA* walipewa eneo la kujenga *godown* au kiwanda katika Halmashauri ya Mji wa Babati kwa ajili ya kuchakata mahindi yetu kuongezea thamani, pamoja na kuwapa kiwanja hicho

au eneo hilo zaidi ya heka sita mpaka leo mwaka wa tatu *NFRA* hawajafika kujenga *godown* kiwanda hicho. Naomba nifahamu ni lini *NFRA* watafika katika Halmashauri ya Mji wa Babati kujenga kiwanda hicho?

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wetu wengi katika Mkoa wa Manyara na katika Halmashauri ya Mji wa Babati msimu huu wa kilimo cha mahindi hawajapata pembejeo za kilimo, hawajapata mbegu na mbolea, wamelazimika kupanda mahindi ya mwaka jana waliyovuna mashambani, mbegu hawajapatiwa. Mbegu zilizopo zinazuwa kwa bei ya juu kilo mbili shilingi 12,000.

Naomba nipate kauli ya Serikali ni kwanini hampunguzi bei ya mbegu za mahindi ili wananchi wetu waweze kupanda mbegu hizo badala ya kuwaachia sasa wanapanda mahindi ya mwaka jana? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote pia na mimi naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo kama alivyosema amekuwa akifuatilia jambo hilli tangu miaka mitatu iliyopita. Vilevile naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi wote wa Jimbo la Babati Mjini kwa jinsi ambavyo wanafuatilia na kuzingatia umuhimu wa kilimo na vilevile kuweza kutoa ardhi kwa ajili ya kujenga mradi huu wa maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo ninaomba nitamke hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba mradi huu tayari umeshakamilika na ninamuagiza Mtendaji Mkuu wa *NFRA* kuanza kazi mara moja ifikapo mwisho wa mwezi wa tatu. Huu mradi unaghanimu milioni 8000. Kwa hiyo, Mtendaji Mkuu wa *NFRA* hilli ni agizo, mwezi wa tatu mwishoni mradi huu uanze kazi mara moja kwa ajili ya kuongeza thamani ili wananchi hawa wa Babati waweze kupata ajira na thamani ya mazao yao pia iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge ameuliza suala zima la mbegu. Katika suala zima la mbegu, sisi kama Serikali mbegu huwa zinakusanywa na makampuni binafsi na ndiyo maana unakuta bei inakuwa ni kubwa, lakini kupitia Wakala wetu wa Taifa wa Mbegu tumeanzisha mpango mahsuswa kuhakikisha kwamba tutakuwa tunazalisha mbegu ambayo inaitwa *hybrid* kwa ajili ya kuboresha ili iweze kuwa na bei punguvu.

Vilevile tunashirikiana na makampuni binafsi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanapata mbegu bora na kwa bei nafuu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Susan Lyimo.

Na. 67

#### **Baadhi ya Shule na Vyuo Kutokidhi Matakwya ya Sheria**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y MHE. ZUBEDA H. SAKURU)** aliuliza:-

Baadhi ya Shule na Vyuo nchini vinaendelea kudahili wanafunzi pamoja na kutokidhi matakwa ya sheria mbalimbali.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti vyuo na shule zinazoendelea kudahili wanafunzi huku zikiwa na mapungufu?

(b) Je, mpaka sasa ni vyuo vingapi na shule ngapi zilizofutiwa usajili kwa kutokukidhi matakwa ya kisheria.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina taratibu za kudhibiti ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa shulenii na vyuoni kupitia Idara ya Udhhibitii Ubora wa Shule katika maana ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Baraza la Taifa la Elimu la Ufundii (*NACTE*) kwa vyuo na taasisi zinazotoa elimu ya kati na Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*) kwa taasisi zinazotoa elimu ya juu. Shule na vyuo vinavyobainika kukiuka taratibu za utoaji elimu na mafunzo huchukuliwa hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusitisha udahili wa wanafunzi, kusitisha programu zitolewazo, kupunguza idadi ya wanafuzni waliozidi na kufuta usajili wa taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imefuta usajili kwa shule saba za awali na msingi na shule moja ya sekondari. Vilevile vituo 16 vilivyokuwa vime dahili wanafunzi wa elimu ya awali na msingi kabla ya kusajiliwa villagizwa kuwatawanya wanafunzi hao kwa kuwapeleka katika shule zilizosajiliwa na kufunga vituo hivyo. Katika mwaka 2016/2017 Serikali kupitia *NACTE* ilifanya uhakiki katika vyuo na taasisi 103 za elimu ya ufundii ambapo vyuo na taasisi 31 zilibainika kuwa na mapungufu na hivyo kufutiwa usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika mwaka 2017/2018 uhakiki mwingine ulifanyika katika vituo, vyuo na taasisi 454 za elimu ya ufundii ambapo jumla ya vyuo na taasisi 59 za elimu ya ufundii zilibainika kuwa na mapungufu na hivyo walitakiwa kurekebisha mapungufu ndani ya kipindi cha miezi mitatu kuanzia tarehe Mosi Februari, 2018. Chuo kitakachoshindwa kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa ndani ya kipindi kilichopangwa kitafutiwa usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vyuo vikuu Serikali kupitia *TCU* ilifanya uhakiki wa vyuo vyote vya elimu

ya juu nchini kati ya mwezi Oktoba, 2016 na Januari, 2017 ili kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa vyuoni. Taarifa ya uhakiki ilionyesha mapungufu katika baadhi ya vyuo, kufuatia taarifa hiyo *TCU* kwa mwaka wa masomo 2017/2018 ilisitisha udahili wa wanafunzi wa Programu za Afya na Uhandisi kwenye vyuo vitano. Vilevile *TCU* ilisitisha udahili katika programu zote kwa mwaka wa kwanza kwa vyuo 14, aidha, katika mwaka huo wa masomo *TCU* imedhibiti na kuzuia vyuo vikuu kudahili wanafunzi katika programu ambazo hazijapata ithibati zipatazo 75 katika vyuo vikuu 22.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo swalii la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na jitihada za kudhibiti ubora wa elimu hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuanzia shule ya awali mpaka vyuo vikuu, naishukuru Serikali kwa juhudii hizo kwa sababu siku zote Upinzani tumekuwa tukizungumzia suala la ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua ni nini hatma ya wanafunzi katika vyuo vile ambavyo vimefutiwa usajili wakiwa tayari wanaendelea na masomo? Kwa mfano, unakuta vijana hao tayari walishalipa ada lakini na muda wao. Je, Serikali inatuambia nini au inawaambia nini wanafunzi ambaao tayari walikuwa kwenye masomo lakini wakaondolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili ni kweli kwamba huu ukaguzi ni mzuri sana lakini kumekuwa na ubaguzi mkubwa kwenye ukaguzi kwa maana ya shule za msingi za Serikali na zile za *private*, hali inayopelekea kuwa na *double standard*, kwa sababu wanafunzi wa shule za *private* kila mwanafunzi anatakiwa alipe shillingi 5000 kwa ajili ya ukaguzi, lakini wanafunzi wa shule za Serikali ni bure. Hamuoni kwamba kwa ubaguzi huu ndiyo inayopelekea kuporomoka kwa elimu hasa kwenye shule za Serikali na ndio sababu kunakuwa na matokeo mabaya? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezekano wa wanafunzi wanaondelea na vyuo kuathirika na hatua ambazo tunachukua wakati wa kuhakikisha kwamba kuna ubora katika vyuo vyetu.

Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila wakati tunapochukua hatua tunahakikisha kwamba wanafunzi hawataathirika lakini ifahamike kwamba kwa sababu tokea awali vyuo hivyo vinafahamu kuhusu utaratibu ambaao wanatakiwa wafuate, pale tatizo linapotokea maana yake wenyewe watatakiwa kurejesha gharama hizo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusiana na tofauti aliyotaja ya ada ya ukaguzi kati ya shule za Serikali na zile za watu binafsi, Serikali haioni kwamba tofauti hiyo ina athari zozote zile katika ubora wa elimu. Ni utaratibu tu ambaao umewekwa wa kuhakikisha kwamba hiyo ada inalipwa lakini hatuoni kwamba shilingi 5000 kulipa kwa shule binafsi kwamba ina athari katika ubora wa elimu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swalii la mwisho Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcemba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 68

**Ujenzi wa Nyumba za Askari Polisi na Magereza**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Hali ya nyumba za Polisi na Magereza nchini ni mbovu sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za askari hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hali ya makazi kwa Askari wetu siyo nzuri, hata hivyo Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo na kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo husika kujenga makazi mapya na kufanya ukarabati wa majengo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 12.3 fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa makazi ya askari wetu katika maeneo mbalimbali nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mcchemba swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na jitihada zote zinazofanywa na Serikali kutatua tatizo la makazi ya askari. Je, kwa kipindi hiki cha 2017/2018 Mkoa wa Tabora umetengewa kiasi gani?

Swali la pili, kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la wakimbizi kutoka Congo na kwa kuwa hivi karibuni pia wamesema kwamba baadhi ya wakimbizi wale wametawanyika katika Mkoa wa Kigoma inawezekana wakaja na Mkoa wa Tabora. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanne Mcemba kwa swali lake zuri la pili la nyongeza kutokana na changamoto ya mfumuko wa Wakimbizi ambao wanaingia nchini kutoka DRC hasa kutoka katika maeneo ya Kivu kutokana na changamoto ya hali ya usalama nchini DRC. Kabla sijatoa ufanuzi wa swali lake hilo la pili nimjibu kwamba kwa bajeti ambayo nimezungumza ya maendeleo ambayo nilisema ni takribani bilioni 12.3 ya mchanganuo mbalimbali ikiwemo shilingi bilioni 7.2 ya Magereza ni fedha ambazo zimetengwa kwa maendeleo nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jeshi la Magereza hakuna utaratibu wa *sub vote* kwenye Jeshi hilo ingawa Jeshi la Polisi ipo lakini kwa ujumla kwa mwaka huu wa fedha hakuna fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya miradi wa maendeleo kwa Tabora *specifically*, lakini kwa sababu tunatambua kwamba kuna maeneo mengi nchini ambayo kuna majengo mengi ya Polisi ambayo yapo katika hatua za mwisho kukamilika, kwa mfano, kule Mtambaswala - Mtwara, Njombe, Mabatini Mwanza, Musoma na kadhalika, kwa hiyo fedha hii ya maendeleo mwaka huu tunataka tulekeze katika majengo ambayo tayari yapo katika hatua za mwisho kukamilika kabla hatujaanza miradi mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii sasa kuweza kuzungumzia hoja yake ya pili muhimu ya wimbi la wakimbizi kutoka DRC. Mpaka hivi naomba nitoe taarifa rasmi kwamba Wakimbizi ambao wametoka DRC kuingia nchini tokea Januari wanakadiriwa kufika zaidi ya 2,500 na katika hao takribani wakimbizi 1,960 tayari wameshakuwa wamehifadhiwa katika Kambi ya Wakimbizi Nyarugusu na wengine 300 na zaidi wapo kwenye vituo vya kupokelea Wakimbizi. Changamoto ambayo amezungumza ya kwamba kuna baadhi ya wakimbizi ambao wamekuwa wana desturi aidha ya kutoroka kwenye makambi kutoka

DRC na kuingia mitaani ama kupita njia za panya kuingia nchini kwetu kwa kisingizio cha machafuko DRC.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe kauli ifuatayo, jambo la kwanza nataka nitoe angalizo ama onyo kali kwa wakimbizi kama hao kuacha desturi hiyo. Tumeshatoa maelekezo katika vyombo vyetu vya usalama nchini kuhakikisha jambo la kwanza kwa Idara ya Uhamiaji kuendelea kufanya msako kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, ikiwemo Jeshi la Polisi hasa katika Mkoa wa Kigoma ambao una changamoto kubwa sana ya wakimbizi, hii inadhihira na takwimu ambavyo zipo kwa mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani asilimia 30 ya wahamiaji haramu waliokuja Tanzania wametokea katika Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, tumewekeza nguvu nyingisana katika Mkoa wa Kigoma kuhakikisha kwamba inadhibiti wimbi la wahamiaji haramu kuingia. Vilevile tumetoa maelekezo kwa Idara ya Wakimbizi ambayo ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhakikisha kwamba inafanya uhakiki na kuimarisha ulinzi katika makambi yetu hasa Kambi ya Nyarugusu ambayo ndiyo kambi ambayo inapokea wakimbizi kutoka DRC ili kuhakikisha kwamba wale wote ambao watakiuka sheria na utaratibu wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria ya wakimbizi kwa kushtakiwa ili baadaye sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo kauli ya Serikali kuhusiana na swali lake la pili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwanza kabisa kabla ya matangazo kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nimpe salamu za Mheshimiwa Spika anakukaribisha sana Bungeni na tunaamini kwamba tutaweza kufanya kazi kwa pamoja. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, pia nitambue kurudi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili msije mkaanza kumpelekeea hoja Mheshimiwa Mwakyembe. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesharejea kwa hivyo yupo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo tuliyonayo ya wageni tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika nao ni wageni sita wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao wamekuja kushuhudia akiapishwa ambao ni viongozi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Ndugu Paul Joel Ngwembe, karibu sana Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Pia ameongozana na Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Ndugu Casmir Kyuki, pia familia ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikiongozwa na mke wake Ndugu Natalia Kilangi, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Madiwani wawili na Wenyeviti wawili wa Vitongoji, wakiongozwa na Mzee Adamson Mwakabwale huyo anatoka Kata ya Kajunjumele na Ipyana, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na huyu ni mgeni wa Mheshimiwa George Lubeleje ambaye ni mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam naye anaitwa Ndugu Mariam Mapunda, karibu sana.

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo kundi la kwanza ni wageni 35 ambao ni watumishi wa kristo wa Kanisa la *Tanzania Assemblies of God* kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. Tunao pia Mapadri nane kutoka Seminari ya Shirika la Damu ya Yesu wa Kanisa Katoliki wa Mkoani Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Susan Lyimo ambaye ni Makamu Mwenyekiti

wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania anawatangazia Wabunge wote wanawake kuwa leo tarehe 5 Februari, 2018 kutakuwa na semina kwa ajili Wabunge Wanawake wote. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kuahirishwa Kikao cha Bunge kuanzia saa 7.00 mchana. Waheshimiwa Wabunge wanawake mnaombwa kuhudhuria. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine linatoka Idara ya Kamatiza Bunge..., Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti nadhani wanaume wanataka kualikwa ndiyo minong'ono hiyo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka Idara ya Kamati za Bunge na mnatangaziwa Waheshimiwa Wabunge wote kuwa fomu za kuomba kupangiwa Kamati za Kudumu za Bunge zinapatikana sehemu ya mapokezi ya Ukumbi huu wa Bunge.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kila mmoja kuchukua nakala yake ya fomu ili aweze kujaza na zote zirejeshwe hapo hapo mapokezi kabla ya tarehe 10 Februari, 2018. Hii ni kuzingatia masharti ya Kanuni ya 116(7) ya Kanuni za Bunge kuhusu ukomo wa ujumbe katika Kamati za Kudumu za Bunge ifikapo mwisho wa Mkutano huu wa Kumi wa Bunge. Kwa hiyo, mnakumbushwa kuchukua fomu na kuzijaza.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kwa leo sitazitaja hapa, lakini kuna Wizara ambazo majibu yake ya msingi ni marefu sana na uzuri watendaji wako hapa, ambao ndio watayarishaji wa hayo majibu watusadie kupunguza urefu wa majibu wasitoe historia ndefu sana, kwa sababu maswali huwa yanakuwa yameulizwa jambo mahsus. Kwa hiyo, tusitoe historia kwenye hayo maswali. Pia Waheshimiwa Wabunge mnaoweka mazingira magumu sana Mawaziri pamoja na Kiti hapa kwenye kuyakataa maswali yenu mapya mnayoyaliza ambayo hayakuwepo kabisa kwenye swali la msingi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba sana tusome yale maswali kama hukuliona kabla ukifika hapa soma swali linahusu nini. Swali linahusu wodi ya wazazi, unauliza dawa. Swali linahusu jengo unauliza mbegu sasa tafadhali ama swali linahusu majengo wewe unazungumzia kitu tofauti. Sasa kuliko kuwaambia Mawaziri hawajajibu sawasawa kwa sababu na sisi tunasikiliza hapa majibu ni afadhali maswali yetu yaoulize kitu mahsusimba ambacho kinahusika na swali la msingi ili Mbunge usiambiwe umeuliza swali ambalo halihusiki, pia wizara isilazimike kujibu jambo ambalo halikuwa limeulizwa kwenye swali la msingi. Maswali yote ya nyongeza yanatokana na maswali ya msingi na majibu yaliyotolewa na upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa Mwongozo wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 47 sambamba na masharti yake yaliyopo kwenye Kanuni ya 48. Ilikupendeza unaweza ukaamua, aidha Bunge lijadili kama itakupenda ama Serikali itoe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu sisi haifuati misingi ya dini, lakini sisi wananchi tunaoishi kwenye hii nchi tuna dini zetu na dini zimegawanyika katika madhehebu mbalimbali, ukiingia kwenye dini ya kiislamu ina madhehebu mengi na ukienda kwenye dini ya kikristo ina madhehebu mengi. Viongozi wetu wamekuwa wakilitambua na kulijua hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mwongozo wako kwa nini kwa upande wa dini ya kiislamu Serikali

imekuwa ikifanya kazi na ikitambua taasisi au dhehebu moja tu linaloitwa BAKWATA ikiacha madhehebu mengine. Ukiacha BAKWATA, taasisi hii inayoitwa BAKWATA, lakini taasisi zingine zote hata zikiwa na shughuli zake kubwa zimekuwa hazitambuliki na wakati mwingine hata ushiriki wa viongozi wakubwa wa Kiserikali hawaonekani. Kwa hiyo nilikuwa naomba mwongozo wako kwamba je hivi BAKWATA ndio taasisi pekee iliyopewa mamlaka na Serikali ya kuwasemea waislamu wa nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nimesimama hapa kwa hisani ya Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiti chako mara kadhaa kimekuwa kikiri kwamba kuna idadi kubwa sana ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge na muda ambaو upo kwa ajili ya kujibu hautoshi kwa maswali yote kupata nafasi. Kwa maelezo hayo tulitegemea kwamba kigezo kitakachokwuwa kinatumika kwa kujibu maswali ni ile *first in, first out*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilikuwa najaribu kuitia maswali ambayo yameulizwa hapa nikagundua kwamba swalı kwa mfano la Mheshimiwa Goodluck Mlinga aliuliza siku nyingi sana, Mheshimiwa Pauline Gekul aliuliza mwaka 2016, Mheshimiwa Constantine Kanyasu aliuliza mwaka 2016, Mheshimiwa Daimu Mpakate hakumbuki, lakini Mheshimiwa Mussa Mbarouk aliuliza Novemba 2017. Kwa uchache ukiangalia utagundua kumbe kigezo siyo *first in, first out*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwanza tujue ni kigezo gani kinatumika kupanga maswali ili yaweze kujibiwa? Pili kwa nini hatupati *acknowledgement letter* pale tunapopeleka maswali angalau tuambiwe kwamba, swalı lako limepokelewa, lipo kwenye mchakato, siku likipata nafasi litajibiwa. Angalau tuwe na kitu cha

kuonesha kwamba, swali langu lipo maana hivi tunavyokaa, mimi binafsi nina maswali sita toka mwaka 2016 hayajajibiwa. Sasa nashindwa kujua kwamba, hayo maswali yameshatupwa kapuni au yapo kwenye foleni ya kusubiri kujibiwa au la?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia maswali mengine yanapokaa mwaka mzima yanapoteza ule umuhimu wake. Linapoletwa kuja kujibiwa hapa yale majibu yanakuwa tena siyo *relevant* kwa wakati ambao tuliliza. Kama muda wa kujibu maswali ni mdogo kwa nini basi, isiangaliwe baadhi ya maswali au maswali ya muda mrefu yajibewe kwa maandishi kwa sababu haya maswali mengine tunatumwa na wananchi, sasa unapokaa mwaka mzima haliulizwi na huna majibu inaleta mchanganyiko na mengine tunatumwa na Mabaraza yetu ya Halmashauri kwamba fuatilia hili. Sasa kwa nini basi tusijibewe hata kwa maandishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, baada ya muda gani Mbunge atambue kwamba swali langu sasa litakuwa limetupwa kapuni na halitaulizwa tena ili kama anaweza aandike tena au achukue maamuzi mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Bobali na pia Mheshimiwa Mtolea. Nitaanza na Mheshimiwa Bobali ambaye amesimama akiomba Mwongozo halafu akataja Kanuni ya 47 na Kanuni ya 48.

Maeleo aliyojatoa Mheshimiwa Bobali amezungumza kuhusu nchi yetu kutokuwa na dini na kwamba wananchi wake ndio wenye dini na hilo ni wazi wote tunalifahamu, na ameeleza katika dini hizi kwamba yako madhehebu mbalimbali.

Mheshimiwa Bobali anaomba Mwongozo wangu kwamba kwa nini, Serikali inaitambua BAKWATA pekee kwa

upande wa waislamu na kwamba madhebu mengine hata yanapokuwa na matukio makubwa Serikali haishiriki kwenye matukio hayo. Pia ameuliza kwamba je, BAKWATA ndicho chombo kinachowasemea waislamu wote hata wale ambao madhehebu yao hayapo chini ya BAKWATA?

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo unaombwa chini ya Kanuni ya 68(7) kwa jambo ambalo limetokea mapema Bungeni na mapema ilishatafsiriwa kwamba ni mapema siku hiyo. Jambo hili aliloliomba Mheshimiwa Bobali kutolewa Mwongozo na Kiti hapa halijatokea hapa Bungeni. Kwa hiyo, kama anahitaji Bunge hili kutoa maelezo kuhusu jambo hilo atumie Kanuni inayohusika na afuate utaratibu unaotakiwa. Mwongozo unaombwa kwa jambo lilitokea Bungeni mapema.

WNimeombwapia Muongozo na Mheshimiwa Mtolea kuhusu maswali. Mheshimiwa Mtolea ametoa maelezo kwa kirefu, kwa kufupisha tu amezungumza kwamba maswali mengine yanachukua muda mrefu zaidi na yako maswali ambayo yalikuja siku nydingi na hayajasikika na Waheshimiwa Wabunge hawana hakika kama hayo maswali bado iko siku yatapangiwa ama hapana. Ametoa mfano wa maswali yaliyoulizwa leo ambayo mengine ni ya muda mrefu na kwa hivyo, majibu yanavyotolewa leo mambo mengine yalishafanyika zamani.

Sasa ameuliza kuhusu vigezo vya kupangwa maswali na pia namna gani ya kutambua kwamba, maswali yamepokelewa, ikiwa Mbunge hapewi maandishi yoyote kwamba sasa swalii lako limepokelewa. Pia, ameuliza kwamba ni baada ya muda gani ukipita hatajua kama swalii lake litajibiwa ama halitajibiwa.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge linapopokea maswali ya Wabunge kuna vitu vingi ambavyo huangaliwa, si kwa lengo la kuzuia maswali yasijibiwe, lakini ni Bunge linataka kujiridhisha na vile vitu vinavyoulezwa. Wakati mwingine maswali yanakuwa yakilingana ya Mbunge mmoja na mwingine, kwa hiyo, hawawezi wote kupewa fursa ya kuuliza

maswali yanayolingana, lakini jambo kubwa la msingi ni kwamba maswali yanachukua muda mrefu.

Waheshimiwa Wabunge, katika maswali kuchukua muda mrefu, nadhani yeye amesema ya kwake ni ya mwaka 2016 na hii ni 2018 naamini kwamba ni yote maana hujaeleza, nimeshawahi kukusoma hapa ukiwa na swali la msingi, sijui hilo utakuwa uliletä lini, lakini huenda una maswali mengi na mengine hayajajibwa. Sasa ili upate majibu mahsusii kuhusu maswali yako wewe inabidi uende kwenye Kitengo chetu kinachoshughulikia maswali ili uone utaratibu wa hayo maswali yako.

Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo alivyokiri muomba muongozo, Waheshimiwa Wabunge tuko 393 kila mtu anapeleka maswali idadi anayoona yeye inafaa. Sasa yako maswali mengine kuuliza vitu ambavyo pengine Kikanuni ama kisheria haviruhusiwi, kwa hiyo, hayo hayawezi kuja, lakini yale ya jumla ambayo yanaruhusiwa kuja, idadi ya maswali ni kubwa kuliko fursa zinazojitokeza.

Hata hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao pengine walishaleta maswali mengi sana huko nyuma na hakuna hata moja lililopata nafasi, basi waende wapate kujua kama hayo maswali yote yameruhusiwa Kikanuni kwa hivyo, yatapangiwa muda ama yako yale ambayo hayako sawa Kikanuni, kwa hiyo hayataweza kuwepo ili Wabunge hao waweze kuleta maswali mapya.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Mwongozo wangu ni kwamba Mheshimiwa Mt Olea pamoja na Wabunge wengine wenye hoja kama yake waende kwenye Kitengo chetu kinachopokea hayo maswali ili waweze kutolewa ufanuzi wa maswali yao yamefikia wapi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Bunge lipokee na Kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu  
ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati  
kwa Mwaka 2017 na Kamati ya Kudumu ya Nishati na  
Madini kuhusu Shughuli za Kamati  
kwa Mwaka 2017**

**NAIBU SPIKA:** Tutaanza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ni maelezo ya jumla. Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 117(15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtiririko wa Taarifa hii umegawanyika katika maeneo makubwa manne yafuatayo:-

- (a) Sehemu ya Kwanza – maelezo ya jumla.
- (b) Sehemu ya Pili - uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati.
- (c) Sehemu ya Tatu - maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati.
- (d) Sehemu ya Nne - hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati; kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 6(8), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imepewa jukumu la kusimamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Katika kusimamia Wizara hiyo, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Aprili, 2016 imeainisha majukumu ya Kamati kama ifuatavyo:-

- (a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inayoisimamia.
  - (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara husika.
  - (c) Kufuatilia Utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inayoisimamia.
  - (d) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara husika.
  - (e) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3)(b) cha Katiba.
- Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelizwa katika kipindi cha mwaka 2017/2018; katika kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi mwezi Januari 2018, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao mbalimbali pamoja na ziara kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, vika; vikao vya kushughulikia taarifa za utendaji wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ambayo Kamati inaisimamia; Vikao hivyo vilihusisha Mamlaka ya Bandari Tanzania – *TPA, Railway Holding Company – RAHCO*, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania – *TAA*, Kampuni ya Meli Tanzania – *MSCL*, Wakala wa Barabara Tanzania – *TANROADS*, Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, *TEMESA*, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Kampuni ya Simu Tanzania, Tume ya TEHAMA na Shirika la Posta.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilifanya ziara, ilipata fursa ya kutembelea mikoa karibu 22 ya Tanzania Bara; kujionea jinsi Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unavyopeleka mawasiliano katika maeneo yaliyoko pembezoni. Mikoa iliyotembelewa ni pamoja na Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma, Singida, Tabora, Mwanza, Simiyu, Mara, Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Kagera na Geita.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilipata nafasi ya kushiriki uzinduzi wa ujenzi wa reli ya kisasa (*standard gauge*) kutoka Dar es Salaam – Morogoro, uwekaji wa jiwe la msingi kwa ajili ya kuongeza kina cha Bandari ya Dar es Salaam Gati Namba Moja mpaka Saba, Bandari ya Mtwara pia uzinduzi wa barabara mbalimbali zikiwemo Msata – Bagamoyo na katika Mikoa mingine ya Singida, Tabora, Kigoma, Kagera na Geita na daraja la Furahisha Mjini Mwanza. Aidha, Kamati ilihudhuria uzinduzi wa viwanja vya ndege vya Tabora na Bukoba pamoja na kiwanja cha ndege cha Chato na uzinduzi wa *Hostel* za Chuo Kikuu zilizojengwa na *TBA*.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati iliendelea na kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Sekta ya Ujenzi Fungu 98, Sekta ya Uchukuzi Fungu 62 na Sekta ya Mawasiliano Fungu 68.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilifanya vikao vya kuchambua Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa iliyopendekezwa kuridhiwa. Katika kipindi cha mwaka mmoja, Kamati ilichambua Miswada na Mikataba ifuatayo:-

i. Muswada wa Sheria ya Reli Tanzania ya mwaka 2017.

ii. Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Tano ya mwaka 1994, Itifaki ya Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya mwaka 2004, Itifaki ya Nyongeza ya Nane ya mwaka 2008 na Itifaki ya Nyongeza ya Tisa ya mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

iii. Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa mwaka 2017.

iv. Muswada wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na mapendekezo na makadirio kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliidhinishiwa shilingi triliioni 4.5. Mgawanyo wa fedha hizi katika kila Sekta ni kama ifuatavyo:-

i. Shilingi 1,929,707,714,000/= Sekta ya Ujenzi;

ii. Shilingi 2,569,073,208,000/= Sekta ya Uchukuzi; na

iii. Shilingi 18,104,139,000 Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa mwenendo wa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta hii ni mzuri na umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali sana kwa kuipa Sekta ya Miundombinu kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*); Mamlaka ya Bandari Tanzania ina majukumu ya kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendeshaji wa bandari. Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara pamoja na Bandari Ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na Bagamoyo. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) inamiliki bandari kadhaa za Maziwa Makuu kama Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeelezwa kwamba, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania – *TPA* inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

a. Uwezo mdogo wa kuhudumia meli kubwa inayotakana na kina kifupi katika bandari ya Dar es Salaam pamoja na Tanga.

b. Uchakavu wa miundombinu ya bandari nchini.

c. Uwepo wa bandari bubu na ushindani wa bandari zingine kama vile za Beira-Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizo, Kamati inaipongeza Serikali kuitia Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kuanza kutekeleza baadhi ya ushauri wake kama ifuatavyo:-

(i) Mgongano uliokuwepo kwa tozo za hifadhi za mizigo (*Warehouse Rent*) inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na *Storage Charges* zilizokuwa zinatozwa na Bandari umerekebishwa.

(ii) Pia Himaya ya Forodha kwa Pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mizigo wa Congo, Kamati imejulishwa kuwa Serikali imetoa *notice* ya muda wa mwezi mmoja, ili kuvunja Mkataba huo ambao umekuwa ukileta utata na kupunguza motisha kwa wafanyabishara wa Congo kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

(iii) Aidha, Serikali imefuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (*Value Added Tax-VAT*) kwa huduma zitolewazo na mawakala kwenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani (*VAT on transit goods*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam, Kamati imejulishwa kuwa hatua mbalimbali za utekelezaji zimefikiwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuhusu ujenzi wa Gati Namba Moja hadi Saba na gati la kushushia meli za magari; Mkandarasi yupo katika eneo la kazi na kwa sasa imefanyika kazi kwa asilimia 15.

(ii) Kuhusu kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli, kazi hii ipo katika hatua mbalimbali za kutangazwa kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mtaalam mwelekezi.

(iii) Ujenzi gati Namba 12-14; utekelezaji wa ujenzi wa gati hizi utafanyika katika awamu ya pili ya maboresho na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam. Kwa sasa Serikali bado ipo kwenye majadiliano na wafadhili ili kufanya upembuzi yakinifu wa namna bora ya kuhamisha *Kurasini Oil Jet* na miundombinu yake kwa ajili ya kupisha ujenzi wa magati hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ukarabati na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam unaendelea; ni vyema Serikali ikaanza pia ukarabati wa bandari nyingine muhimu kama vile Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara, Bandari ya Mwanza, Bandari ya Kigoma na Bandari ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli; Kamati inatoa pongezi kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ili kufufua na kuimarisha mtandao wa reli nchini. Mionganoni mwa juhudhi hizo ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (*standard gauge*). Hivyo, katika kuendeleza juhudhi hizo mnamo mwezi Septemba, 2017, Serikali illeta Muswada wa Sheria ya Reli wa 2017 ambao moja kati ya majukumu yake ilikuwa ni kuanzisha Shirika jipya la Reli (*Tanzania Railway Corporation – TRC*) ambalo pamoja na mambo mengine, litakuwa na jukumu la kusimamia, kuendeleza miundombinu ya Reli na kutoa huduma za usafiri wa reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya Sekta ya Uchukuzi ya mwaka 2017/2018, mionganoni mwa malengo yaliyowekwa kuhusu kuimarisha miundombinu ya reli nchini ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa reli ya kisasa. Hivyo, Serikali kwa kutambua umuhimu wake imetenga karibu bilioni 900 kwa ajili ua jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imejulishwa kuwa ujenzi wa reli hii umegawanyika katika sehemu tano zifuatazo:-

- (i) Dar es Salaam – Morogoro, kilometra 205, ujenzi umeshaanza.
- (ii) Morogoro – Makutupora, kilometra 336, mradi unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Februari, 2018.
- (iii) Pia Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya Makutupora – Tabora, kilometra 295.
- (iv) Tabora – Isaka kilometra 133.
- (v) Isaka – Mwanza kilometra 250.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa katika maeneo mengine nchini kwa kiwango cha kisasa (*standard gauge*), ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara hadi Mbaba Bay na matawi yake kuelekea Liganga na Mchuchuma kilometra 1,092 upembuzi yakinifu umekamilika. Vilevile reli ya kutoka Tanga – Arusha – Musoma yenye urefu wa kilometra 1,108 na Arusha kilometra 438, shughuli za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maendeleo mazuri katika mradi wa ujenzi wa reli hii ya kisasa, mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i. Usajili wa raia wa kigeni katika bodi za taaluma nchini, yaani wafanyakazi wa reli.
- ii. Upatikanaji wa maeneo ya ujenzi (ardhi) nje ya maeneo yanayomilikiwa na *RAHCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ndege ya Tanzania – *ATCL*; Kamati imejulishwa kuwa pamoja na ndege mbili mpya aina ya Dash 8 Q400 kwa sasa, Kampuni inamiliki ndege tatu ambazo zinafanya ziara zake ndani ya nchi. Kamati imejulishwa kuwa mwezi Julai, 2018; Serikali inategemea kupokea ndege zingine mbili ambapo moja ni Dash 8 Q400 na nyingine ni ndege kubwa aina ya Boeing 787 yenye uwezo wa kubeba abiria 262.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*); jukumu kubwa la wakala huu ni kuhudumia mtandao wa barabara ambao unakadiriwa kuwa na urefu wa jumla ya kilometra 35,000 ambapo kati ya hizo, kilometra 12,786 ni barabara Kuu, na kilometra 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara ziweze kuitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaaji wa uchumi, kama ilivyofafanuliwa katika Mpango na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Wakala wa Barabara anakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- (a) Kutokutolewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hali inayosababisha kazi zilizopangwa kwa baadhi ya miradi kutotekelezwa ama kutekelezwa kwa kiasi kidogo;
- (b) Msongamano wa magari barabarani hasa Jiji la Dar es Salaam, na miji mingine inayokuwa kwa kasi, kama vile Jiji la Mbeya, Mwanza na Arusha;
- (c) Baadhi ya wasafirishaji kuendelea kuzidisha uzito wa mizigo kwenye magari na kusababisha uharibifu wa barabara; na
- (d) Uwezo mdogo wa wakandarasi wa ndani katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara kutokana na kukosa mitaji vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matuta barabarani. Licha ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*)kuahidi kuendelea kurekebisha matuta makubwa, ili kuyaweka katika viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa Wizara kuhusu usanifu wa barabara wa mwaka 2011, bado kumeendelea kuwapo matuta makubwa hasa katika barabara kuu ambapo yamekuwa chanzo cha uharibifu wa barabara, kwani magari

yenye mizigo hulazimika kwenda mwendo mdogo; hivyo uzito kuwa mkubwa na kusababisha barabara kutitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, matuta barabarani yamekuwa yakisababisha mizigo kuhama na kuelemea upande mmoja; jambo ambalo wakati mwininge limekuwa chanzo cha ajali kwa magari mengi ya mizigo. Pia matuta husababisha myumbo wa matairi (*wheel alignment*) hivyo kuchochea ubovu na kuongeza uwezekano wa ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanja vyatya ndege nchini umeendelea kutekelezwa chini ya Sekta ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Kamati katika kutekeleza majukumu yake imebaini kuwa ujenzi wa viwanja vyatya ndege umeendelea kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwepo na changamoto ya kupatikana kwa fedha kwa wakati kwa ajili ya ujenzi wa viwanja ndege nchini. Hata hivyo, Kamati imejulishwa kuwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vyatya ndege kwa sasa ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa jengo la abiria (*Terminal III*) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, mkataba ulisainiwa 18 Aprili, 2013. Hadi kufikia Desemba, 2017; utekelezaji wa kazi uliflikia asilimia 68 ambapo kazi zilizoendelea ni kuezeka na kumalizia kazi za kusimika mitambo ya umeme, viyoyozi na utandazaji wa nyaya na mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza ulianza mwezi Oktoba, 2012 na ulipangwa kukamilika mwezi Septemba, 2014. Hata hivyo, hapo awali mradi huu ulikuwa ukikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati hivyo kusababisha utekelezaji wake kuwa ndogo. Lakini sasa hali ya fedha imetengamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe mkoani Mbeya ulianza mwaka 2000

ambapo ujenzi umekuwa ukitekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kiwanja hiki ni muhimu sana kwa wakazi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na hata wasafiri kutoka nchi jirani za Zambia na Malawi. Tangu kiwanja hiki kilipofunguliwa rasmi mwaka 2012 kumekuwepo na ongezeko kubwa la abiria na ndege. Hata hivyo, pamoja na umuhimu mkubwa wa kiwanja hiki, mradi huu pia umekuwa ukitekelezwa kwa kasi ndogo, jambo linalosababisha mradi kutokukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na changamoto hizo katika ujenzi wa kiwanja hiki, Kamati toka mwaka 2016 imekuwa ikishauri mara kwa mara umuhimu wa kuwekwa kwa taa za kuongozea ndege ambazo zitasaidia ndege kutua nyakati za usiku na hata mchana wakati wa ukungu mkubwa. Hali kadhalika kuwekwa kwa uzio kuzunguka mipaka yote ya kiwanja ili kuongeza usalama wa kiwanja na kuepuka uvamizi na wananchi wa maeneo jirani kukatiza katika maeneo ya kiwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha ndege cha Kigoma. Pamoja na kuwa mradi huu upo mingoni mwa miradi inayogharamiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Kamati imejulishwa kuwa ilikubaliwa kuwa kabla ya fedha za mkopo kuanza kutoka Serikali iwe imeshalipa fidia kwa wananchi wote watakaothiriwa na ukarabati na upanuzi wa kiwanja hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mawasiliano, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania yaani *TCRA*. Serikali kuititia *TCRA* imeweka mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu ambao umechangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni zilizopo katika udhibiti wa mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha mabadiliko ya teknolojia ili kuongeza ubora wa huduma na kuendana na kasi ya mabadiliko yanayotokea. Mfumo wa *TTMS* pamoja na mambo mengine mpaka kufikia Desemba, 2017 umewezesha mambo yafuatavyo:-

- (a) Kuhakiki mawasiliano ya simu za ndani;

- (b) Mfumo wa kubaini simu za ulaghai;
- (c) Mfumo wa kuhakiki mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano;
- (d) Kudhibiti uhalifu katika mitandao;
- (e) Uanzishwaji wa maabara ya kisasa ya kiuchuguzi ya kidijitali; na
- (f) Kuweka viwango vipyta vya mwingiliano baina ya mitandao ya simu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) ulianzishwa kwa lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibashara. Mwezi Oktoba, 2017 Kamati ilipata nafasi ya kutembelea maeneo mbalimbali ili kujionea ikiwa huduma za mawasiliano zinapatikana katika sehemu hizo ambazo minara imejengwa. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea takribani mikoa 20 ya Tanzania Bara na Kamati ilibaini changamoto zifuatazo;-

(a) Serikali za Mikoa, Wilaya pamoja na wananchi hawajui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kwamba miradi hiyo ya ujenzi wa minara inatoka kwenye ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana iliyoko maeneo mengi ni kuwa minara inajengwa na Makampuni ya simu yenyewe, hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki.

(b) Pamoja na kuwa makampuni yamepewa masharti ya kuwajibika katika kutoa huduma za jamii katika maeneo yanayofanya shughuli zake za kibashara kwa kiasi kiasi kikubwa makampuni haya yamekuwa hayatoi huduma hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa minara kwa kutumia Kampuni ya *TTCL* ulikuwa ukisucasua kwa siku za nyuma, hata hivyo baada ya Kamati kufanya ziara ya ukaguzi wa minara mwaka wa jana, *TTCL* imekamilisha miradi yake

yote iliyokuwa inadaiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi Katika maeneo mengi ambayo Kamati imetembelea minara yamebainika wazi kuwa na migogoro ya umiliki wa maeneo husika. Pia kumekuwa na changamoto ya wizi wa vifaa vyta minara kama vile mafuta, betri na nyaya aina ya *fiber*. Pia Minara mingi iliyojengwa inatumia umeme wa jua (*solar power*), hii inasababisha nyakati za usiku hasa kipindi cha mvua maeneo mengi kuwa na mawasiliano hafifu kwa sababu jua haliwaki kipidi kirefu. Makampuni pia yanajenga minara pasipo kuweka huduma za kijamii kama choo, kibanda cha mlinzi na huduma zingine za msingi kwenye maeneo ya mnara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ni mapendeleko na ushauri wa Kamati. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza miundombinu nchini ambapo bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali iliendelea kuongeza tengeo la fedha katika sekta ya miundombinu hadi kufikia shilingi trillioni 4.5.

Mheshimiwa Maibu Spika, hii inaonyesha kwa kiasi kikubwa serikali imezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo katika nchi yetu kwani miundombinu ndiyo itawezesha tija na utendaji bora wa sekta nyingine. Hata hivyo pamoja na shabaha nzuri ya serikali katika masula ya miundombinu kamati inazitiza fedha kutolewa kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka limbikizo la madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uchukuzi; Mamlaka ya Bandari Tanzania; kwa kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ndiyo mamlaka iliyopewa jukumu la kusimamia jukumu la bandari nchini; na kwa kuwa mamlaka hii inayo miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa bandari ambapo kwa sasa mamlaka ipo katika hatua ya kuboresha na kufanya ukarabati wa bandari kama vile Mtwara na ujenzi wa magati pamoja uchimbaji wa kina katika Bandari ya Dar es

Salaam; kwa hiyo basi Kamati inaishauri Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Asilimia 20 ya mapato ya bandari yabaki bandarini ili kuwezesha Mamlaka ya Bandari Tanzania iweze kutekeleza baadhi ya miradi kama vile miradi ya ujenzi wa bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara ambayo jumla inagharimu bilioni 20, wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni wastani wa bilioni 270;

(b) Kuharakisha mchakato wa ununuzi wa *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Kamati ilitembelea bandari na kuona tatizo la kutokuwepo na *flow meter* na hivyo kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia Bandari ya Dar es Salaam. Ni rai ya Kamati kuwa *flow meter* inunuliwe kwa haraka. Hivi tunavyoongea sasa tatizo hilli bado halijashughulikiwa; na

(c) Kuunganisha zabuni za ujenzi wa bandari ya Kigoma ili kuweza kupata mzabuni mwenye uwezo atakayefanya kazi hiyo; kwani imekuwa ikitangazwa mara kadhaa bila kupata mzabuni kutokana na gharama ya maandalizi (*mobilization*) kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli nchini; kwa kuwa Serikali imeonyesha nia dhati ya kujenga reli ya Kati katika kiwango cha kisasa (*standard gauge*) ambapo mradi huu umeanza tangu mwezi Aprili, 2017na unatekelezwa kwa awamu tano; na kwa kuwa katika uhalisia tawi la kutoka Tabora – Kigoma - Uvinza - Msongati na Kaliua - Mpanda - Kalema ndilo lenye mizigo mingi inatoka na kwenda nchi jirani kama vile DRC Kongo Burudi na Ruanda. Hivyo basi kamati inaishauri serikali ifuatavyo:-

(a) Reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbe zaidi kiwekwe katika tawi la Tabora, Kigoma Tabora – Kigoma - Uvinza - Msongati; Kaliua – Mpanda – Kalema na Tabora – Mwanza.

(b) Kuwapeleka kwenye mafunzo zaidi wataalamu ili kuweza kuhudumia miundombinu za treni za kisasa inayoendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*); kwa kuwa kumekuwa ya migogoro mingi ya uvamizi wa maeneo ya viwanja vya ndege, na kwa kuwa utatuzi wa migogoro hiyo umekuwa ukigharimu Serikali fedha nyingi kulipa fidia na kuchelewesha baadhi ya miradi ya ujenzi wa viwanja hivyo; hivyo basi kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Kuhakikisha kwamba *TAA* inapata hati za viwanja kwani Kamati imejulishwa kuwa viwanja vya ndege vinane tu ndivyo vyenye hati miliki kati ya viwanja 58 vinavyomilikiwa na mamlaka ya viwanja vya ndege. Bado kuna haja ya kuhakikisha kuwa viwanja vingine vimebaki vinapilmwa na kupatiwa hati miliki;

(b) Ili kuepuka ongezeko la gharama za ujenzi ni vema serikali ikakamilisha miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege vilivyoanza vikiwemo viwanja vya ndege vya Julius Nyerere vya Terminal Three na Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na Kiwanja cha Ndege cha Songwe na kulipa fidia kama inavyotakikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ndege *ATCL*. Kwa kuwa serikali imeonyesha nia ya dhati ya kufufu kampuni ya Ndege Tanzania; na kwa kuwa biashara ya ndege inahitaji mikakati mikubwa ya biashara ili kuweza kuingia katika soko la ushindani, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) *ATCL* ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi, Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*); kwa kuwa Wakala Barabara nchini (*TANROADS*) ndio waliokabidhiwa jukumu la ujenzi na ukarabati wa barabara nchini, na kwa kuwa pamoja na jitihada za Serikali kujenga barabara maeneo mbalimbali hivyo basi Kamati inashauri ifuatavyo:-

- (a) Kuhakikisha inaunganisha miji yote na mikoa iliyosalia kama vile mkoa wa Katavi – Kigoma, Katavi – Tabora, Kigoma – Kagera, Njombe - Makete - Mbeya kwa barabara za lami ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo hayo.
- (b) Ukarabati wa baadhi ya barabara za mikoa iliyokatika hali isiyoridhisha na kutopitika na hasa wakati wa mvua na kuadhere shughuli za kiuchumi na kilimo.
- (c) Pia matuta madogo madogo ya barabarani maarufu kwa jina la rasta na matuta makubwa yasiyo na kiwango yaondolewe kwa kuwa yanasaababisha ajali na uharibifu wa magari. Aidha, matuta yabaki sehemu zenye umuhimu tu na yawe na kiwango maalum. (*Makofii*)
- (d) Kununua mizani ya kisasa ambayo ina uwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*weight in motion*). Kamati inaendelea kushauri kwamba mizani hii ya kisasa ifungwe pia katika maeneo mengine yenye kusababisha msongamano mkubwa wa kupima magari; kwa mfano, Himo – Moshi, Mizani ya Mikese Morogoro, Kihonda, Morogoro, Makambako na Kwa Mpemba nikitaja kwa uchache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam; kwa kuwa Serikali imeonyesha nia ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam kwa kuweka barabara za juu (*flyovers*) eneo la Tazara na Ubungo na kwa kujenga barabara za michepuko; na kwa kuwa msongamano katika jiji la Dar es Salaam umekuwa ukisababisha adha kubwa, kwa hiyo basi kamati inashauri serikali yafuatayo:-

(a) Barabara za juu maarufu kama *flyovers* zijengwe hasa katika makutano ya barabara kuu zenyé msongamano mkubwa kama vile Magomeni, Morocco na Mwenge.

(b) Wadau kama mifuko ya jamii inaweza kushirikishwa katika kujenga barabara za kulipia.

(c) Pia kukamilisha ujenzi wa barabara zinazosaidia wakazi kufika maeneo yao bila kupita katikati ya Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kukamilisha barabara za kutoka Goba-Madale-Wazo Hill, Goba-Kimara-Ardhi-Makongo nakadhalika.

(d) Pia barabara za mitaani yaani *Wingroads* nazo zifunguliwe kwa kuwekwa lami kwani zitapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Mawasiliano; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*); kwa kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kusimamia mawasiliano nchini, na kwa kuwa kumekuwepo changamoto mbalimbali zinazotokanana ukuaji wa Technolojia hivyo basi kamati inashauri serikali ifuatavyo:-

(a) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia mitandao na ili kuimarisha usalama wa watu mali zao.

(b) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta uvumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya simu za ndani kwa kutumia mitambo ya *TTMC* ili serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia simu za mkono. Kuendelea kuchelewesha kulitekeleza suala hili kunazidi kuikosesha nchi kodi stahiki kutokana na makapuni haya ya kutoza kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*); kwa kuwa mfuko huu ulianzishwa wa

lengo la kupeleka mawasiliano sehemu sizizokuwa na mvuto wa kibiashara na kwa kuwa kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa miradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu hizo hivyo basi Kamati inashauri Serikali yafuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *TCRA* kuweka masharti ya kutoa leseni kwa makampuni ya simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango kwa jamii (*Corporate Social Responsibility*).

(b) Kuhakikisha Makampuni ya simu yanatoa kiwango kilichopangwa cha asilimia 0.9 kama tozo za huduma (*Service Levy Rate*).

(c) Katika maeneo ambayo vijiji vimetoa ardhi bure kwa ajili ya ujenzi wa minara; basi makampuni husika zichangie/ itoe ruzuku kwa kijiji husika kila mwaka.

(d) Mahakama na vyombo vingine viambata kama vile Jeshi la Polisi, watoe kipaumbele na kuharakisha kutoa haki kwenye masuala ambayo yanagusa umma moja kwa moja. Kuchelewa kutoa haki kwani kunachelewesha utekelezaji wa miradi hiyo.

(e) Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa anuani za makazi na misimbo ya posta; kwa kuwa mradi huu una manufaa makubwa kwani utawezesha kuwepo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimaye kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa; na kwa kuwa utekelezaji wa mradi huu umekuwa ukisuasua; kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaz; TAMISEMI na Ujenzi,

Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuharakisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa na pia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kama zilivyoidhinishwa na kwa wakati ili mradi huu ukamiliike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, ili Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Idara zake zote ziendelee kufanikiwa ni lazima uteuzi na ajira za watendaji zifuate weledi, jambo ambalo Kamati inaamini limezingatiwa. Pili, watendaji wa taasisi hizo na dodi wasiingiliwe na watunga sera bali wapimwe kwa uzalishaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia; pili, watendaji wa taasisi hizo na bodi wasiingiliwe na watunga Sera bali wapimwe kwa uzalishaji wao. (*Makofii*)

Tatu, sheria na taratibu zinazowekwa kwenye taasisi zinazofanya biashara zifasili malengo mama ya taasisi hizo. Kama ni sheria au taratibu swali liwe uwepo wa sheria au taratibu hizo zinasaidia kuongeza ufanisi na faida katika taasisi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili likizingatiwa tutakuwa na nafasi ya kuwahukumu watendaji na bodi kwa haki.

Mheshimiwa Spika, shukrani, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee sana napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano rafiki yangu, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa (Mb) akishirikiana na Naibu Mawaziri Mheshimiwa *Engineer Atashasta Nditiye*, (Mb) na Mheshimiwa Elias Kwandikwa. (*Makofii*)

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii, Mhandisi Joseph Nyamuhanga kwa maana Sekta ya Ujenzi, Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho - Sekta ya

Uchukuzi), Mhandisi Dkt. Maria Sasabo Sekta ya Mawasiliano pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Angelina Madete...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako umekwisha naomba umalizie hoja yako na pia kulieleza Bunge kwamba taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING – MWENYEKITI WA AMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante napenda kuwashukuru Katibu na wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelawa na Kamati maoni na ushauri sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee lijadili na kuikubali taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari, 2017/2018 pamoja na maoni na ushauri katika taarifa hii

Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KWA KIPINDI CHA JANUARI 2017 HADI JANUARI 2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

### **SEHEMU YA KWANZA**

#### **1:0 MAELEZO YA JUMLA 1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 117 (15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018.

**Mheshimiwa Spika**, mtiririko wa Taarifa hii umegawanyika katika maeneo makubwa manne yafuatayo:-

- a. Sehemu ya I- Maelezo ya Jumla (Utangulizi);
- b. Sehemu ya II- Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati;
- c. Sehemu ya III- Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati; na
- d. Sehemu ya IV- Hitimisho

## **1.2 Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe .Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb ..
5. Mhe. James Francis Mbatia, Mb ..
6. Mhe. Mansoor Shanif Hirani, Mb ..
7. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb ..
8. Mhe. Saul Henry Amon, Mb ..
9. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb ..
10. Mhe. Quambalo Willy Qulwi, Mb ..
11. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb ..
12. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb ..
13. Mhe.Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb ..
14. Mhe. Mary Deo Muro, Mb ..
15. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb ..
16. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb ..
17. Mhe. Dua William Nkurua, Mb ..
18. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb ..
19. Mhe. Lathifah Hassan Chande, Mb ..
20. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb ..
21. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb ..

- |  |   |
|--|---|
| 22. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb | “ |
| 23. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb    | “ |
| 24. Mhe. Charles Kitwanga, Mb              | “ |
| 25. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb      | “ |
| 26. Mhe. Rukia Kassim, Mb                  | “ |
| 27. Mhe. Dkt. Pudenciana W. Kikwembe, Mb   | “ |

### **1.3 Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 6(8), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imepewa jukumu la kusimamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Katika kusimamia Wizara hiyo, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Aprili, 2016 imeainisha majukumu ya Kamati kama ifuatavyo:-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inayoisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara husika;
- c) Kufuutilia Utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inayoisimamia;
- d) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara husika; na
- e) Kufuutilia Utekelezaji unaofanywa na Wizara kwa Mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

### **1.4 Shughuli zilizotekelizwa katika Kipindi cha Mwaka 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi mwezi Januari, 2018 , Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao mbalimbali pamoja na ziara kama ifuatavyo:-

- a) Vikao vya kushughulikia taarifa za utendaji wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ambayo Kamati inaisimamia; Vikao hivyo vilihusisha Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA, Railway Holding Company-RAHCO , Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania- TAA, Kampuni ya Meli Tanzania- MSCL, Wakala wa Barabara Tanzania- TANROADS,Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, *Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency*-TEMESA, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, Kampuni ya Simu Tanzania- TTCL, Tume ya TEHAMA, Shirika la Posta Tanzania;
- b) Ziara- Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mikoa ishirini na miwili (22) ya Tanzania Bara; kujiona jinsi Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unavyopeleka Mawasiliano katika maeneo yaliyoko pembezoni. Mikoa iliyotembelewa ni pamoja na Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma, Singida, Tabora, Mwanza, Simiyu, Mara, Pwani, Lindi, Mtwara, Songea, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Kagera na Geita;
- c) Kamati pia ilipata nafasi ya kushiriki uzinduzi wa ujenzi wa reli ya kisasa (*Standard Gauge*) kutoka Dar es Salaam – Morogoro, uwekaji wa jiwe la msingi kwa ajili ya kuongeza kina cha Bandari ya Dar es Salaam Gati Na. 1-7, Bandari ya Mtwara pia uzinduzi wa barabara mbalimbali zikiwemo Msata – Bagamoyo na katika Mikoa mingine ya Singida, Tabora, Kigoma, Kagera na Geita na daraja la Furahisha – Mwanza. Aidha, Kamati ilihudhuria uzinduzi wa viwanja vya ndege vya Tabora na Bukoba pamoja na kiwanja cha ndege cha Chato (Geita).
- d) Vikao vya kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Sekta ya Ujenzi Fungu 98, Sekta ya Uchukuzi Fungu 62, Sekta ya Mawasiliano Fungu 68;
- e) Vikao vya kuchambua Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa iliyopendekezwa kuridhiwa. Katika kipindi cha mwaka mmoja, Kamati ilichambua Miswada na Mikataba ifuatayo:-

- i) Muswada wa Sheria ya Reli Tanzania ya Mwaka 2017 (*The Railways Bill, 2017*);
- ii) Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki ya Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki ya Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Itifaki ya Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani;
- iii) Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa Mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*);
- iv) Muswada wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania wa Mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies Corporation Bill, 2017*)

### **SEHEMU YA PILI**

#### **2.0            UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

##### **2.1            Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; pamoja na Mapendekezo na Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliidhinishiwa shilingi trillioni **4.5 (4,516,885,061,000)**. Mgawanyo wa fedha hizi katika kila Sekta ni **1,929,707,714,000** Sekta ya Ujenzi, **2,569,073,208,000** Sekta ya Uchukuzi na **18,104,139,000** Sekta ya Mawasiliano.

Kamati imebaini kuwa mwenendo wa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta hii ni mzuri na umekuwa ukiongezekwa

mwaka hadi mwaka. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipa Sekta ya Miundombinu kipaumbele.

## 2.2 Sekta ya Uchukuzi

### 2.2.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Bandari Tanzania ina majukumu ya kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia Sekta binafsi katika uendelezaji za uendeshaji wa bandari. Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na Bagamoyo. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki bandari kadhaa za maziwa makuu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Bandari licha ya kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi; pia inahudumia nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

Kamati imeelezwa kwamba, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- a) Uwezo mdogo wa kuhudumia meli kubwa na kina kifupi katika bandari ya Dar es Salaam pamoja na Tanga;
- b) Uchakavu wa miundombinu ya bandari nchini; na
- c) Uwepo wa bandari bubu na ushindani wa Bandari zingine kama vile Beira-Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizo, Kamati inaipongeza Serikali kuitia Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kuanza kutekeleza baadhi ya ushauri wake kama ifuatavyo;-

- i) Mgongano uliokuwepo kwa tozo za hifadhi za mizigo ''Customs Warehouse Rent'' inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA na ''Storage Charges'' zinazotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA ambapo yalikuwa yanatozwa kwa pamoja. Kamati imejulishwa kuwa tozo hizi sasa zimewekewa utaratibu ambapo Mamlaka ya Bandari itakuwa inatoza kwa muda wa siku thelathini tu (30) mizigo ukiwa bandarini. Shehena itakayokaa zaidi ya siku hizo na kupelekwa kwenye hifadhi (*yard*) za Mamlaka ya Mapato Tanzania ndio zitatozwa ''Storage Charges'';
- ii) Kuhusu Himaya ya Forodha kwa Pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mizigo wa Congo, Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeanza kutekeleza kwani imetoa ''*notice*'' ya muda wa mwezi mmoja ili kuvunja Mkataba huo ambao umekuwa ukileta utata na kupunguza motisha kwa wafanyabishara wa Congo kutumia Bandari ya Dar es Salaam; na
- iii) Aidha, Serikali imefuta kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax-VAT*) kwa huduma zitolewazo na mawakala kwenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani (*VAT on transit goods*);

**Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam, Kamati imejulishwa kuwa hatua mbalimbali za utekelezaji zimefikiwa kama ifuatavyo:-

- i) Kuhusu ujenzi wa gati namba 1 hadi 7 na gati la kushushia meli za magari (*RoRo berth*); Mkandarasi yupo katika eneo la kazi na kwa sasa kazi imefanyika kwa asilimia kumi na tano (15%);
- ii) Kuhusu kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli, kazi hii ipo katika hatua za kutangazwa zabuni ya awali kwa ajili ya kumpata mkandarasi na Mtaalam mwelekezi; na
- iii) Ujenzi gati namba 12-14; utekelezaji wa ujenzi wa gati hizi utafanyika katika awamu ya pili ya maboresho na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam. Kwa sasa, Serikali bado ipo kwenye majadiliano na wafadhili ili kufanya upembuzi yakinifu wa namna bora ya kuamisha Kurasini Oil Jet na miundombinu yake kwa ajili ya kupisha ujenzi wa magati hayo.

**Mheshimiwa Spika**, wakati ukarabati na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam unaendelea; ni vyema Serikali ikaanza pia ukarabati wa bandari nyingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, bandari ya Mtwara, bandari ya Mwanza, bandari ya Kigoma, bandari ya ziwa Nyasa.

## 2.2.2 Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kampuni hii inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa Meli kutokana na kutokufanyiwa matengenezo makubwa kwa wakati na hivyo kusababisha gharama kubwa. Mfano, MV Butiama ambayo haifanyi kazi tangu mwaka 2010, MV Victoria nayo haifanyi kazi toka mwaka 2014 na MV Liemba ambayo inafanya kazi lakini kwa kususua.

Wakati Kamati ilipokuwa ikifuatilia utatuzi wa changamoto hii ilijulishwa kuwa, Serikali imetenga **shilingi bilioni 24.496 (24,496,000,000)** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya kununua meli mpya mbili (2) ambazo moja ni kwa ajili ya kubeba abiria na mizigo Ziwa Tanzanyika na ya pili ni kwa ajili ya kubeba abiria na mizigo katika Ziwa Victoria. Aidha, fedha hizo pia zitatumika katika ukarabati wa MV Victoria, MV Liemba, MV Butiama, MV Umoja na MV Serengeti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa fedha hizo zimeshatolewa tangu Agosti, 2017 na utekelezaji wa miradi hii uko katika hatua mbalimbali. Kamati inampongeza Mkurugenzi mpya wa MSCL kwa hatua alizochukuwa za kufuutilia uendeshaji wa meli na sasa mapato yameanza kuongezeka.

## 2.2.3 Ujenzi wa Reli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa pongezi kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ili kufufua na kuimarisha mtandao wa reli nchini. Miongoni mwa juhudhi hizo ni pamoa na; kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge*). Hivyo, katika kuendeleza juhudhi hizo mnamo mwezi Septemba, 2017, Serikali ililetta Mswada wa

Sheria ya Reli, 2017 ambao moja kati ya madhumuni yake ilikuwa ni kuanzisha Shirika jipya la Reli (*Tanzania Railway Corporation-TRC*) ambalo pamoja na mambo mengine litakuwa na jukumu la kusimamia, kuendeleza miundombinu ya Reli na kutoa huduma za usafiri wa Reli.

Katika mipango ya Sekta ya Uchukuzi ya Mwaka 2017/2018, mionganoni mwa malengo yaliyowekwa kuhusu kuimarishe miundombinu ya reli nchini ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Reli ya kisasa. Hivyo, Serikali kwa kutambua umuhimu wake imetenga **shilingi bilioni 900(900,000,000,000.00)**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa ujenzi wa reli hii umegawanyika katika sehemu kuu tano ambazo ni:-

- i. Dar es Salaam -Morogoro (km 205) -ujenzi umeshaanza;
- ii. Morogoro-Makutupora (km 336)- mradi unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Februari,2018;
- iii. Makutupora-Tabora (km 295), Tabora-Isaka (km 133) na Isaka -Mwanza (km 250)- Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande hivi;

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa katika maeneo mengine nchini kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge*), ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara hadi Mbaba Bay na matawi yake kuelekea Liganga na Mchuchuma (km 1, 092) upembusi yakinifu umekamilika.

Vilevile, Reli ya kutoka Tanga- Arusha-Musoma (km 1,108), kwa kipande cha Tanga- Arusha (km 438) shughuli ya upembusi yakinifu na usanifu wa awali zimekamilika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maendeleo mazuri katika mradi wa ujenzi wa reli hii ya kisasa, mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazaji:-

- i. Kuchelewa kupatikana kwa fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi kwa upande wa RAHCO kama watekelezaji wa Mradi;

- ii. Matumizi kutokea mfuko wa uendelezaji Reli;
- iii. Usajili wa raia wa kigeni katika bodi za taaluma nchini; na
- iv. Upatikanaji wa maeneo ya ujenzi (ardhi) një ya maeneo yanayomilikiwa na RAHCO.

## **2.2.4      Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa pamoja na ndege mbili mpya aina ya Dash 8 Q400. Kwa sasa, Kampuni inamiliki ndege tatu (3) ambazo zinafanya ziara zake ndani ya nchi. Kamati imejulishwa kuwa mwezi Julai, 2017; Serikali inategemea kupokea ndege zingine mbili ambapo moja ni Dash 8 Q400 na nyiningine ni ndege kubwa aina ya Boeing 787 yenye uwezo wa kubeba abiria 262.

## **2.3      Sekta ya Ujenzi**

### **2.3.1      Wakala wa Barabara Tanzania- TANROADS**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa barabara ulianzishwa kwa taarifa ya Serikali iliyotolewa kwenye Gazeti la Serikali Na. 293 mwaka 2000 chini ya kifungu 3(1) cha Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997. Jukumu kubwa la wakala huu ni kuhudumia mtandao wa barabara, ambao unakadiriwa kuwa na urefu wa jumla ya kilometra 35,000; ambapo kati ya hizo, kilomita 12,786 ni barabara kuu, na kilometra 22,214 ni barabara za Mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara ziweze kuitikika kwa urahisi na hatimaye, kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi, kama ilivyofafanuliwa katika Mpango na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo Wakala wa Barabara unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- a. Kutokelewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hali inayosababisha kazi zilizopangwa kwa baadhi ya miradi kutotekelezwa ama kutekelezwa kwa kiasi kidogo;

- b. Msongamano wa magari barabarani hasa jiji la Dar es Salaam, na miji mingine inayokuwa kwa kasi, kama Mbeya, Mwanza na Arusha;
- c. Baadhi ya wasafirishaji kuendelea kuzidisha uzito wa mizigo kwenye magari na kusababisha uharibifu wa barabara;
- d. Uwezo mdogo wa Makandarasi wa ndani katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara kutokana na kukosa mitaji ya kutosha pamoja na mitambo ya kisasa; na
- e. Ongezeko la gharama za ujenzi, ambazo ni kikwazo kwa ujenzi wa nyumba za kutosha za gharama nafuu kwa ajili ya makazi ya watumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na migogoro na mvutano kutoka kwa wananchi mbalimbali unaotokana na wasiwasi wa kutolipwa fidia au kulipwa fidia kwa kiasi kidogo ambacho hakiendani na hali ya uchumi wa sasa; jambo hili linasababisha wananchi kugoma kuondoka katika maeneo ya miradi; na kusababisha kuchelewa kuanza kwa miradi.

Aidha, changamoto kubwa katika ujenzi wa barabara kwa sasa imekuwa uvamizi wa barabara, uliofanyika miaka iliyopita ambapo wananchi walikuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi za barabara bila kujali Sheria ya barabara Namba 13 ya Mwaka 2007.

Ni rai ya Kamati kwamba, vyombo vyaya usimamizi wa Sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara azuiwe na abomolewe mapema kuliko kumwacha na kusababisha misuguano baadaye.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu matuta barabarani, licha ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kuahidi kuendelea kurekebisha matuta makubwa, ili kuyaweka katika viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa Wizara kuhusu usanifu wa barabara wa mwaka 2011, bado kumeendelea kuwapo

matuta makubwa hasa katika barabara kuu ambapo yamekuwa chanzo cha uharibifu wa barabara, kwani magari yenyé mizigo hulazimika kwenda mwendo mdogo; hivyo uzito kuwa mkubwa na kusababisha barabara kutitia. Aidha, matuta barabarani yamekuwa yakisababisha mizigo kuhama na kuelemea upande mmoja; jambo ambalo wakati mwingine limekuwa chanzo cha ajali kwa magari mengi ya mizigo. Pia, matuta husababisha myumbo wa matairi hivyo kuchochea ubovu na kuongeza uwezekano wa magari.

### **2.3.2 Barabara za Jiji la Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudí mbalimbali zinazofanywa katika kuhakikisha jiji la Dar es Salaam linakuwa halina msongamano mkubwa wa magari. Juhudi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa miundombini ya mabasi yaendayo kasi (BRT), kujenga barabara za juu (*flyovers*) katika eneo la TAZARA na maaandalizi ya ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) katika eneo la Ubungo pamoja na kukamilisha barabara nydingine za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam. Sehemu barabara hizo ni pamoja na Ardhi-Makongo- Goba, na Goba- Madale -Wazo Hill.

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kuwa Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari unaotokana na sababu mbalimbali zikiwemo ofisi nydingi za umma kujengwa sehemu moja na kusababisha wakazi wa jiji kuwa na uelekeo mmoja, ubovu wa barabara za mliso (*feeder roads*), utegemezi usafiri wa barabara kwa kiasi kikubwa, uduni wa huduma za usafiri wa umma na ongezeko kubwa la idadi ya magari ikilinganishwa na uwezo wa barabara.

Aidha, msongamano huu unaendelea kujitokeza katika majiji mengine kama vile Mwanza, Mbeya na Arusha, na sasa Manispaa Dodoma na sababu zikiwa ni ongezeko kubwa la idadi ya magari ikilinganishwa na uwezo wa barabara. Ni

lazima sasa kuweka mipango kabambe ya kuongeza barabara za michepuko katika majiji haya ili kuepusha na kupunguza msongamano kwani unaathari nyingi za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

### **2.3.3 Mizani za Barabarani**

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya majukumu ya TANROADS ni ujenzi na utunzaji wa barabara, kudhibiti uzito wa magari ili kuhakikisha barabara zinadumu kwa muda mrefu. Hata hivyo, pamoja na jukumu hilo bado changamoto imekuwa ni uharibifu wa barabara unaosababishwa na magari kubeba mizigo yenye uzito mkubwa. Kwa Mfano, magari mengi ya aina ya fuso kwa wastani yanatakiwa kubeba mizigo usiozidi tani 3.5, lakini mengi yanazidisha na kubeba mizigo hadi tani 8. Hali hii ni hatari sana kwani mara nyingi yamekuwa yakisababisha ajali pamoja na uharibifu wa barabara kwani matairi yake ni membamba ambapo huchimba barabara na kusababisha mabonde.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto ya magari yanayobeba mizigo kupita kiasi kinachostaili, mizani ndicho chombo muhimu sana katika udhibiti uzito wa magari ambayo husababisha uharibifu wa barabara. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza za udhibiti wa uzito wa magari na sasa kuna mizani 38 ya kudumu, mizani 22 zinazohamishika na mizani moja (1) inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo.

### **2.3.4 Ujenzi wa Viwanja vya Ndege Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa viwanja vya ndege nchini umeendelea kutekelezwa chini ya Sekta ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Kamati katika kutekeleza majukumu yake imebaini kuwa ujenzi wa viwanja vya ndege nchini umeendelea kwa kasi kubwa.

Aidha, Kamati imejulishwa kuwa, ushauri wa Kamati kuhakikisha kuwa viwanja vyote vinakuwa na Hati Miliki

umeanza kutekelezwa. Hata hivyo, kati ya viwanja hamsini na nane (58) vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- TAA, viwanja vilivyofanikiwa kupata Hati Miliki ni vinane (8) tu. Kamati imejulishwa kuwa viwanja vingine kumi (10) viko kwenye mpango wa kupata Hati Miliki mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kulikuwepo na changamoto ya kupatikana fedha kwa wakati kwa ajili ya ujenzi wa viwanja ndege nchini. Hata hivyo, Kamati imejulishwa kuwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege kwa sasa ni mzuri.

### **2.3.5 Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

#### **a) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa jengo la tatu la abiria (*terminal III*) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, mkataba ulisainiwa 18 Aprili, 2013.

Hadi kufikia Desemba, 2017; utekelezaji wa kazi ulifikia asilimia 68 ambapo kazi zinazoendelea ni kuezeka na kumalizia kazi za kusimika mitambo ya umeme, viyoyozi na utandazaji wa nyaya na mabomba.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Upatikanaji wa fedha; Kamati imejulishwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea kufwatilia taratibu za upatikanaji wa fedha za ndani; pamoja na kuangalia fedha za mkopo wa masharti nafuu;

ii. Changamoto nyingine ni Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa bidhaa. Kwa mujibu wa Mkataba vifaa vya ujenzi kwa ajili ya mradi huu vilisamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Hata hivyo, Sheria Mpya ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) ya Mwaka 2014 iliyoanza kutumika mwaka 2015 ilifuta msamaha wa Kodi ya VAT katika mradi huu.

**b) Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ndicho Kiwanja kikubwa cha Ndege kwa eneo la Kanda ya Ziwa. Kutokana na umuhimu wake; Serikali imekuwa ikikiendeleza Kiwanja hiki kwa kukipanua ili kiweze kukidhi mahitaji mengi ya sasa ya wakazi wa Kanda ya Ziwa na hatimae ndege kubwa za Kimataifa kutua. Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja hiki ulianza mnamo mwezi Oktoba 2012 na ulipangwa kukamilika Mwezi Septemba, 2014. Hata hivyo, hapo awali mradi huu ulikuwa ukikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati hivyo kusababisha kasi ya utekelezaji wa mradi kuwa ndogo.

**c) Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe Mkoani Mbeya ulianza mwaka 2000 ambapo ujenzi umekuwa ukitekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kiwanja hiki ni muhimu sana kwa wakazi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na hata wasafiri kutoka nchi jirani za Zambia na Malawi. Tangu Kiwanja hiki kilipofunguliwa rasmi mwaka 2012 kumekuwepo na ongezeko kubwa la abiria na ndege.

Hata hivyo, pamoja na umuhimu mkubwa wa Kiwanja hiki, mradi huu pia umekuwa ukitekelezwa kwa kasi ndogo jambo linalosababisha mradi kutokukamilika kwa wakati.

Aidha, pamoja na changamoto hizo katika ujenzi wa Kiwanja hiki, Kamati toka mwaka 2016 imekuwa ikishauri mara kwa mara umuhimu wa kuwekwa kwa taa za kuongozea ndege ambazo zitasaidia ndege kutua nyakati za usiku na hata mchana wakati wa ukungu mkubwa. Hali kadhalika, kuwekwa kwa uzio kuzunguka mipaka yote ya Kiwanja ili kuongeza usalama wa kiwanja na kuepuka uvamizi na wananchi wa maeneo jirani kukatiza katika maeneo ya Kiwanja.

**d) Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

**Mheshimiwa Spika**, Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kilianzishwa mwaka 1954. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha kuwa miundombinu ya Kiwanja hiki inaboreshw na kuweza kutoa huduma za kuridhisha.Ukarabati wa Kiwanja hiki unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 utekelezaji ulikuwa wa awamu ya pili ambapo linahusisha ujenzi wa jengo la abiria, mnara wa kuongezea ndege, ukarabati wa maegesho ya ndege na usimikaji wa taa za kuongozea ndege.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa mradi huu upo mingoni mwa miradi inayogharamiwa kwa Mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Kamati imejulishwa kuwa; ilikubaliwa kuwa kabla ya fedha za mkopo kuanza kutoka, Serikali iwe imeshalipa fidia kwa wananchi wote watakaothiriwa na ukarabati na upanuzi wa Kiwanja hiki. Baadhi ya wananchi wamekuwa na madai ya kupunjwa fedha za fidia na baadhi ya maeneo yao kurukwa katika zoezi la ulipaji fidia lililofanyika mwaka 2013. Hata hivyo, tathimini imefanyika upya na kuanisha mahitaji ya ziada ili kulipa madai hayo.

**2.4 Sekta ya Mawasiliano**

**2.4.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

**Mheshimiwa spika**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA ilianzishwa chini ya Sheria Na. 12 ya Mwaka 2003 ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania baada ya kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Utangazaji Tanzania na Tume ya Mawasiliano Tanzania-TCC. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni kusimamia Makampuni ya Mawasiliano nchini yakiwemo Makampuni yanayotoa huduma za Simu, Utangazaji, Intaneti, Posta na Usafirishaji wa Vifurushi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TCRA imeweka mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu, ambao umechangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni

zilizopo katika udhibiti wa mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha mabadiliko ya teknolojia ili kuongeza ubora wa huduma na kuendana na kasi ya mabadiliko yanayotokea.

Mfumo wa TTMS; pamoja na mambo mengine, mpaka kufikia Desemba 2017 umeweza kufanya yafuatayo:-

**a) Kuhakiki Mawasiliano ya Simu za Ndani**

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017; TCRA iliendelea kusimamia uendeshaji wa mfumo wa mawasiliano ya simu za ndani za kutoka mtandao mmoja kwenda mwagine (*local off-net traffic*) na kuwezesha kupatikana kwa takwimu za idadi ya dakika zilizotumika pamoja na idadi ya simu zilizopigwa.

Aidha, katika kipindi hiki TCRA iliendelea kusimamia uendeshaji wa mfumo wa mawasiliano ya simu za ndani (*local on-net traffic*) na kuiwezesha TCRA kujua idadi ya mawasiliano ya simu za ndani zilizopigwa pamoja na idadi ya dakika zilizotumiwa na wateja katika maongezi ya simu yaliyofanyika ndani ya mtandao mmoja.

**b) Mfumo wa Kubaini Simu za Ulaghai**

TCRA iliendelea na zoezi la kuzitambua na kuzifungia namba za simu ambazo zimekua zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia za ulaghai, na kusababishia Serikali pamoja na watoa huduma upotevu wa mapato. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 TCRA ilifanya zoezi la kuwatafuta wahalifu na ilifanikiwa kuwakamata wahalifu watatu wenye asili ya Somalia na kuwafikisha kwenye vyombo vya Sheria kwa kosa la kuingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia za udanganyifu.

**c) Mfumo wa kuhakiki Mapato yatokanayo na Huduma za Mawasiliano**

Hadi Decemba 2017, TCRA iliendelea na uboreshaji wa Mfumo wa TTMS kwa kufunga mfumo wa kuhakiki mapato yatokanayo na huduma zote za mawasiliano (sauti, data na jumbe fupi, miamala ya kifedha, pamoja na mapato yatokanayo na huduma za ziada zinazotolewa na watoa huduma hapa nchini. Kazi zifuatazo zilikuwa zimeshafanyika:

- a) Kusimikwa kwa vifaa kwa upande wa watoa huduma (Vodacom, Tigo, Airtel, Viettel, Zantel, Smile, Smart, TTCL na Simbanet ambavyo vinavyokusanya taarifa ya huduma za mawasiliano yanayofanyika;
- b) Kufungwa kwa vifaa vya kuchakata taarifa kutoka kwa watoa huduma katika kituo cha kusimamia Mfumo wa TRAs hapa TCRA;
- c) Kufungwa kwa Mfumo wa kuchakata taarifa (*data processing*) na kuonesha taarifa mbalimbali za matumizi (*dashboard*) na mapato ya Makampuni ya watoa huduma hapa TCRA; na
- d) Kusimikwa kwa mfumo wa kuonesha taarifa mbalimbali za mapato yatokanayo na huduma za Mawasiliano.

**d) Uhalifu katika Mitandao**

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia yamechangia kukuwa kwa Sekta ya Mawasiliano kwa kasi kubwa. Mabadiliko haya yamekuja na changamoto mbalimbali za usalama na uhalifu katika mitandao. Changamoto hizi ni pamoja na ulaghai, utapeli, wizi n.k. Kamati ilijulishwa kuwa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kudhibiti vitendo hivi kwa kujenga uwezo kwa watumishi wake; pamoja na kushirikiana kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama.

Aidha, katika kipindi cha 2017, TCRA iliratibu na kuwezesha mafunzo ya uchunguzi wa vifaa vya kieletroniki na mawasiliano (*Digital forensic Training*) kwa kuvishirikisha vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la uhalifu katika mitandao.

**e) Uanzishwaji wa Maabara ya Kisasa ya Kiuchuguzi ya Kidijitali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika kipindi cha Julai-Desemba, 2017; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, imeanzisha maabara ya kisasa ya kidijitali ya uchunguzi

(*digital forensic Lab*) pamoja na usimikaji wa vifaa na mifumo mbalimbali ili kusaidia kukabiliana na wimbi la makosa ya kimtandao na kurahisisha utendaji wa kazi.

**f) Kuweka viwango vypa vya mwingiliano baina ya Mitandao ya Simu Nchini**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekamilisha kazi ya kuchunguza na kubaini gharama halisi za muingiliano ya mitandao ya simu (*cost -based interconnection Rates*) baina ya mitandao ya simu nchini. Uchunguzi huo ulifanywa kwa kusaidiwa na mtaalamu mwelekezi (M/s Incyte Consulting) ambapo alipendekeza viwango vya muingiliano kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (mwaka 2018-2022) kama inavyooneshwa katika jedwali. Viwango hivyo vitatumika kwa muda wa miaka mitano kuanzia 1 Januari 2018 hadi 31 Desemba 2022.

*Jedwali lifuatalo linaonesha; Viwango vya muingiliano ya mitandao ya simu kwa Shilingi kwa Dakika*

Maeleo / Mwaka	2018	2019	2020	2021	2022
Gharama za mwingiliano wa simu za maneno kwa dakika kwa Shilingi ya Tanzania.	15.6	10.4	5.2	2.6	2.0

*Chanzo; Taarifa ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, 2018*

**2.4.2 Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta**

**Mheshimiwa spika**, mradi wa anuani za makazi ni muhimu sana kwani utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kuweza kufanyika kwa urahisi na kuokoa muda. Mionganoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na; huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto ,magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa inayoukabili mradi huu ni ujenzi holela na kutokuwa na maridhiano juu upatikanaji wa majina ya mitaa.

Vilevile, changamoto nyingine kutokuwa na fedha za kutosha, kutokuwapo kwa takwimu halisi za idadi ya barabara/mitaa katika kata, uharibifu wa miundombinu kama vile nguzo za majina ya mitaa na vibao vyana namba za nyumba hata sehemu zilizopangwa.

**Mheshimiwa spika**, Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa. Vile vile fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu zimekuwa hazitolewi kwa wakati. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga **shilingi bilioni 3 (3,000,000,000.00)**, kwa ajili ya uendelezaji wa mradi katika mji wa Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza na Mbeya. Hata hivyo, hadi kufika mwezi Decemba, 2017 Fedha hizo zilikuwa bado hazijatolewa.

#### **2.4.3 Shirika la Posta Tanzania**

**Mheshimiwa spika**, shirika hili linahitaji mtaji ili liweze kuijidesha kibiashara na kukabiliana na ushindani uliopo na changamoto ya soko katika sekta ya posta. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeendelea kufanya kazi changamoto ya Shirika hili ili liweze kuijidesha ikiwa ni pamoja na kulipa madeni mbalimbali. Aidha, shirika limeshatoa kiasi cha **shilingi billion 6.7** mpaka mwezi Disemba, 2017 kwa ajili ya kulipa *pension* za wastaafu wa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki kwa niaba ya Serikali kwa makubaliano ya kurejeshewa fedha hizo na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ushauri wa Kamati uliotolewa 2016/2017, Serikali imefanikisha yafuatayo:-

- i) Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kulipa deni la **shilingi billion 6.7** la wastaafu ambao ajira zao zilianzia kwa liliokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki. Hadi kufikia Novemba 2017, Serikali imeshalipa **shilingi billion 2.7**;

- ii) Wizara ya Fedha na Mipango inaangalia uwezekano wa kuweza kuliondoa Shirika hili kwenye Mashirika ya Umma yanayosubiri kurekebishwa ili liweza kuwa na sifa ya kupata mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha;
- iii) Shirika kuweza kutoa huduma ijlikanayo kama posta mlangoni kufikisha barua, nyaraka na vipeto hadi mteja alipo. Huduma hii imeanza kutolewa katika maeneo ambayo miundomninu ya postikodi imekamilika; maeneo hayo ni kama Arusha (kata 8), Dodoma( kata 8) na Dar es salaam (kata 32).

#### **2.4.4 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**Mheshimiwa spika**, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulianzishwa kwa lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Hata hivyo, kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu na muda ambao mfuko huu umekuwepo toka kuanzishwa kwake, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijijini. Kamati imebaini kuwa, moja ya sababu ya kuwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huu ni kwa kuwa Makampuni makubwa ya simu bado hayajahimizwa vya kutosha kupanua huduma zao katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara kama mojawapo ya uwajibikaji wao kwa jamii (*corporate social responsibility*).

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Oktoba, 2017; kamati ilipata nafasi ya kutembelea maeneo mbalimbali ili kujiona ikiwa huduma za mawasiliano zinapatikana kwa sehemu ambazo minara ilijengwa na makampuni ya simu kwa kutumia ruzuku kutoka Mfuko wa Mawasiliano. Katika ziara hiyo, ambayo Kamati ilitembelea takribani Mikoa 20 ya Tanzania Bara, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo;-

- a) Serikali za Mikoa, Wilaya pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; na kwamba, miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana

iliyoko maeneo mengi ni kuwa minara inajengwa na Makampuni ya ya simu yenye; hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki kabisa;

b) Pamoja na kuwa Makampuni yamepewa masharti ya kuwajibika katika kutoa huduma za jamii; katika maeneo yanayofanya shughuli zake za kibashara, kwa kiasi kikubwa Makampuni haya yamekuwa hayatoi huduma hizi;

c) Ujenzi wa minara kwa kutumia Kampuni ya TTCL ulikuwa ukisuasua kwa siku za nyuma, hata hivyo baada ya Kamati kufanya ziara ya ukaguzi wa minara mwaka jana; TTCL imekamilisha miradi yake yote iliyokuwa inadaiwa na UCSAF;

d) Migogoro ya ardhi; Katika maeneo mengi ambayo Kamati imetembelea minara yamebainika wazi kuwa na migogoro dhidi ya umiliki wa eneo husika.

e) Wizi wa vifaa vya minara kama vile mafuta, betri na nyaya aina ya “fiber”;

f) Minara mingi iliyojengwa inatumia umeme wa jua (*solar power*), hii inasababisha nyakati za usiku hasa wakati kipindi cha mvua maeneo mengi kuwa na mawasiliano hafifu kwa sababu jua haliwaki kipidi kirefu;

g) Makampuni yanajenga minara pasipo kuweka huduma za kijamii kama choo, kibanda cha mlinzi na huduma zingine za msingi kwenye maeneo la mnara.

#### **2.4.5 Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano-TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika** Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ilianzishwa kwa amri ya Rais kupitia tangazo la Serikali na 532 la mwezi Novemba 2015. Majukumu yake kukuza TEHAMA, kukuza uwekezaji katika maeneo ya kimkakati ya uzalishaji wa bidhaa za TEHAMA nchini, kufanya utafiti na kushauri masuala ya TEHAMA. Majukumu mengine ni uendelezaji wa miundombinu nchini; pamoja na kukuza na kuvutia uwekezaji kwenye sekta ya TEHAMA, ili

kutengeneza ajira na kuweza kuchangia katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Kamati imejulishwa kwamba katika Afrika Mashariki; Tanzania ndio nchi iliyochelewa kuwa na taasisi ya TEHAMA. Nchi za Afrika Mashariki zimekuwa na taasisi za TEHAMA tangu mwaka 2006-2008. Kamati imejulishwa kuwa nchi kama Kenya imeshafikia mahali wanaendesha kilimo kwa TEHAMA. Kamati imebaini kuwa, ikiwa Serikali itaweka mkazo kwenye sekta hii tunaweza kupiga hatua haraka katika kuwaletea maendela wananchi wa Tanzania.

## **SEHEMU YA TATU**

### **2.0 MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI**

#### **2.1 Bajeti ya Miundombinu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza miundombinu nchini ambapo katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018; Serikali iliendelea kuongeza tengeo la fedha katika sekta ya Miundombinu hadi kufikia jumla ya shilingi **shilingi trilioni 4.5 (4,516,885,061,000)**. Hii inaonesha kwa kiasi kikubwa Serikali imezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo katika nchi yetu kwani miundombinu ndio itawezesha tija na utendaji bora wa sekta zingine. Hata hivyo, pamoja na shabaha nzuri ya Serikali katika masuala ya miundombinu, Kamati inasilitiza fedha kutolewa kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka limbikizo la madeni.

#### **2.2 Sekta ya Uchukuzi**

##### **2.2.1 Mamlaka ya Bandari Tanzania**

**Mheshimiwa Spika, kwa Kuwa**, Mamlaka ya Bandari Tanzania ndio Mamlaka iliyokasimwa jukumu la kusimamia bandari nchini;

**Na kwa Kuwa**, Mamlaka hii inayo miradi minge ya ujenzi na ukarabati wa bandari ambapo kwa sasa Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua ya kuboresha kwa kufanya ukarabati bandari kama vile Mtwara na ujenzi wa magati pamoja na uchimbaji wa kina katika Bandari ya Dar es Salaam;

**Kwa hiyo Basi**, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

- a) Asilimia ishirini (20%) ya mapato ya bandari yabaki bandarini ili kuwezesha Mamlaka ya Bandari Tanzania iweze kutekeleza baadhi ya miradi kama vile miradi ya ujenzi wa bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara ambayo inaghariimu takribani **shilingi bilioni 20** wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni **shilingi bilioni 270**;
- b) Wafanyakazi wapewe nafasi ya kwenda kujifunza katika Bandari zingine zinazofanya vizuri ili kuweza kufahamu wenzao wanachokifanya na hatimae kuweza kubaini mbinu za ushindani na bandari zingine katika biashara;
- c) Kuendelea kushughulikia changamoto zingine zinazoikabili Mamlaka ya Bandari, ili Bandari iweze kufanya vizuri zaidi na kuweza kushindana na nchi zingine shindani;
- d) Kuharakisha mchakato wa ununuzi wa *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Kamati ilitembelea bandari na kuona tatizo la kutokuwepo na *flow meter*, na hivyo kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam. Ni rai ya Kamati kuwa "*flow meter*" inunuliwe kwa haraka. Hivi tunavyoongea sasa tatizo hili bado halijashughulikiwa; na
- e) Kuunganisha zabuni za ujenzi wa bandari ya Kigoma ili kuweza kupata mzabuni mwenye uwezo atakayefanya kazi hiyo; kwani imekuwa ikitangazwa mara kadhaa bila kupata mzabuni kutokana na gharama ya maandalizi (*mobilization*) ya miundombinu.

## 2.2.2 Ujenzi wa reli nchini

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, Serikali imeonesha nia ya dhati ya kujenga upya Reli ya Kati katika kiwango cha kisasa (*standard gauge*); ambapo mradi huu umeshaanza tangu mwezi April, 2017 na unatekelezwa kwa awamu tano;

**Na kwa Kuwa**, katika uhalisia Tawi la kutoka Tabora- Kigoma-Uvinza- Msongati na Kaliua-Mpanda-Kalema ndilo lenye mizigo mingi inayotoka na kwenda nchi za jirani kama vile DR Congo, Burundi na Rwanda;

**Kwa hiyo Basi**, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

a) Reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika tawi la Tabora – kigoma - Uvinza- Msongati; Kaliua – Mpanda –Kalema; na Tabora-Mwanza;

b) Kuwapeleka kwenye mafunzo zaidi wataalam ili kuweza kuhudumia miundombinu ya treni za kisasa inayoendelea kujengwai;

## 2.2.3 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, kumekuwa na migogoro mingi ya uvamizi wa maeneo ya viwanja vya ndege;

**Na kwa kuwa**, utatuzi wa migogoro hiyo umekuwa ukiigharimu Serikali fedha nyingi kulipa fidia na kuchelewesha baadhi ya miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege;

**Kwa Hiyo Basi**; Kamati inaishauri Serikali,

a) Kuhakikisha inapata hati za Viwanja vya Ndege kwani Kamati imejulishwa ni kuwa viwanja vya ndege vinane (8) vimeshapatiwa hati miliki kati ya viwanja hamsini na nane (58) vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, bado kuna haja ya kuhakikisha kuwa viwanja vingine vilivyobakia vinapimwa na kupatiwa hati miliki pamoja na

kuwekwa uzio ili ili kujiepusha na uvamizi wa maeneo jambo ambalo huleta migogoro na wananchi na kusababisha Serikali kuingia gharama kubwa kwa ajili ya fidia;

- b) Aidha, kuongeza udhibiti na ulinzi katika Viwanja vya Ndege vilivyopo Mikano hasa vilivyopo mpakani kama vile Mtwara, Kigoma na Kagera ili kuepuka viwanja hivi kupitishwa biashara haramu;
- c) Ili kuepuka ongezeko la gharama za ujenzi; ni vyema Serikali ikakamilisha miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege vilivyoanza vikiwemo; Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (Terminal III), Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na Kiwanja cha Ndege cha Songwe; na
- d) Kuharakisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa viwanja vya ndege kama kama vile Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (Terminal III) Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na Kiwanja cha Ndege cha Songwe.

## **2.2.4      Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL**

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, Serikali imeonesha nia ya dhati ya kufufua Kampuni ya Ndege ya Tanzania;

**Na kwa kuwa**, biashara ya ndege inahitaji mikakati mikubwa ya kibiashara ili kuweza kuingia katika soko la ushindani;

**Kwa hiyo Basi**, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:

- a) Kuwa na mikakati ya kitaifa ya kuhakikisha kuwa ATCL inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida;
- b) TCL iangaliwe kama Kampuni ya kibiashara na sio kutoa huduma; na
- c) ATCL ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi

mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi.

### **2.3 Sekta ya Ujenzi**

#### **2.3.1 Wakala wa Barabara Tanzania-TANROAD**

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa,** Wakala wa Barabara nchini-TANROADS ndio wamekabidhiwa jukumu la ujenzi na ukarabati wa barabara kuu nchini;

**Na kwa Kuwa,** pamoja na jitihada za Serikali kujenga barabara; bado maeneo mengi nchini barabara zake hazipitiki hasa wakati wa masika;

**Kwa hiyo Basi,** Kamati inaishauri Serikali yafutayo:-

- a) Kuhakikisha inaunganisha Miji yote Mikuu na Mikoa iliyosalia kama vile Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera na Njombe-Makete-Mbeya kwa barabara za lami ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo hayo;
- b) Kukarabati baadhi ya barabara za Mikoa zilizo katika hali isiyordhisha na kutopitika hasa wakati wa mvua na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii;
- c) Wizara ya Ujenzi isimamie Sheria za barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vyaya habari kama runinga, magazeti na redio. Pia kufanya mikutano na kuweka alama zitakazoonesha mwisho wa eneo la barabara;
- d) Kuendelea na ujenzi wa barabara za lami hasa maeneo yanaaochochea Uchumi wa Taifa letu kama vile maeneo yenye vivutio vyaya utalii, kilimo na viwanda na madini;
- e) Matuta madogo madogo ya barabarani maarufu kwa jina la rasta na matuta makubwa yasiyo na kiwango yaondolewe kwa kuwa zinasababisha ajali na uharibifu wa magari. Aidha matuta yabaki sehemu zenye umuhimu tu na yawe na kiwango maalumu;

- f) Kamati imekuwa ikishauri na inaendelea kushauri kwamba ili kuilinda miundombinu yetu hasa alama za barabara na reli; upo umuhimu mkubwa wa kutungwa kwa Sheria ya kudhibiti uuzaaji wa chuma chakavu ili kunusuru miundombinu yetu iliyogharimu fedha nyingi na kwa usalama wa watumiaji wa barabara zetu; na
- g) Kununua mizani ya kisasa ambazo zinauwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weight in Motion*). Kamati inaendelea kushauri mizani hizi za kisasa zifungwe pia katika maeneo mengine yanye kusababisha msongamano mkubwa wa kupima magari Mfano, Himo-Moshi, Mizani ya Mikese- Morogoro, Kihonda-Morogoro, Makambako kwa mpemba n.k.

### **2.3.2 Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, Wakala wa Barabara Tanzania umepewa jukumu la ujenzi wa Viwanja vya Ndege nchini;

**Na kwa kuwa**, bado kuna changamoto kubwa ya uboreshaji na ujenzi wa viwanja vya ndege;

**Kwa hiyo Basi**, Kamati inashauri Serikali yafuatayo;-

- a) Kuhakikisha inamaliza kwa wakati malipo ya fedha yaliyoidhinishwa ya kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha ndege cha Mwanza, Songwe na Mtwara. Vile vile, kuweza kulipa fidia kwa viwanja vya ndege vya Julius Nyerere International Airport- JNIA, Mwanza, Bukoba, Msalato, Kigoma, Shinyanga, Songwe, Sumbawanga, n.k; na
- b) Kuharakisha kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la tatu (*Terminal III*) la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika. Aidha, Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi; na

c) Kuhakikisha viwanja vya ndege vinawekewa uzio kwani viwanja vingi havina uzio jambo linalohatarisha usalama.

### **2.3.3 Kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, Serikali imeonesha nia ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam kwa kuweka barabara za juu (*flyovers*) eneo la TAZARA na Ubungo na kwa kujenga barabara za michepuko;

**Na kwa kuwa**, msongamano katika jiji la Dar es Salaam umekuwa ukisababisha adha kubwa;

**Kwa hiyo Basi**, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

a) Barabara za juu maarufu kama (*flyovers*) zijengwe hasa katika makutano ya barabara kuu zenyne msongamano mkubwa kama vile, Magomeni, Morocco, Mwenge. Wadau kama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweza kushirikishwa kwa kujenga barabara za kulipia.

b) Kukamilisha ujenzi wa barabara zinazosaidia wananchi kufika maeneo yao bila kupita katikati ya Jiji la Dar es salaam, ikiwa ni pamoja kukamilisha barabara kutoka Goba-Madale-WazoHill, Goba -Kimara, Ardhi-Makongo-Goba n.k. Pia barabara za mitaani (*ring roads*) nazo zifunguliwe kwa kuwekwa lami kwani zitapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa;na

### **2.4 Sekta ya Mawasiliano**

#### **2.4.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA**

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kusimamia mawasiliano nchini;

**Na kwa Kuwa**, kumekuwepo changamoto mbalimbali zinazotokana na ukuaji wa teknolojia;

**Kwa Hiyo Basi**, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:

- a) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kuititia njia ya mtandao na ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao; na
- b) Kuendelea kukabiliana na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake kama vile uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kuisaidia Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya *Cyber Crime* na kuwabana wahalifu; na
- c) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya simu za ndani kwa kutumia mtambo wa *TTMS* ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kuititia simu za mkononi. Kuendelea kuchelewa kulitekeleza suala hili kunazidi kuikosesha nchi kodi stahiki kutokana na Makampuni haya kutotozwa kodi stahiki;

#### **2.4.2 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF**

**Mheshimiwa Spika, kwa Kuwa**, mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kupeleka mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara;

**Na kwa Kuwa**, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu hizo;

**Kwa Hiyo Basi**, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

- a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA kuweka masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti

mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (*Corporate Social Responsibility*);

b) Kuweka mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakani ambapo mara nydingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki ya kukosa taarifa za nchi yao;

c) Kuhakikisha Makampuni ya simu yanatoa kiwango kilichopangwa cha 0.9% kama tozo za huduma (*services Levy Rate*) ilikuongeza uwezo wa kifedha kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kumaliza shida ya mawasiliano vijiji;

d) Katika maeneo ambayo vijiji vimetoa ardhi bure kwa ajili ya ujenzi wa minara; basi Kampuni husika ichangie/ itoe ruzuku kwa kijiji husika kila mwaka;

e) Mahakama na vyombo vingine viambata kama vile jeshi la Polisi, kwenye watoe kipaumbele na kuharakisha kutoa haki kwenye masuala ambayo yanagusa umma moja kwa moja, kutoa haki kwani ucheleweshwaji wa kesi hasa zinazohusu ujenzi wa minara ya simu, unachelewesha maendeleo katika maeneo husika;

f) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuhakikisha Makampuni ya simu yanapopewa fedha na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa minara yanafanya kazi hiyo katika muda uliopangwa na kwa kiwango kizuri kinachotarajiwa;

g) Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano kwa haraka;

h) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi watoe ushirikiano wa ulinzi ili vifaa vyya minara view salama; na

- i) Kuongeza rasilimali watu kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili Mfuko uweze kusimamia ipasavyo kwa kukagua na kutembelea maeneo ambayo Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa minara na kuhakikisha kazi hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama iliyokusudiwa; na
- j) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ufanye kazi kwa kushirikiana kwa karibu na Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili waweze kufahamu miradi ujenzi wa minara inayofadhiliwa na Serikali inayojengwa katika maeneo yao.

#### **2.4.3 Mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta**

**Mheshimiwa Spika, kwa Kuwa,** mradi huu unamanufaa makubwa kwani utawezesha kuwepo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimae kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa;

**Na kwa Kuwa,** utekelezaji wa mradi huu umekuwa ukisuasua;

**Kwa Hiyo Basi,** Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

- a) Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa; na
- b) Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kama zilivyoidhinishwa na kwa wakati ili mradi huu ukamilike.

#### **SEHEMU YA NNE**

#### **3.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusitiza kuwa, ili Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Idara zake zote ziendelee kufanikiwa ni lazima uteuzi na ajira za watendaji zifuate ueledi jambo ambalo Kamati inaamini limezingatiwa.

Pili, watendaji wa Taasisi hizo na Bodi wasiingiliwe na watunga Sera bali wapimwe kwa uzalishaji wao.

Tatu, sheria na taratibu zinazowekwa kwenye taasisi zinazofanya biashara zifasili malengo mama ya taasisi hizo; kama ni sheria au taratibu swali liwe uwepo wa sheria au taratibu hizo zinasaidia kuongeza ufanisi na faida katika taasisi hizo?

**Mheshimiwa Spika**, hili likizingatiwa tutakuwa na nafasi ya kuwahukumu watendaji na bodi kwa haki.

### 3.1 Shukrani

**Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Prof. Makame Mbarawa Mnyaa (Mb) akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mhe.Eng. Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias Kwandikwa, (Mb). Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph Nyamuhanga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Angelina Madete. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalam wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson M. Bisile, Makatibu wa Kamati Ndg. Hosiana John na Ndg. Richard Masuke. Vilevile, nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

### 3.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa na Kamati, Maoni na Ushauri, sasa naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018 pamoja na Maoni na Ushauri katika Taarifa hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb  
**Mwenyekiti**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**  
05 Februari, 2018

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, nilikuwa naangalia ni wangapi wamesimama nisije nikasema imeungwa mkono kabla haijaungwa. Ahsante sana Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea; sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, Mbunge wa Ludewa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika kipindi cha mwezi Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda kuwa mfupi sintaweza kusoma taarifa yote, hivyo naomba taarifa yote pamoja na sehemu ambazo sitazisoma iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2017 Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanuni, kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake kikanuni, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kupokea na kujadili taarifa mbalimbali kwa Wizara pamoja na taasisi zake na kupata mafunzo na semina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kikanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelizwa na Wizara ya Nishati na Madini. Ziara hizo zillifanyika katika Mikoa wa Dar es Salaam, Tanga na Geita kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati na Madini iliyotengewa fedha na kupelekwa fedha kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017. Miradi iliyokaguliwa na kamati yako kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini changamoto kadhaa zinazochangia kuzolota kwa utekezaji wa miradi katika maeneo mbalimbali hasa yaliyokaguliwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ilibainika kuwa katika ukaguzi wa miradi yote ni ukosefu wa fedha za miradi ya maendeleo. Kielelezo namba moja na namba mbili vinatoa ufanuzi kuhusu mchanuo wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, zilizoidhinishwa kwa mwaka husika pamoja na ufanuzi wa upatikanaji huo kwa asilimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya sekta ya madini iliyokaguliwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Dhahabu wa *Buckreef*, Kamati ilibaini kwamba licha ya leseni zote za uchimbaji wa utafiti kukabidhiwa kwa kampuni ta *TANZAM* hakuna kazi yoyote iliyokwishafanyika katika kuendeleza mgodi huo tangu kampuni hiyo ingie mkataba na *STAMICO*. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini inapoingia ubia katika miradi ya sekta ya madini ili kuepuka wabia wa aina hii ambao hawazingatii ushauri wa mbia mwenza (*STAMICO*) jambo linalosababisha hasara zisizo na msingi.

Mheshimiwa Spika, Migodi ya Wachimbaji Wadogo Waliopata Ruzuku ya Serikali, Geita (*Blue Reef Mining* na *Mgusu Mining*). Katika Mkoa wa Geita jumla ya wachimbaji wadogo saba wamenufaika na ruzuku ya Serikali vikiwemo vikundi vyta wajasiriamali wanaoshughulika katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Katika ziara ya ukaguzi wa migodi ya wachimbaji wadogo waliopata ruzuku Kamati ilridhishwa na utendaji wa wachimbaji wadogo watatu tu kati ya saba waliopata ruzuku ambao wameendeleza shughuli zao za uchimbaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo kwa baadhi ya wanufaika Kamati ilibaini changamoto kubwa ya usimamizi wa fedha usioridhisha kwa wachimbaji wadogo. Aidha, wanufaika hao wa ruzuku kwa namna moja ama nyingine hawakutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, migodi ya wachimbaji wa kati (*Busolwa Mining na Nyarugusu Processing Plant*). Mgodi wa *Busolwa Mining* ni mgodi unaomilikiwa na Mtanzania (mzawa) kwa asilimia 100 na Kamati ilijionea jinsi inavyoendesha shughuli zake kwa kutekelezasheria na kanuni mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zote za Serikali. Tangu mgodi huo uanze mwaka 2014 umeshalipa kodi kiasi cha shilingi bilioni 120; mrabaha bilioni 562; kodi ya zuio la mwaka 2017 shilingi bilioni 20 na *service levy* shilingi bilioni 48. Pamoja na mgodi huo kuendesha shughuli zake kwa ufanisi Kamati ilibaini kwamba unakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa eneo hasa la kutupia mabaki yatokanayo na

shughuli za mgodi (*TSF*). Ni mapendekezo ya Kamati kuwa maombi ya mgodi huo kupatiwa eneo lingine yashughulikiwe mapema ili kusaidia kuongeza uhai wa mgodi huo ambaao umeajiri zaidi ya Watanzania 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya madini; sekta ya vito ya *Tanzanite*. Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Spika kwa hatua yake ya kuunda Kamati Maalum iliyoshughulikia masuala ya uchimbaji, usimamizi, na biashara ya madini ya *Tanzanite* na kubaini changamoto nyingine mbalimbali hususan katika usimamizi wa biashara kwa ujumla. Mkataba wa ubia katika ya *Tanzanite One, Tanzania Limited* na Serikali, kupitia Shirika la Madini nchini (*STAMICO*), haukutoa fursa kwa Serikali kupata faida, kutokana na kuwepo kwa vipengele kadhaa kandamizi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilioongozw na Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuamua kujenga ukuta kuzunguka eneo la mgodi ili kuongeza udhibiti wa biashara ya *Tanzanite* na kupunguza utoroshwaji wa madini hayo ambaao ulikuwa ni changamoto kubwa katika kudhibiti mauzo. Aidha, Kamati inaunga mkono jitihada zinazoendelea za kushughulikia kwa kina mkataba huo baina ya *TML* na *STAMICO* kwa kutumia sheria mpya za rasilimali ambazo zinaruhusu kurejea makubaliano hasi katika mikataba ya ubia ili Taifa liweze kunufaika na madini haya ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya madini nchini imeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi hasa katika suala ukusanywaji wa kodi za Serikali. Sekta hii imekuwa ikichangia asilimia nne tu katika pato la Taifa, mchango ambaao ni kidogo sana ikilinganishwa na ongezeko la uzalishaji katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inamiliki mgodi mmoja tuu kwa asilimia mia moja ambayo ni Mgodi wa *Stamigold* kupitia Shirika la *STAMICO*. Mgodi huu licha ya

kuajiri Watanzania zaidi 700 bado kumekuwa na jitihada ndogo za Serikali katika kuusaidia katika masuala ya msingi kwa lengo la kuundeleza. Baadhi ya masuala hayo ya msingi ni pamoja na kama ilivyoorodhwa hapo chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Magufuli kwa maamuzi ya kuigawanya Wizara ya Nishati na Madini na kuwa Wizara mbili tofauti. Hii itachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa Wizara. Aidha, Kamati inaipongeza Wizara ya Madini kwa kasi walioanza nayo katika utatuzi wa changamoto mbalimbali ikiwemo hii ya uzalishaji wa madini ya dhahabu pamoja na malalamiko mbalimbali ya wananchi wanaozunguka maeneo ya migodi katika ulipwaji wa fidia. Pia Kamati inaipongeza Serikali na Bunge kwa ujumla kwa kufanya mabadiliko katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo yanaanzisha kamisheni mpya itakayosimiwa na kuratibu sekta ya madini kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya gesi, Kamati haikuridhirishwa na mahusiano ya ubia wa kuendeleza miradi ya gesi asilia inayotekewa na *TPDC*, *Pan Africa Energy*, *Songas*, pamoja na *TANESCO*. Kamati iliona kuna haja ya Bunge kuingilia kati ya kupata vyema ufanuzi wa ziada ili kuweza kuishauri Serikali juu ya mikataba na mahusiano baina ya wabia hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Spika binafsi kwa kuunda Kamati Maalum ambayo imeshughulikia masuala ya maendeleo na matumizi ya sekta hii ya gesi asilia nchini na namna ambavyo matumizi ya gesi asilia yatasaidia kuongeza mapato katika nchi yetu kuititia Kamati hiyo Bunge litaweza kuwa na uelewa wa kiwango cha juu na kupata namna bora zaidi ya kuishauri Serikali katika sekta hii ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha

2016/2017 kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukaguzi wa miradi Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Madini haukuwa wa kuridhisha kwa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazikuwasilishwa kwa wakati, na miradi mingine haikupelekewa fedha kabisa. Miradi mingi ya *REA* katika awamu ya pili haikukamilika kutokana na kasoro mbalimbali kama vile uainishaji wa maeneo bila kuzingatia vijiji na vitongoji ambavyo tayari vina wananchi wengi na ufungaji wa mashine umba (*transformer*) nydingi kutokizi mahitaji ya eneo husika.

Mheshimiwa Nabu Spika, Serikali iangalie upya namna bora ya kuwasaidia wachimbaji wa kati kwa kuwapatia maeneo ya kutosha kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza sekta ya madini. Ruzuku iliyotolewa na Serikali kuititia Wizara ya Nishati na Madini kwa wachimbaji wadogo wadogo haikusimamiwa vizuri na hivyo kushindwa kuleta tija kwa wananchi waliokusudiwa. Aidha, Serikali inapaswa kutoa elimu ya kutosha kwa wachimbaji juu ya ruzuku wanazopokea kutoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango mizuri ya *TPDC* katika kuendeleza sekta ya gesi asilia nchini, ni lazima Serikali iwekeze fedha za kutosha katika miradi ya gesi ili kuharakisha azma ya nchi yetu kuingia katika uchumi wa viwanda na Serikali itenye fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimkakati kama vile Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira, ambao mpaka sasa hakuna shughuli zozote za uendelezaji wa mgodi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara za mafunzo na semina kwa wajumbe wa Kamati ni kama ilivyoonyeshwa katika jedwali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi mahsusini zilizotekelizwa na Kamati ni kuwa Kamati ya Nishati na Madini katika kipindi cha mwaka mzima imetekeliza majukumu kama inavyoonesha kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ujumla. Ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha nusu mwaka cha Julai hadi Desemba 2017. Katika mwaka 2017/2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilitengewa jumla ya bilioni 998.34. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 222.53, sawa na asilimia 44.58 ya lengo la bajeti ya nusu mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 499.17. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 198.66 ni za miradi ya maendeleo, na sawa na asilimia 42.33 ya lengo la fedha ya maendeleo kwa kipindi hicho cha nusu mwaka ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 469.32 na shilingi bilioni 11.74 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (*OC*) ambayo ni sawa na asilimia 81.44 ya lengo la nusu mwaka ambalo ilikuwa ni shilingi bilioni 14.74.

Katika fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 21.78 zilikuwa kwa ajili ya sekta ya madini ambapo shilingi bilioni 14.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 7.83 ni kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Nishati na Madini; ili kubaini utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo Kamati ilipokea taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini zilizohusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo pamoja na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini. Aidha, taasisi zifuatazo ziliwasilisha taarifa kwenye Kamati na kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa Wakala huu. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zilivyoainishwa katika jedwali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudini na hatua mbalimbali zilizochukua na inazoendelea kuchukua kusambaza umeme vijijiini. Aidha, Kamati inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kushirikiana na Serikali katika maeneo ambayo bado yanahitaji maboresho katika utekelezaji wa miradi hii ya *REA* Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*); Kamati ilipokea na kujadili taatifa ya utekelezaji wa hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia Desemba, 2017 Kutoka Shirika la Umeme *TANESCO* ambalo linatekeleza majukumu ya kuzalisha, kufua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme nchini. Pamoja na *TANESCO* kudai kiasi cha fedha katika kipindi hicho cha kufikia Desemba 2017, *TANESCO* ilikuwa inadaiwa na wazabuni kiasi cha shilingi bilioni 913. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini changamoto zilizonesha katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uande wa Kampuni ya Uendelezaji wa Joto Ardhi nchini (*TGDC*); katika mwaka 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 36.7 zilitengwa na Serikali kwa ajili ya kampuni ya *TGC* kwa ajili ya miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo. Hadi Desemba 2017 Kampuni ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 1.35 sawa na asilimia 44.78 ya fedha zilizotengwa kwa kipindi cha nusu mwaka. Aidha, ni vyema kuzingatia kwamba fedha zote za ndani zinatoka kampuni mama *TANESCO*. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na *TGDC* katika kuendeleza nishati hii ya joto ardhi bado zipo changamoto kadhaa kama zilivyooneshwa katika jeswali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*); katika kipindi hiki cha nusu mwaka Julai/Desemba 2017 *TPDC* imewenza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 161.41 sawa na asilimia 55 ya malengo ya nusu mwaka ya kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 295.47 fedha zilizotenga kukutumika katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 ni shilingi bilioni 3.1. Hadi kufikia Desemba 2017 shilingi bilioni 2.1 sawa na asilimia 67 ya lengo zilitumika katika kutekeleza

miradi mbalimbali ya maendeleo. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na shirika hili katika ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vingine bado inakabiliwa na changamoto kama zilivyoainshwa katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Madini; kwa mwaka fedha 2017/2018 chuo hakikutengewa fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo, hata hivyo, miradi ya maendeleo ya chuo hiki imetelezwa kuitia vyanzo vingine vya fedha wakiwemo wabia wa maendeleo. Pamoja na mafanikio mbalimbali ambayo Kamati ilielezwa changamoto kubwa ni kama zilivyoainshwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala wa Jiologia Nchini; hadi kufikia Desemba 2017 Wakala ulikuwa umepokea jumla ya shilingi milioni 642.57 sawa na asilimia 27.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Wakala ulikuwa umepokea shilingi bilioni 2.53 kwa ajili ya utekelezaji wa utafiti kwenye Mradi wa *SMMRP*, hata hivyo, licha ya majukumu hayo mazito aliyonayo *GST* changamoto ni kama zilivyoainshwa hapo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Madini la Taifa; kuanzia mwezi Julai hadi Desemba 2017 Shirika lilikuwa limepokea shilingi bilioni 1.66 sawa na asilimia 12 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kipindi cha nusu mwaka 2017/2018. Shilirika limekwama kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu ya msingi ya kuendeleza sekta ya madini kutokana na changamoto kama zilivyoainshwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta ndogo ya mafuta na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini; pamoja na mafanikio ya Serikali ya kuanzisha Wakala wa Uingizaji Mafuta kwa Pamoja Nchini sekta hii bado inakabiliwa na changamoto kama zilivyoainshwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya upatikanaji wa umeme nchini; ili kufikia azma ya nchi yetu kujenga uchumi

wa viwanda ni lazima miradi mingi ya umeme ipelekewe fedha kama ilivyopangwa, sambamba na miradi ya *REA* inayotekelawa nchi nzima. Aidha ukarabati wa matengenezo wa mitambo ya kufua umeme ni jambo muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na mchakato wa bajeti wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 miradi mingi haikuweza kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha za kuendeleza miradi. Ni ushauri wa Kamati kwamba bajeti iliyotengwa ya miradi ya maendeleo itolewe yote na kwa wakati, na kuwe na usimamizi mzuri wa fedha hizo ili ziweze kuleta tija. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kufanya maoni kufanya kazi maoni na ushauri wa kamati kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya taarifa hii ni maoni na mapendekezo na nianze na maoni ya Kamati. Baada ya kupokea taarifa mbalimbali ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini ziara za ukaguzi wa miradi pamoja na kukutana na wadau wa sekta zote mbili za nishati na madini Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Fedha za miradi ya maendeleo zinapaswa kuwasilishwa kwa wakati kwani kutopatikana kwake kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

(ii) Serikali iendelee kutafuta na kubuni vyanzo vingine mbalimbali nya mapato.

(iii) Serikali itekeleze kwa ukamilifu miradi mipy ya usafirishaji na usambazaji umeme na kupanua gridi kwenye maeneo ambayo hayajaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

(iv) Serikali iimarishe doria katika njia za umeme pamoja na kuhamasisha wananchi kushiriki ulinzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.

(v) Serikali iwekeze katika vyanzo vingine vyatuzishati nishati mbadala. Aidha, kuwekeza zaidi katika nishati jadidifu ambayo uzalishaji wake ni nafuu na rafiki kwa utunzaji wa mazingira kutasaidia kuongeza nishati ya umeme.

(vi) Serikali inapaswa kupunguza tozo nyingi za taasisi kwenye bei ya Mafuta ili kumpunguzia mizigo mwananchi/ mtumiaji.

(vii) Serikali kuwekeza katika uvumbuzi wa teknolojia ya hali ya juu ili kuweza kushindana na nishati mbadala, kama vile nishati jadidifu (*renewable energy*) na hata miradi ya *LNG* kwa nchi nyingine kama Msambiji ni tishio kwa biashara ya gesi na mafuta kwa siku za usoni. Hivyo basi, Serikali inapaswa kuwekeza miradi ya gesi asilia mapema iwezekanavyo.

(viii) Fedha za miradi ya *REA* zinapaswa kuwasilishwa kwa wakati ili kuepuka ongezeko la gharama kutokana na ucheleweshaji au ukamilishaji wa miradi hiyo.

(ix) Miradi ya *REA* Awamu ya *Tatu hasa* miradi ya *densification* izingatie utekelezaji wa maeneo yaliyorkwa katika awamu ya kwanza na awamu ya pili ya utekelezaji wa miradi ya *REA*.

(x) Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (*TPDC*) liwezeshe kupata pesa za kuijendesha na sio kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu ambazo huchelewa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uendelezaji wa gesi asilia. Aidha, Serikali iangalie namna itavyoweza kutatua changamoto ya madeni ya taasisi zake katika shirika hili.

(xi) Serikali iangalie namna ya kulikwamua Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) pamoja na migodi inayosimamiwa na shirika hili ili shirika liweze kusimama na kuijendesha kibiashara.

(xii) Serikali iweke utaratibu mzuri wa ufungaji wa *flow meters* ili iweze kupata takwimu sahihi wakati wa upakuaji wa mafuta.

(xiii) Wakala wa Jiolojia nchini iendelee kufanya utafiti ambao una tija na kuwafikia wananchi hasa elimu za utafiti wa maafa na majanga.

(xiv) Serikali iangalie namna ya kuiwezesha Wakala wa Jiolojia nchini kua ndio mtafiti pekee wa masuala ya madini na kuweza kutoa takwimu zitakazohifadhiwa kwa manufaa ya taifa. Hatua hiyo itapunguza watafiti wengine wa nje ya nchi kuja kufanya utafiti kwa muda mrefu bila kutoa takwimu na kuharibu maeneo ya nchi kwa shughuli za uchimbaji. (*Makofii*)

(xv) Wachimbaji wa kati na wadogo wadogo wapewe kipaumbele na Serikali ili waweze kuendeleza sekta ya madini kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

(xvii) Serikali ilisaidie Shirika la *TANESCO* kujikwamua na madeni mengi ambayo yanalifanya lishindwe kuijendesha.

(xviii) Bunge lipewe Bajeti ya kutosha ili kuliwezesha kutekeleza makujuku yake ya kikatiba na kikanuni, hasa kufanya ukaguzi katika miradi mbalimbali inayotekelawa na Serikali ili liweze kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea shughuli zilizotekelawa na Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijijini; kwa kuwa, miradi mingi ya *REA* imeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na kucheleweshwa na kutolewa chini ya kiwango kwa fedha zilizokusanywa kutoka kwenye tozo za mafuta na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge lako.

Na kwa kuwa, hali hiyo imesababisha ongezeko la ghamama za miradi husika kutokana na sababu mbalimbali

ikiwemo fidia kwa wakandarasi na kupanda kwa thamani ya dola hapa nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali kutoa fedha za miradi ya *REA* na zipelekwe kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha ili miradi iliyokusudiwa itekelezwe kwa wakati na hivyo kuepusha Serikali kulipa gharama za fidia kwa wakandarasi zinazochelewesha miradi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, urukwaji wa maeneo muhimu ya huduma za kijamii katika miradi; kwa kuwa maeneo mengi ya kijamii na kiuchumi katika vijiji na vitongoji vingi yalirukwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya awamu ya kwanza na ya pili ya utekelezaji wa mradi wa umeme vijijini.

Na kwa kuwa hali hiyo ilikwamisha kufikiwa kwa malengo ya mradi, kuibua malalamiko kutoka kwa viongozi wa maeneo husika kwa madai ya kutoshirikishwa, pamoja na kusababisha kero kwa wananchi hasa kwenye maeneo yaliyorukwa.

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali ihakikishe maeneo ya kijamii na ya kiuchumi yanapewa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu. Aidha, viongozi wa maeneo ambayo mradi utapita washirikishwe kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Miradi mingi ya *REA* iliyotekelzeza katika awamu ya kwanza na ya pili ilibainika kukosa usimamizi mzuri.

Na kwa kuwa hali hiyo ilisababisha miradi hiyo kutekelezwa kwa kiwango duni ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na mashine umba (*transformer*) zisizo na ubora unaokidhi viwango.

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti katika utekelezaji wa miradi ya *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania; kutokana na uchambuzi wa Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kuhusu *TANESCO*, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

(i) Bunge linaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka na madhubutii ili kupata ufumbuzi wa madeni ili kuiwezesha *TANESCO* kuepuka na kujidoresha kwa hasara.

(ii) Wateja wengi kutolipa ankara za umeme kwa wakati; kwa kuwa *TANESCO* imebainisha kuwepo kwa wateja wengi wanaochelewa au kutolipa ankara za umeme kama inavyotakiwa.

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia kupunguza uwezo wa kifedha wa *TANESCO* na hivyo kuathiri utendaji na uendeshaji wa shughuli za Shirika.

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali iingilie kati na kuhakikisha wadeni wote wa *TANESCO* (ikiwemo Serikali na taasisi zake) wanalipa ankara zao kikamilifu na watakaoshindwa waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa mitambo ya kufua umeme; mitambo mingi ya kufua umeme imekuwa ikiharibika na kushindwa kufanya kazi kutokana na kutokufanyiwa matengenezo kwa wakati. Kuharibika kwa mitambo hiyo mara kwa mara husababisha kukosekana kwa umeme wa uhakika nchini jambo linaloigharimu *TANESCO* na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge linaishauri Serikali kutenga na kupeleka fedha za kutosha kwa *TANESCO* ili kuiwezesha kuifanyia matengenezo mitambo ya kufua umeme na hivyo kuepusha adha ya ukosefu wa umeme wa uhakika kwa wananchi na hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme unachangia kupotea umeme mwangi njiani. Upotevu huo unaathiri kwa kiasi cha

umeme kinachowafikia watumiaji, na hivyo kuikosesha mapato *TANESCO* na kuathiri uzalishaji katika uchumi nchini. Bunge linaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuiwezesha *TANESCO* kufanya matengenezo rekebishi (*rehabilitation*) katika vituo na miundombinu ya kusafirishia umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Petroli Tanzania (*TPDC*), Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

(a) Shirika linakabiliwa na madeni mbalimbali kutoka kwa wadau mbalimbali. Shirika pia linaidai Taasisi ya *TANESCO* ambao ndio mlaji/mnunuaji mkubwa wa gesi.

(b) Bunge linaishauri Serikali kuweka utaratibu mahsus wa kumaliza madeni haya ya taasisi hizi za kiserikali; aidha, kuangalia namna bora ya kuendelea kupeana huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji wa gesi nydingi kuliko Inavyonunuliwa; *TPDC* haina uwezo wa kujenga miundombinu ya kusambazia gesi inayozalisha na hivyo kushindwa kulifilia soko la watumiaji. Hali hiyo inasababisha *TPDC* kushindwa kuuza gesi na hivyo kukosa mapato yatakayoizesha kuijendesha kibiashara kama ilivyo kusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge linaishauri Serikali kuiwezesha *TPDC* kutekeleza mradi wa usambaza gesi katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kujenga miundombinu ya kusambaza gesi kwa watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufinyu wa bajeti kwa shughuli za *TPDC*; bajeti inayotengwa na Serikali kwa ajili ya *TPDC* ni ndogo na fedha zake hazipatikani kikamilifu na kwa wakati. Hali hiyo inachangia kuikwamisha *TPDC* katika utekelezaji wa shughuli zake.

Bunge linaishauri Serikali kuipatia *TPDC* bajeti ya kutosha na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya msingi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Madini Dodoma kinakabiliwa na ukosefu wa fedha kutokana na kutotengewa fedha za maendeleo katika bajeti iliyopita. Hali hiyo inasababisha chuo kushindwa kukarabati miundombinu ya mafunzo ili kiweze kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani za ufundi mchundo na ufundi sanifu katika sekta ya madini. Bunge linaishauri Serikali kukiwezesha chuo hiki kwa kukitengea bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Jiolojia nchini...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga kwa hiyo omnia yaingie yote, nadhani ulishaomba mwanzoni, kwa hiyo hitimisha hoja yako.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika, Job Ndugai, Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Tulia Ackson, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama na yaingie katika *Hansard*.

Pia ninatoa pongezi kwa Wizara ya Nishati...

**MHE. NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba utoe hoja.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA – MAKAMU WENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni

na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE  
YA NISHATI NA MADINI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI  
CHA KUANZIA JANUARI, 2017 HADI JANUARI, 2018 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Kutokana na muda kuwa mfupi, sitawezza kusoma taarifa yote, hivyo naomba taarifa yote, pamoja na sehemu ambazo sitazisoma iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge "Hansard".

**1.1 Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2017, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanuni kama ilivyoanishwa katika Kanuni ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Pamoja na majukumu mengine Kamati imetekeleza majukumu ya msingi yafuatayo :-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini;
- b) Kushughulikia Taarifa za Mwaka za Utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini pamoja na;

c) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

## **1.2 Njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake kikanuni, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kupokea na kujadili taarifa mbalimbali kwa Wizara pamoja na taasisi zake, na kupata mafunzo na semina mbalimbali.

## **1.3 Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekeliza na Wizara ya Nishati na Madini.

Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Geita kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati na Madini iliyotengewa fedha na kupelekewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni hii ifuatayo:-

- i) Miradi ya Umeme Vijijini katika Wilaya ya Tanga;
- ii) Miradi ya Umeme Vijijini katika Wilaya ya Geita;
- iii) Mradi wa Umeme wa Gesi wa Kinyerezi I Extension (MW 185);
- iv) Mradi wa Umeme wa Gesi wa Kinyerezi II (MW 240);
- v) Ukarabati wa Kituo cha kufua Umeme cha Hale;
- vi) Mradi wa Umeme wa Bulyanhulu – Geita KV 220;
- vii) Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef;

viii) Migodi ya Wachimbaji wadogo waliopata Ruzuku ya Serikali; na

ix) Migodi ya Wachimbaji wa kati.

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi huo Kamati ilibaini changamoto kadhaa zinazochangia kuzorota kwa utekelezaji wa Miradi katika maeneo mbalimbali hasa yaliyokaguliwa na Kamati. Changamoto kubwa iliyobainika katika ukaguzi wa miradi yote ni ukosefu wa fedha za miradi ya maendeleo.

Kielelezo **Na. 1** na **Na. 2** vinatoa ufanuzi kuhusu mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka husika pamoja na ufanuzi wa upatikanaji huo kwa asilimia.

**MWENENDO WA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA KIPINDI**

**CHA MIAKA MITANO KUANZIA 2013/2014 HADII 2017/2018**

*Kielelezo: 1*

MWAKA	KILICHOIDHINISHWA (Tsh. Bilioni)	KILICHOTOLEWA (Tsh. Bilioni)	%
2013/2014	1,100	614	55.82
2014/2015	957.2	271.57	28.37
2015/2016	502.3	579	115.27
2016/2017	1,056	698.61	66.17
2017/2018	938.32	198.66	21.17

#### *1.4 Miradi ya Sekta ya Madini iliyokaguliwa na Kamati*

##### **1.4.1 Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef**

**Mheshimiwa Spika**, Mgodi wa Dhahabu wa Buckleef ulioko mkoani Geita, una Leseni ya Uchimbaji Mkubwa (Special Mining License) SML Na. 04/92 na unamilikiwa kwa mkataba wa ubia (Joint Venture Agreement)ulioingiwa mwaka 2011 kati ya Serikali kupitia STAMICO na Kampuni ya TANZAM 2000.

Kupitia mkataba huo, STAMICO inamiliki **asilimia 45** na TANZAM 2000 inamiliki **asilimia 55** ya hisa. Kwa mujibu wa mkataba huo TANZAM 2000 ina jukumu la kutafuta fedha za kuendesha Mgodi (Operator) wakati jukumu la STAMICO lilikuwa kuhamishia Leseni zake 12 kwa Kampuni hiyo.

Kamati ilibaini kwamba, licha ya Leseni zote za uchimbaji na utafiti kukabidhiwa kwa Kampuni hiyo, hakuna kazi ye yeyote iliyokwishafanyika katika kuendeleza Mgodi huo tangu Kampuni hiyo iingie Mkataba na STAMICO.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kampuni kuripoti kuwa imekamilisha ufungaji wa Mtambo mpya wa kuchenjulia dhahabu, Kamati inasikitishwa na kitendo cha mbia huyo kutozingatia ushauri wa STAMICO kuhusu aina ya mtambo unaofaa kutumika katika eneo hilo, hatua ambayo inaisababishia Serikali hasara. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini inapoingia ubia katika miradi ya sekta ya madini ili kuepuka wabia wa aina hii ambao hawazingatii ushauri wa mbia mwenza, (STAMICO) jambo linalosababisha hasara zisizo za msingi.

Kamati haikuona jitihada zozote za mbia huyo za kuendeleza Mgodi kama walivyokubaliana kwenye Mkataba. Vilevile, Kamati imesikitishwa na usimamizi mbovu wa STAMICO katika Mgodi huo licha ya kuwa na mashapo yenyehakika wa kuzalisha dhahabu na kuliingizia Taifa mapato. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, hatua stahiki zichukuliwe ili kurekebisha kasoro ambazo zimebainika katika ubia huo.

#### **1.4.2 Migodi ya Wachimbaji Wadogo waliopata Ruzuku ya Serikali-Geita (Blueleef Mining na Mgusu Mining)**

**Mheshimiwa Spika**, katika awamu zote mbili za malipo, jumla ya **Shilingi 8,071,000,000/=** zimetolewa na Serikali kwa kuratibiwa na Wizara ya Nishati na Madini, na jumla ya Wachimbaji Wadogo 115 wamenufaika kwa kupata ruzuku hizo katika mikoa mbalimbali. Katika awamu ya kwanza ya malipo, kiwango cha juu kwa kila mnufaika kilikuwa ni **Dola za Kimarekani 50,000** na awamu ya pili kiwango cha juu cha mnufaika kilikuwa ni **Dola za Marekani 100,000**. Kwa maoni ya Kamati, viwango hivyo vya fedha ni vikubwa ikilinganishwa na usimamizi mdogo unaotolewa na Wizara ya Madini.

Katika Mkoa wa Geita jumla ya Wachimbaji Wadogo Wadogo Saba (7) wamenufaika na ruzuku ya Serikali, vikiwemo Vikundi vya Wajasiriamali wanaoshughulika katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Katika ziara ya ukaguzi wa Migodi ya wachimbaji wadogo waliopata ruzuku, Kamati iliridhishwa na utendaji wa wachimbaji wadogo watatu (3)

tu kati ya Saba (7) waliopata ruzuku ambao wameendeleza shughuli zao za uchimbaji katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo kwa baadhi ya wanufaika, Kamati ilibaini changamoto kubwa ya usimamzi wa fedha usioridhisha kwa Wachimbaji Wadogo. Aidha, Wanufaika hao wa ruzuku kwa namna moja ama nyingine hawakutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa na Serikali.

Kwa kuwa, katika awamu zote mbili za utoaji wa ruzuku kwa Wachimbaji Wadogo kumekuwa na kasoro mbalimbali kwenye matumizi na usimamizi wa ruzuku hizo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini (evaluation) ya fedha hizo kabla haijaanza awamu nyingine ili kuhakiki na kutatua changamoto nyingi ambazo zipo kwa sasa.

#### **1.4.3 Migodi ya Wachimbaji wa Kati (Busolwa Mining na Nyarugusu Processing Plant)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa Migodi ya Busolwa Mining na Nyarugusu Processing Plant, iliyopo Mkoa wa Geita. Lengo la ziara lilikuwa ni kujifunza jinsi Wachimbaji wa Kati wanavyoendesha shughuli zao na kubaini mchango wao katika mapato ya Serikali.

Busolwa Mining ni Mgodi unaomilikiwa na Mtanzania, yaani mzawa kwa aslimia mia moja, na Kamati ilijionea jinsi unavyoendesha shughuli zake kwa kutekeleza Sheria na Kanuni mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zote za Serikali. Tangu Mgodi huo uanze kazi mwaka 2014, umeshalipa kodi kiasi cha **shilingi bilioni 120, Mrabaha shilingi Bilioni 562, kodi ya zuio kwa mwaka 2017 shilingi Milioni 20 na Service Levy shilingi Milioni 48.**

Pamoja na mgodi huo kuendesha shughuli zake kwa ufanisi, Kamati ilibaini kwamba, unakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa eneo hasa la kutupia mabaki yatokanayo na shughuli za Mgodi yaani (TSF). Ni mapendekezo ya Kamati kuwa, maombi ya Mgodi huo kupatiwa eneo lingine

yashughulikiwe mapema ili kusaidia kuongeza uhai wa Mgodi huo ambao umeajiri zaidi ya Watanzania 300.

## **1.5 SEKTA YA MADINI**

### **1.5.1 Madini ya Vito ya Tanzanite**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kutoa maoni na mapendeleko yake kuhusu madini ya Tanzanite, bado utekelezaji wake ulikua wa kusua sua sana kwa upande wa Serikali. Changamoto ya usimamizi usioridhisha katika mgodi huu umesababisha Taifa kupoteza mapato mengi sana. Migogoro ya muda mrefu kati ya wachimbaji wadogo wadogo (mitobozano), utoroshwaji wa madini ya Tanzanite nje ya nchi ya Tanzania ambapo madini hayo yalikua yanasaferishwa kama madini ghafi, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka, 2010.

**Mheshimiwa Spika**, kwa umahiri wako wa kuzingatia changamoto hizo za muda mrefu katika madini hayo, Kamati inakupongeza kwa dhati kabisa kwa hatua yako ya kuunda Kamati Maalum iliyoshuhulikia masuala uchimbaji, usimamizi na biashara ya madini ya Tanzanite na kubaini changamoto nyingine mbalimbali hususani katika usimamizi na biashara kwa ujumla.

Mkataba wa ubia kati ya Tanzanite One (T) Ltd na Serikali kupitia Shirika la Madini nchini STAMICO haukutoa fursa kwa Serikali kupata faida kutokana na kuwepo kwa vipengele kadhaa kandamizi kwa Serikali kikiwepo kipengele kinachotamka kuwa faida itakayogawanywa kwa wabia itakuwa ni faida mabaki (residual net profit) ambayo kimsingi tangu kuanza kwa mkataba huo tarehe 20 Juni, 2013 faida hiyo hajjawahi kupatikana kutokana na gharama kubwa za uendeshaji. Faida mabaki ni faida ambayo inapatikana baada ya kutoa gharama zote za moja kwa moja za uzalishaji na gharama zisizo za moja kwa moja kutoka katika mauzo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe.

Rais John Pombe Magufuli, kwa kuamua kujenga ukuta kuzunguka eneo la mgodi ili kuongeza udhibiti wa biashara ya Tanzanite na kupunguza utoroshwaji wa madini hayo, ambao ulikuwa ni changamoto kubwa katika kudhibiti mauzo. Aidha, Kamati inaunga mkono jitihada zinazoendelea za kushughulikia kwa kina Mkataba huo baina ya TML na STAMICO kwa kutumia sheria mpya za rasilimali ambazo zinaruhusu kurejea makubaliano hasi katika mikataba ya ubia, ili Taifa liweze kunufaika na madini haya ya Tanzanite.

### **1.5.2 Madini ya Dhahabu**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Madini nchini imeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi hasa katika suala la ukusanyaji wa Kodi za Serikali. Sekta hii imekuwa ikichangia asilimia 4% tu katika pato la Taifa, mchango ambao ni kidogo sana ikillinganishwa na ongezeko la uzalishaji katika Sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Wawekezaji nchini hasa kwenye sekta ya Madini, wakiidai Serikali marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT returns*) ambayo kiutaratibu inapaswa kulipwa baada ya Migodi kukamilisha hesabu zao na kuwasilisha TRA. Serikali hajjalipa fedha hizo kwa Migodi hiyo kwa madai ya kuwepo changamoto kadhaa ambazo ilikuwa inazifuatilia ili kujiridhisha kabla ya kuzilipa. Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo ili Migodi hiyo iweze kulipwa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inamiliki mgodi mmoja tu kwa asilimia mia moja ambao ni Mgodi wa Stamigold kupitia Shirika la STAMICO. Mgodi huu licha ya kuajiri Watanzania zaidi ya mia saba (700), bado kumekuwa na jitihada ndogo za Serikali katika kuusaidia katika masuala ya msingi kwa lengo la kuuendeleza. Baadhi ya masuala hayo ya msingi ni pamoja na:-

1. Serikali kutousaidia Mgodi kupata fedha za kufanya utafiti katika leseni zinazozunguka eneo hili ili kuongeza uhai wa mgodi;

2. Mgodi haujasaidiwa kupata msamaha wa kodi ya mafuta na vipuli vya uendeshaji kama ilivyo kwa migodi mingine ya wawekezaji nchini;
3. Kukosekana kwa Mining Development Agreement (MDA) kwa muda mrefu kunaukwamisha Mgodi kujiedesha kibashara kama ilivyo kwa Migodi mingine nchini;
4. Mgodi huu unakabiliwa na deni kubwa kutoka kwa Wazabuni mbalimbali wanaotoa huduma katika Mgodi huo. Kamati inaishauri Serikali kuingilia kati deni hilo ili kuepusha shughuli za Mgodi huo kusimama na kusababisha hasara kubwa.

Kamati inapongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa maamuzi ya kuigawanya Wizara ya Nishati na Madini na kuwa Wizara mbili tofauti. Hii itachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa Wizara hizi.

Aidha, Kamati inapongeza Wizara ya Madini kwa kasi waliyoanza nayo katika utatuzi wa changamoto mbalimbali ikiwemo hii ya uzalishaji wa Madini ya Dhahabu pamoja na malalamiko mbalimbali ya wananchi wanaozunguka maeneo ya migodi kama vile Mgodi wa North Mara hasa maeneno ya **Nyamichele** katika vijiji vya **Nyakunguru, Murwambe, Matongo** na **Nyamongo** katika ulipwaji wa fidia zao. Hata hivyo, juhudhi hizo zitakuwa na tija iwapo Wananchi wa maeneo hayo ambao wameteseka toka mwaka 2012 wakidai kulipwa fidia ya maeneo yao kutoka Mgodi wa North Mara, watalipwa stahiki yao ili waweze kujikwamua na hali mbaya ya kiuchumi inayosababishwa na kutoendeleza maeneo yao yaliyofidiwa na mgodi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali na Bunge kwa ujumla kwa kufanya mabadiliko katika Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ambayo yanaanzisha kamisheni mpya itakayosimamia na kuratibu sekta ya madini kwa ufanisi.

## 1.6 SEKTA NDOGO YA GESI

**Mheshimiwa Spika**, Gesi Asilia iligundulika nchini mwaka 1974 ambapo ugunduzi wa kwanza ulibainika katika Kisiwa cha Songo Songo na kufuatiwa na ugunduzi mwingine mwaka 1982 katika eneo la Mnazi Bay (Mtwara). Gesi asilia hiyo haikuendelezwa kwa kuwa ilionekana kutokuwa na manufaa kiuchumi. Ili kuhakikisha nchi inanufaika na gesi iliyogunduliwa, miaka ya 1990 Serikali ilifanya tafiti za kuangalia namna bora ya kutumia gesi asilia hiyo. Utafiti wa mwaka 1991 ulionesha kuwa na tija kiuchumi hivyo ikaonekana ni bora gesi asilia isafirishwe hadi Dar es Salaam kwa ajili ya kutumika viwandani pamoja na kuzalisha umeme.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kugundulika kwa gesi hiyo hapa nchini, jumla ya Viwanda 41 na Taasisi 2 vimekwisha unganishwa katika mtandao wa matumizi ya gesi asilia. Kamati inapongeza Serikali kwa kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia. Miradi hiyo mikubwa inayotarajwa kukamilika ifikapo Juni, 2018 inakusudiwa kuongeza zaidi ya Megawati 425 kwenye Gridi ya Taifa, na hivyo kupunguza tatizo la upungufu wa umeme nchini.

Aidha, Kamati haikuridhishwa na mahusiano ya ubia wa kuendeleza miradi ya gesi asilia inayotekelawa kati ya TPDC, PANAFRICAN ENERGY, SONGAS pamoja na TANESCO. Kamati iliona kuna haja ya Bunge kuingilia kati na kupata vyema ufanuzi wa ziada ili kuweza kuishauri Serikali juu ya mikataba na mahusiano baina ya wabia hao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakupongeza sana wewe binafsi kwa kuunda Kamati Maalum ambayo imeshuhulikia masuala ya maendeleo na matumizi ya sekta hii ya gesi asilia nchini na namna ambavyo matumizi ya gesi asilia yatasaidia kuongeza mapato katika nchi yetu. Kupitia Kamati hiyo, Bunge litawenza kuwa na uelewa wa kiwango cha juu na kupata namna bora zaidi ya kuishauri Serikali katika sekta hii ya gesi.

## **1.7 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

- i) Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara ya Nishati na Madini, haukuwa wa kuridhisha kwa kuwa Fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazikuwasilishwa kwa wakati na miradi mingine haikupelekewa fedha kabisa;
- ii) Miradi mingi ya REA katika Awamu ya Pili haikukamilika kutokana na kasoro mbalimbali kama vile uainishaji wa maeneo bila kuzingatia vijiji na vitongoji ambavyo tayari vina wananchi wengi, na ufungaji wa Mashine Humba (*Transformer*) nyingi kutokidhi mahitaji ya eneo husika;
- iii) Serikali iangalie upya namna bora ya kuwasaidia Wachimbaji wa Kati kwa kuwapatia maeneo ya kutosha kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza Sekta ya Madini;
- iv) Ruzuku iliyotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa Wachimbaji Wadogo Wadogo, haikusimamiwa vizuri na hivyo kushindwa kuleta tija kwa Wananchi waliokusudiwa. Aidha Serikali inapaswa kutoa elimu ya kutosha kwa wachimbaji juu ya ruzuku wanazopokea kutoka kwa Serikali;
- v) Pamoja na Mipango mizuri ya TPDC katika kuendeleza Sekta ya Gesi asilia nchini, ni lazima Serikali iwekeze fedha za kutosha katika miradi ya Gesi ili kuharakisha azma ya nchi yetu kuingia katika uchumi wa viwanda; na
- vi) Serikali itenye fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimkakati kama vile Mgodi wa makaa ya Mawe wa Kiwira ambaao mpaka sasa hakuna shughuli zozote za uendelezaji wa mgodi huu.

## 1.8 Ziara za mafunzo

**Mheshimiwa Spika**, baadhnishai ya Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kusafiri kwenda nchini Marekani kwa ajili ya kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu sekta za Nishati hususani Umeme wa Upepo (Wind Energy). Lengo la ziara hii ilikuwa ni kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika masuala ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo vingine ambavyo ni rahisi na vinapatikana katika mazingira yetu.

Mafunzo hayo yamekuza uelewa kwa Wajumbe kuhusu masuala ya kuzalisha Umeme kwa njia ya upepo na hivyo kuwasaidia kutoa ushauri kwa Wizara ya Nishati kuhusu uzalishaji wa umeme kwa njia ya upepo. Umeme utakaozalishwa kutowana na upepo utakuwa wa gharama ndogo, na hivyo utauzwa kwa bei nafuu na utakuwa wa kuaminika.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo Wajumbe walipata wasaa wa kukutana na wadau mbalimbali katika sekta za Nishati. Aidha, walitembelea maeneo mbalimbali ambako umeme wa njia ya upepo unazalishwa, na kuweza kujenga uelewa zaidi juu ya uzalishaji wa umeme huu pamoja na gharama za utumiaji. Aidha, Wajumbe walipokea ushauri juu ya kutoa vipaumbele vya wawekezaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji katika sekta ya Nishati. Nishati ya umeme wa upepo ni rafiki kwa mazingira

## 1.9 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati yako, Ofisi ya Bunge iliandaa semina elekezi kuititia mradi wa *Legislative Support Program* unaonfadhliliwa na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), kuhusu masuala ya kutunga Sheria pamoja na Kanuni mbalimbali. Mafunzo haya yamekua muhimu sana katika kuongeza uelewa kwa Wajumbe wa Kamati.

Pia Wizara ya Nishati na Madini kupitia taasisi ya TPDC na TGDC iliwapatia Wajumbe wa Kamati, semina ya siku moja kuhusu Miradi ya mpango wa matumizi ya gesi asilia pamoja na uendelezaji wa nishati ya joto ardhi nchini. Lengo la semina hiyo, lilikuwa ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kufahamu vyema mpango mkakati wa gesi asilia nchini pamoja na matumizi ya nishati ya jotoardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi isiyo ya kiserikali ya *Natural Resource Government Institute* (NRGI) imekuwa ikiandaa semina za mara kwa mara kwa lengo la kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika sekta hizi muhimu za madini, mafuta na gesi. Semina hizo pia zimekuwa zikilenga kufafanua sheria mbalimbali zinazohusu udhibiti na ukusanyaji wa mapato katika sekta hizi kwa maendeleo ya uchumi wetu.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati yako ilipata mafunzo kuhusiana na matumizi ya Umeme wa Upepo kupitia kampuni ya Wind East African Energy ambayo ilitoa mafunzo juu ya matumizi ya umeme wa upepo ikianisha faida na namna ya kuutumia umeme huu.

Kamati pia ilipata mafunzo kuhusiana na matumizi ya rasilimali kupitia taasisi ya OXFAM, ambayo yalijikita yalijikita katika uchambuzi wa sekta ya uchimbaji wa madini, gesi asilia na kutunza mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia mafunzo hayo Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, wamepata uelewa mpana kuhusu sekta hizi muhimu wanazozisimamia kwa kuelewa vyema mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kushauri na kuisimamia Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini.

### **1.9.1 KAZI MAHSUSI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Nishati na Madini katika kipindi cha mwaka mzima imetekeliza majukumu yafuatavyo:-

- i) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2016/2017;
- ii) Kupokea na Kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 pamoja na uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018;
- iii) Kupokea Taarifa ya nusu Mwaka ya upatikanaji wa Fedha na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 na;
- iv) Kupokea na kujadili Taarifa za utendaji wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini.

### **1.9.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Ujumla**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kurejea Hatii idhini ya Serikali Na. 144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 (Government Instrument). Lengo lilikuwa ni kuoanisha bajeti inayotengwa, iliopokelewa, matokeo ya utekelezaji wa bajeti na matarajio ya wananchi kwa Serikali yao.

Ili kujiridhisha na utekelezaji wa Bajeti, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2017). Katika mwaka 2017/18 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 998.34**. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 222.53** sawa na asilimia **44.58** ya lengo la bajeti ya nusu mwaka wa fedha 2017/18 ambayo ilikuwa ni **shilingi bilioni 499.17**.

Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 198.66** ni za miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 42.33** ya lengo la Fedha za maendeleo kwa kipindi hicho cha nusu mwaka ambalo lilikuwa ni **shilingi bilioni 469.32**, na **Shilingi bilioni 11.74** ni

kwa ajili ya matumizi mengineyo (O.C) ambayo ni sawa na **asilimia 81.44** ya lengo la nusu mwaka ambalo lilikuwa ni **shilingi bilioni 14.74**.

Katika Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka 2017/18 jumla ya **shilingi bilioni 21.78** zilikua kwa ajili ya sekta ya madini ambapo **shilingi bilioni 14.7** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 7.83** ni kutoka nje.

## **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI YA NISHATI NA MADINI**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini, Kamati ilipokea taarifa mbalimbali zinazohusu Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini pamoja na sekta ndogo ya Mafuta nchini.

Ili kubaini utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo, Kamati ilipokea taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini zilizohusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo pamoja na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini. Aidha, Taasisi zifuatazo zilizowasilisha taarifa kwenya Kamati na kujadiliwa;

#### **2.1 Wakala wa Nishati Vijijini ( REA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wakala wa Umeme vijijini kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme pamoja na upatikanaji wa fedha za miradi hadi kufikia Disemba, 2017.

Katika mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali imetenga **shilingi bilioni 469.09** kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini. Kiasi cha **shilingi bilioni 234.54** kilitarajiwu kupokelewa kwenye mfuko kutoka kwenye vyanzo mbalimbali katika kipindi cha Nusu mwaka (Julai – Disemba, 2017). Hata hivyo, hadi kufika Disemba, 2017, kiasi cha **shilingi bilioni 190.58**

(sawa na **asilimia 81.26**) ndiyo kilikuwa kimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya REA Awamu ya Tatu.

Aidha, Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa Wakala huu. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

- a) Mwitikio mdogo wa wateja kuunganishiwa umeme kwenye maeneo ambayo ujenzi wa miundombinu umekamilika;
- b) Msamaha wa kodi kwa vifaa vyta miradi ya nishati bado ni changamoto;
- c) Baadhi ya maeneo kurukwa wakati wa kupeleka umeme, hasa katika maeneo muhimu kama Zahanati, Shule na maeneo mengine ya kijamii;
- d) Baadhi ya mashine za utekelezaji wa miradi kua ni vifaa duni na kutokukodhi mahitaji ya maeneo husika. Mfano ni mashine humba (Transformer) katika baadhi ya maeneo zimebainika kuharibika mara kwa mara au kuwa na uwezo mdogo wa kufanya kazi; na
- e) Ushirikishwaji mdogo wa Viongozi pamoja na Wananchi katika maeneo ya miradi hasa wakati wa uainishaji wa vijiji/vitongoji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudini na hatua mbalimbali ilizochukua na inazoendelea kuchukua kusambaza umeme vijiji, Aidha, Kamati inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kushirikiana na Serikali katika maeneo ambayo bado yanahitaji maboresho katika utekelezaji wa miradi hii ya REA Awamu ya Tatu.

## **2.2 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji na hali ya upatikanaji wa Fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia Disemba, 2017 kutoka Shirika la

Umeme (TANESCO) ambalo linatekeleza majukumu ya kuzalisha/kufua, kusafirisha,kusambaza na kuza umeme nchini. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2017, TANESCO imeunganisha wateja wapya **105,844** katи ya **124,990** walilotarajiwa kuunganishwa katika kipindi hicho. Idadi hiyo ni sawa na **asilimia 85** ya lengo.

Shirika hilo lilikusanya **shilingi bilioni 730** kutokana na mauzo ya umeme na michango ya wateja wapya walioomba kuunganishiwa umeme (consumer contribution). Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 84** ya lengo ambalo lilikuwa ni kukusanya shilingi **bilioni 866**. Hadi kufika tarehe 31 Disemba, 2017 Shirika lilikuwa linadai Wateja wake (Serikali na Taasisi zake pamoja na wateja binafsi) kiasi cha **shilingi bilioni 277.4**. Kati ya deni hili wateja binafsi wanadaiwa **shilingi bilioni 83.8** na Serikali na taasisi zake pamoja na shirika la umeme Zanzibar (ZECO) wanadaiwa **shilingi bilioni 193.7**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na TANESCO kudai kiasi hicho cha fedha, katika kipindi hicho cha kufikia Disemba, 2017, ilikuwa inadaiwa na Wazabuni kiasi cha **shilingi bilioni 913**.

Katika mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali ilitenga **shilingi bilioni 293.41** kwa ajili ya maendeleo kwa TANESCO. Hadi mwezi Disemba, 2017 jumla ya **shilingi 42.13** sawa na **asilimia 14** ya fedha zilizotengwa tayari zilikuwa zimepokelewa na TANESCO kutoka Serikalini.

**Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-**

- a) Madeni ya TANESCO yanababisha kuzorota kwa utendaji wa shirika. Aidha, madeni yameendelea kuongezeka na hakuna jitihada zozote za Serikali za kusaidia kumaliza madeni haya;
  
- b) Garama kubwa za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta hasa kwenye maeneo ambayo hayajaunganishwa na gridi ya Taifa;

- c) Wateja wengi zikiwemo Wizara na Taasisi za Serikali, kutolipa ankara za umeme kwa wakati hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya shirika;
- d) Uharibifu wa mara kwa mara wa mitambo ya kufua umeme unaosababisha mitambo hiyo kuzimwa kwa muda mrefu, kunaligharimu shirika na Taifa kwa ujumla kwa kukosekana kwa umeme wa uhakika katika maeneo mengi hapa nchini;
- e) Ukosefu wa umeme wa kutosha kutokana na Serikali kushindwa kuwekeza kwenye mitambo ya kuzalisha umeme kwa muda mrefu licha ya ongezeka kwa mahitaji ya umeme nchini; na
- f) Upotevu wa umeme kutokana na uchakavu kwa mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.

### **2.3 Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Nchini (TGDC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi nchini ilisajiliwa mwezi Disemba, 2013 na kuanza kazi Julai, 2014. TGDC ni kampuni tanzu ya TANESCO na inamillikiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia mia moja (100%). Kampuni hii ina jukumu la kuharakisha uendelezaji wa nishati ya jotoardhi nchini ili kuchangia kukuza uchumi na kuongeza ajira.

Katika mwaka 2017/18 jumla ya **shilingi bilioni 36.7** zilitengwa na Serikali kwa ajili ya kampuni ya TGDC kwa ajili ya miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo. Hadi Disemba, 2017 Kampuni ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi bilioni 1.35** sawa na **asilimia 44.78** ya fedha zilizotengwa kwa kipindi cha nusu mwaka. Aidha, ni vyema kuzingatia kwamba, fedha zote za ndani zinatoka kampuni mama ya TANESCO.

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na TGDC katika kuendeleza nishati hii ya joto ardhi, bado zipo changamoto kadhaa zikiwemo:-

- a) Kukosekana kwa sheria mahususi ya Jotoardhi nchini;
- b) Gharama kubwa za kulipia leseni za umiliki wa maeneo ya kufanyia kazi, ikizingatiwa kwamba TGDC hajawa na chanzo cha fedha za kulipia leseni;
- c) Upatikanaji wa fedha za miradi ya Jotoardhi; na
- d) Uhaba wa wataalam wenye ujuzi stahiki katika soko la ajira nchini.

#### **2.4 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC). Katika uchambuzi huo ilibainika kwamba, ugunduzi wa gesi nchini bado haujawanufaisha wananchi kwa kiwango cha kuridhisha.

Katika kipindi hiki cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2017) TPDC imeweza kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 161.41** sawa na **asilimia 55** ya malengo ya nusu mwaka ya kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni 295.47**. Fedha zilizotengwa kutumika katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2017 ni **shilingi bilioni 3.1**. Hadi kufikia Disemba, 2017, **shilingi bilioni 2.1** sawa na **asilimia 67%** ya lengo zilitumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha, kutolipwa kwa wakati kiasi cha shilingi bilioni 398.69 ambazo Shirika linawadai wateja wake, kunaliathiri shirika katika utekelezaji wa majukumu yake ipasavyo. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na shirika hili katika ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vingine, bado linakabiliwa na changamoto zifuatazo;

- a. Ukosefu wa soko la uhakika na la kuaminika la gesi inayozalishwa nchini;
- b. Bajeti ndogo inayotengwa kwa Shirika ambayo inalifanya shirika lishindwe kutekeleza majukumu yake muhimu kwa Taifa hasa uwekezaji na utafiti wa gesi na mafuta nchini;

- c. Kucheleweshwa kwa fedha za maendeleo kunakwamisha utekelezaji wa miradi. Mfano, mradi wa kusambaza Gesi asilia katika mkoa wa Dar es Salaam;
- d. Uendelezwaji wa rasilimali watu unaotokana na kupungua kwa mikataba ya utafiti wa mafuta na gesi, kumesababisha kupungua kwa fedha za mafunzo (Annual training fees) zilizokua zinatokana na mikataba hiyo. Hali hii imerudisha nyuma shughuli za uendeshaji wa rasilimali watu katika shirika hasa ukizingatia kuwa sekta hii inahitaji utaalami na teknolojia ya hali ya juu.
- e. Ushindani katika sekta ya gesi kutokana na mataifa mbalimbali pamoja na vyanzo mbadala vyta nishati.

## **2.5 Chuo cha Madini (MRI)**

Chuo cha Madini ni chuo cha ufundi kilichoanzishwa kwa ajili ya kupata mafundi sanifu wa kada ya kat i ili kusaidia utafiti wa madini nchini, pamoja na kutoa ushauri elekezi (consultancy) katika sekta za madini, mafuta na gesi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa Fedha wa 2017/18 Chuo hakikutengewa fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hata hivyo miradi ya maendeleo ya chuo hiki imetekelawa kupitia vyanzo vingine vya fedha, wakiwemo wabia wa maendeleo. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2017 Chuo kilikuwa kimepokea jumla ya **Shilingi Milioni 144.34** tu sawa na **asilimia 11.48** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2017/18. Utilewaji huu wa fedha hauridhishi kwani unakwamisha maendeleo ya chuo hiki muhimu kwa Taifa kwa ajili ya Mafundi sanifu na Mafundi Mchundo ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta hii ya Madini.

Pamoja na mafanikio mbalimbali ambayo Kamati ilielezwa, changamoto kubwa zifuatazo zilibainika:-

- a) Bajeti ndogo isiyokidhi mahitaji ya msingi ya chuo;
- b) Kucheleweshwa kwa Fedha za bajeti iliyoidhinishwa;

- c) Upungufu wa ofisi za watumishi, ukumbi wa mikutano na mihadhara;
- d) Uhaba wa wakufunzi katika fani za uhandisi na usimamizi wa mazingira migodini, masomo mtambuka na sayansi za mafuta na gesi;
- e) Hakuna sehemu za kutosha za wanafunzi wao kufanya mafunzo kwa vitendo na;
- f) Kukosekana kwa ulinzi madhubuti katika kampasi ya Nzega, hivyo kusababisha uvamizi kutoka kwa wachimbaji wadogo na wizi wa mara kwa mara katika kampasi hiyo.

## **2.6 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Jiolojia nchini ana majukumu ya kukusanya, kuchambua, kutafsiri, kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za kijiosayansi (jiolojia, jiochemia na jiofizikia), kutengeneza na kusambaza ramani, takwimu na taarifa mbalimbali zinazoainisha kuwepo kwa aina mbalimbali za miamba nchini.

Vilevile, wakala hufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimbali nchini na kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi, mionzi asili n.k.

Hadi kufika Disemba, 2017 wakala ulikuwa umepokea jumla ya **shilingi milioni 642.57** sawa na **asilimia 27.5** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, wakala ulikuwa umepokea shilingi bilioni 2.53 kwa ajili ya utekelezaji wa utafiti kwenye mradi wa SMMRP.

Hata hivyo, licha ya majukumu haya mazito walijonayo GST, changamoto zifuatazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa majukumu yake:-

- a) Kuathirika kwa ukusanyaji wa maduhuli kutokana na kupungua kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji madini nchini;
- b) Kutopatikana kikamilifu na kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti na kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na wakala, mafunzo, ukosefu wa watumishi na vitendea kazi;
- c) Upungufu wa wataalam wenyewe taaluma stahiki kama vile wakemia, wajijolojia, wahandisi jiolojia na maslahi duni; na
- d) Mabadiliko ya teckonolojia na maendeleo makubwa ya jiosayansi duniani yanaongeza gharama za uendeshaji wa kazi za wakala.

## **2.7 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya STAMICO. Shirika hili la madini limepeewa jukumu la kusimamia sekta ya madini kwa kufanya tafiti na uwekezaji katika migodi ya madini kama zilivyo kampuni zingine kwa niaba ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kuanzia mwezi Julai hadi Disemba 2017, shirika lilikuwa limepokea **shilingi bilioni 1.66** sawa **asilimia 12** ya Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kipindi cha nusu mwaka 2017/18.

Shirika limekwama kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu ya msingi ya kuendeleza Sekta ya Madini kutokana na changamoto zifuatavyo:-

- a) Ukosefu wa Fedha, na hivyo kukwamisha shughuli za shirika na kushindwa kuanzisha miradi mingine;
- b) Uwekezaji ulifanyika katika miradi mingi haujaanza kutoa faida. Mfano, ni Mgodi wa Tanzanite One, Stamigold/ Tulawaka, Kiwira n.k;

- c) Shirika kukabidhiwa majukumu mengi licha ya bajeti ndogo inayotengwa kwa mwaka; na
- d) Ukosefu wa Mikataba katika migodi ya Stamigold na Kiwira kunakwamisha migodi hiyo kukopesheka.

## **2.8 Sekta Ndodo ya Mafuta na hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Wizara pamoja na wadau wa Sekta ndodo ya mafuta nchini kuhusu mfumo mzima wa uingizaji wa mafuta pamoja na maendeleo ya sekta hiyo. Katika taarifa hizo Kamati ilipata uelewa wa hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Pamoja na mafanikio ya Serikali ya kuanzisha Wakala wa uingizaji wa mafuta kwa pamoja nchini, Sekta hii bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- a) Uwezo mdogo wa mita za upokeaji mafuta (flow meters), hali inayosababisha mita hizo kushindwa kwenda na kasi inayokubalika ya kushusha tani 1200 kwa saa na badala yake imekuwa ikishusha mafuta kwa kasi ya tani 400 kwa saa;
- b) Ukosefu wa Matanki makubwa ya kuhifadhia mafuta (*Farm Tanks*) baada ya kupakuliwa kutoka Melini kunasababisha hasara kwa Makampuni yanayoingiza mafuta pamoja na kuikosesha Serikali mapato;
- c) Gharama kubwa ya uwekiwa wa Vinasaba (Tsh. 12 kwa lita) ikilinganishwa na nchi jirani kama Kenya gharama ni Tsh. 1 kwa lita na Uganda Tsh. 2 kuna muongozea mzigo mwananchi; na
- d) Tozo za Taasisi mbalimbali za Serikali kwenye bei ya mafuta ni mzigo kwa Wafanyabiashara wa Sekta ya mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, ukosefu wa matanki ya kuhifadhi Mafuta yaani (*Farm Tanks*) ni changamoto kubwa. Hata hivyo, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua zinazoendelea za utekelezaji wa mradi huu ikiwa ni pamoja na mchakato wa kubadilisha kanuni ya uagizaji wa mafuta kwa pamoja (The Petroleum (Bulk Procurement) Regulations ya mwaka 2017 ili kuingiza vipengele vya upokeaji wa mafuta sehemu moja (Single Receiving Terminal).

## 2.9 Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini

**Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji umeme nchini bado ni changamoto katika baadhi ya maeneo hasa mkoa wa Dar es Salaam, ambako umeme umekua si wa uhakika na umekua ukikatika mara kwa mara na hivyo kuathiri wananchi katika uendeshaji wa shughuli za kiuchumi. Tatizo la miundombinu chakavu limechangia hali duni ya upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Hata hivyo, Katika maeneo mengine hususani vijiji, mafanikio ya kupatikana umeme yameonekana kwa kiasi kikubwa kutokana na ukamilishwaji wa miradi mingi ya REA awamu ya kwanza na awamu ya pili.

Kwa sasa nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha MW 1300 na matumizi ya juu kabisa ya nchi yetu yameweza kufikia hadi MW 1041. Matumizi haya yanakadiriwa kuongezeka siku hadi siku kutokana na mahitaji ya nishati hii kukua kwa kasi nchini. Mahitaji haya ya umeme yanapaswa kabisa kuendana na kasi ya ukamilishaji wa miradi mingi ya Umeme inayotekelzwu hapa nchini. Kamati inaishauri na kuitaka Serikali kupeleka fedha katika miradi yote ya umeme ili iweze kukamilika kwa wakati na kufikia malengo ya wizara iliyojivekea ya kufika MW 5000 ifikapo 2021.

**Mheshimiwa Spika**, ili kufikia azma ya nchi yetu kujenga uchumi wa viwanda ni lazima miradi mingi ya umeme ipelekewe fedha kama ilivyopangwa, sambamba na miradi ya REA inayotekelzwu nchi nzima. Aidha, ukarabati na matengenezo ya mitambo ya kufua umeme ni jambo muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

**2.9.1 Kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na mchakato wa bajeti wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na kuchambua Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2016/2017 miradi mingi haikuweza kukamilika kutokana na ukosefu wa Fedha za kuendeleza miradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyoelezwu kwenye taarifa ya Kamati ilivyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 19 Juni, 2017 tunaipongeza Serikali kwa kutenga bajeti ya kutosha katika miradi ya maendeleo hususani miradi ya umeme itakayosaidia wananchi kupata umeme wa uhakika katika maeneo mengi ya nchi na kuwesheha dhana ya uchumi wa viwanda kutekelezeka kwa vitendo. Hata hivyo hadi kufika Januari, 2018 pesa zilizopelekwa katika miradi ya maendeleo ni shillingi **bilioni 198.66** sawa na **asilimia 42.33** ya fedha zilizopangwa kupokelewa katika kipindi cha nusu mwaka 2017/18.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, bajeti iliyotengwa ya miradi ya maendeleo itolewe yote na kwa wakati na kuwe na usimamizi mzuri wa fedha hizo ili ziweze kuleta tija. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kufanya kazi maoni na ushauri wa Kamati kwa manufaa ya Taifa.

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO**

#### **3.1 Maoni ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini, ziara za ukaguzi

wa miradi pamoja na kukutana na Wadau wa sekta zote mbili za Nishati na Madini, Kamati ina maoni yafuatayo;

- a) Fedha za miradi ya maendeleo zinapaswa kuwasilishwa kwa wakati, kwani kutopatikana kwake kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa;
- b) Serikali iendelee kutafuta na kubuni vyanzo vingine mbalimbali vyaa mapato. Aidha, kutegemea Serikali Kuu pamoja na wafadhili pekee kunakwamisha utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo;
- c) Serikali itekeleze kwa ukamilifu miradi mipya ya usafirishaji na usambazaji umeme na kupanua gridi kwenye maeneo ambayo bado hayajaunganishwa kwenye gridi ya taifa;
- d) Serikali iimarishe doria katika njia za umeme pamoja na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;
- e) Serikali iwekeze katika vyanzo vingine vyaa kuzalisha nishati mbadala. Aidha kuwekeza zaidi katika nishati jadidifu ambayo uzalishaji wake ni nafuu na rafiki kwa utunzaji wa mazingira kutasaidia kuongeza nishati ya umeme;
- f) Serikali inapaswa kupunguza tozo nyngi za taasisi kwenye bei ya Mafuta ili kumpunguzia mizigo mwananchi/ mtumiaji wa mafuta;
- g) Serikali kuwekeza katika uvumbuzi wa teknolojia ya hali ya juu ili kuweza kushindana na nishati mbadala, kama vile nishati jadidifu (renewable energy), na hata miradi ya LNG kwa nchi nyngine kama Msumbiji ni tishio kwa biashara ya gesi na mafuta kwa siku za usoni. Hivyo basi Serikali inapaswa kuwekeza katika miradi ya gesi asilia mapema iwezekanavyo ili kutoa huduma ya uhakika na kuteka soko mapema;

- h) Fedha za miradi ya REA zinapaswa kuwasilishwa kwa wakati, ili kuepuka ongezeko la gharama kutokana na kucheleweshamukamilishaji wa miradi hiyo;
- i) Miradi ya REA Awamu ya Tatu hasa miradi ya *Densification* izingatie utekelezaji wa maeneo yaliyorukwa katika Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili ya utekelezaji wa miradi ya REA;
- j) Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini TPDC liwezeshe kupata pesa za kuijendesha na sio kutegemea Fedha kutoka Serikali Kuu ambazo huchelewa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uendelezaji wa gesi asilia. Aidha, Serikali iangalie namna inavyoweza kutatua changamoto ya madeni ya taasisi zake katika shirika hili;
- k) Serikali iangalie namna ya kulikwamua Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) pamoja na migodi inayosimamiwa na shirika hili ili shirika liweze kusimama na kuijendesha kibashara;
- l) Serikali iweke utaratibu mzuri wa ufungaji wa *Flow Meters* ili iweze kupata takwimu sahihi wakati wa upakuaji wa mafuta;
- m) Wakala wa jiolojia nchini iendelee kufanya utafiti ambao una tija na kuwafikia wananchi hasa kuhusu elimu za utafiti wa maafa na majanga;
- n) Serikali iangalie namna ya kuiwezesha wakala wa jiolojia nchini kua ndio mtafiti pekee wa masuala ya madini na kuweza kutoa takwimu zitakazohifadhiwa kwa manufaa ya Taifa. Hatua hiyo itapunguza watafiti wengine wa nje ya nchi kuja kufanya tafiti kwa muda mrefu bila kutoa takwimu na kuharibu maeneo ya nchi yetu kwa shughuli za uchimbaji;
- o) Wachimbaji wa Kati na Wadogo wadogo wapewe kipaumbele na Serikali ili waweze kuendeleza sekta ya madini kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu;

- p) Serikali ilisaidie Shirika la TANESCO kujikwamua na madeni mengi ambayo yanalifanya lishindwe kujiendesha kikamilifu;
- q) Bunge lipewe Bajeti ya kutosha ili kuliwezesha kutekeleza makujuku yake ya kikatiba na kikanuni, hasa ya kufanya ukaguzi katika miradi mbalimbali inayotekelawa na Serikali ili liweze kuishauri Serikali ipasavyo.

### **3.2 Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuelezea shughuli zilizotekelawa na Kamati, naomba kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

#### **3.2.1 Wakala wa Nishati Vijiji (REA)**

##### **a) Hali ya upatikanaji wa Fedha za Miradi ya REA kwa wakati**

**Kwa kuwa**, miradi mingi ya REA imeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na kucheleweshwa na kutolewa chini ya kiwango kwa fedha zilizokusanywa kutoka kwenye Tozo za Mafuta na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge lako;

**Na kwa kuwa**, hali hiyo imesbabsha ongezeko la gharama za miradi husika kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo fidia kwa wakandarasi na kupanda kwa thamani ya dola hapa nchini;

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri fedha za miradi ya REA zipelekwe kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha ili miradi ili yokusudiwa itekelezwe kwa wakati na hivyo kuiepusha Serikali kulipa gharama za fidia kwa wakandarasi inaochelewesha malipo yao.

##### **b) Urukwaji wa maeneo muhimu ya huduma za kijamii katika Miradi**

**Kwa kuwa**, maeneo mengi ya kijamii na kiuchumi katika vijiji na vitongoji vingi yalirukwa wakati wa utekelezaji wa miradi

ya awamu ya kwanza na ya pili ya utekelezaji wa mradi wa umeme vijijini,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo ilikwamisha kufikiwa kwa malengo ya mradi, kuibua malalamiko kutoka kwa viongozi wa maeneo husika kwa madai ya kutoshirikishwa, pamoja na kusababisha kero kwa wananchi hasa kwenye maeneo yaliyorukwa,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linaishauri Serikali ihakikishe maeneo ya kijamii na ya kiuchumi yanapewa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu. Aidha, viongozi wa maeneo ambayo mradi utapita washirikishwe kikamilifu.

**c) Utekelezaji wa Miradi ya REA awamu ya tatu**

**Kwa kuwa**, Miradi mingi ya REA iliyotekeliza katika awamu ya kwanza na ya pili ilibainika kukosa usimamizi mzuri,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo ilisababisha miradi hiyo kutekelezwa kwa kiwango duni ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na mashine humba (Transformer) zisizo na ubora unaokidhi viwango,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti katika utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu.

### **3.2.2 Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)**

**Mheshimiwa Spika**, kutohana na uchambuzi wa Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kuhusu TANESCO, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:

**a) Madeni**

**Kwa kuwa**, Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO) linakabiliwa na madeni mbalimbali kutoka kwa Wazabuni na Serikali na taasisi zake, na madeni hayo yamekuwa yakiongezeka,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo imeifanya TANESCO ishindwe kuijendesha na kutekeleza majukumu yake kikamilifu,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka na madhubuti ili kupata ufumbuzi wa madeni hayo ili kuiwezesha TANESCO kuepukana na kuijendesha kwa hasara.

**b) Wateja wengi kutolipa Ankara za umeme kwa wakati**

**Kwa kuwa**, Taarifa za TANESCO zimebainisha kuwepo kwa wateja wengi wanaochelewa au kutolipa Ankara za umeme kama inavyotakiwa,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo inachangia kupunguza uwezo wa kifedha wa TANESCO na hivyo kuathiri utendaji na uendeshaji wa shughuli za Shirika,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali iingilie kati katika kuhakikisha wadeni wote wa TANESCO (ikiwemo Serikali na Taasisi zake) wanalipa Ankara zao kikamilifu na watakaoshindwa waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

**c) Uharibifu wa Mitambo ya kufua umeme**

**Kwa kuwa**, mitambo mingi ya kufua umeme imekuwa ikiharibika na kushindwa kufanya kazi kutokana na kutokufanyiwa matengenezo kwa wakati,

**Na kwa kuwa**, kuharibika kwa mitambo hiyo mara kwa mara husababisha kukosekana kwa umeme wa uhakika nchini jambo linaloigharimu TANESCO na Taifa kwa ujumla,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linaishauri Serikali kutenga na kupeleka fedha za kutosha kwa TANESCO ili kuiwezesha kuifanyia matengenezo mitambo ya kufua umeme na hivyo kuepusha adha ya ukosefu wa umeme wa uhakika kwa wananchi na hasara kwa Taifa.

**d) Uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme**

**Kwa kuwa**, uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme unachangia kupotea kwa umeme mwingi njiani,

**Na kwa kuwa**, upotevu huo unaathiri kiasi cha umeme kinachowafikia watumiaji, na hivyo kuikosesha mapato TANESCO na kuathiri uzalishaji katika uchumi wa nchini,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuiwezesha TANESCO kufanya matengenezo rekebishi (rehabilitation) katika vituo na miundombinu ya kusafirishia umeme nchini.

**3.2.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)**

**Mheshimwa Spika**, kuhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kamati ina mapendekezo yafuatayo:

**a) Madeni**

**Kwa kuwa**, Shirika linakabiliwa na madeni mbalimbali kutoka kwa wadau mbalimbali.

**Na kwa kuwa**, Shirika pia linaidai Taasisi ya TANESCO ambao ndio mlaji/mnunuaji mkubwa wa gesi,

**Hivyo basi**, Bunge linashauri Serikali kuweka utaratibu mahususi wa kumaliza madeni haya ya Taasisi hizi za kiserikali. Aidha, kuangalia namna bora ya kuendelea kupeana huduma.

**b) Uzalishaji wa Gesi nyingi kuliko inavyonunuliwa**

**Kwa kuwa**, TPDC haina uwezo wa kujenga miundombinu ya kusambazia gesi inayozalisha na hivyo kushindwa kulifilia soko la watumiaji,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo inasababisha TPDC kushindwa kuuza gesi hiyo na hivyo kukosa mapato yatakayoiwezesha kuijendesha kibiashara kama ilivyo kusudiwa,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali kuiwezesha TPDC kutekeleza mradi wa kusambaza gesi katika Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kujenga miundombinu ya kusambaza gesi kwa watumiaji.

**c) Ufinyu wa bajeti kwa shughuli za TPDC**

**Kwa kuwa**, bajeti inayotengwa na Serikali kwa ajili ya TPDC ni ndogo na fedha zake hazipatikani kikamilifu na kwa wakat,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo inachangia kuikwamisha TPDC katika utekelezaji wa shughuli zake,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali kuipatia TPDC bajeti ya kutosha na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya msingi kama inavyotakiwa.

**3.2.4 Chuo cha Madini Dodoma (MRI)**

**Kwa kuwa**, Chuo cha Madini kinakabiliwa na ukosefu wa fedha kutokana na kutotengewa fedha za maendeleo katika bajeti iliyopita,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo inasababisha chuo kushindwa kukarabati miundombinu ya mafunzo ili kiweze kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani za ufundi mchundo na ufundi sanifu katika sekta ya madini,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali kukiwezesha chuo hiki kwa kikitengea bajeti ya kutosha na kukipatia fedha kwa wakati. Aidha Serikali iangalie uwezekano wa kukifanya chuo hiki kishirikiane na taasisi nyingine za kitaaluma ili kuendeleza taaluma hizi adhimu nchini.

**3.2.5 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)**

**Kwa kuwa**, Wakala wa Jiolojia nchini imepewa jukumu muhimu la kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza taarifa mbalimbali za kijiosayansi, kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya ardhi (earth),

**Na kwa kuwa**, ufinyu wa bajeti kwa Taasisi hiyo kunachangia kwa kiasi kikubwa kuathiri utekelezaji wa majukumu hayo na hivyo kusababisha Taifa kukosa taarifa za msingi kuhusiana na jiolojia ya nchi,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali kuiwezesha kibajeti GST ili itekeleze kwa ufanisi majukumu yake, ambayo yanahuishisha pia kufanya tafiti mbalimbali kuhusu majanga (matetemeko ya ardhi, milipuko ya Volkano na maporomoko ya ardhi), ili kuiliwezesha Taifa kukabiliana nayo.

### **3.2.6 Sekta Ndogo ya Mafuta**

**Mheshimwa Spika**, kwenye Sekta ya Mafuta nchini, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:

- a) Uwezo mdogo wa mita za upokeaji mafuta (*flow meters*)

**Kwa kuwa**, mita za kupokelea mafuta zina uwezo mdogo wa kupokea mafuta,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo inasababisha mita hizo zishindwe kwenda kwa kasi inayokubalika wakati wa kupakua mafuta,

**Hivyo basi**, Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho kwenye mita za upokeaji mafuta ili ziweze kuendana na kasi ya upokeaji mafuta itakayowezesha kushusha tani 1200 kwa saa badala ya tani 400 kama ilivyo sasa.

### **b) Umuhimu wa Matenki ya Kuhifadhiya Mafuta**

**Kwa kuwa**, Serikali haina sehemu moja ya kupakulia mafuta yaani *Single Storage Terminal*, ambayo ingekuwa ndio kitovu cha upakuaji wa mafuta,

**Na kwa kuwa**, kukosekana kwa sehemu hiyo kumesababisha kuripotiwa kwa matukio ya hujuma kutoka kwa makampuni ya mafuta nchini,

**Kwa hiyo basi**, Bunge linashauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa mpango wa kuwa na sehemu moja ya kupakulia mafuta yaani *Single Storage Terminal* jambo ambalo litaiwezesha Serikali kuwa na udhibiti wa kutosha katika upakuaji wa mafuta.

#### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mhe. Job Ndugai, Spika, Mhe. Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yangu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb	<b>M/Mwenyekiti</b>
2. Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb	Mjumbe
3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Susan limbweni Kiwanga, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Zainab Mussa Bakar, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Desderius John Mipata, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb	Mjumbe

23. Mhe. John Wegesa Heche, Mb                          Mjumbe  
24. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb                          Mjumbe

Pia ninatoa pongezi kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini pamoja na Viongozi wake, Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani (Mb), Naibu wake Mhe. Subira Khamis Mgali, pamoja na Waziri wa Madini, Mhe. Angellah Jasmine Kairuki pamoja na Manaibu Waziri wake Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), a Mhe. Dotto Mashaka Biteko (Mb), na Watendaji wote wa Wizara hizi mpya kwa ushirikiano walioutoa katika kipindi hiki, ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake kwa Kamati. Pia namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Frank Mgonja kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb  
**M/Mwenyekiti**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini**  
**Februari, 2018**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa mawasilisho sasa tutaanza michango. Nimepata majina kadhaa hapa mbele ya wachangiaji kutoka Chama cha Mapinduzi, Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Chama cha Wananchi (CUF). Sasa majina kidogo yamezidi kwenye uwiano, kwa hiyo muda ambao Waheshimiwa Wabunge mtapangiwa kuchangia tutakuwa tukiangalia tunao muda kiasi gani. Tutaanza na Mheshimiwa Charles Kitwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha.

Nimekumbushwa hapa na Katibu, wachangiaji dakika 10.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo amekuwa mwema pamoja na matatizo nillyopa sasa ni mzima kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu wa Spika, nianze kwanza kwa kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu itakayowezesha uchumi wetu kupaa. Serikali imejikita katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na reli, tunakuwa na viwanja vya ndege, tunakuwa na barabara na tunakuwa na mashirika ambayo yanaweza kweli kweli kuonekana kwamba ni mashirika ambayo yana nia ya kuonesha kwamba tunajenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kikubwa ambacho nikiseme ni jinsi ambavyo Serikali imeweka kipaumbele kuhakikisha kwamba inatumia fedha zake za ndani. Hili nilisisitize kwa sababu kuna watu hapa wanasema kwamba kukopa si fedha za ndani. Hicho ni chanzo kingine katika kuhakikisha kwamba unajipatia pesa katika Serikali yako. Aidha, unaweza ukakusanya ushuru, unakusanya pesa na kupata *revenue*. Vilevile unaweza ukakopa ukapata hizo pesa na baadaye utalipa kwa kutumia pesa zako za ndani. Kwa hivyo kukopa ni pesa zako za ndani.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, pamoja na pongezi hizo niangalie tu namna ambavyo tunaweza tukahakikisha kwamba uchumi wetu unapaa kwa haraka sana. La kwanza ni *linkages*. Tunapo jenga reli, tunapopanua bandari ni lazima tuangalie ni kwa namna gani hiyo bandari itaweza kuharakisha uchumi wetu. Huwezi kuwa na bandari iliyo nzuri halafu mizigo inafika huna mahala pa kuiweka. Kwa hiyo, *dry ports* ziwekewe umuhimu unaolingana na jinsi ambavyo tunapanua bandari zetu, ikiwemo *dry port* ya pale Fela katika Jimbo la Misungwi.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, vilevile niipongeze Serikali kwa kuweka umuhimu wa pekee katika kuhakikisha kwamba Shirika letu la Simu la *TTCL* linaimarishwa. Nizungumzie umuhimu uliopo kwa Shirika la *TTCL* na tuangalie ni kwa namna gani Serikali iliangularie shirika hili kwa umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tukiingia vitani Airtel wakaondoka, Vodacom wakaondoka na mashirika ya binafsi yakaondoka tutawasiliana vipi? Ni vyema tukaona huu umuhimu na tukaweka nguvu sahihi ya kuhakikisha kwamba Shirika letu la Simu la *TTCL* linapewa kila msaada na isiwe msaada tu wa pesa au vifaa kwa sababu matatizo mengine yanatokana na namna ya uendeshaji, na hili nitajaribu kulizungumzia na nitoa ushauri kwa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu wa Spika, ushauri wa kwanza ni kuhusu usimamizi na katika kusimamia niombe Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na mfumo wa *eyes on hands off*. Serikali isiingillie ingilie haya mashirika hasa hasa yale ambayo Serikali imeya-own kwa asilimia kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni kwa nini kama Serikali imejenga ikaweka bodi imara na bodi yenyewe ikaajiri Mkurugenzi au Mtendaji Mkuu imara, na kukawa na mfumo mzuri wa mawasiliano kila siku Katibu Mkuu au Waziri aende kuweka mkono wake kwenye shirika hilo. Yeye Waziri, Katibu Mkuu na Wizara mama ihangaike na kuhakikisha kwamba tuna sera zilizo sahihi na hizo sera zinajengewa mfumo wa

utekelezaji na hao wajumbe wa Bodi pamoja na menejimenti yake kuweza kutekeleza ile sera ambayo Serikali ingependa itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, vilevile kujengwe mahusiano mazuri ya mawasiliano. Sioni kwa nini kama menejimenti wanakaa kila wiki kwa vyovyote vile wataitaarifu bodi kinachoendelea labda kila *quarter*, lakini Bodi nayo iwajibike kumweleza Waziri na Katibu Mkuu nini kinachoendelea kwenye shirika hilo angalau kwa muda ambao watakuwa wamejipangia. Hapo kila mtu atakuwa ametekeleza wajibu wake yake bila kumwingilia mwингine. Tunaangalie vilevile nilikuwa nakizungumzi *issue* ya *linkage*, hii ni kitu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unakuta tunahangaika kutengeneza reli, reli inapokuwa inajengwa kutoka Dar es salaam kuja Morogoro unaweka reli ya umeme. Ukishafika Morogoro kuja Dodoma kwanza tofauti ile *standard gauge* na ile reli iliyopo zinatofautiana. Sijui unaanza kupakua hiyo mizigo uweke kwenye ile reli nyngine ile ya zamani na vichwa vile vya ... Mimi nadhani kuwe na mpango ambao unakuwa ni wa jumla utachukua muda, lakini mnakuwa na umuhimu wa kusema kwamba tutajenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, tutajenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, kitakachokuwepo pale ni kwamba kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro itachukua muda huu; na kutoka Morogoro kwenda Dodoma itachukua muda huu na Dodoma kwenda Mwanza au kwenda Kigoma itachukua muda huu. Na katika muda huo lazima kuwe na mipango thabiti ambayo tunasema kwamba hiyo ni *transition period* ambayo itakuwa inaeleweka kwa wafanyabiashara na watu wenye viwanda nchini ambapo watakuwa na matarajio yanayoelewka, na mipango hii ifuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana kwanza nimeipongeza Serikali kwa namna ya kutafuta *revenue*.

Hakuna sababu ya kuanza kujenga nusu nusu wakati hujui kinachofuatia na huna mpango wa kupata hela. Ni vyema ukawa umejipanga kwamba nikitoka Dar es Salaam kufika Morogoro nitakuwa nimepata hela za kutoka Morogoro kwenda Dodoma na nikianza kujenga kutoka Morogoro kwenda Dodoma nitakuwa nimepata hela za kutoka Dodoma kwenda Tabora. Tusiwe na mipango ya zima moto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize hili la usimamizi wa taasisi na ili watu wengi hatuliwekei umuhimu na hatujui madhara yake. Sielewi kwa nini kwa mfano *TCRA* ambayo ni shirika ambalo kwa vyovyote vile kulingana na *sources* za *funding* yake lazima litajitegemea. Kwa hiyo, pale kinachotakiwa ni kuwa na bodi ambayo ni imara yenye watu wenye kuwaza mawazo mapana. Yale yaliyoko kwenye utaratibu au kwenye sheria *TCRA* hayo ni ya kawaida, mtu yejote anaweza akayafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, *these people should think beyond that* na tunahitaji watu wanaoweza ku-*think beyond that*, na hicho ndicho kinatupa tatizo. Watanzania wengi tunajaribu kuwaza leo nitakula nini na jioni nitakula nini. Tukitaka kuendelea ni lazima tuwaze leo tutakula nini, kesho kuna nini, kesho kutwa chakula kitapatikana wapi na wiki ijayo nini tufanye. Haya mawazo ya kuwaza leo hii, halafu kesho hujui, kesho inapofika ndipo unaanza kuwaza, tuondokane nayo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Kengele hiyo? Ni ya kwanza? (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitwanga ahsante sana kwa mchango wako, umeshamaliza muda wako, ahsante sana. Mheshimiwa Maryam Msabaha atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, dakika chache kama zitabaki tutamalizia na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa kunipatia fursa hii niweze kutoa nami maoni yangu, nami pia ni mjumbe wa Kamati, mengi tumeshayachangia kwenye Kamati; na yale mazuri pia tulivoishauri Wizara na Serikali pia wayachukue kwa mustakabari wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona haya mambo yanavyokwenda katika hii Wizara na hii Wizara haijawahi kumuacha mtu salama. Tumeona migogoro mingi ambayo imetokea kwenye hii Wizara ya Nishati na Madini, mpaka Mheshimiwa Rais akachukua jukumu la kutenganisha hizi Wizara zikawa Wizara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinii kuna mambo mbalimbali ambayo yamefanyika kwenye Kamati hizi. Tumeona yale masuala ya makinkia, mambo ya michanga yalivyo kwenda, sasa Watanzania wengi bado wanahoji pia wanataka angalau wapate taarifa kile ambacho tulikuwa tunakidai kiko wapi na ni kitu gani tulichonufaika nacho mpaka sasa hivi. Si vibaya sana tukitoa taarifa tukawaambia Watanzania kama kipindi kile tulivyokuwa tumewashirikisha namna tulivyokuwa tunaibiwa kwenye masuala ya migodi. Kwa hiyo, niiombe Serikali na Wizara itoe taarifa ili wananchi wajue ni kiasi gani tulichokipata mpaka kwa sasa hivi kwa suala lile la mchanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la wachimbaji wadogo wadogo; hawa wachimbaji wadogo wadogo huwa kuna wachimbaji ambao wanapatiwa ruzuku na Serikali. Lakini umeangalia katika suala letu la taarifa iliviyotoka umeona ni namna gani ni wachimbaji wachache sana ambao wamepata ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri sana Serikali na Bunge lako Tukufu kuhusu hii Serikali ya wachimbaji wadogo wadogo, tuangalie humu ndani kwa kina hizi pesa zimekwenda wapi, huku tukianza kuangalia tukichimbua kwa kina kuna vitu vingi sana vimefichika huku kwa wachimbaji juu ya hizi ruzuku zilizotolewa kwa Serikali kwa

ajili ya kuwafikia wachimbaji wadogo wadogo. Umeona ni namna gani wamepata wale wachimbaji, waliopata ni watatu. Sasa tuangalie zile pesa ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo hizi fedha zimekwenda wapi? Na kama zimeishia kwenye mifuko ya watu au kama watu wamepiga *deal* basi naomba haya masuala yafuatiliwe kwa kina zaidi ili tuzidi kugundua huu uozo ambaao uko kwenye Kamati ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *GST*, hawa ni wataalam na endapo tungekuwa tumewatumia vizuri hata hawa wawekezaji wanaokuja kwa kweli wasingeweza kuvamia maeneo kabla hawajapata utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie hii bajeti ambayo tunaitenga katika hii Wizara, hizi taasisi zinafikiwa au zinapelekwa kwa wakati? Sasa kama vitu kama hivi hawa *GST* hawawezeshwi kwa wakati, sasa tuangalie ni namna gani hii Wizara tuwawezeshe hawa *GST* kabla wachimbaji hawajaenda kuvamia maeneo wafanye kama utafiti kama kweli huko wanakoenda kuchimba kuna madini au wanaenda kufanya uharibifu wa mazingira. Hata kama wawekezaji wamekuja hawa wafanye kwanza utafiti wa kutosha na waangalie pale kuna madini kiasi gani ili waruhusu wawekezaji sasa nao wachimbe yale madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie wataalam ni namna gani Serikali sasa mnaweza kuwapa kipaumbele ili tuangalie tunadhibiti haya madini tunayosema tumeibiwa kwa siku nyingi yawanufaishe Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi sana kuhusiana na masuala ya *REA*. Niipongeze Serikali kwa haya masuala ya *REA*, lakini bado kijijini kuna tatizo sugu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unapotolewa utakuta wale wafanyabiashara au mtu ana shule yake, au mtua ana uwezo, basi wanaruka vijiji vya wale watu ambaao hawana uwezo. Niombe hao watu wakusanywe kwa pamoja umeme kama unapita usibague huyu ana uwezo,

huyu hana uwezo, ili wapate wote kwa wakati muhafaka hayo yanatotakiwa kwenye umeme wa REA.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye madeni ya *TANESCO*. Hili Shirika limekuwa likijiendesha sana kwa hasara, kama ulivyooma tulivyotoa maoni yetu kwenye Kamati yetu. Tuangalie na hawa wadaiwa sugu wanachukuliwa hatua gani na Serikali ili wapate kulipa. Hata kama ni taasisi za Serikali basi tuhakikishe ni namna gani wanarejesha haya madeni *TANESCO* ili *TANESCO* iweze kuijidesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Kamati yetu tumechambua mambo mengi mazuri yaliyoongelewa humu kwenye Kamati, naomba yachukuliwe, lakini sana sana pia niende kwenye suala la barabara. Kuna barabara hizi ambazo tumekuwa tukizijenga, lakini barabara hizi tunazijenga kwa gharama kubwa halafu zinaharibika kwa muda mchache. Sasa niulize Serikali hawa wakandarasi wanaohusika na hizi barabara wanachukuliwa hatua gani endapo zile barabara zinaharibika kwa kipindi ambacho ni cha... na watoe *guarantee* kama hizi barabara wanazozijenga zitachukua muda gani, na zikiharibika kabla ile *guarantee* haijaisha basi wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuangalie suala la bandari. Tuangalie bandari hizi bandari bubu ambazo ni tatizo, kuna vitu vingi sana vinapita kwenye bandari bubu. Sasa tunazidhibiti viperi hizi bandari bubu ili tuache kupitisha, ziache kupitisha mizigo, vitu vyaharamu na mambo mengine ili wale ambao wanakwepa kodi nao wadhibitiwe ili zile kodi zirudi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala Bandari ya Dar es Salaam kwenda Zanzibar bado kuna malalamiko sana kwa wafanyabiashara ambao wanatoka Zanzibar. Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye suala hili la wafanyabiashara wa Zanzibar. Unakuta umelipia mizigo wako Zanzibar, ule mizigo ukifika tena pale bandarini unakuwa-*charged* ushuru. Unakuta umetoka na kiporo (mfuko) chako kidogo, labda ni kiporo cha mchele au vitu

vyako vidogo vidogo umenunua unapeleka Zanzibar, kwa hiyo ukifika pale unachajiwa ushuru. Sasa tuangalie ni namna gani ili suala la Muungano kuhusu masuala ya bandari ni namna gani sasa tuliweke ili pande zote mbili zinufaikie, upande wa Zanzibar wasilalamike na upande wa Tanzania Bara usilalamike. Tusiwe kule tumeshalipa kodi wakija tena huku wanalipa kodi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa mchango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la REA, na katika hili suala la REA nianze kwa kuipongeza Serikali. Kupitia REA Serikali inafanya kazi nzuri ya kuwapelekea vijijini huduma hii muhimu katika maendeleo ya Watanzania. Pamoja na jitihada nzuri za kupeleka umeme vijijini kupitia REA, changamoto za REA ukiziangalia kwa kwa undani zinasababishwa na mambo makubwa mawili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, mimi nipo kwenye Kamati ya Nishati na Madini, tumekuwa tukiishauri Serikali zile tozo za kutoka kwenye mafuta kwenda kwenye mfuko wa REA zimekuwa *ring-fenced* lakini kumekuwa kuna mkwamo, ile hela haiendi moja kwa moja kwenye mfuko ili iweze kwenda kwenye REA kuhudumia usambazaji wa umeme vijijini.

Kwa hiyo, nipende kuiomba Serikali wakati wanafanya *wind up* tusikie upande wa Serikali ni lini hii *automation* ya *transfer* ya hela, kwa sababu mwananchi akienda kununua mafuta kwenye sheli (*Shell/Petrol Station*)

ile tozo inatozwa pale pale analipa *cash*, sasa kwanini kunakuwa kuna mkwamo? Kwa nini hii hela isiente moja kwa moja kwenye mfuko wa *REA* ili wakala wa *REA* waweeze kusambaza umeme vijiji bila kusuasua? Pia kwenye *REA* hapo hapo kwa upande wa *TANESCO* ukiangalia *TANESCO* na *REA* wanavyofanya kazi ni sawa na treni ambayo ina mabehewa mengi lakini ina kichwa cha treni ambacho uwezo wa *engine* yake ni mdogo sana.

Mheshimiwa MNaibu Spika, kichwa cha *engine* ni upande wa *TANESCO*; *TANESCO* ina madeni makubwa imefika kwenye *point* ambapo inaweza ika-*collapse* kwa sababu inadaiwa na inashindwa kutoa huduma ya umeme nchini kwa sababu ya madeni makubwa zile *cost* za *maintenance* zimekuwa *accumulative*. Kwa hiyo, ile *speed* ya *REA* kusambaza umeme vijiji inakwamishwa na *TANESCO* kushindwa kufanya majukumu yake kwa sababu haina pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipendekeze Serikali ifike mahali idara zile za *REA* ambazo zinahusika na kusambaza umeme vijiji tuvi-*merge* na *REA* ili ule ufanisi wa *REA* zile idara ambazo zipo upande wa *TANESCO* ambazo zinahusika na huduma za umeme vijiji viwe-*merged* kwenye *REA* ili *REA* iendelee kufanya kazi vizuri kama inavyofanya; halafu *TANESCO* inayobaki iendelee kutoa huduma ya umeme maeneo ya mjini. Tukifanya hivyo wananchi wetu vijiji watapata umeme vizuri bila kusua sua na upande wa mijini *TANESCO* itajikita kutoa umeme mjini. Hii itatupeleka kwenye dhamira ya kwenda kwenye uchumi wa viwanda na kwenda kwenye uchumi wa kati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumza ni miradi mikubwa ambayo Watanzania wanaisubiri kwa hamu kubwa sana ya kutufikisha kwenye uchumi wa viwanda. Miradi hii ni pamoja na Mradi wa *Stigler's Gauge* ambaa ni mradi mkubwa sana. Ninamshukuru Rais Magufuli na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kulisimamia hili. Mradi wa *Standard Gauge Railway* ni mradi mkubwa sana, Tanzania itakuwa kama Ulaya miradi hii ikitekelezwa. Hata hivyo sisi Bunge tunatakiwa tuwe

sehemu ya kui-*facilitate* Serikali iweze kutekeleza miradi hii kwa kasi ya haraka sana kwa sababu Watanzania wanasubiri miradi hii kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nipende kupendekeza kwa mikopo ya nje ambayo inaweza ikawezesha Serikali kutekeleza miradi hii. Ifike mahali tuangalie *mechanism* ya Bunge ya kuwa na *oversight* kwa Serikali lakini bila kuikwamisha Serikali katika kuwa na wigo wa kwenda kukopa mikopo ya bei nafuu. Wakati tunajadili Kamati ya bajeti hapa kulikuwa kuna hoja kwamba kwa nini Serikali imekopa *additional* ya shilingi bilioni 1.46 kabla ya kuja Bungeni.

Sasa nipende kupendekeza kwamba Serikali mje na *mechanism* ambayo itatufanya sisi ile *checks and balance* yakuisimamia Serikali inakuwepo. Lakini Serikali bado mnakuwa na *freedom* pale fursa inapojitokeza ya kukaa na hizi *Development Financial Institutions*, kukaa na wale wanaoweza kutupa mikopo ya bei nafuu kwa ajili ya miradi ya bei nafuu kama *Stigler's Gauge* na *SGR* muweze kufanya hivyo kwa sababu hakuna Serikali ambayo inadhamira ya njema na Watanzania kama Serikali ya Awamu ya Tano. Sasa kwanini tuwe sehemu ya kikwazo badala ya kui-*facilitate* ili iweze kutoa maendeleo ambayo tumewaaahidi Watanzania kwa kasi ambayo Serikali inataka twende. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu upande wa sekta ya madini hasa hasa wachimbaji wa kati na wadogo. Kwa miaka mingi tumeona watu wanaochukua hizi *Special Mining Licenses*, tumehangaika nao, lakini kwa sababu ya uchanga wa sekta na taasisi zetu kuendelea kuzijengea uwezo tumekuwa na changamoto kubwa sana ya kupata *fair share* ya *tax collection*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nipende kupendekeza kwamba Serikali ifike mahali jitihada zote tuzipeleke kwenye hawa wachimbaji wa kati ambao tukiweza kuwa-*facilitate* wataweza kutengeneza ajira humu humu nchini na pia yale mapato ambayo wanayapata

yatawekezwa hapa hapa Tanzania, badala ya kuendelea kuangaika na ku-*facilitate* wawekezaji wakubwa wa Kimataifa ambao wanafanya *tax planning*, madini yetu yanaenda kodi hatuzioni, wanatuachia mapango tu kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Serikali kwa sababu ipo katika ku-*reform* ili kuhakikisha *resources* za nchi zinawanufaisha Watanzania jambo hili nadhani limefika mahali pake. Tumetembea kwenye mikoa ambayo inachimba dhahabu wachimbaji wa kat i wana uwezo mkubwa sana. Teknolojia za dunia sasa hivi zinaweza zikawa adopted na hawa wachimbaji wa kat i wakaweza kuisimamima migodi vizuri lakini pia wakaajiri Watanzania na mapato wanayopata yanabaki hapa hapa nchini.

Kaka yangu Mheshimiwa Lubeleje ameniomba dakika chache nimuachie kwa hiyo naomba niishie hapo ili Mheshimiwa Lubeleje kaka yangu uweze kutumia hizo dakika. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa George Malima Lubeleje

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, na nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kunipa hizi dakika tano. (*Makofii*)

Kwanza kabisa nzungumzie *REA*. *REA* awamu ya kwanza, *REA* awamu ya pili usimamizi wake haukua mzuri ndiyo maana miradi mingi ilikwama. Kwa mfano kuna vijiji vya Tambi, Nambori, kijiji cha Saa Zima, kijiji cha Igoji Moja na Igoji Mbili, tayari nguzo zipo na nyaya zipo lakini *transformer* hakuna. Kwa hiyo nilikuwa naomba sana katika *REA* hii ya awamu ya tatu waweke *transformer* ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna vijiji ambavyo havijafikiriwa kabisa kupata umeme. Kijiji cha Kiboriani, Ngaramilo, Mkanana, Chamanda pamoja na

Iwondo hazijapelekwa nguzo wala nyaya. Kwa hiyo naomba sana hii REA awamu ya tatu wawakumbuke basi wapate umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, kukatika katika kwa umeme Mji wa Mpwapwa na maeneo mengine imekuwa ni kero kubwa sana, kila wakati kwa siku umeme unaweza kukatika mara mbili/tatu. Sasa kwanza unaweza kupata hasara ukaunguza vitu kwenye *fridge*, lakini pili kwa sababu wananchi wanalipa *bill* kwa hiyo lazima huduma ya umeme iwe nzuri. Sasa kisingizio cha TANESCO kwamba kwa sababu ya mvua na kuna baadhi ya nguzo zipo kwenye mabwawa, nguzo zingine zimeoza.

Mimi nashauri wabadilishe nguzo zote zile ambazo zimeoza. Kama inawezekana nguzo ziwekwe za chuma ambazo haziwezi kuoza, haziwezi kuliwa na mchwa hii inaweza kusaidia sana ili wananchi waweze kupata huduma ya umeme Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla. Kwa hiyo ya kwangu yalikuwa ni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. (*Makofii*)

#### **NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje.

Waheshimiwa Wabunge, nitasoma majina ya wachangiaji wetu wa mchana kabla hatujaendelea, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Boniface Getere Mwita, Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, Mheshimiwa Menrad Kigola, Mheshimiwa John Heche, Mheshimiwa Marwa Ryoba, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Kiza Mayeye.

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo watakuwa wachangiaji wetu wa mchana, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na wachangiaji wetu ambao nilikuwa nimewataja asubuhi kabla hatujatoka na tutaanza na Mheshimiwa Dustan Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa John Heche ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba mbili hizi za Kamati; Kamati ya Miundombinu lakini vilevile Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Miundombinu imesisitiza umuhimu wa kuimariswa barabara zetu. Katika ule ukurasa wa 37, anazungumzia umuhimu wa kuunganisha makao makuu ya mikoa kwa mikoa. Vilevile katika ukurasa wa 38, naomba kunukuu kipengele (d), anasema, kuendelea na ujenzi wa barabara za lami hasa maeneo yanayochocha uchumi wa Taifa letu kama vile maeneo yenye vivutio vya utalii, kilimo, viwanda na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili, napenda niikumbushe Serikali, imekuwa ikitoa ahadi nyingi kwa barabara za namna hii hasa katika Mkoa wa Tanga na upande kwa Kilimanjaro. Ipo barabara inayounganisha Mkoa wa Tanga na Kilimanjaro lakini ni barabara ya kimkakati maana inapita kwenye maeneo muhimu ya ukuzaji wa uchumi, utalii na viwanda. Ni barabara kutoka Tanga - Mabokweni - Maramba - Mtoni Bombo - Mlalo - Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili kwanza linagusa usalama wa nchi yetu, maana ni eneo la mpakani lakini vilevile kiutalii ni eneo ambalo ukitokea ukanda wa Tanga mpaka kule Same unazungumzia kuunganisha utalii kutoka Mombasa, Saadani na Mbunga ya Mkomazi ambayo inaanzia upande wa Mkinga inakuja mpaka Mlalo, inakuja mpaka Same tunaelekeea Kilimanjaro na maeneo ya namna hiyo.

Kwa hiyo, rai yangu, barabara hii imekuwa ikipewa ahadi kwa muda mrefu, ni wakati sasa upembuzi yakinifu ufanyike barabara hii iwekewe utaratibu wa kuwekewa lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka kwenye taarifa ya Kamati hiyo, sasa nizungumzie taarifa ya Kamati ya Nishati. Nataka niipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayofanya kwa kupeleka umeme vijiji kupitia mradi wa *REA*. Tulipoanza na *REA* / tulifanya makosa lakini ilikuwa ni sawasawa tufanye makosa kwa sababu tulikuwa tunajifunza. Tumekwenda *REA* // hali kadhalika tumefanya makosa, yapo tuliyorekebisha lakini bado kuna makosa tumefanya katika usimamizi wa miradi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeingia *REA III*, hatuna nafasi ya kufanya makosa kwa sababu tulishapata fursa ya kufanya majaribio na ku-test jinsi yakwenda. Tunakwenda kwenye *REA III* tumekubaliana kwamba kila kijiji kitakachoguswa tuhakikishe hakuna kitongoji kinaachwa. Naisihi sana Serikali tusije tukarudia makosa ya *REA I* na *REA II* ya kuacha baadhi ya vitongoji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu zipo changamoto tumeanza kuziona. Kule Jimboni kwangu kwenye maeneo ya Kidiboni, Kitongoji cha Chakachani kimesahaulika. Ninayo ahadi kwamba kitafanyiwa kazi naiomba Serikali ilikumbuke hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipofanya *REA* / tulialiha baadhi ya sekondari, Sekondari za Reanzoni, Duga na Kigongoi. Tunapokwenda sasa kwenye *REA III* kwa sababu sekondari hizi zipo jirani na maeneo haya basi tuhakikishe tunaziingiza kwenye mpango ili ziweze kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nataka kuzungumzia deni la *TANESCO*. Ukienda ukurasa wa 23, Kamati inasema, madeni ya *TANESCO* yanasaababisha kuzorota kwa utendaji wa shirika. Aidha, madeni yameendelea kuongezeka na hakuna jitihada zozote za Serikali za kusaidia kumalizika madeni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo hali nzuri, *TANESCO* ina madeni makubwa. Ukienda kwenye ukurasa ule inaonesha kwamba deni la *TANESCO* limefikia bilioni 913 na katika hizo takribani bilioni 200 ni madeni yanayotokana na taasisi za Serikali. Naisihi sana Serikali ije na mkakati maalum wa kuhakikisha deni hili la *TANESCO* linalipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati tuliwahi kuletewa taarifa kwamba Serikali ina mpango wa kukopa fedha Benki ya Dunia ili tulipe madeni haya. Naisihi sana Serikali yangu isiende kukopa Benki ya Dunia ili tulipe madeni haya, tutafute njia nyingine za kulipa madeni haya. Wenzetu Afrika Kusini wana mzigo mkubwa sana kutokana na *ESKOM* inashindwa sasa kufanya kazi, inakuwa mzigo hata kwa nchi zinazopata umeme kutokana na Shirika la Umeme la South Africa. Tusije tukaingia kwenye mtego huo wa kusababisha tukapata umeme kutoka Afrika Kusini ambao bei yake ni ghali. Tuisaidie *TANESCO* iweze kutupatia umeme kwa bei ya chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba tujifunze kwa wenzetu wa Ghana. Wenzetu Ghana waliamua kuanzisha *energy bond* na katika kufanya hivyo wameweza kukusanya dola milioni 750 ambazo zinaelekezwa katika sekta ya umeme. Kama tunataka kusaidia *TANESCO* tuangalie *option hii*, tujifunze wenzetu walifanya nini, tuone kama tunaweza kuleta *energy bond*, wananchi wanunue *bond* hizo na tuweze kusaidia Shirika letu la *TANESCO* liondokane na mzigo wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nataka kuipongeza sana Serikali kwa uamuvi wake thabiti wa kuamua kuja na Mradi wa Umeme wa Mto Rufiji, ni hatua kubwa ya kimapinduzi, tumechelewa. Wenzetu Ethiopia wameamua kuwa *energy hub* saa hizi wanazungumzia kuzalisha *megawatt* 10,000 kutokana na chanzo cha Mto Nile. Sisi tutumie mto huu vizuri kuwekeza ili tuweze kupata umeme wa uhakika ili ndoto yetu ya kuwa na uchumi wa viwanda iweze kutimia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu tuko katika hatua za mwanzo ambazo utekelezaji utaanza hivi karibuni. Naipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji huu kwa kutumia bajeti za Wizara mbalimbali ili hatua za mwanzo ziweze kutekelezwa. Rai yangu, Bunge hili lishirikishwe ipasavyo, Wabunge wa Bunge hili wapate semina ya nguvu ili kujenga ulewa wa pamoja ili tutakapokuja kuleta bajeti ya mradi huu iweze kupita kwa urahisi tukiwa kitu kimoja, tukiwa tunaelewana kwamba jambo hili ni jambo la kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa John Heche na Mheshimiwa Marwa Ryoba ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo ili nami niweze kuchangia Kamati hizi mbili. Awali ya yote nizipongeze Kamati zote mbili kwa uwasilishaji wa umakini kabisa na kazi nzuri iliyofanywa na Kamati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nielekeze ushauri kwa Serikali. Serikali ya Awamu ya Tano au Serikali ya Chama cha Mapinduzi hebu tupunguze umakini unaotupelekea kutokuwa makini. Kwa mfano, mradi huu wa reli ya *standard gauge* tumesaini mwaka mmoja na Kenya, Kenya wamemaliza lakini sisi kwa sababu ya umakini tumechelewa mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam yuko mwekezaji pale aliletä ombi lake la kujenga *grain terminal* miaka kumi na moja (11) imekwisha mpaka leo haijajengwa amekwenda Msumbiji amepewa miaka miwili *grain terminal* inafanya kazi. Tanzania tuko makini mno, huu umakini ndiyo unaotupozea muda na kuonekana tuko nyuma. Naomba hilo mlichukue kama ni changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye hotuba za Kamati mbalimbali. Kamati zote ambazo zimeshawasilisha hapa taarifa zake, tatizo hili la upatikanaji wa fedha kila Kamati lazima iguse. Tunalo tatizo kwenye Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya utoaji wa pesa, pamoja na kwamba tulipopitisha bajeti Wizara nyingi zilikuwa zinalalamikiwa kwamba pesa hazitoshi lakini hata zile kidogo zilizotengwa bado haziendi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limekuwa likigharimu sana miradi yetu ya maendeleo kukwama. Miradi mingi hapa ambayo leo hii hajatekelezwa tatizo kubwa ni upatikanaji wa pesa. Sasa hatuelewi tatizo hili ni nini na dawa yake ni nini, ni tatizo sugu kwa mimi ninavyoliona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi wa bandari hasa nikianzia na bandari yetu ya Dar es Salaam. Kabla sijaingia kwenye Bunge hili Gati namba saba, moja na mengine tangu mwaka 2008 linatajwa mpaka leo lipo kwenye vitabu tu. Mnaendelea kutuchafulia makaratasni tu Gati namba tatu , namba nne hatuelewi nini kinachoendelea. Tunawaombeni sana sana wote sisi tuna uchungu na nchi hii hebu tufanye kazi tuache kufanya kazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanja vya ndege. Nashukuru Serikali imetuletea takwimu hapa, viwanja vingi vinaonekana vinataka kufanyiwa ukarabati, lakini hivi kweli tunajenga hivi viwanja hivi kwa mikakati ya kiuchumi au kukidhi matakwa ya kisiasa? Kwa sababu mimi kama ungeniuliza mikakati ya kiuchumi ningekutajia viwanja kama cha Mtwara, Kigoma, Songwe - Mbeya na hicho cha Mwanza ambacho mmekikazania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa zaidi hatuna vipaumbele, tuna viwanja hapa tumeviandika lukuki lakini mwisho wa mwaka vyote hivi hakuna kilichokwenda. Hivi kwa nini hatuwezi kuamua tu mwaka huu tunashughulika na kiwanja namba A, mwaka mwingine namba B ili twende kuliko kurundika viwanja vya ndege lukuki ambavyo vyote hivi mwisho wa siku hatuwezi kuvifanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Wakandarasi kwa mujibu wa sheria ndiyo mlezi wa wakandarasi lakini hivi kweli bodi hii inalea wakandarasi hasa hawa wazawa, tunawajengea uwezo kiasi gani? Mikakati ya kuwajengea uwezo wakandarasi hawa wadogo tunayo, mbona haileweki? Mimi naionomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi sisi wote nchi hii ni ya kwetu, wote ni wazalendo na haya tunayashauri kwa uzalendo mkubwa sana, naomba myachukue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati pametajwa sera ya kuunganisha mikoa yetu kwa barabara, mikoa kadhaa imetajwa, lakini nisikitike tu Mwenyekiti wangu alisahau tu, Mkoa wa Lindi na Morogoro hajautaja. Lindi na Morogoro unaunganishwa kwenye Wilaya ya Liwale na Wilaya ya Mahenge na hili tumelipigia kelele sana lakini kwenye vitabu hivji bado halijaweza kuonekana. Nawaombeni sana jambo hili ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*USCAF*). Huu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa mujibu wa taratibu unachangiwa na makampuni mbalimbali ya simu, hatujapata malalamiko kwamba makampuni haya hayajawahi kuchangia lakini tunapata malalamiko (*USCAF*) wana uhaba wa pesa. Sasa uhaba huu wa pesa unatoka wapi, iwapo haya makampuni yanachangia? Maana ukienda kuwaauliza wanasesma miradi mingi haitekelezwi kwa sababu ya pesa lakini source zile za pesa zinapatikana kwamba hawa wanachangiwa na kampuni za simu na zinachangia. Kwa nini pesa hizi Serikali hamtaki kuwapa hawa watu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mimi niende upande wa madini...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka nakuongeza dakika moja, muda wako mnagawana na Mheshimiwa Kiza Mayeye, kwa hiyo, malizia hoja yako.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niangalie tu upande madini, kule kwetu Mtwara kuna Kanda ya Mtwara ambayo ofisi yake moja iko Nachingwea, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ina madini na soko lake liko Nachingwea. Sisi watu wa Halmashauri wa Wilaya ya Liwale tunapataje faida zaidi ya kuachiwa yale mashimo iwapo soko la madini liko Nachingwea na mratibu wa Kanda yuko Nachingwea. Naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie hili limekaaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa John Heche, atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajilandae.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia ili niweze kusema kidogo kuhusu hoja zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya matatizo makubwa ambayo nchi yetu imekuwa ikitabiliwa nayo ni ufisadi mkubwa unaolelewa na Serikali hii ya CCM. Ufisadi huu umekuwa kwenye miradi mbalimbali ya Serikali na kila mipango inayopangwa ukiangalia ndani yake unakuta kuna mkono wa kifisadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010 mpaka mwaka 2013/2014, kulikuwa na msukumo mkubwa sana kuhusu suala la gesi kule Kusini. Msukumo wa hali ya juu kweli kweli, wananchi kule wakapigwa, wakawekwa ndani, likapelekwa mpaka Jeshi, watu wakawa *tortured* kwelikweli. Wakati ule hapa Bungeni kikaingizwa kitu tunaambiwa kwamba sasa tunataka *ku-shift* kutoka kutumia umeme wa *hydropower* tunakwenda kwenye umeme wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni Serikali ya Kikwete na ilikuwa ni mipango ya Serikali ya Kikwete. Watu

wakalazimishwa kule likajengwa bomba pesa zikakopwa kwa walipa kodi maskini wa nchi hii wakawekewa kitu kwa kubambikiwa. Wananchi wa Kusini hawakukubali lakini mkatumia nguvu nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo baada ya miaka mitatu, minne tume-*shift* tena tunaambiwa sasa tunakwenda kwenye *Stiegler's Gorge*. Serikali iliyoingia hii sasa na yenye we inatafuta jinsi ya kupiga, tutapigia wapi, sasa tupigie kwenye *Stiegler's Gorge*. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba la gesi liliojengwa kwa gharama kubwa kweli kweli matumizi yake tumeambiwa kwenye Kamati ni mpaka sasa ni asilimia sita tu peke yake na tuliaminishwa na Watanzania wakaaminishwa kwamba sasa hatutaki tena kutumia umeme wa maji kwa sababu *is not anymore reliable*. Sasa umeme unaoamini ka ni umeme wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali hiihii, ya Chama kilekile, Rais aliyeo ndiye alikuwa Waziri kwenye Serikali hiyohiyo, alikuwa kwenye Baraza la Mawaziri linalopanga mipango, leo amekuja anatuambia sasa tunaenda *Stiegler's Gorge*. *Stiegler's Gorge* hajawahi kuingia kwenye bajeti. Ukisoma kitabu cha bajeti cha mwaka jana hakuna kitu tulichojadili kuhusu *Stiegler's Gorge*. Hakuna pesa zilizopangwa kwa sababu Bunge hili ndilo lipo kwa niaba ya wananchi kupanga mipango na ku-authorize matumizi ya pesa kwa niaba ya wananchi wa nchi hii ambao ndiyo walipa kodi. Bunge hili halikuwahi kupanga hicho kinachoitwa *Stiegler's Gorge*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sawa ni mradi mzuri na wote tunautaka, lakini kama tuliwekeana utaratibu na kama mwaka juzi tu tumechukua pesa za walipa kodi tukapeleka kwenye bomba, kwa nini tusi-utilize bomba kwa matumizi ya asilimia mia moja kabla hatujahamia kwenye hiki kinachoitwa *Stiegler's Gorge*? Kama siyo kwamba kuna wingu la kaufisadi kapya kanatengenezwa hapa kwa sababu

ufisadi uliokuwepo sisi hatukugusa? Kwa nini leo tunachukua pesa wakati bomba hili tunalitumia kwa asilimia sita peke yake? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri ni lazima Serikali ije hapa na majibu, iwaambie Watanzania kwamba gesi tulyowaaminisha miaka miwili, mitatu, iliyopita kwa Serikali hii hii ya Chama kilekile ni nini kimeikumba gesi. Kwa nini gesi inatumika kwa asilimia sita na sasa tunahama tena kurudi kwenye *hydro* ambayo tuliwaambia wananchi kwamba haiko *reliable* kwa sababu mvua zetu haziaminiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili bwawa tumeambiya juzi kwenye semina tarehe 3 lina urefu wa kilometra 100 yaani kama unatoka Chalinze mpaka Dar es Salaam na upana wake ni kilometra 25. Mimi ninachotaka kutoka hapa Waziri atuambie hizo pesa ambazo angalau wamefikiria kwamba wanataka kuzitoa kwa ajili ya ujenzi wa hili bwawa, wanakadiria kutoa shillingi ngapi na kwenye bajeti ipi na waliipitisha wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wamesema *within three months* tayari kutakuwa na *mobilization* inafanyika pale kwa ajili ya kuanza kujenga bwawa. Sasa huyo aliywapitishia hizo hela ni nani? Nani anatoa mamlaka ya pesa nyngi hizo kupitishwa kinyemela hivyo bila Bunge hili? Ni nini kazi ya Bunge hili ambalo wananchi maskini kila siku wanatoa kodi, wanajinyima kwelikweli, mama zetu hawawezi hata kununua vidonge lakini wanalipa kodi kutulipa sisi mamillioni ya pesa tukae hapa tujadili mipango yao na hatufanyi hiyo kazi, tuna haja gani ya kuendelea kuwa hapa? Tunataka Waziri atuambie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye *REA*. Mwaka jana tulizindua kitu kinaitwa *REA* wakaja wakandarasi na Naibu Waziri wakati ule sasa hivi Waziri rafiki yangu kweli, tulikuwa naye pale Bunda. Wakaja wakandarasi wakatuaminisha kwamba kufikia Desemba, kwa mfano, miradi ya *densification*, Waziri ni rafiki yangu na yeye yuko

hapa atathibitisha ninachokisema, kwamba *densification* Desemba umeme unawaka. Kwanza ilikuwa Oktoba baadaye ikasemekana sijui imekuwaje Desemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza maeneo kwa mfano ya Sirari kwenye mji ambao una *population* ya watu 45,000, hawana umeme pale. Hata mradi wa *densification* wenyewe tulioahidiwa hakuna kitu wala hakuna hata nguzo zilizopelekwa mpaka sasa hivi mradi tulioambiwa Desemba utakuwa umewaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi pesa za *REA* Mheshimiwa Waziri ziko wapi? Kwa sababu hizi pesa siyo za bajeti wala sio za nini, ni pesa za walipa kodi maskini ambapo kila siku tunanunua *petrol* tunakatwa Sh.50. Mama kijijini kule akinunua mafuta ya taa mnakata pesa au hizi pesa tena mnachukua mnaenda kununulia Madiwani wakati hizi pesa zinatakiwa zilete umeme? Zinaenda wapi pesa ambazo ziko *ring-fenced*? Pesa ambazo zinatolewa kabisa zikiwa na matumizi, mtu anaenda kununua mafuta anajua matumizi yake ni kwamba zituletee umeme wa *REA*, ziko wapi na ni kwa nini haziendi kwenye *REA*? Nataka Waziri atuambie hiso pesa ziko wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wamesema *TANESCO* inadaiwa na sisi wote ni wajumbe tunajua *TANESCO* inadaiwa. *TANESCO* hiyo ambayo inadaiwa iko hoi, wameenda tena kubomoa na jengo lake linalokadiriwa kufikia bilioni 54, sijui ni la kwake au walikuwa wamepanga au nini. Yaani mgonjwa ambaye yuko mahututi kwelikweli anaweza kufa sasa wamenyang'anya hadi sehemu ya kulala ananyeshewa na mvua. Sasa hawa hivi mipango yao ni ipi? Ni kwenda mbele au wanaenda mbele hatua mbili, wanarudi kumi na tano nyuma wanajipongeza? Kwa sababu sasa hivi wamedhibiti vyombo vyaya habari, wanadhibiti hata Wabunge kuongea, wakiongea tu wanashughulikiwa yaani wao wenyewe wanajifungia wanafanya maamuzi ambayo miaka mitatu ijayo mbele au kwa sababu wanajua mwaka 2020 hawarudi sasa wanataka tukiingia Serikalini tusikute chochote hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama leo wanakwenda kukopa kwenye benki za kibiashara kuwekeza kwenye mradi mkubwa kama wa *Stieglers Gorge* wanalipaje hizi pesa? Kama siyo kwamba wanataka Serikali itakayokuja ishindwe kufanya kazi yake? (*Makofii*)

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche kwanza kengele imegonga, kwa hivyo, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mlinga amemaliza kuchangia, kwa hiyo huwezi kumpa taarifa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Naomba niseme machache kuhusu Kamati hii ya Miundombinu na hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa naona kuna Wabunge wamejiuzulu Ubunge wao na Madiwani eti wanamuunga mkono Magufuli kwamba amefanya mambo mazuri sana katika nchi hii. Huwa nakaa najiuliza mpaka leo sijapata majibu, kwamba Magufuli amefanya mambo makubwa kwelikweli. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikachukulia *sample* ya Mkoa wangu wa Mara mpaka leo haujaunganishwa na barabara ya lami na Arusha ambayo Muasisi wake ni Nyerere

mwenyewe. Nyerere akafa akawaachia wengine kuongoza nchi hii mpaka leo na Magufuli amekuwa na historia ya kuwa Waziri wa Wizara hiyo kwa muda mrefu sana. Mwaka 2013 wameanza kutengeneza barabara ya kuunganisha Mkao wa Mara na Mkao wa Arusha wakaanza na kilometra 50. Imepita miaka sita kilomita 50 hazijakwisha hata kilometra sita tu wameshindwa kumaliza. Hiyo ndiyo Serikali ya CCM, nijiuzulu leo nimuunge mkono wakati barabara imemshinda. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016/2017 ikatengwa shilingi bilioni 20 kwenye barabara hiyo, upande wa Mara bilioni 12 upande wa Arusha bilioni nane. Upande wa Arusha wakatangaza tenda wameshaanza kulima. Upande wa Mara bilioni 12 kipande cha Mugumu - Nata mpaka sasa hivi wanaendelea kutangaza tenda, bajeti ya 2016/2017. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Ryoba niko tayari kujiu zulu kuwaunga mkono, lakini mbona sioni sababu ya kuwaunga? Nipeni sababu ya mimi kujiu zulu kuwaunga kama barabara ndogo tu ya kuunganisha Mkao wa Mara na Arusha imewashinda. Kwa hiyo, bado, bado sana. Kwa hiyo, niwaambie wananchi wa Mkao wa Mara adui yao ni CCM na Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo mkoa ambao ametoka Muasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hata Uwanja wa Ndege hakuna. Hakuna uwanja wa ndege wa maana Mkao wa Mara. Nani leo, Waziri gani, Mbunge gani wa CCM asimame hapa aniambie Mkao wa Mara haustahili kuwa na Uwanja wa Ndege tena wenye hadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016/2017 ilitengwa bilioni mbili kwenye Uwanja wa Chato, baadaye nikasikia bilioni 39.15 zimetokea wapi mbona hatujawahi kuziona kwenye bajeti mniambie! Kama kweli mnampenda Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, unachukua bilioni 39 unapeleka Chato kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani Mheshimiwa Waziri wewe ni rafiki yangu lakini naongea mambo ya kitaifa kidogo inauma. Pale ambapo anatokea Muasisi wa Taifa hata uwanja wa ndege na barabara hakuna. Leo Mkoa wa Mara kwa mfano hakuna Jimbo hata moja ambapo wanakunywa maji safi na salama, hakuna! Asimame yejote hapa aniambie Mkoa wa Mara kuna Jimbo lenye chujio, wapi? Tarime wanakunywa matope, Musoma Mjini wanakunywa jinsi yalivyo, wanaugua *amoeba* na minyoo hivyo, sasa ninyi niwaunge kwa lipi, si mnisaidie? (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua nilikuwa napita kwenye hiki kitabu cha Kamati ya Miundombinu, ninyi Wajumbe wa Kamati mniambie, nimesikia mmeitisha mpewe taarifa ya Uwanja wa Chato, Waziri amegoma kuwaleta na umetumia billioni 39! Kwenye kitabu humu naangalia naona viwanja vingine, hivi uwanja wa Chato unajengwa au haujengwi na kama unajengwa kwa nini haumo humu? Wajumbe wa Kamati nataka majibu, kwa nini hauko humu? Wabunge nataka majibu kwa nini hauko humu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu mkandarasi anayejenga huo uwanja unajua ni nani? Ni yule ambaye ameshindwa kumaliza zile kilometra 50 pale Mkoa wa Mara, ndiyo amepewa Mayanga nani mwingine si ndiyo huyo? Kisa rafiki yake na nani, Magufuli, ooh haya, twende kazi. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleee...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa naomba ukae, Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuheshimu sana mchango wa Mheshimiwa Mbunge lakini naomba nitumie Kanuni ya 68(1) ya Utaratibu na Kanuni ya 68(7) ya Mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kanuni ya 68(1) ya Utaratibu, Mheshimiwa Mbunge anayo hoja ambayo imewekwa mbele yetu na inachangiwa, lakini anapoendelea na mchango wake ameendelea kugusa pia Kanuni ya 64(1)(b) na (d) na nitazisema hizo Kanuni ambazo nimezitaja hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza Kanuni ya 64(1)(d), Kanuni hiyo inatukataza kabisa katika kutumia maneno ndani ya Bunge ili kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote ama kuwashawishi Wabunge waelewé jambo hilo lakini kwa kutumia jina la Rais, hiyo inakatazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Marwa hapa anajaribu kuliaminisha Bunge kwamba mchakato wa tenda ambayo inaendelea katika uwanja wa Chato, mkandarasi amepewa kazi hiyo eti tu kwa sababu ni rafiki wa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, hiyo siyo sahihi na hiyo ni kuvunja Kanuni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukienda katika Kanuni ya tisa (9), kila Mbunge atalisemea jambo ambalo liko katika mjadala tu na jambo ambalo Mheshimiwa Ryoba amelizungumza sasa hivi, ameendelea kudai kwamba tunaendelea na shughuli hizi za michakato ya miradi lakini tunachokifanya ni kuendelea kuwanyanyasa wananchi wa Mkoa wa Mara, jambo ambalo si la kweli. Mawaziri watakaposimama watatoa mifano ya namna gani Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo makubwa sana katika Mkoa wa Mara na mikoa mingine katika nchi hii ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kwa sababu mchangiaji anaendelea kuvunja Kanuni na kadri anavyoendelea kushangiliwa yeye anaendelea kuvunja Kanuni. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako ili kanuni hizi zisiendelee kuvunjwa. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Msigwa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama ametoa maelezo kwa kirefu kiasi kuhusu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikilizana, tuisipende kuropoka kila wakati, tafadhali. Mheshimiwa Khenani, mimi nazungumza na wewe unazungumza, unataka kufanya nini?

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jenista amesimama akitaja Kanuni ya 68(1) na Kanuni ya 68(7) lakini pia Kanuni ya 64(1)(b) na (d). Kanuni ya 68 inataka Mheshimiwa Mbunge anayesimama na kusema kuna Kanuni inavunjwa ataje Kanuni inayovunjwa, Mheshimiwa Jenista ametaja Kanuni ya 64 akisema inavunjwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha katika mchango wake.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 68(4), Spika anaweza kutoa uamuzi papo hapo juu ya jambo la utaratibu ama kuahirisha kutoa uamuzi huo mpaka baadaye na pale anapoona inafaa fasili ya (5) anaweza akatuma jambo hilo kwenye Kamati ya Kanuni ili iweze kumshauri. Kanuni ambayo Mheshimiwa Jenista anasema imevunjwa ni Kanuni ya 64(1)(b) ambayo inazungumza kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni na mojawapo inazungumzia Mbunge hatozungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala na pia (d) inasema hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika

mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.

Waheshimiwa Wabunge, nimesikiliza maelezo ya Mheshimiwa Jenista lakini pia nimesikiliza mchango wa Mheshimiwa Ryoba Chacha kwa sababu sisi kama Bunge tulishatunga sheria ya namna ya kufanya michakato na watu kupewa zabuni kwa hivyo si sawasawa kwamba kuna mtu amepewa zabuni kwa urafiki labda tu kama Mbunge anao ushahidi na kama upo nitautaka huo

Waheshimiwa Wabunge lakini kwa kuwa sinao hapa mbele na haujawasilishwa kwangu Mheshimiwa Ryoba Chacha nitakuruhusu uendelee lakini hayo maneno uliyozungumza kuhusu mchakato kwamba amepewa rafiki wa Mheshimiwa Rais kujenga kiwanja cha ndege Chato utayafuta halafu tutaendelea na mjadala. Kwa hiyo uyafute halafu uendelee na mjadala.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa unazijua taratibu, siwezi kukuruhusu wewe kuongea kabla sijamaliza hoja moja na Mbunge mmoja. Kwa hiyo, kaa tumalize ile hoja halafu utapewa nafasi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mbona hatugombani, nilikuwa naomba tu Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa naomba ukae. Mheshimiwa Ryoba naomba ufute hayo maneno halafu uendelee na mchango wako.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifute, lakini ujumbe umefika. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ryoba, naomba ukae.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na nilimtaja Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atafuatia na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia. (*Makof*)

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, si nimefuta niendelee na dakika zangu, *what is wrong?*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kushukuru kupata nafasi hii ya kuongea. Naomba niseme neno dogo kidogo, hata unapoamua kumnyonga mnyonge lakini mpe haki yake. Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano inafanya kazi nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuzungumze kwa takwimu, tuwe tunazungumza kwa takwimu. Kwanza nazungumzia Kamati ya Nishati na Madini, nazungumzia upande wa madini sasa. Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Rais Magufuli imefanya mambo makubwa mawili na mambo haya yamewavutia Madiwani wengine wanakuja wenyewe. (*Makof*)

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kudhibiti madini yasipotee na jambo la pili ni upande wa ukusanyaji wa pesa za madini. Serikali ya CCM ya Awamu ya Tano kwa kipindi hiki cha mwaka 2017/2018 nusu tu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Basi mnyamaze niseme. Kipindi nusu tu tuhatujafika mwaka 2018, Serikali imekusanya asilimia 80.4 ya makusanyo ya mwaka mzima. Lengo ilikuwa mwaka 2017/2018, Serikali ikusanye bilioni 194.397 hadi

mwaka 2018 Desemba lakini Serikali hii imekusanya bilioni 156.311 sawa na asilimia 80, sasa utasema hiyo Serikali inacheza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, msiwasikilize hawa, tumewazoea, sisi tunaangalia kazi inayofanywa na wananchi angalieni vizuri Serikali ya Awamu ya Tano inachapa kazi. Ningeshangaa sana Serikali inavyochapa kazi iungwe mkono na hawa, ningeshangaa, lazima hawa wakasirike. Kwa hiyo, msipate tabu Waheshimiwa Wabunge, twendeni kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye suala la *REA*, nipongeze Bunge la Kumi ndilo lilikuja na hii tozo ambayo imeleta manufaa kwa nchi yetu. Naomba nikubali kwamba jambo lolote linapoanza lina changamoto, huwezi kuanza jambo mara ya kwanza ukalifanya kwa asilimia 100, mara ya pili ukalifanya asilimia 100, kidogo kidogo *REA* itasimama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe takwimu, mwaka 2008 umeme vijijini ulikuwepo kwa asilimia 2.2 tu kabla ya kuwa na *REA*. Ilipofika 2015 umeme vijijini ukafikia asilimia 21.02, hayo ni madogo jamani? Serikali inachapa kazi, sasa. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** (*Allongea bila kuwasha kipaza sauti*)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Nyamaza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 mpaka Desemba, 2017 angalieni Serikali ya Awamu ya Tano inavyochapa kazi, umeme vijijini umefikia asilimia 49.5. Sasa najiuliza hivi hamuyaoni hayo, wenzetu mna macho gani, tafuteni miwani. Serikali inachapa kazi jamani Wabunge wa CCM tujivune. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Subira Mgusu, anajitahidi sana. Wiki iliyopita alikwenda Kilimanjaro, nampongeza sana, kuangalia

matatizo yaliyotokana na *REA I* na *REA II*. Kwa hiyo, Serikali inafahamu kwamba kuna changamoto, alikwenda Mwanga, Rombo na akaja Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemshangaa, Kata ya Vulha, Kata ambayo Mawaziri wachache sana wanafika, amefika Subira. Kule kuna mradi wa *REA II*, nilipambana nayo sana ile, Serikali ikapeleka umeme kule lakini haikumaliza. Mheshimiwa Waziri amekwenda kuangalia na amekwenda kuwashakikishia wananchi kwamba *REA III* inakwenda kumalizia, Serikali inafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Nishati pamoja na Naibu Waziri mlikwenda Kilimanjaro lakini kuna Wilaya ina matatizo sana naomba nisimame hapa niiombee umeme kule ambapo haujafika, Wilaya ya Siha. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Siha kuna Kata moja ambayo ina vijiji vinne, hiyo Kata inaitwa Donyomurwakna. Kuna vijiji vinne kwenye kata hii, vijiji viwili vina umeme na vijiji viwili bado umeme haujafika. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kitu kimoja, waacheni hawa, hakuna Serikali ambayo inaweza ikafanya mambo yote kwa wakati mmoja, haipo duniani. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Haipo.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiombea Wilaya yangu ya Siha kwamba vile vijiji ambavyo Mheshimiwa Waziri nimekuletea kimaandishi uhakikishe vinapata umeme na Alhamisi ya wiki hii nahamia Siha. Naomba Watanzania wawe na uhakika kwamba Siha litakuwa Jimbo la Chama cha Mapinduzi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikisha Watanzania kwamba CCM inashinda Siha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Abdulrahaman Ghasia, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mheshimiwa Kiza Mayeye ajiandae.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuzungumza. Nianze kwa kuwapongeza Wenyevitî wote wa Kamati kwa taarifa nzuri sana waliyowasilisha lakini pia bila kumsahau dada yangu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ameimalizia hivi punde. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri sana ambayo imefanya. Kuna watu ambao wanakaa wanasema tangu uhuru hatujafanya chochote, siwezi kuwakatalia kwa sababu wengi ni watoto wa miaka ya 80 na 90. Sisi ambao tumezaliwa tukiwa tunapita katika Mto Rufiji tukivuka kwa pantoni na sasa hivi tunapita katika Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji tunajua wapi tulikotoka na kazi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Wizara ya Miundombinu kwa kazi kubwa sana inayoiifanya katika kupanua bandari zetu. Katika taarifa na hata hivi karibuni mimi mwenyewe nimeshuhudia uzinduzi wa upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam pamoja Bandari ya Mtwara. Kazi kubwa sana inafanyika kule kuhakikisha kwamba kule Mtwara tunaongeza Gati namba mbili ambalo litakuwa na urefu wa mita 300. Nina uhakika kabisa baada ya hapo

korosho zetu na mizigo yetu ya Mtwara itakuwa inapita bila matatizo yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara - Newala - Masasi. Sasa hivi tayari mkandarasi yupo kazini, anajenga kipande cha Mtwara - Mivata zaidi ya kilometra 50. Niombi Serikali yangu kile kipande kilichobaki basi mkandarasi mwengine sawa na ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alivyoahidi kwamba vipande vyote vilivyobaki vitatafutiwa wakandarasi, hivyo tutafutiwe wakandarasi kwa sababu sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kazi yetu kuunga mkono bajeti yetu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba ile miradi yetu itekelezwe na wale ambao wanaikataa bajeti wasishangae katika maeneo yao kuona mpaka sasa hivi hakuna kinachofanyika kwa sababu hakuna bajeti waliyoipitisha kwa ajili ya miradi katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge* ambao unaendelea sasa hivi kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro na pia kutoka Morogoro hadi Makutupora. Pia suala la ujenzi wa viwanja vyta ndege, naipongeza sana Serikali yangu na naipongeza sana kwa kulifufua Shirika letu la Ndege kwa kununua *bombardier* zile ambazo kwa kweli wote bila kujali vyama tunazipanda na tunazitumia kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina changamoto moja tu ambayo nataka kuishauri Wizara ya Miundombinu, ndege zetu hizi zinalala au zina-park saa 10.00 au saa 11.00. Tatizo kubwa sana *bombardier* zinaweza kutua Uwanja wa Songwe, Kigoma, Mtwara, Bukoba na Songea lakini viwanja hivi vingi havina taa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Waziri wa Miundombinu ahakikishe kwamba viwanja hivi

vinawekwa taa ili ndege zetu hizi ziweze kutumika kwa ufanisi zaidi. Tunaweza kwenda Mtwara hata saa 4.00 au saa 6.00 usiku kama uwanja una taa lakini unakuta ndege zinakimbizana na jua, jua likizama na zenyewe zina-park. Pia viwanja hivi tukiweka taa tunaongeza hata usalama kwa ndege ambazo zinapita katika anga za kimataifa kukiwa na matatizo ya kutaka kutua wawe na viwanja mbadala vya kuweza kutua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanja vyetu vingi vinakosa sifa ya kuweza kutua usiku kwa sababu ya ukosefu wa taa. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa katika bajeti inayokuja ahakikishe viwanja vyote ambavyo *bombardier* inatua basi viwekewe taa ikiwemo pamoja na Kiwanja cha Mtwara. (*Makofii*)

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

## T A A R I F A

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftah, Taarifa.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Hawa Ghasia anayezungumza hivi sasa kwamba viwanja hivi viwekee taa. Taarifa ninayompa ni kwamba juzijuzi tumeweza kumsikia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa anazungumza kwamba Kiwanja cha Mtwara kimetengewa shilingi bilioni 41 kwa ajili ya kukarabati na kuweka taa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ninayompa kwamba aisisitize tu Serikali zile pesa ziweze kuletwa kweli kwa ajili ya kukarabati taa za Uwanja wa Ndege wa Mtwara. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa hiyo inaonekana mnaipokea kwa niaba ya Mheshimiwa Hawa Ghasia. Mheshimiwa unaipokea taarifa hiyo? (*Makofii*)

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa naipokea, ni kweli hizo pesa Mheshimiwa Rais amesema lakini lazima nikumbushe kwa sababu viwanja vilivyo kwenye huo mpango ni vingi, kwa hiyo, Waswahili wanasema lazima kamba kila mtu anavutia kwake. Kwa hiyo, naikubali taarifa na mimi namsisitiza Waziri kwamba zile pesa zilizotengwa hizo taa ziwekwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na upande wa Wizara ya Nishati. Nataka nizungumzie deni la *TANESCO*. Deni la *TANESCO* ni la historia, tunalo kwa muda mrefu kwa sababu muda mrefu shirika letu lilitaka kubinafsishwa. Sasa yale madeni tukisema tuiachie *TANESCO* yenye we iweze kuyalipa sidhani kama tunaitendea haki. Naishauri Serikali yangu ione uwezekano wa kuisaidia *TANESCO* kulipa yale madeni ili iweze kujikwamua na kuweza kutekeleza majukumu yake kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba *TANESCO* inadai taasisi za Serikali lakini na yenye we inadaiwa na taasisi kubwa ambayo inaidai *TANESCO* ni *TPDC*. *TPDC* inashindwa kutekeleza miradi yake mingi kwa sababu inapeleka gesi *TANESCO* na *TANESCO* anashindwa kulipa na *TPDC* naye anachukua gesi kwa watu. Kwa hiyo, naomba *TANESCO* isaidiwe kama tunataka ikimbie, tukiachachya yenye we itakwenda kila siku ikitambaa. Kwa hiyo, nataka tuiwezeshe *TANESCO* kwa yale madeni aidha Serikali iyachukue au tuwasaidie kuyalipa au tuwasaidie kukopa ili waweze kujidhesha kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka nichangie ni kwamba tuwe na *gas master plan* au mpango kabambe wa matumizi ya gesi kwa sababu sasa hivi kila mwekezaji anaweka kiwanda eneo ambalo analitaka yeye. Sidhani kama Serikali itakuwa na uwezo wa kumpelekea kila mtu gesi pale ambapo amejenga kiwanda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitenga maeneo maalumu, tukaonyesha mpango kabambe wetu kwamba

bomba la gesi litapita katika maeneo haya na yeote anayetaka kutumia gesi akaweke kiwanda chake katika maeneo hayo, nina uhakika kabisa kwamba ndani ya muda mfupi tutakuwa na uwezo wa kuwafikishia gesi katika viwanda hivyo. Bila kuwapa maelekezo kila mtu akajenga anapotaka mwenyewe, tutakuwa na gesi nyngi lakini tutashindwa kuitumia kwa sababu gharama ya kuwafikishia watu gesi itakuwa ni kubwa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kwa kuiomba Wizara ya Miundombinu kuunganisha barabara ya kutoka Mtwara - Kilambo kwa kiwango cha lami kwa sababu barabara hii inatuunganisha na nchi majirani zetu Msumbiji. Ni Sera ya Taifa kwamba barabara za Kitaifa ziunganishwe kwa kiwango cha lami. Natambua kwamba tayari kwa upande wa Mtambaswala tumeunganisha lakini watu wengi zaidi wanatumia kivuko cha Kilambo kwa ajili ya kwenda Mozambique kwa sababu ndiyo njia fupi zaidi kuliko upande mwininge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali wakati wa bajeti mara nyngi hapa tumekuwa na utaratibu wa watu kukataa kila bajeti, lakini inapokuja wakati wa utekelezaji walewale walioikataa bajeti ndiyo wanakuwa wa kwanza kulalamika kwamba kwao haijapelekwa. Mheshimiwa Rais aliomba kula kwa wananchi na alikuwa na ahadi zake na Wabunge tuliomba kura kwa wananchi tulikuwa na ahadi zetu. Kwa hiyo, zile ahadi zetu tutakuja kuulizwa sisi 2020 tumetekeleza kwa kiasi gani. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Boniface Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Kiza Mayeye, Mheshimiwa Akbar Ajali ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia. Kwanza nawashukuru Wenyeviti wa Kamati, Mawaziri wote wa Wizara hizi tatu na Watendaji wao na Manaibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanatufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia nijielekeze kwenye Wizara ya Nishati. Wizara ya Nishati kuna maeneo mawili; kuna eneo la *Densification* na eneo la *REA III*, lakini yote inatoka kwenye *REA*. Kasi ya utendaji kazi wa Wakandarasi katika Jimbo la Bunda kwa upande wa *densification* ni mdogo sana, ninavyozungumza hapa, wako *site* lakini wanaenda pole pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *REA* katika vijiji, kasi yake nayo imekuwa ndogo ingawa Mheshimiwa Waziri anafanya kazi kubwa sana ya kuanzisha hii miradi katika maeneo mbalimbali. Nami wakati fulani namhurumia, anatembea sana, lakini Wakandarasi wanaenda *slow* sana. Sasa, sijui ni upungufu wa hela au ni nini, sielewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri sasa awahimize hawa Wakandarasi katika maeneo na hasa Wilaya ya Bunda, hususan Jimbo la Bunda katika maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri alikuja akafanya uzinduzi wa Mradi wa *REA III* katika eneo la Maiwanda katika Jimbo la Bunda. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Mheshimiwa Waziri akahimiza wakaja kwenye kutenda hiyo kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *REA* kuna mambo huwa siyaelewi vizuri. Moja, ni kitu kinaitwa kilometa. Unakuta kuna upungufu kati ya watu wa *surveyya TANESCO* na *survey* ya Mkandarasi, *TANESCO* ukiwaliza, nani amefanya *survey* ya kumpa Mkandarasi aende kujua Kijiji 'A' kila kilometa tatu, kina kilometa moja na Kijiji 'B' kinawekewa transfoma mbili na Kijiji 'A' kinapewa transfoma tatu au kilometa mbili. Sasa ukiuliza *TANESCO*, wanasema ni *REA*; ukiuliza *REA*, wanakuja na takwimu, hawahusishi wanakijiji wale kujua toka mwanzo kwamba kijiji hiki kitapata kilometa mbili au mtandao wa umeme wa kilometa mbili na transfoma tatu na voti ngapi

katika hiyo transfoma. Kwa hiyo, hilo nalo ni tatizo liko hapa, Mheshimiwa Waziri naomba uliangalie vizuri ili tuweze kwenda vizuri katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Wizara ya Miundombinu. Kuna masuala ya barabara ya lami kutoka Nyamswa kwenda Bunda na kutoka Bunda kwenda Bramba na Bramba kwenda Kisorya, imechukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri anayehusika aweze kuiangalia kwa makini zaidi kwenye hiyo barabara. Kuna barabara ambayo inatoka Sanzati kwenda Mgeta na Mgeta kwenda Nata, nayo tunaomba Mheshimiwa Waziri anayehusika aweze kuiangalia vizuri hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema mambo yafuatayo:-

Kwanza, ni kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoiifanya kwenye Mkao wa Mara. Sisi Mara hatuna upungufu wa kupata Rais, tumewahi kupata Rais miaka 24, kwa hiyo, hatuwezi kulalamika kwamba Rais amefanya nini kwa miaka miwili iliyokuwepo hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kwenda India kumshuhudia mtu anafanyiwa operesheni; kuna operesheni ndogo na kubwa. Operesheni kubwa ni zile zinazohusisha matumbo kwa ndani; unatoa labda figo na vitu vingine. Mtu yejote atakayekatwa kisu kwa operesheni kubwa lazima agune na lazima arushe miguu. Kwa hiyo, ninachoona wenzangu hapa wanarusharusha miguu, naona kama operesheni ya Mheshimwia Dkt. Magufuli imewafikia. Kwa hiyo, sioni matatizo ya namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo yote anayoyafanya. Kwanza, ni kutupa Mkao wa Mara shilingi bilioni 10 za uwanja wa ndege. Kwa mara ya kwanza Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli akiwa madarakani, juzi Waziri Mkuu ametua pale na ndege kubwa. Sasa tunamlamuje kwa mambo haya? Tunapozungumza,

site watu wanaendelea na kazi. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Mkoa wa Mara shilingi bilioni nne kwa ajili ya Hospitali ya Kongwa ambayo imekuwepo toka mwaka 1975. Inaendelea kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Niabu Spika, kwa hiyo, sisi Mara tunamlaumu kwenye jambo gani? Kwa hiyo, mambo mengine yapo, yanaendelea. Naona watu wanarusha miguu tu, lakini hali ya hewa ni nzuri. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Rais pia kwa kudhibiti rushwa, kuweka nidhamu ya kazini, kudhibiti wazembe na wala rushwa, kutoa elimu bure, kuanzisha miradi mikubwa ya *Stigler's Gorge* na miradi mingine inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunachokiona hapa ni kitu kimoja; wenzetu wameshaona Messi wa CCM ni Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Kwa hiyo, ni lazima mshikeshike miguu. Wana-CCM lazima tukae tayari kumlinda Messi wetu asiumizwe, asilete madhara katika mambo hayo. Kwa hiyo, nafikiri kwamba haya ni mambo ya msingi ya kufanya, lakini naomba Wizara zinazohusika ziangalie Jimbo la Bunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kiza Mayeye, atafuatiwa na Mheshimiwa Akbar Ajali na Mheshimiwa Mendrad Kigola, ajiandae.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya leo. Nikiwa kama Mwanakamati wa Kamati ya Nishati na Madini, napenda kuipongeza Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuongelea suala la *TANESCO*. *TANESCO* ni taasisi ambayo tunaitegemea

katika nchi yetu, lakini imeshindwa kufanya kazi yake ipasavyo kwa sababu ya haya madeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la Kigoma. Mpaka leo mikoa hii ya Magharibi ambayo ni Katavi, Kigoma, tunatumia umeme wa dizeli ambaao kwa namna moja ama nyiningine unasababisha hasara kubwa kwa Serikali yetu. Sasa naiomba Serikali ijithahidi kadri inavyoweza, kwa sababu tayari wameanza mpango huu wa Gridi ya Taifa, basi mikoa hii ya Magharibi, Kigoma na Katavi tuweze kuingia katika Gridi ya Taifa haraka inavyowezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee suala la wachimbaji wadogo wa madini. Wachimbaji wadogo wengi wa madini ni vijana wa Kitanzania ambaao wengi wameamua kujishughulisha wasiingie katika wizi na wafanye kazi. Nalomba sasa Serikali iwasaidie vijana hawa, iwasaidie elimu, iwasaidie vifaa. Leo tumeona vijana wengi wamekuwa wakifunika na vifusi katika migodi kwa sababu hawana uelewa wanapoingia kule chini. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijithahidi kadri inavyoweza itoe elimu kwa vijana hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine niongelee kuhusu *REA*. Naipongeza sana Serikali, pamoja na kufanya kazi vizuri katika *REA* // lakini kuna changamoto ambazo zimejitokeza. Naomba wanapokwenda katika *REA* /// wajithahidi changamoto zile zisirudie. Kwa sababu tumeona vijiji vingine umeme unapita barabarani, lakini hauendi katika hospitali na shule. Umeme unakwenda Kijiji 'A,' lakini unaruka unakwenda Kijiji 'C', Kijiji 'B' kinakosa umeme. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, pamoja na kazi nzuri ambayo wanafanya katika Mradi huu wa *REA*, *REA* /// iende vizuri na vijiji vyote vipate umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la Chuo hiki cha Madini cha *MRI*. Tunahitaji wasomi ambaao wamebobeaa katika suala zima la madini. Leo Tanzania tunatengeneza *Tanzanite*, lakini *Tanzanite* hii ambayo tukiipeleka katika Soko la Dunia ambayo imechachuliwa

hana Tanzania, inaonekana haina hadhi sawa na ile ya India au *South Africa*. Naiomba sasa Serikali iwasomeshe watu, iwapeleke nje, wakapate ujuzi ili kesho *Tanzanite* yetu hii ioneckane sawa na ile ya India au ya *South Africa*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Waswahili wanasema mnyonge, mnyongeni haki yake mpeni. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka ukuta huu Mererani ambaa unalinda madini yetu ya *Tanzanite* yasiweze kuibiwa. Leo madini yetu hayataweza kuibiwa, yatatoka na yatapelekwa moja kwa moja kwa asilimia 100 na hakuna wezi ambaa watapitisha tena haya madini kwa njia ya chocho. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu Mbunge mmeona amemalizia na kuunga mkono hoja. Hizi hoja ni za Wenyevit wa Kamati. Sasa sisi Wabunge kama hatuziungi mkono, sjui tunasubiri nini? Wengine walikuwa wanasema Waziri ajibu; hizi hoja ni za Kamati zetu, ndiyo zimeletwa hapa. Kwa hiyo, tukumbuke tu hilo Waheshimiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Akbar Ajali, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Subira Mgala ajiandae.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Mchango wangu umegawanyika katika maeneo mawili. Kama hoja za Kamati zilivyozungumza, maana yake Mawaziri wanashauriwa kwamba miundombinu ifanye kazi kufuata utaratibu ule ambaa kwa kweli unashauriwa na Kamati, nashauri miundombinu ishirikiane na Wizara nyingine. Kwa sababu leo *TCRA* haitaki kushirikiana na Halmashauri ambazo zipo huko Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba sasa hivi tunaenda kwenye bajeti, Halmashauri nyingi zinakuwa hazina mapato, lakini minara ya simu ipo

katika Halmashauri zote, lakini *Service Levy* inakuwa hailipwi katika Halmashauri husika. Kwa hiyo, naomba Wizara iishinikize *TCRA* itoe takwimu ambazo ni sahihi ili Halmashauri ipate kutoza *Service Levy*. Kwa sababu leo minara ya simu inalipa *Service Levy* bila kuwa na habari, lakini *TCRA* ina uwezo wa kujua kwamba ni simu kiasi gani zinakuwa zinaingia kwa kila mnara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze, je, kulipa *Service Levy* ni sheria au mtu analipa kwa hiari yake? Kwa sababu kuna baadhi ya makampuni hayalipi kabisa na mengine yanalipa kwa kiwango kidogo sana. Kwa hiyo, Wizara ya Miundombinu iishinikize *TCRA* isaidie Halmashauri ili Halmashauri iweze kutoza ule ushuru kutegemeana na simu ambazo tunazitumia kutoka hayo maeneo ambayo yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama vile ambavyo nimezungumza kwamba Wizara iširikiane na Wizara nyininge, vilevile tumezungumzia hapa kuhusu Wizara ya miundombinu. Ukiangalia sana kwa mfano kule Mtwara, leo ni eneo ambalo kwa kiasi kikubwa sana wanalima korosho. Kwa asilimia karibu 70 ya *export* ya korosho inalimwa Mtwara, lakini ukienda kuangalia kule, zile barabara zote za Kitangali, Mtopwa, Luagala na Nanyamba, zimebaki mashimo. Mapato yetu ya *Export Levy*, kwa mfano mwaka huu tumepata shilingi bilioni 140 na hizo fedha huwa zinapatikana kila mwaka. Hizo fedha asilimia 65 zinakwenda kule kwa ajili ya kuboresha zao la korosho, lakini zile barabara haziboreshwii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuangalie uwezekano wa miundombinu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuona ni namna gani zile fedha ambazo zinapatikana zinakwenda kuboresha zile barabara ambazo zinahusiana na mambo ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani leo zile fedha zote ambazo ni asilimia 65 zinaondoka halafu asilimia 35 zinakwenda katika Mfuko Mkuu. Nasema kwamba kama kila

mwaka tungeamua sisi Mtwara tutumie tu *Export Levy*, basi barabara zote za Mtwara zingekuwa na lami. Sasa sisi hatutaki lami, tunataka angalau kifusi kiwepo katika zile barabara ambazo zinatumika na ambapo magari makubwa yanakuwa yanapita kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba katika bajeti yake inayokuja, basi ashirikiane na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Kilimo vilevile iangalie uwezekano, ni namna gani watajitoa kusaidia zile barabara zao? Wasiangalie tu kupata zile fedha asilimia 35 ambazo zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu na asilimia 65 ambazo zinaenda kwenye Bodii. Waangalie namna gani wananchi wananchiwanufaika kwa barabara zao kuwa bora? Isiwe kama maeneo ambayo wanachimba madini, watu wanachukua yale madini wanaondoka halafu wanaacha mashimo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri afanye jitihada za kushirikisha maeneo yote hayo mawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu nizungumzie kuhusu *REA*. Mtwara ni eneo ambapo gesi inatoka kwa wingi sana, lakini mpaka leo kuna tatizo kubwa sana la umeme. *Okay*, sisi hatuna shida kuhusu umeme, lakini hawa wananchi wana shida ya maji. Leo maji ule umeme unaopatikana Mtwara, hauwezi kusukuma maji kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ule umeme uliopo Mtwara hautoshi, achukue hatua za dharura ili ahakikishe kwamba ananunua mashine za dharura ili tuweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo hii huwezi kupata malalamiko ya maji kwa kuwa mvua zinanyesha. Itakapofikia mwezi wa tatu *it is a crisis*, itakuwa ni *war*. Asitake Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara, Nachingwea au Lindi tuje tuombe hapa chini ya dharura, kwa sababu itakuwa ni tatizo kubwa sana kupita kiasi. Kama gesi ipo Mtwara, inawezekana vipi umeme ukosekane? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri afanye jitihada zote za

kuleta mashine mpya za gesi aende akafunge katika *station* ya Mtwara. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu wa leo. Ahsanteni sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgali na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango kwenye Kamati hizi mbili; Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kutoa pongezi nyingi sana kwa Serikali. Kuna watu wengine wamekuwa wanachangia; kwanza, nimesikitika sana kwa sababu kuna kitabu hapa ambacho ni taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda ukurasa wa 12 kuna kipengele kidogo, wameeleza vizuri Serikali imefanya nini? Imeeleza vizuri kabisa, kwamba katika miundombinu; ukichukua kipengele kimoja, sitaki nichukue vitu vingi, kwa mfano pale kwenye ujenzi wa reli na tulishaongea ili nchi iweze kusonga mbele, uchumi wa Taifa ukue ni lazima tuhakikishe kwamba tumeimarisha usafiri wa reli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nilikuwa nasoma kwamba Serikali katika mipango yake mizito kuna ujenzi wa reli wa Dar es Salaam – Morogoro kilometra 205; kuna ujenzi wa reli kutoka Morogoro – Makutupora kilometra 336; kuna ujenzi wa reli Makutupora – Tabora kilometra 295; kuna Tabora – Isaka, kilometra 133; kuna Isaka – Mwanza, kilometra 250; halafu mtu mwingine anasema haoni. Jamani, hayo ni maendeleo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tukitaka uchumi wa nchi uendelee lazima Serikali

ijikite kwenye miundombinu ya reli ili tuweze kusafirisha mizigo mizito kwenye reli zetu na barabara za lami tuweze kusafirisha mabasi yetu na magari madogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishasema ndani ya Bunge hili, Serikali imefanya mambo mengi sana na tunayaona kwa macho. Nami kama Mbunge, naiunga mkono Serikali na iendelee na mikakati mizuri. Tunategemea kwamba tukifika mwaka 2020 nadhani maswali mengi sana yatakuwa yamejibowi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujenzi wa barabara kuna barabara nyingine zina changamoto. Naishukuru sana Serikali kwamba kwenye mipango ile ya Serikali ilishawekwa tayari. Kuna barabara moja ambayo wanaisema kila siku na huko kuna viwanda vingi na tunesema nchi yetu ni ya viwanda; kuna barabara ile ya Mafinga – Mgololo kilometra 84. Naiomba Serikali kama ilivyokuwa imeahidi, basi utekelezaji wake ukianza kwenye bajeti inayokuja nitafurahi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kuna barabara ile ya Nyororo mpaka pale Mtwani. Hiyo barabara ikiwekwa kiwango cha lami itatusaidia sana kwa sababu kule kuna viwanda vingi sana halafu maeneo yale mvua zinanyesha sana kiasi kwamba magari makubwa yanashindwa kupita na kusafirisha ile mizigo mizito. Kwa hiyo, naiomba Serikali, katika ukanda huu wa Kusini, ikitujengea zile barabara za lami, basi itakuwa imefanya vizuri ili wenyewe viwanda vikubwa waweze kusafirisha mizigo yao. Vile vile hii barabara tunajua kabisa tuna kiwanda kikubwa cha Mgololo ambacho kinatengeneza karatasi kule, kinashindwa kusafirisha mizigo mizito, kwa hiyo, itakuwa imetusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye nishati na madini kwa sababu muda ni mdogo; kwanza, nitoe pongezi kwa Serikali. Natoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Kwa kweli alifanya ziara kwenye Jimbo langu na aliongea na wananchi na kupongeza sana. Alichokiongea siku ile, utekelezaji wake umeanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo moja la Watanzania, unataka kitu kifanyike mara moja, siku moja; lazima kuwe kuna hatua. Mimi nampongeza Waziri, sasa hivi ninavyoongea mkandarasi yuko *site*, kama alivyoongea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, bahati nzuri ameandika kwenye ripoti yake; kuna maeneo yale ambayo yalirukwa. Katika *survey* kuna vitongoji vingine vimerukwa, naomba vile vitongoji ambavyo vimerukwa viweze kupewa *survey* tena ili viweze kupewa umeme kwa sababu wananchi wanalamika, wanajua kama hawatapewa. Nakuomba kwenye majumuisho yako uwaambie wananchi kwamba yale maeneo yote ambayo yalikuwa yamerukwa, hayakufanyiwa *survey* kwamba mtafanya *survey* na watapewa umeme kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile gharama za uingizaji umeme, naomba kwenye majumuisho tuwaambie wananchi zижиликане vizuri. Kwa sababu kuna watu wengine wanasema ile ya 177,000 kuna wengine kuna ile 27,000, kwa hiyo, inaleta mchanganyo kidogo. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anapotoa majumuisho, aliweke sawa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengine wameanza kuchangia, wanasema wachangie fedha ya nguzo. Yaani mtu anataka aweke umeme pale, anaambiwa na TANESCO kwamba achangie fedha fulani. Mwananchi mmoja alisema anaambiwa achangie Sh.500,000 kwa ajili ya nguzo. Namwomba Mheshimiwa Waziri hili aliweke sawa, kwamba zile nguzo ni bure au kuna watu wengine wanatakiwa wachangie pale? Tunaona tunapata mchanganyiko sisi Wabunge tunaulizwa maswali ya namna hiyo. Kwa hiyo, leo tunategemea Mheshimiwa Waziri atupe majumuisho, masuala ya nguzo tuhakikishe kwamba kama ni bure ijulikane watu wanapelekewa bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna shule nydingi tu zimerukwa. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri, zile

Taasisi hasa shule, Zahanati na Vituo vya Afya, basi kama kuna *exemption* ya kuweka umeme kwenye hizi Taasisi, basi Mheshimiwa Waziri tunaomba majumuisho tuelezwe vizuri ili wananchi waelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wachimbaji wadogo wadogo; taarifa ya Kamati, imejikita na kuonesha faida na hasara zilizojitokeza wakati pesa za ruzuku zinatolewa kwa hawa vijana na vikundi vyao. Bado naona kuna haja ya Serikali kuhakikisha inazisimamia pesa hizi za ruzuku kwa wanufaika wa ruzuku hizi na kuwapa semina za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tu Mkoa wa Katavi leo baadhi ya vijana (vikundi vya wachimbaji wadogo wadogo) katika machimbo ya Isula, Milomo, Kapanda, Ibindi, Mtisi, Kampuni na Stalika, vijana hawa hawajapata mafunzo na hivyo mikopo au ruzuku chache zilizopatikana walizitumia kwa matumizi yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa pesa ya ruzuku kwa wachimbaji wadogo wadogo, Kamati imeshauri iongezwe kwa usimamizi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira na manyanyaso kwa vibarua wa wachimbaji wadogo wadogo; hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana bila waajiri wao kuwapatia vitendea kazi vyenye usalama katika mazingira magumu. Je, Serikali ina wachukulia hatua gani wachimbaji hawa wanaoajiri hawa vibarua hususan katika machimbo ya Ibindi, Kapanda, Mtisi na maeneo mengine kama Isulamilomo?

Mheshimiwa Naibu Spika, vibarua hawa wananyanyaswa na kunyimwa mishahara yao na wakihoji kuhusu maslahi yao wanafukuzwa kazi kwa sababu wamehoji. Je, Serikali hii ya CCM imeshindwa kusimamia unyanyasaji huu kwa vibarua wa wachimbaji wadogo wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa utoaji wa leseni kwa wachimbaji wadogo wadogo, usumbufu wanaopata wachimbaji hawa wanapofuutilia leseni zao kuna urasimu mkubwa sana kupitia Maafisa Madini wa Wilaya na Mikoa pamoja na Kamishna wa Kanda wa Madini, ni kwa nini leseni hizi zinatolewa kwa usumbufu mkubwa na kusababisha wachimbaji hawa kushindwa kufanya kazi zao na kupelekea kuporwa machimbo yao kumbe wanacheleweshwa ili wanyang'anywe machimbo yao. Je, Serikali hamwonki kwamba jambo hili linakwamisha uchumi, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaongeza watumishi wa madini ili kuondoa usumbufu huu wa gharama wachimbaji kusafiri kutoka wilaya moja kwenda wilaya nytingine, mkoa kwa mkoa, kufuatilia leseni zao. Maoni ya Kamati yazingatiwe pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa *REA Vijiji*, changamoto za umeme vijiji ni kubwa na kama Kamati iliviyoshauri Serikali ihakikishe inasimamia uwekaji wa umeme katika vijiji vyenye vipaumbele si kubagua vijiji na kuviruka baadhi ya vijiji hili jambo si sawa. Serikali iliangularie jambo hili kwa sababu upatikanaji wa umeme vizuri unapelekea uchumi kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa umeme katika Mikoa na Miji mfano, Dar es Salaam; mpaka sasa umeme Mkoa wa Dar es Salaam bado ni tatizo na Mikoa mingine kama Katavi, Mbeya na Rukwa bado tatizo ni kubwa. Je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha Taifa linapata umeme wa uhakika, maji ya kutosha halafu ndio mjipange kwa ajili ya mabadiiliko ya uchumi wa viwanda, Je, Serikali haioni kuwa mnafanya kiini macho kuelekea uchumi wa viwanda?

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa uongozi wake wa kuwathamini wananchi kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kuona inapunguza ghamama ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta, kama ilivyo mikoa kadhaa ya nchi ikiwemo Mkoa wa Rukwa, Katavvi na kadhalika. Tunaomba kuunganishwa na gridi ya Taifa kwa sasa takribani mikoa yote. Mfano Rukwa tunatumia mafuta na umeme wa kutoka Zambia. Hii harakati ya kuanzisha viwanda tunahitajika kuwa na umeme wa kutosha na kukidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Kusini kuna nafaka za kutosha, tunahitaji kuziongeza thamani, hivyo umeme ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia umeme *REA III* ufikishwe kwenye vijiji na vitongoji vyote nchini, kwa hatua ya sasa, ikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipaye kupongeza Kamati ya Nishati na Madini kwa taarifa na kwa utendaji ambao umepelekea kudhibiti mianya ya utoroshaji wa rasilimali yetu ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuiomba Serikali kuharakisha uchakataji wa gesi yetu ili iweze kupunguza shida ya nishati hii ambayo inasababisha ukataji miti holela na hivyo kusabisha uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kuharakisha ulipaji fidia kwa wananchi mahali ambako miradi ya umeme inapita kwani imesababisha umaskini kwa jamii pale ambapo wameweka *X* na kushindwa kulipa hivyo kusababisha wananchi kushindwa kuendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kupunguza urasimu kwa wawekezaji wa miradi ya madini kwani kunawakatisha tamaa wawekezaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishauri Serikali kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapa hitaji la muda mrefu kwani wameshindwa kupata pato kubwa kutokana na vifaa duni wanavyotumia katika uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kuangalia kwa upya juu ya Shirika la *TANESCO* kwa kulipunguzia mzigo wa kufufua umeme, kusafirisha na kuuza kunakopelekea utendaji ambao ni mgumu na usiokuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri elimu kwa wachimbaji wadogo ili kusaidla kuwezesha kuchimba kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kulipa malipo ya *TANESCO* kwani inapunguza utendaji wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kujenga matenki ya Serikali ya kupoolea mafuta ili kudhibiti kwa urahisi upotevu wa mafuta unaopelekea Serikali kukosa kodi halisi ya mafuta hayo.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, naipongeza Kamati kwa ufuatiliaji wa miradi mbalimbali na kwa ripoti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za gesi ziko juu sana mpaka wananchi wanashindwa kununua gesi hiyo. Naomba Serikali ione ni namna gani bei zinapungua na kuwawezesha kununua kwa bei nafuu. Kwa namna nyingine watu wataendelea kuharibu mazingira kwa kukata miti hovyo kwa ajili ya kutengeneza mkaa na kutumia kuni kwa ajili ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*); nashukuru Serikali inajitahidi kupeleka umeme hadi vijijini, lakini kuna tatizo limezuka la kukatika umeme kila mara. Mfano, Mjini Njombe na baadhi ya maeneo hapa Dodoma hasa eneo la Kisasa umeme unakatika mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ione namna gani inarekebisha miundombinu ya umeme ili usikatike mara kwa mara, *iimarishe* miundombinu kama *transformer* na nguzo na waya wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*); bei za mafuta zinapanda kila kukicha hii inatokana na kuwa tunategemea kutoka nje maana sisi hatuna matanki kwa ajili ya kuhifadhi mafuta hayo. Naiomba Serikali iweke matanki yake kwa ajilli ya kuhifadhi mafuta haya ili bei ishuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina madeni *TANESCO*; hii inasababisha uendeshaji unakuwa mgumu na Shirika limekuwa likijiendesha kwa hasara. Serikali iwachukulie hatua watu wenye madeni sugu lakini pia Serikali yenye we ilipe madeni yake

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika taarifa ya shughuli za Kamati hii. Aidha, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Kamati wote kwa kuandaa na kuiwasilisha kwa umakini kabisa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia taarifa hii napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa usambazaji umeme vijijini; napenda kuwapongeza Serikali yetu kwa

hatua na spidi nzuri ya kuwapelekea wananchi wa vijijini huduma hii. Umeme kwa sasa sio tena *luxury* ila ni kitu muhimu kwa maendeleo ya nchi hii na wananchi. Hata hivyo, bado inaonekana kuwa kasi ya usambazaji umeme haiendi sawa na kasi ya matumizi au uungaji wa huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika suala hili Serikali iendelee kuwaelimisha wananchi wa vijijini umuhimu wa huduma. Ni vyema vikaundwa vikundi nya kitaalam na kuwezeshwa ili waweze kwenda vijijini kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vyema kukawa na msamaha wa gharama za kuunga umeme kwa wateja wa awali ili kuwahamasisha kujitokeza kwa wingi wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Kamati ya Nishati na Madini kwa taarifa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utekelezaji mzuri wa miradi ya *REA*, naungana na Kamati kupendekeza kuwepo kwa usimamizi mzuri wa hii miradi ili iwe endelevu kitaalam. Usambazaji kwa maeneo ya vijijini, waya zinawekwa umbali mrefu na pia miundombinu ya nguzo za kawaida ni changamoto kutokana na mazingira ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *REA*, napendekeza Serikali iwe na mkakati wa kuimarisha wataalam wa *TANESCO* ili waendane na ongezeko na kasi ya usambazaji wa umeme kwa mpango wa *REA*. Kutokana na ongezeko la usambazaji wa umeme kumesababisha kuzorota kwa huduma za dharura (*emergency*) hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgali; atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini; na Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Nditiye ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa nami niweze kuchangia taarifa ya Kamati ya Nishati. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kibali chake na kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge lako. Pia naishukuru sana Kamati yetu ya Nishati na Madini kwa taarifa yake nzuri ambayo iliwasilishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri hasa katika Sekta yetu ya Nishati kwa kuwa natambua kabisa na wao wana tambua kwamba sekta yetu ni mtambuka na wezeshi kwa sekta nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zimejitokeza hoja nyingi, lakini naomba nijielekeze kwenye hoja ya umeme vijiji; na hapa naomba nijieleke kwenye miradi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema, kwamba miradi kuna miradi ya REA II ambayo pengine haikukamilika kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyeikitii, naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeshughulikia na ninavyosema sasa, Wakandarasi mbalimbali wameteuliwa kwa ajili ya kutekeleza miradi REA II ambayo ilikwama. Hapa nasemea kwa Mkoa wa Kilimanjaro na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, Mama Anne Kilango Malecela na nimtaarifu katika Jimbo la Siha, Jimbo la Siha peke yake lilibakiwa na vijiji vitano tu ambapo REA II sasa ndiyo vinakamilisha. Ndiyo maana naamini Mbunge yule alishawishika baada ya kuona Jimbo zima umeme upo kasoro vijiji vitano, ambapo kama alivyosema Mheshimiwa

Mbunge, Mama Anne Kilango Malecela, Mkandarasi Njalita yupo *site* na anaendelea na kazi ya kukamilisha upungufu uliojitokeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, mikoa mbalimbali yote ambayo ina upungufu kwenye *REA II*, naomba nitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wakandarasi wale walikuwa hawajamaliza kazi katika kipindi cha uangalizi. Kwa hiyo, nawathibitishia, katika kipindi cha uangalizi ni kwamba Wakandarasi watamaliza upungufu uliojitokeza; na kwenye *REA III* tunawaahidi kwamba upungufu hautajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwenye suala la nishati vijiji imejipanga vizuri. Ndijo maana sasa tumeanza safari ya vijiji vilivyosalia 7,873 na Wakandarasi. Ni kweli kipindi cha miezi sita walikuwa na *survey*, lakini sambamba na hilo Wakandarasi katika kipindi hicho chote walikuwa wameagiza vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakubaliana nami kwamba Mikoa mbalimbali ambayo tumefanya ziara Wakandarasi wameanza kazi. Ninaposimama leo kusema ndani ya Bunge lako Tukufu, yapo maeneo vijiji vimeshawasha umeme. Kwa mfano, Mkoa wa Geita, Rukwa, Tanga, Pwani na mikoa mingine, Wakandarasi wapo *site* na wanaendelea na kazi. Ndijo maana tarehe 13 tulikutana nao tukawapa maelekezo mbalimbali ya namna ya kuanza miradi hii kwa kasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nalithibitishia Bunge Tukufu kwamba tumepokea changamoto ambazo zimeelezwa. Tuwataarifu tu kwamba Wizara hii chini ya Waziri wangu tumejipanga vizuri katika usimamizi. Ndijo maana kwa sasa ngazi ya Mkoa yupo *Engineer* pekee kwa ajili ya miradi ya *REA*; ngazi ya Wilaya yupo *Technician* kwa ajili ya miradi ya *REA*; na ngazi ya Kikanda yupo mtu wa *REA* kwa

ajili ya kusimamia miradi hii tu. Kwa hiyo, hii yote imefanywa ili kuboresha usimamizi na kuona changamoto ambazo lizijitokeza *REA* Awamu ya Pili hazijitokezi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilithibitishie Bunge lako kwamba kwa sasa hata miradi ya *Densification* ambayo lengo lake ni kuvifikia vijiji 305 inaendelea vizuri katika maeneo mbalimbali. Sambamba na hilo, hata mradi huu ambao unaendana sambamba na *REA III*, huu wa Msongo wa KV 400 wa Mikoa ya Iringa, Dodoma, Shinyanga na Tabora nao unaendelea vizuri ambapo vijiji 121 vitafikiwa na miundombinu ya umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kama ambavyo Mheshimiwa Mama Anne Kilango amesema, ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, imeongeza usambazaji umeme kwa asilimia 28 milaka miwilli; naamini na ninawathibitishia, kwa miaka ambayo tumejipanga 2018/2019, 2019/2020 vijiji vyote vilivyosalia 7,873 vitapata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie; tulitoa maelekezo kwamba kisirukwe Kijiji chochote, Kitongoji chochote, Taasisi ya Umma yoyote, iwe Sekondari, iwe Shule ya Msingi, iwe Zahanati. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wamesema hilo na sisi ndiyo mwongozo ambao tumetoa na nawaomba Wakandarasi wafanye kama ambavyo Serikali imewaelekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na tunawaahidi Utumishi uliotukuka. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Atashasta Nditiye na Waziri Mheshimiwa Dkt. Kalemani ajiandae.

### **NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H.**

**NYONGO):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo. Kwanza kabisa natoa shukrani za dhati kabisa kwa Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri walioifanya. Kamati ya Nishati na Madini kipekee kabisa tumekuwa tukipokea mchango mkubwa, ushauri maelekezo mbalimbali kutoka katika Kamati hii. Kwa kweli ushauri wao tunaupokea na ni ushauri mzuri na tutaendelea kushirkiana na Kamati hii kwa maana kuisukuma Sekta hii ya Madini iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe 14 waliochangia, wametoa michango mizuri michango yenyenye mashiko. Namshukuru na mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango kwa *complement* aliyo tupu. Kweli kabisa kwamba Wizara yetu imekuwa ikikusanya maduhuli kwa hali ya juu. Tunapambana usiku na mchana kuhakikisha tunakusanya maduhuli ambayo tunayapeleka katika Mfuko wa Serikali na Watanzania wote waweze kupata fedha au kupata huduma mbalimbali kutokana na makusanyo tunayokusanya kutoka katika Wizara yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunakusanya kwa kiasi kikubwa na ni mfano tuseme wa kuigwa kwa sababu mpaka hapa tulipo tuko katika nusu ya mwaka wa fedha wa kibajeti. Tumekusanya zaidi ya asilimia 80.4 ya maduhuli. Tunashukuru sana mama kwa kuliona hilo na tunashukuru kwa pungezi ulizotupa; na tutaendelea kukaza msuli kuhakikisha kwamba tunaendelea kukusanya maduhuli ili Watanzania wote waweze kupata huduma kutokana na mapato yanayopatikana katika Sekta ya Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mingi imeongelewa, nami napenda kuungana na waliochangia hasa katika ukurasa wa tano wa taarifa ya Kamati kuhusiana na mradi wa *Buckreef*. Ni kwamba *STAMICO* iliingia mkataba na *Buckreef* na kampuni ya *TAZAM 2000* wakatengeneza Kampuni ya *Bacliff* ambapo *STAMICO* wanashikilia asilimia 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama ilivyosema Kamati tumelitazama hili, huyu mbia kwa kweli havutii na tumeamua kuangalia kwa namna nyingine ambapo *STAMICO* inawabidi wakae chini na wanasheria waweze ku-review mkataba huu ili tuweze kuangalia na ikiwezekana tutafute mbia mwingine ili *STAMICO* wahakikishe kwamba yule mbia atayepatikana basi aweze kufanya kazi vizuri na uchimbaji uendelee na Serikali iweze kujipatia kipato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ambayo imeongelewa kuhusu pesa za ruzuku pamoja na pesa za mikopo zilizokuwa zinatolewa na Wizara. Kweli kabisa kwamba kuna watu walikuwa wanapokea ruzuku kutoka Serikalini, yaani kutoka Wizara ya Madini kuititia Benki ya *TIB*, walikuwa wanapata fedha kwa ajili ya kuendeleza migodi. Ilikuwa ni fedha maalum kwa kuendeleza wachimbaji. Kuna wachimbaji wengine walifanikiwa, wamefanya vizuri sana. Kuna wachimbaji wengine wamekwama, lakini inaonekana kabisa walikuwa na juhudzi za kufanya vizuri lakini wamekwama. Wachimbaji wengine walichukua zile fedha na kwenda kuzitumia kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wachimbaki tisa kwa taarifa tulizonazo. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaeleza kwa mara mwisho, nilitoa tamko nikiwa Singida, warudishe hizo fedha. Nachukua nafasi kusema kwamba nimetoa tena tamko la mwisho, wala sina haja ya kutoa siku nyingi, ni kwamba ndani ya hizi siku 14 zinazofuata, wajisalimishe wenyewe, wazirudishe hizo fedha kwa sababu wamewanyima Watanzania wengine kuweza kupata fedha hizo na kufanya shughuli za uchimbaji wakaweza kuendeleza Sekta hiyo ya Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la wachimbaji wadogo, Wizara imejipanga vizuri, sasa hivi tumeshatenga zaidi ya heka za mraba laki 238 kwa ajili ya kuwapa wachimbaji wadogo waweze kuchimba, lakini tunahakikisha kwamba wachimbaji hao wadogo wakae ndani ya vikundi, tuwatambue tuwarasimishe wachimbe ili na Serikali nayo

iweze kukusanya kodi, maduhuli na Halmashauri husika ziweze kupata ushuru wa huduma (*Service Levy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *GST* limezungumziwa. *GST* ndiyo Taasisi pekee ambayo inaweza ikafanya kazi vizuri kwa maana ya kufanya tafiti mbalimbali na kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo kuwapatia maeneo ambayo tayari yameshafanyiwa utafiti, yana taarifa za kutosha kwa maana maeneo ambayo yana dhahabu ya kutosha au madini mengine ambayo tayari yamefanyiwa utafiti wa kutosha ili kuепusha wachimbaji kuchimba kwa kubahatisha. Tumejipanga na *GST*na kuja kuleta taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia. Kwa migogoro iliyopo, tunaifanya kazi na hasa ule mgogoro wa *North Mara* na watu wa Nyamongo, maongezi yanaendelea. Taratibu zinafanyika na makundi yote tunayashirikisha. Tunachotaka ni Serikali itatue mgogoro wa Nyamongo ili wachimbaji waendelee na wananchi waendelee na shughuli zao za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba Kamati imeshauri kwamba kuna wachimbaji wa Kitanzania tuwape maeneo, akiwepo mchimbaji wa Busolwa. Tunahakikisha mchimbaji huyo tunampa eneo ili aongeze muda wa mgodi, Watanzania waneemeke na ajira katika mgodi huo na Serikali tuendelee kupata kodi kutoka katika mgodi huo kwa sababu mgodi huo unafanya kazi. Hakuna haja ya kumnyima eneo ambalo tunadhani Serikali tunaweza tukampa na kukamsaidia mchimbaji mdogo na wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengine wote wanaotaka kuwekeza katika Sekta ya Madini, tuko tayari kuwasaidia kuwapa maeneo mazuri wachimbe na tutaweza kuwasaidia kwa namna ambayo watatoa ajira kwa Watanzania wengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyongo. Mheshimiwa Atashasta Nditiye, Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, halafu Mheshimiwa Dkt. Kalemani, tutamalizia na Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya miundombinu. Kwanza nachukua nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu kwa taarifa yao nzuri kabisa ambayo imetupa mwongozo kama Serikali katika kutekeleza majukumu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe wote kwa ushauri mbalimbali ambao mmeendelea kutupatia ambao umetuimarisha katika kutekeleza majukumu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda wenyewe siyo rafiki sana, nitajikita moja kwa moja kwenye suala la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Tulipata maelekezo na ushauri mzuri sana kutoka kwa Kamati kuhusu namna ya kuweka mipaka kwenye viwanja vyetu ambavyo kwa kweli vinavamiwa. Nakiri ukweli kwamba viwanja vyetu vingi sana vinavamiwa na Watanzania aidha, kwa kujua au wakati mwingine kwa kutojua. Tumeendelea kuwasiliana na mamlaka zinazohusika kuhakikisha kwamba viwanja vyetu vinabaki salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashauri Watanzania, kabla hawajafanya maendelezo ya sehemu yoyote waliyopata nafasi ya kiwanja karibu na Taasisi za Kiserikali ni vizuri sana wakawasiliana na mamlaka zinazohusika kabla ya kuweka maendelezo ya kudumu. Kwa upande wetu Serikali, sasa hivi tunajiandaa na tunatengeneza Kitengo maalum cha *Real Estate* kwa mamlaka ya viwanja vya ndege ambacho kitafanya kazi ya kufuatilia viwanja vyetu vyote kubaini mipaka yetu yote na kufuatilia kupata

hati. Kwa sababu bila kutengeneza Kitengo hicho cha *Real Estate* tutapata matatizo kidogo katika kufuatilia hizo hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Nashukuru sana kwa pongezi ambazo Kamati wametupatia, tunazipokea kama Serikali na tunakiri kwamba *TCRA* kwa kweli inafanya kazi nzuri sana kuhakikisha kwamba *ina-regulate* masuala ya mawasiliano hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishauri *TCRA* na tunaielekeza kabisa kwamba wale wamiliki wa ving'amuzi binafsi ambao wanatakiwa watoe *channel* za bure kwa Watanzania watekeleze. Kama hawatakeleza kwa wakati unaotakiwa, basi *TCRA* ijpange kuwachukulia hatua stahiki ili Watanzania waendelee kupata huduma za *free channel* kama leseni ya wale watoa huduma inavyowataka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita vilevile kwa suala la *TTCL*. Kwanza nitoe shukrani za dhati kwa ushauri wa kuimarisha *TTCL* ambao umetolewa na Kamati. Tunawashukuru kwanza kwa hatua mliyoichukua ya kui-support Serikali katika uanzishaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*). Tunawashukuru kwa jinsi ambavyo mmeendelea kuipigania iweze kuwa imara. Huo ni moyo wa kizalendo ambao kwa kweli sisi Serikali tunaunga mkono; na tunaishukuru sana Kamati kwa jinsi ambavyo mnaipambania *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *TTCL* inatengeneza muundo wa shirika. Baada ya hapo shirika limeshafunguliwa kama Shirika la Umma. Hivi sasa inaendelea na shughuli za kimkakati. Kwa mfano, sasa hivi ninayo furaha kueleza Bunge lako Tukufu kwamba kuna mkakati ambao *TTCL* unaendelea nao wakishirikiana na *TANROAD* wa kuhakikisha mizani yote Tanzania inawekewa vifaa maalum au inaunganishwa na mkongo wa Taifa kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika magari yote yanayopita yanaonekana kuanzia Makao Makuu ya *TANROAD* na hata Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi huu tunategemea kutekeleza kwa awamu mbili. Awamu ya Kwanza tumeanza na Vituo 19. Mpaka sasa hivi nihapoongea Vituo 14 vimeshaunganishwa na mkongo wa Taifa, ambapo kila gari inayopita inaonekana lakini ina uzito unaoongezeka unaonekana. Kwa maana hiyo, hata *charge* wanayochangiwa kikawaida inaonekana moja kwa moja kwenye mitando.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwa kutekeleza mradi huu, mapato ya Serikali hayatapotea, lakini ile *human intervention* tutaipunguza kwa kiwango kikubwa sana. Kwa sababu ni kweli kwamba kupitia kwenye mizani Serikali tumekuwa tukipoteza mapato. Njia rahisi kabisa ambayo tumeona ni ya kutufaa ni kuanzisha hii *system* ambapo *TTCL* wameonesha uwezo mkubwa sana katika kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mfumo huu utaweza ku-share na mifumo mingine ya *TANROADS* ambapo ni mifumo kama ya fedha, mifumo ya *emails*, hata rasilmali watu. Kati ya vituo hivyo tunaamini kabisa tutakapoingia awamu ya pili tutatekeleza na vituo vingine vitakavyofuata ili kuhakikisha kwamba mapato yote ya Serikali hayapotei kupitia mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nditiye muda wako umekwisha. Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Waziri wa Nishati. (*Makof!*)

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, lakini kwa upande wa Nishati. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza kwa kiasi

fulani mipangilio yetu kuhusiana na miradi ya umeme vijijini. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano jinsi inavyotoa pesa za kutosha katika kutekeleza miradi ya *REA* awamu ya tatu. Kwa takwimu tulizonazo katika kipindi kama hiki, mwaka wa fedha 2015/2016, tulipata asilimia 78.8 katika kipindi kama hiki cha miradi ya *REA* awamu ya tatu. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, tulipokea asilimia 79.3, kwa hiyo, tuliongeza asilimia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu katika kipindi hiki cha nusu ya mwaka, tumepokea asilimia 81.3. Kwa niaba tu ya Wizara yangu na wengine, nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara yetu inavyoshirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape tu uhakika wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa utaratibu huu, tuna uhakika mkubwa kwamba miradi hii itatekelezwa kwa asilimia mia moja ndani ya muda mliotupatia na sisi tutafanya kazi kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba kazi inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetaja mikoa ambayo tumeshaanza kutekeleza, lakini nichukue nafasi hii kuwaeleza wananchi na Waheshimiwa Wabunge, mpaka sasa tumeshawasha umeme vijiji 24 chini ya mpango huu mpya wa *REA* awamu ya tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Heche. Nitoe tu taarifa kwamba kwenye Jimbo lake tumeshawasha Kijiji cha Nyangere kwenye Jimbo lake. Kwa hiyo, tayari tumeshamwashia umeme kwenye ile awamu ya tatu. Hata kule Butiama tumeshawasha umeme Masusura; kule Mwanza tumeshawasha Ipanga na Nguge; Geita tumeshawasha Nyangomango; kule Mtwara tumewasha

Nalingo; kule Arusha tunawasha Didigo; tunakwenda kuwasha kijiji hadi kijiji. Kwa hiyo, nitoe taarifa kwamba tunakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo kwenye suala la madeni ya *TANESCO*. Nami nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuunga mkono kwamba Shirika letu kwa kweli linahitaji kupewa msukumo wa aina yake. Nazipongeza pia Taasisi za Serikali ambazo zilikuwa zinadaiwa kwa kiasi kikubwa, zimeanza kulipa madeni yake. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge jinsi mnayosukuma kwenye Halmashauri zenu, kiasi ambacho sasa tumeanza kupata mapato mazuri kutoka kwenye Taasisi za Maji, Jeshi letu, Mambo ya Ndani na Taasisi nyiningine za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa deni kidogo limepungua. Lilikuwa shilingi bilioni 297, sasa limebaki shilingi bilioni 277. Kwa hiyo, ni maendeleo makubwa. Nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge kuititia kwenye taasisi zetu, basi tuendelee kuliunga mkono Shirika letu ili liweze kuwahudumia vizuri na kwa asilimia ambazo wananchi wetu wana matarajio nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo kuhusiana na mradi wa *Stieglers*. Mheshimiwa Heche amezungumza kwamba tumeanza kuutekeleza. Niseme tu, utekelezaji wa mradi wa aina yoyote una hatua zake. Hatua ya kwanza ya kawaida ya kutekeleza mradi ni maandalizi ya mradi. Hatua ya pili ni kufanya matayarisho ya miundombinu wezeshi kutekeleza mradi; na hatua ya tatu ni ya kujenga mradi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunachofanya ni kuandaa na kutayarisha mazingira wezeshi ya kuutekeleza mradi huo kabambe. Ndiyo maana hivi sasa kwa upande wa miundombinu ya umeme tumeanza kujenga miundombinu ya umeme kuititia Shirika letu la *TANESCO* ambalo bajeti yake ilipita katika mwaka wa fedha huu

tunaoendelea nao. Shilingi bilioni 7.7 zilipitishwa kwa ajili ya miradi ya Morogoro; na mradi unaojengwa sasa kwenda kule ni kupitia bajeti ya Serikali kupitia *TANESCO*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo tutafanya utaratibu na tunaendelea na utaratibu sasa wa kutangaza tenda. Tutakapoukamilisha, ndipo sasa tutajua ni kiasi gani na utekelezaji wa mradi huo utaanza na taratibu za kawaida za kibajeti kuja kwenye Bunge lako Tukufu zitafuatwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba bado maandalizi yanaendelea, lakini nawaomba wananchi na Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono juhudzi za Serikali za Mheshimiwa Rais za kuujenga mradi huu kwa sababu utatutoa kwenye shida za upungufu wa umeme na kuwa na umeme wa uhakika wa kujenga uchumi wa viwanda tunaotarajia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nizungumze kidogo kuhusiana na miradi ya umeme kule Mtwara na Lindi. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara na Lindi kwa jinsi ambavyo mwezi Novemba tulikuwa na shida kidogo, lakini tuliungana pamoja, mwezi Novemba Mtwara tulibaki na mashine tatu zinazofanya kazi hadi kufika Novemba, 2017. Hata hivyo, nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba hivi sasa mashine zinazofanya kazi kwa Mtwara na Lindi, mashine zote sasa tisa sasa zinafanya kazi. Zimekarabatiwa, zinafanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara kwamba mliomba mashine mbili mpya, tumeshazileta na zimeshaanza kufungwa. Ni matarajio yetu ndani ya miezi miwili nazo zitakamilika. Kwa hiyo, Mtwara na Lindi tutaanza kupata umeme wa *megawatts* nne za ziada. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali yetu na Waheshimiwa Wabunge mnavyotuunga mkono katika jitihada hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda tu niseme; kweli kabisa katika Mikoa ya Ruvuma na Mtwara tuna changamoto ya miundombinu, lakini tunaendelea kukarabati na kujenga miundombinu mingine mipyä. Katika Mikoa ya Sumbawanga, Kigoma pamoja na Katavi ni kweli tunatumia mafuta mazito kwa sasa, lakini Serikali Tukufu kuititia Bunge hili katika bajeti ya mwaka huu mlituidhinishia shilingi bilioni 13.2 kwa ajili ya kujenga umeme mkubwa wa *kilovolts* 400 wa kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda, Kigoma, Nyakanazi, Geita mpaka Bulyanhulu. Hivi sasa utekelezaji umeshaanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipande cha Geita – Nyakanazi, Mkandarasi yuko *site* ameshaanza ujenzi; kwa kipande cha Bulyahkhulu kwenda Geita Mkandarasi yuko *site*, ameshaanza ujenzi na kwa kipande cha kutoka Mbeya kwenda Sumbawanga, Mkandarasi taratibu za kwanza za kufanya *survey* anakamilisha; na kufika Julai mwaka huu ataanza ujenzi rasmi. Kwa hiyo, upande wa Sumbawanga napo utapata umeme mkubwa wa *kilovolts* 400 kwa ajili ya ujenzi wa uchumi wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda la mwisho kwa sababu ya muda nizungumze kidogo kuhusiana na suala la bei za umeme wa *REA* pamoja na *TANESCO*. Bei ya umeme kijijini ni Sh.27,000/= basi, hakuna bei zaidi ya hapo. Kwa miradi ya *TANESCO* ambayo iko katika Mitaa na katika Halmashauri za Mijini ni Sh.177,000/= basi. Hizi ni bei ambazo Serikali kwa kiasi kikubwa imechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii bado kuipongeza Serikali. Hakuna nchi kwa nchi zinazoendelea zenye gharama ya umeme Sh.27,000/= hata vijijini, hakuna. Tanzania ni bei yetu ya kwanza. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa utaratibu huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mteja anayelipia nguzo. Ni vizuri nikaliweka bayana suala hili. Gharama za umeme wananchi tunachangia. Gharama ya kununua nguzo moja ni Sh.200,000/= hadi Sh.250,000. Sasa kama ingekuwa

ni kulipia nguzo ingekuwa gharama kubwa sana. Kinachofanyika ni kutoa huduma kwa umbali wa huduma zinazoweza kupewa kwa mteja, lakini siyo kulipa nguzo. Kwa hiyo, nguzo hazilipiwi, ni kuchangia juhudi za Serikali katika kutandaza umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie tu na kusema kwamba, kwa vile sasa hivi tunatekeleza miradi ya umeme vijijini, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, lengo letu ni kupeleka umeme kijiji kwa Kijiji, Kitongoji kwa Kitongoji, nyumba kwa nyumba, taasisi kwa taasisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge katika Taasisi za Umma muwashawishi na kuwashauri Wenyevit wa Halmashauri waanze kutenga fedha kldogo ili kuzifikishia taasisi zetu umeme. Haipendezi na siyo matarajio ya mradi, nguzo kuning'inia karibu na Taasisi ya Umma halafu Taasisi ya Umma isipate umeme ndani ya nyumba. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaelekeza na kuwashauri Waheshimiwa Wakurugenzi walipo waanze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nachukua nafasi hii kuwaagiza Wakandarasi popote walipo, tumeshawaelekeza, mwisho wa kuanza kazi ambao hawajaanza ni tarehe 2 Machi, lakini kwa kiasi kikubwa wameshaanza kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. Nashukuru kwa kunisikiliza (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa

rehema kwa kutujaalia kufanya shughuli zetu tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru sana Kamati yangu ya Miundombinu kwa taarifa nzuri na kwa mwongozo mzuri. Nachukua fursa hii kuunga mkono taarifa ya Kamati ya Miundombinu. Naomba niwahakikishie tu Kamati yetu kwamba maelekezo yote waliyotoa tutayatekeleza kwa maslahi ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2017/2018, tulitengewa shilingi trillioni 4.5. Fedha hizi tumezitumia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sekta ya Uchukuzi kwa upande wa Bandari; Bandari yetu ya Dar es Salaam imeanza kuimarika vizuri kwa sababu sasa hivi tumeongeza uadilifu mkubwa na tumejipanga katika kuboresha miundombinu. Kwa taarifa tu, katika mwaka wa fedha 2016/2017, tani milioni 14.7 zilipita kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Katika kipindi cha miezi minne kutoka Julai mpaka Septemba, miezi mitatu, *quarter* ya mwanzo, mizigo ya nchi za jirani imeongezeka kutoka tani milioni 1.16 mpaka tani milioni 1.479. Hii imetokana na kujipanga vizuri na wafanyakazi wetu kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mapato, mwaka 2016/2017, Bandari ya Dar es Salaam au Bandari zote zilitengeneza karibu shilingi bilioni 734.9 wakati matumizi yalikuwa shilingi bilioni 446. Salio lilikuwa ni shilingi bilioni 288. Kwa *quarter* ya kwanza kuanzia mwezi Julai mpaka Septemba mwaka 2017/2018, Bandari ya Dar es Salaam imekusanya mapato ya shilingi bilioni 207.5 wakati matumizi ni shilingi bilioni 67. Inaonesha sasa Bandari ya Dar es Salaam imejipanga kuhakikisha kwamba hata matumizi yenye we wanapunguza kwa kiasi kikubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni kwamba pato halisi ni shilingi bilioni 139.6. Hii ina maana, kama

tutaendelea namna hii, itakapofika mwisho wa mwaka wa fedha huu, bandari itaweza kuwa na mapato halisi takriban shilingi bilioni 450. Hajjawahi kutokea katika historia ya bandari zetu za Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yote hayakuja bure, yamekuja kutokana na miundombinu ambayo sasa hivi inaendelea hapo Bandari ya Dar es Salaam. Tukianzia Bandari ya Dar es Salaam sasa hivi, tuna mradi mkubwa wa uboreshaji wa gati ya kwanza mpaka gati namba saba ambayo tutatumia takriban shilingi bilioni 336. Kazi kubwa inayofanyika ni kuongeza kina cha maji kwenye bandari hiyo, pia na kuboresha bandari yenewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya ukarabati huo, tutahakikisha sasa meli kubwa zenye uwezo wa kuchukua kontena 19,000 za tani 20 zinaingia Bandari ya Dar es Salaam bila matatizo yoyote. Tunaamini tukifanya hivyo, tutaweza kushindana na bandari zote zilizopo katika maeneo ya jirani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukusimama hapo tu, lakini hata Bandari ya Mtwara tuna mradi ambao sasa tunajenga gati jipya lenye urefu wa mita 350 ambalo lenyewe litagharimu shilingi za Kitanzania bilioni 149 na Mkandarasi yuko kwenye *site* na kazi inaendelea. Hatukusimamia hapo, lakini tumeendelea na ujenzi wa matishari ambayo tuyatumia kwa ajili ya kupeleka mizigo katika bandari zetu za kule Kyela na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mradi wa ununuzi wa *scanner* ambapo tayari sasa *scanner* nane zimefika Dar es Salaam. Kwa mara ya kwanza katika Bandari ya Dar es Salaam mwaka huu tumeingiza *scanner* maalum kwa ajili ya reli. Pia tumeingiza *scanner*nyingine nne (*mobile scanners*) pamoja na *scanner*nyingine tatu ambazo gharama yake ni shilingi bilioni 52.2. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *flow meter*, kazi tunaendelea nayo ya utaratibu wa ununuzi wa *flow meter* na hivi karibuni manunuzi hayo yatakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuwa na Bandari imara kama huna usafiri wa barabara imara. Kwa kulijua hilo, Serikali ya Awamu ya Tano tumeanza ujenzi wa reli ya kiwango cha *standard gauge*. Awamu ya kwanza imeanza Dar es Salaam mpaka Morogoro yenyе urefu wa kilometa 300. Treni hii ni ya kipekee katika nchi za Afrika ya Mashariki na Kati. Treni hii itatumia umeme na itakuwa inakwenda mwendokasi wa kilometa 160 kwa saa. Itakuwa na uwezo wa kubeba tani milioni 17 kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utagharimu takribani shilingi za Kitanzania trillioni 2.7. Jumatano hii Mungu akipenda, Wajumbe wa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Miundombinu watatembelea eneo la ujenzi; na nawataka Wajumbe hawa watembelee usiku, ndiyo unaona raha ya ujenzi, siyo mchana. Pale watu wanafanya kazi saa 24 kwa wiki, siku saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafurahi kama ninavyosema; na nimemwalika hapa Mheshimiwa atembelee lakini atembelee usiku, siyo mchana, kwa sababu usiku ndiyo utaona ile raha ya ujenzi wenyewe. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza awamu ya pili. Awamu ya pili inaanzia Morogoro mpaka Makutupora yenyе urefu wa kilometa 442. Wiki iliyopita Serikali ililipa *advance payment*, yaani malipo ya awali dola za Kimarekani milioni 215 sawa na shilingi bilioni 483. Wakati wowote mwezi huu tutaweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa kutoka Morogoro mpaka Makutupora ili kazi iendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020 ifikapo mwezi Juni, Watanzania wataanza kufurahia treni ya kisasa kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma ambapo sasa watatumia

masaa mawili na nusu mpaka masaa matatu kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi haikuishia hapo tu, tunaendelea na mpango wa kuanzia Makutupora mpaka Tabora, Tabora - Isaka, Isaka – Mwanza. Tunatoka Tabora – Kigoma – Uvinza - Msongati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita, wenzetu wa Rwanda walikuja hapa na tuliweka makubaliano sasa ya kujenga reli ya kisasa kutoka Isaka mpaka Kigali yeny urefu wa kilometra 521 na tunategemea jiwe la msingi litawekwa mwezi Oktoba mwaka huu, kwa vile tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba Bandari ya Dar es Salaam tunaiboresha kwa miundombinu ya aina yoyote ili kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usafiri wa anga; ili anga zetu ziwe salama tunajipanga tunanunua *radar* nne za kisasa ambapo *radar* moja itafungwa Dar es Salaam, moja itafungwa Mwanza, moja itafungwa Mbeya na nyingine itafungwa Kilimanjaro. Hiyo imegharimu takriban shilingi za Kitanzania bilioni 63. Tunafanya hivyo kwa sababu tunapoteza mapato mengi kwenye sehemu ya madini, watu wanaingia na ndege ndogo hatuwezi kuona.

Tunaamini sasa, tukiweka *radar* hizo za kisasa ndege yoyote itakayoingia Tanzania hasa ndege hizi za kiraia, tutaweza kuiona na tutakusanya mapato yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viwanja vya ndege; tunaendelea na ujenzi wa jengo la abiria pale Dar es Salaam ambalo litakuwa na uwezo wa kuchukua abiria milioni sita ikilinganishwa na jengo la abiria *terminal II* lenye uwezo wa kuchukua abiria milioni mbili na nusu. Jengo hili litagharimu shilingi takriban bilioni 560 litakapomalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakati mmoja kwenye jengo lile zitaweza kukaa ndege 22 kwa wakati mmoja. Kwa kweli ni jengo la kisasa ambapo kazi inaendelea na ujenzi

umefika asilimia 70. Kwa upande wa Mwanza, tumetenga takriban shilingi bilioni 110 ambapo tunajenga *runway* na maegesho mengine kuhakikisha kwamba uwanja wa Mwanza sasa unakuwa uwanja wa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uwanja wa Shinyanga tumetenga shilingi bilioni 49.18 na Mkandarasi tumeshampata kwa ajili ya ujenzi. Kwa upande wa uwanja wa Sumbawanga tumetenga shilingi bilioni 55 na Mkandarasi tumempata. Kwa upande wa uwanja wa Songwe vile vile tumetenga bilioni 17 na kazi inaendelea. Uwanja wa Musoma, Songea na Iringa tayari tunahangaika kuwatafuta Wakandarasi kuhakikisha kwamba nako mambo yanakwenda vizuri. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Naona kwa sababu umeshataja viwanja vyote vya ndege hapo, Waheshimiwa Wabunge tumeshakuelewa. Kwa hiyo, muda wetu umekwisha. Naona bado umesimama, nakupa dakika moja.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali hii imejipanga kuunganisha mikoa yote ya Tanzania kwa kiwango cha lami. Sasa hivi kuna mradi unaendelea kutoka Katavi mpaka Tabora ambapo Serikali itatumia shilingi bilioni 770. Huu ni mradi mkubwa na tutajenga barabara ya kisasa. Pia kuna mradi unaendelea baina ya Katavi na Kigoma, Kigoma - Kagera, Kigoma - Tabora na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja ya Kamati yangu ya Miundombinu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa habari njema hizo. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawaita

watoa hoja, tutaanza na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ili aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wametoa michango yao. Naomba uniruhusu niwatambue kwa majina hasa wale ambao wameandika, kwa sababu wale ambao wamechangia hapa ndani wote mliwaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Shelukindo, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa *Eng.* Ramo Makani, Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mheshimiwa Silafu, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Lucia, Mheshimiwa Zainab na Mheshimiwa Lucy Owenya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka kumbukumbu sawasawa, nadhani ni Mheshimiwa Shekilindi badala ya Mheshimiwa Shelukindo. Umetaja Shelukindo hapo, nadhani ni Mheshimiwa Shekilindi. Sasa sema ili kumbukumbu rasmi za Bunge ziwe na jina linalotuhusu kwa sasa.

**MHE. NORMAN A. SIGALLA KING - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na michango mingi ya Wabunge pia nichukue nafasi hii kipekee kuwapongeza Mawaziri kwa maana Waziri Mheshimiwa Profesa Mbalawa pamoja na Naibu wake kwa michango yao kwenye hoja hii. Nitoe ufanuzi katika mambo machache. Kwanza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wameipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayofanya, nasi tunapokea pongezi hizo. Pia wengi wameongelea umuhimu wa kuunganisha barabara za lami, nashukuru kwamba Mheshimiwa Wazir amefafanua vizuri jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ya kuangalia uwezekano wa kuunganisha barabara za mikoa, nashukuru Mheshimiwa Waziri pia ametoa ufanuzi mkubwa kwenye hilo. Pia kuna hoja ya uwanja wa Chato na pia hoja ya kujenga uwanja Mkoa wa Mara; nafikiri haikujibiwa na ni vizuri nitoe ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako lifahamu; mimi nimeshiriki kwenye uwekaji wa jiwe la msingi uwanja wa Chato. Shilingi bilioni 39 zilizotajwa ni gharama za ujenzi mradi ukikamilika. Kilichofanyika Chato ni kuweka jiwe la msingi. Kuhusu fedha za bajeti kwa mwaka huu wa fedha kwa mfano, 2018/2019, wale Wajumbe watakaokuwa kwenye Kamati ya Miundombinu wataona bajeti hiyo. Kinachoonekana sasa ni kama vile umeshajengwa. Haujajengwa, tulichofanya ni kuweka jiwe la msingi. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, pia aliuliza vizuri rafiki yangu, Mbunge wa Sengerema kwamba kwa nini uwanja haujajengwa Mkoa wa Mara? Je, kwa nini Serikali inapeleka nguvu upande wa Chato?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu, ni vizuri watu wafahamu, mpaka Mwalimu Nyerere anatoweka tarehe 14 Oktoba, 1999 viwanja ambavyo vilikuwa vimejengwa Tanzania hii ni vichache sana na hasa viwili vikubwa ni uwanja wa *KIA* na uwanja wa Dar es Salaam. Viwanja vingine vya Kigoma na Tabora na kwingineko, wote tulikuwa tunatua na ndege kwa mashaka, siyo kwa kujengwa. Kwa hiyo, lawama ziende kwa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Dkt. Magufuli ameingia wakati Mheshimiwa Rais wetu Mwasisi wa nchi hii alishaondoka katika nchi hii. Kwa hiyo, siyo sawa hata kidogo kwa hekima yote ile kupeleka lawama kwa Rais wa Awamu ya Tano wakati, Rais wa Awamu ya Pili alikuwepo, ya Tatu alikuwepo, ya Nne alikuwepo na muda huo viwanja havikujengwa kwa sababu ya uwezo wa uchumi kuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utangazaji wa tenda labda nayo niifafanue kidogo. Ni vizuri Bunge lako Tukufu likafahamu, utangazaji wa tenda wa viwanja au miradi mingine ya Serikali imegawanyika katika sehemu kuu mbili; unaweza ukafanya kitu kinachoitwa *open tender* kwa maana ya kwamba unatafuta Mkandarasi wa ujenzi wa uwanja au jambo lolote ndani ya Serikali au *restricted tender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati gani unatumia *restricted tender*? Ni pale ambapo Wakandarasi ambao tayari unao wanafanya miradi mingine; unataka miradi mwingine unaofanana na kazi ambazo tayari Wakandarasi wapo, unataka utekelezwe. Badala ya kupoteza muda kufanya *open tender*, unafanya kitu kinachoitwa *restricted tender*, kwa maana ya kwamba unachagua katika wale ambao tayari wapo na unaangalia nani mwenye bei ndogo halafu unampa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Procurement Act* iko wazi na wala siyo kwamba ni jambo linafanya kwa kificho, liko wazi kwenye kufanya hivyo, kwa hiyo, chochote utakachofanya katika hivyo, ni sahihi. Kwenye Halmashauri zetu tunafanya hivyo na kwenye Serikali Kuu tunafanya hivyo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie dakika chache kupongeza kwa dhati taasisi ambazo Kamati hii inazisimamia. Nianze na taasisi kama *TCRA*; siwezi kuzitaja zote 37 na *CEOs* kokote waliko wajue kwamba nazitaja hizi tu kama mfano. *TCRA*, Kamati iliagiza kwamba watekeleze utaratibu wa *TTMS* ili tuwe na hakika ya mapato ambayo Serikali inapata. Wameshirikiana na wenzao wa *TRA* na sasa kazi inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielekeza *TPA* kwamba wajaribu kurekebisha kero za Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji na siku zinazochukuliwa katika kupakua na kupakia pamoja na tozo mbalimbali. *TPA* wamerekebisha jambo hilo na sasa mambo yamekwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaoagiza mizigo kwa kutumia Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa watakuwa ni mashuhuda kwamba hata vitu vilivyokuwa vinanyofolewa kwenye magari au kwenye magari tunayoagiza, sasa hivi wizi huo haupo tena. Pongezi sana kwa *TPA* pongezi sana kwa *CEO* wa *TPA* pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *Tanzania Building Agency (TBA)* ambayo ndiyo taasisi iliyopewa madaraka ya kujenga miradi mbalimbali ya Serikali na hasa majengo, imefanya kazi nzuri sana. Kwa mfano, imejenga *hostel* pale Chuo Kikuu Dar es Salaam. Gharama za kampuni ya Kichina iliyokuwa *ime-tender* ilikuwa shilingi bilioni 80 kumaliza mradi ule. Wao wametumia shilingi bilioni 10. Pia ukienda kwa mradi wa *hostel* za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo kama hivyo, lakini ukienda mradi mwингine kama wa Ihungo, wengine wali-*tendershilingi* bilioni 60, lakini wao wamemaliza kwa shilingi bilioni 11. Wameenda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda Mlonganzila, hivyo hivyo; wamekwenda wakitekeleza miradi mingi kwa karibu *ten percent of the entire total ukilanganisha* na Wakandarsi wengine. Lazima tuwapongeze sana *TBA* na *CEO* wake kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya katika kutekeleza miradi mbalimbali. Unakuja bodi za Wakandarasi na za Wahandisi; wote wamefanya kazi nzuri sana. Wakandarasi ambao wamekuwa wakizembea kutimiza viwango wameondolewa kwenye *roster* ya Wakandarasi Tanzania. Ni kazi nzuri sana inayofanywa na taasisi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitaja *MSL* pale Mwanza, ameteuliwa Kaimu Mkurugenzi. Kwa muda mfupi tu wa miezi michache aliyokaa, ameweza kuifanya meli ya *MV*. Liemba ambayo ilionekana kama haifai pale Kigoma na ilikuwa inariptiwa kwamba imeleta hasara kila *trip* ya shilingi milioni nne. Yeye kwa *trip* moja ameweza kusimamia na kupata shilingi milioni 15. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu, kwa hiyo, hii inaonesha kwamba kuna

vitu viwili muhimu ambavyo lazima Wizara hii iendelee kufanya. Moja, ni uteuaji kwa kufuata weledi wa Watendaji wanaosimamia taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hii; lakini pili, kufuatilia kwa makini ili kuona jinsi gani ambavyo tunaweza kuisaidia Tanzania na Serikali kwa ujumla kupata maendeleo. Ndiyo maana nimesema nizitaje taasisi kwa uchache.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitakuwa nimekosa fadhila kama nisiporudia kusema nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili kwa michango yao kutoka pande zote kwa vyama vyote. Michango yenu imekuwa ya muhimu sana na tumeichukua, tutazidi kuisheheni na kuiweka vizuri ili kwamba kwenye vikao vijavyo tuweze kuisaidia Serikali yetu kutekeleza mipango yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba taarifa ya utekelezaji ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 sasa ipokelewe na Bunge lako Tukufu kama taarifa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofii)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya  
Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa  
Mwaka 2017 Iliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati hii sasa ni mapendekezo ya Bunge. Kwa hiyo, Serikali iyachukue yote kama yalivyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini.

**MHE. DEOGRATIUS M. NGALAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa ruhusa ya kuja kuongelea mambo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyajadili kuhusu taarifa ya utekelezaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji katika Kamati hii, wamechangia Waheshimiwa Wabunge 23. Kwa kuongea wamechangia Waheshimiwa Wabunge 16 na kwa maandishi wamechangia Waheshimiwa Wabunge saba. Napenda niwataje Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hasa kwa maandishi kwa sababu hawa walioongea wameonekana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir, Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela na mwisho ni Mheshimiwa Silafi J. Maufi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi katika taarifa hii ya Kamati walijikita sana kwenye maeneo ya madeni. Walijikita pia kwenye maeneo ya mradi wa umeme wa maji wa Mto Rufiji ambao tunaita *Stieglers Gorge*, miradi ya REA I, REA II na REA III bila kusahau *Densification Project*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile walizungumzia matumizi ya gesi kwa maana ya kuwepo kwa *master plan* ili

kuweza ku-utilize gesi ambayo ipo kwa sasa ambayo inatumika kwa kiasi kidogo. Pia walizungumzia Taasisi ya *GST*, elimu kwa wachimbaji, ruzuku kwa wachimbaji wadogo, makusanyo ya maduhuli na suala zima la biashara ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kifupi wazungumzaji wengi wameipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji mahiri wa miradi yetu mingi ambayo inatekelezwa sasa na Serikali hii ya Awamu ya Tano. Wachangiaji wengi waliojikita katika madeni hasa ya *TANESCO* na *TPDC* ukiangalia lengo lao kubwa ilikuwa ni kuzifanya hizi taasisi mbili ziweze kuijendesha bila kutegemea ruzuku au mkono wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hoja zilijikita zaidi katika kuhakikisha kwamba wanayasaidia mashirika haya mawili ya *TANESCO* na *TPDC* kuondokana na ule mzigo wa madeni na hasa *TANESCO*. Kwa sababu deni la *TANESCO* wadaiwa na wadai unakuta kwamba *TANESCO* bado anabaki kuwa na deni kubwa. Kwa hiyo, nguvu zilielekezwa nyingi kwa wachangiaji wengi kuona kwamba hili shirika la *TANESCO*, Serikali iweze kuhakikisha kwamba inalisaidia ili iweze kuijendesha yenewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo la *TPDC*; pia *TPDC* ana madeni, lakini madeni ambayo *TPDC* anayo ni madeni machache kuliko madeni ambayo yenewe inadai. Hata ukijaribu kuiangalia *TPDC* kwa undani na kwenye maelezo ya taarifa yetu, unakuta kwamba *TPDC* bado inabaki na hela nyingi kiasi ambacho yenewe inaweza ikajidoresha. Kwa hiyo, michango mingi ilikuwa inaonesha kwamba *TPDC* ina mzigo mkubwa na Serikali inatakiwa kuingiza mtaji mkubwa ili kuhakikissha gesi ile ambayo inatumika itengenezewa miundombinu ya kutosha kwa sababu gesi inayozalishwa ni nyingi kuliko ambayo inatumika sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wengine walijikita sana kwenye mradi wa umeme wa maji wa Mto Rufiji naamini kwamba hii Mheshimiwa Waziri na baadhi ya

Wajumbe waliizungumzia kwa kina kwamba huu mradi siyo kwamba umeanza, ila upo katika maandalizi ya kuanza. Sasa na ni vizuri mara nyingi mradi kabla hujaingia kwenye ile processyenewe kuufahamu, kabla haujaileta bajeti hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bajeti itakuja wakati tayari kila kitu kipo kwenye *table* na vitu hivyo vinakuwa vinaonekana. Kwa hiyo, sisi kama Kamati tunaipongeza Serikali kwa hatua ambazo inazichukua kwa sababu umeme huu wa *stieglers Gorge* utatuletea Megawati 2100 na vilevile itaendana sambamba na *linkage* ambayo inawekwa na *philosophy* ya nchi kwenda kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na miradi ya umeme wa *REA*. Wachangiaji wengi wamezungumzia upungufu ambao umefanyika katika mradi wa *REA* awamu ya kwanza na *REA* awamu ya pili; na mara nyingi ni kule kurukwa kwa baadhi ya vijiji. Umeme unatoka kijiji hiki hapa, kinaruka unaenda kwenye kijiji kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia, wengi wameshauri kwamba ule upungufu ambao tayari umeshaonekana katika hii miradi ya *REA* /na *REA* //maana yake ni kwamba sasa kwenye *REA* ///yafanyike maboresho. Bahati nzuri Serikali imekuja na utaratibu wa *Densification Project* ili kuweza ku-clearupungufu wote ambao umefanyika katika *REA* /na *REA* //na bahati nzuri baadhi ya Wakandarasi tayari wameshapewa *tender* na wapo *site* wanafanya kazi hii ya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matumizi ya gesi; wachangiaji wengi wameona kwamba gesi iliyopo ambayo inazalishwa na *TPDC* ni nyingi. Kwa hiyo, kuna haja sasa ya Serikali kutengeneza miundombinu wezeshi ya kuifanya *TPDC* iweze kupeleka gesi maeneo mbalimbali na hususan kwenye majumba yetu. Kwa hiyo, hiyo *master plan* itaonesha maeneo ambako gesi inapita na hata kama wawekezaji watakuja, maana yake watatumia ile *master plan* ambayo ipo. Vilevile wachangiaji wengine walizungumza kwamba kuna baadhi

ya nchi jirani ambazo na zenyewe zinaenda na mifumo hii. Kwa hiyo, maana yake *TPDC* iwezeshwe ili kuweza kuingia kwenye soko la kiushindani la Kimataifa, kwa sababu gesi iliyopo ni nydingi na watumiaji ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limeongelewa kuhusu *Geological Survey of Tanzania (GST)* kwamba ndio iwe mtafiti pekee wa madini Tanzania na *in case* kama kuna wawekezaji wa uchimbaji, basi wapate *consent* au washirikiane na taasisi hii katika kufanya utafiti huo. Kwa sababu inaonekana baadhi ya taasisi za nje zinafanya hujuma ya kufanya tafiti kwa muda mrefu kiasi ambacho hata zile taarifa nchi inakuwa hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwa kuiunganisha na *GST* kwa kupata *consent* ya *GST* maana yake ni kwamba, nchi kwanza itapunguza ule urasimu ambaa unafanywa na pla nchi itakuwa na *clear picture* ya maeneo ambayo yana madini na vilevile itawafanya baadhi ya wachimbaji wetu wadogo na wa kati kutokutumia gharama zao nydingi katika kuwekeza mahali ambako hawana uhakika wa madini ambako yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kwamba *GST* ikishakuwa mbele ya wachimbaji wetu wa kati na wa chini, maana yake ni kwamba mtu ataenda kuwekeza na atakopa mikopo benki kwa ajili ya uwekezaji huu akijua picha halisi na hali halisi ya madini iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limezungumziwa suala la elimu kwa wachimbaji. Elimu kwa wachimbaji ni muhimu na hata sisi Kamati tumesititiza hilo kwa sababu kuna athari nydingi ambazo zinatokea kule kwa sababu ya kukosa uelewa na kukosa elimu ya kutosha juu ya maeneo hayo, kunakuwepo na athari nydingi na ajali nydingi, kwa mfano kuangukiwa kwa vifusi na vitu vya namna hiyo. Hayo yameelezwaa, nasi kama Kamati tuliona jambo hili ni la muhimu kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilizungumzwa pia suala la ruzuku kwa wachimbaji wadogo. Hapa pia lilizungumzwa

na suala la elimu na ndiyo maana unaona hata kwenye ripoti ya Kamati na Wajumbe walipokuwa wanachangia, kuna baadhi ya pesa za ruzuku ambazo Serikali imepeleka, lakini ilienda kufanya kazi ambayo haikukusudiwa. Watu walienda kuelekeza kwenye maeneo ambayo hawakuyaombea. Kwa hiyo, hapa upatikane usimamizi wa kutosha ili kuhakikisha kwamba hela inayotolewa na Serikali inasimamiwa na inafanya klengo liliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika upande wa madini kuna makusanyo ya maduhuli. Napenda kuipongeza Wizara ya Madini kwa ukusanyaji wa maduhuli asilimia 84 ya lengo ambalo ni la mwaka mzima kwa kukusanywa ndani ya nusu mwaka. Kwa hiyo, kama Kamati tunaipongeza, iendelee na utaratibu huo. Vilevile wapo walioipongeza Serikali kwa kuchuka hatua kuhusu utoroshwaji na ubadhirifu ambaao unapatikana kwenye madini yetu ya *Tanzanite*. Serikali imeshachukua hatua kubwa ya kujenga ule ukuta na pia kupitia mikataba ambayo inaonekana inaitia hasara nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia kwenye Kamati yangu wameipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi inayozifanya, ni kazi njema, ina nia njema na imeonesha uzalendo mkubwa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa hili na maendeleo ya watu wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua hatua hii kukupongeza wewe, Mawaziri wote, kuwapongeza Wabunge wote waliochangia kwenye Kamati yangu na naomba sasa taarifa hii ya utekelezaji ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini ipokelewe na Bunge lako na kuwa ni taarifa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makof)*

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ukuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017 Iliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, hayo ni maoni na mapendekezo ya Bunge kwa Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru sana Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri sana waliyoifanya kwa niaba yetu sote ambao hatuko kwenye Kamati hizo, wamefanya kazi nzuri, wameshirikiana vizuri na Serikali, ndiyo maana tumewasikia hapa Mawaziri wakikubaliana na maoni na mapendekezo ya Kamati na kwamba yote watayafanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo nimeshawahoji, haya siyo maoni tena wala mapendekezo ya Kamati. Kwa upande wa Serikali taarifa hizi mbili za Kamati zimeshakubaliwa na Bunge. Kwa hiyo, hayo ndiyo Maazimio ya Bunge kwa Serikali, kwa maana ya kwamba Bunge sasa limeshaamua mambo gani liinaishauri Serikali na mambo gani lingependa yafanyike ili kuhakikisha kwamba tunawaletea maendeleo wananchi wetu. Kwa hiyo, nawaombe upande wa Serikali mzichukue taarifa hizi za Kamati, myapitie maoni yaliyoko humo na pia mapendekezo yaliyoko humo kwa sababu Bunge limeshahojiwa na hayo ndio mapendekezo ya Bunge na pia maoni ya Bunge.

Kwa upande wa Nishati na Madini na pia kwa upande wa Miundombinu, Bunge limeshafanya kazi yake ya kikatiba ya kuishauri Serikali na maoni yake yapo kwenye hizo taarifa za Kamati. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hata sisi ambao hatuko kwenye Kamati hizo, niwashukuru sana

kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kuweza kuchangia kwa maandishi, lakini pia kuchangia humu ndani ili kuweza kuweka vizuri maoni haya ili Serikali iweze kujuu nini cha kufanya. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwakumbushe tu, huwa tunakumbushana kila wakati, tumeshafika nusu ya kipindi chetu cha Bunge lakini bado hatufuati kanuni. Sijajua kama ni kwa makusudi ama ni kwamba tunasahau. Waheshimiwa Wabunge wengi wananyanya humu ndani wakielekea kila mahali wapendako, wananyanya wapendavyo kama wako kwenye mkutano wa hadhara hivi; lakini kanuni zetu zinatueleza nini cha kufanya unaponyanya kutoka sehemu moja kwenda nytingine.

Sasa tukifika nusu namna hili, halafu bado hatufuati hizo taratibu na siyo jambo zuri kwamba kiti kinakwambia rudi ulipokuwa ili ukafuate utaratibu wa namna ya kunyanya humu ndani. Tufuate utaratibu na nadhani ni mambo hayo kwa sababu hayatiliwi mkazo, ndiyo maana wakati mwingine tunaona tunaweza kujibizana ama kuzungumza namna tunayotaka humu ndani.

Hili Bunge tunapoliita wenyewe Bunge letu Tukufu ni lazima sisi wenyewe tulipe hiyo hadhi, hatuvezi kuwa tunanyanya humu ndani kama tuko darasani ama tuko mahali ambapo hapana utaratibu. Tufuate utaratibu ili akilini kwetu tujue kwamba hili ni jengo la namna gani na tuweze kutoa hiyo heshima ambayo tunaipa sisi wenyewe kwenye kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho Jumanne, tarehe 6 Februari, 2018, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.30 Usiku Bunge lillahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 6 Februari, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*